# HALI YA UCHUMI WA TAIFA

# KATIKA MWAKA 2018

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI ...... VIII**
**KIREFU/TAFSIRI YA MANENO ...... XIV**
**SURA YA I ...... 1**
**HALI YA UCHUMI WA TAIFA ...... 1**
UKUAJI WA UCHUMI ...... 1
MWENENDO WA BEI ...... 8
UKUZAJI RASILIMALI ...... 11
**SURA YA 2 ...... 37**
**FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA ...... 37**
UJAZI WA FEDHA ...... 37
MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA ...... 39
MAMLAKA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SEKTA YA HIFADHI YA JAMII (SSRA) ...... 41
MFUKO WA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA (PSSSF) ...... 42
MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF) ...... 42
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF) ...... 43
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF) ...... 44
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA BIMA TANZANIA (TIRA) ...... 45
BENKI YA MAENDELEO YA KILIMO TANZANIA (TADB) ...... 49
BENKI YA TPB ...... 50
MFUKO WA SELF ...... 51
**FEDHA ZA SERIKALI ...... 57**
UTANGULIZI ...... 57
MAPATO YA NDANI ...... 58
MISAADA NA MIKOPO NAFUU ...... 58
MIKOPO YA NDANI ...... 59
MIKOPO YENYE MASHARTI YA KIBIASHARA ...... 59
MATUMIZI ...... 59
DENI LA SERIKALI ...... 61
DENI LA NJE ...... 62
DENI LA NDANI ...... 63
TATHMINI YA UHIMILIVU WA DENI ...... 64
**SURA YA 4 ...... 70**
**SEKTA YA NJE ...... 70**
BIDHAA ZILIZOUZWA NJE ...... 70
BIDHAA ASILIA ...... 70
BIDHAA ZISIZO ASILIA ...... 72
MAPATO YA HUDUMA ...... 74
BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE ...... 75
MALIPO YA HUDUMA ...... 76
MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI MBALIMBALI ...... 77
MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE ...... 78

**SURA YA 5** .......... **95**
**HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** .......... **95**
UKUAJI WA UCHUMI .......... 95
MWENENDO WA BEI .......... 96
USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA .......... 96
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI .......... 96
JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA .......... 98
UMOJA WA AFRIKA .......... 98
**SURA YA 6** .......... **99**
**RASILIMALI WATU** .......... **99**
IDADI YA WATU .......... 99
MGAWANYIKO WA WATU KIMKOA .......... 99
**SURA YA 7** .......... **104**
**UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI** .......... **104**
UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI NCHINI .......... 104
MGAWANYIKO WA USAJILI WA MIRADI KISEKTA .......... 104
MGAWANYIKO WA MIRADI KIMKOA .......... 105
URAHISI WA KUWEKEZA NA KUFANYA BIASHARA NCHINI .......... 106
UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI .......... 107
USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KATIKA UWEKEZAJI NA MIRADI YA SERIKALI .......... 107
MAENDELEO YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI .......... 108
UWEKEZAJI BINAFSI KUTOKA NJE .......... 108
UWEKEZAJI WA MOJA KWA MOJA NA HISA .......... 109
AJIRA KUTOKANA NA UWEKEZAJI WA MOJA KWA MOJA .......... 109
**SURA YA 8** .......... **112**
**MASUALA MTAMBUKA** .......... **112**
UKIMWI .......... 112
MAZINGIRA .......... 112
USALAMA WA RAIA .......... 114
MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA .......... 116
WAKALA WA USAJILI, UFILISI NA UDHAMINI .......... 116
**SURA YA 9** .......... **118**
**HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU** .......... **118**
UTANGULIZI .......... 118
VIWANGO VYA UMASKINI .......... 118
MGAWANYO WA WATU MASKINI .......... 118
KINA CHA UMASKINI .......... 119
UMASKINI WA WATOTO .......... 121
TOFAUTI YA KIPATO .......... 121
MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI .......... 121
MAENDELEO YA WATU .......... 122

**SURA YA 10** .......... **125**
**MABORESHO YA MWAKA WA KIZIO KWA TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA** .......... **125**
Chimbuko .......... 125
Umuhimu wa Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa .......... 125
Malengo na Mbinu Zilizotumika Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa kwa Mwaka wa Kizio 2015 .......... 126
Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa .......... 127
**SURA YA 11** .......... **134**
**KILIMO NA USHIRIKA** .......... **134**
**KILIMO** .......... **134**
Uzalishaji wa Mazao ya Chakula .......... 134
Uzalishaji wa Mazao ya Biashara .......... 134
Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta .......... 135
Uzalishaji wa Mazao ya Bustani .......... 136
**MIFUGO** .......... **139**
Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake .......... 139
Uzalishaji, Utengenezaji na Usindikaji wa Vyakula vya Mifugo .......... 141
Biashara ya Mifugo na Mazao Yake .......... 141
**MAENDELEO YA USHIRIKA** .......... **144**
**SURA YA 12** .......... **154**
**MALIASILI NA UTALII** .......... **154**
Misitu na Nyuki .......... 154
Wanyamapori .......... 155
Utalii .......... 156
Malikale .......... 157
Uvuvi .......... 158
**SURA YA 13** .......... **171**
**MADINI** .......... **171**
Utangulizi .......... 171
Utafutaji Madini .......... 171
Uuzaji wa Madini .......... 171
**SURA YA 14** .......... **176**
**VIWANDA NA BIASHARA** .......... **176**
Uzalishaji katika Baadhi ya Viwanda Nchini .......... 176
Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo .......... 176
Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa .......... 177
Miundombinu ya Masoko ya Bidhaa za Mazao na Mifugo .......... 178
Mwenendo wa Biashara za Kimataifa .......... 179
**SURA YA 15** .......... **189**
**UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI** .......... **189**
UJENZI .......... 189
Mtandao wa Barabara Nchini .......... 189
Mtandao wa Barabara Zilizo chini ya TARURA .......... 191

Bodi ya Mfuko wa Barabara ..... 192
Wakala wa Nyumba na Majengo ya Serikali ..... 192
Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ..... 193
Bodi ya Usajili ya Wahandisi ..... 193
Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ..... 194
Baraza la Taifa la Ujenzi ..... 194
**MAENDELEO YA ARDHI ..... 195**
Uthamini wa Mali kwa Madhumuni Mbalimbali ..... 196
Mipango ya Matumizi ya Ardhi ..... 197
Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ..... 198
MAENDELEO YA MAKAZI ..... 199
**SURA YA 16 ..... 200**
**MAWASILIANO NA UCHUKUZI ..... 200**
**UCHUKUZI ..... 200**
Usafiri wa Barabara ..... 200
Usafiri kwa Kutumia Reli ..... 201
Usafiri wa Anga ..... 202
Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ..... 204
Uchukuzi Kwenye Maziwa ..... 206
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ..... 207
**HUDUMA ZA MAWASILIANO ..... 208**
Huduma za Posta ..... 208
Huduma za Simu ..... 210
Huduma za INTANETI ..... 211
Huduma za Utangazaji ..... 211
Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ..... 212
Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ..... 212
**HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ..... 213**
Sekta ya Habari ..... 213
Maendeleo ya Sanaa ..... 214
Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ..... 215
Maendeleo ya Michezo ..... 216
**SURA YA 17 ..... 225**
**NISHATI ..... 225**
Ufuaji wa Umeme ..... 225
Uagizaji Mafuta ..... 230
Mwenendo wa Bei za Mafuta ..... 232
Nishati Jadidifu ..... 234
**SURA YA 18 ..... 236**
**MAJI ..... 236**
Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji ..... 236
Huduma ya Maji Vijijini ..... 237
Huduma za Maji Mijini ..... 237

**SURA YA 19** .......... **241**
**ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** .......... **241**
Elimu ya Awali .......... 241
Elimu ya Msingi .......... 241
Elimu ya Sekondari .......... 242
Elimu katika Vyuo vya Ualimu .......... 243
Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu .......... 243
Elimu ya Ufundi na Mafunzo .......... 244
Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi .......... 244
Elimu ya Juu .......... 245
**SURA YA 20** .......... **251**
**AFYA NA MAENDELEO YA JAMII** .......... **251**
**AFYA** .......... **251**
Vituo vya Kutolea Huduma za Afya .......... 251
Huduma za Afya kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja .......... 251
Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba .......... 252
Lishe .......... 253
Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa .......... 253
**MAENDELEO YA JAMII** .......... **255**
Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii .......... 255
Maendeleo ya Wanawake .......... 256
Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto .......... 256
Huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto .......... 258
Huduma za Ustawi kwa Wazee .......... 258
Mashirika Yasiyo ya Kiserikali .......... 258

**Ukurasa**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali A: Takwimu Muhimu Katika Uchumi – Tanzania Bara ..... .xviii

Jedwali B: Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2013 – 2019…....xix

Jedwali 1: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) ............................................. 13

Jedwali 1A Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko – Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika) ............................................... 14

Jedwali 2: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika).......................... 15

Jedwali 2A: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko- Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za miaka inayohusika) .............................................. 16

Jedwali 2B: Pato la Taifa (PLT) na Matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za miaka inayohusika) ............................................... 17

Jedwali 3: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, (Kwa Bei za mwaka 2015) .......................................................... 18

Jedwali 3A: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Kwa Bei za mwaka 2015) ................................................ 19

Jedwali 4: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, (Kwa Bei za mwaka 2015) ................................................ 20

Jedwali 4A: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (Bei za mwaka 2015)........................................................ 22

Jedwali 4B: Pato la Taifa (PLT) na matumizi yake, kwa bei za soko (Bei za mwaka 2015)...................................................... 23

Jedwali 5: Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli (bei za miaka inayohusika)............................................................................24

Jedwali 6: Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya shughuli(Bei za mwaka 2015).25

Jedwali 7a: Mchango katika Ukuzaji Rasilimali kwa aina ya Shughuli (Kwa Bei za Miaka inayohusika) ................. .....................26

Jedwali 7b: Ukuzaji wa Rasilimali katika Sehemu za Uchumi wa Kitaifa na Binafsi ( Kwa bei za Miaka inayohusika).........................26

.

Jedwali 8: Fahirisi za bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (Des. 2015=100)..27

Jedwali 9: Fahirisi za Bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini D'Salaam (Des. 2015=100).......28

Jedwali 10: Fahirisi za bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (Des. 2015=100)................................................................ 29

Jedwali 11: Fahirisi ya Bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na Wafanyakazi wa kima cha kati D'Salaam (Des. 2015=100).30

Jedwali 12: Fahirisi ya Bidhaa na Huduma zitumiwazo na wenye kipato cha juu Dar es Salaam (Des. 2015=100) .......................... 31

Jedwali 13: Fahirisi ya gharama ya maisha ya wenye kipato cha juu Dar es Salaam (Des. 2015=100)................................. 32

Jedwali 14: Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2015=100) ............. 33

Jedwali 15: Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (Des. 2015=100) ..... 34

Jedwali 16: Fahirisi mbali mbali za bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini – Tanzania Bara (Des. 2015=100) ....... 36

Jedwali 17: Mwenendo wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara.53

Jedwali 18: Viwango vya ukuaji wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania Bara................................................................. ..54

Jedwali 19: Mwenendo wa Viwango vya ubadilishaji kati ya Shilingi na Dola ya Marekani ............................................................ 55

Jedwali 20: Mikopo ya benki za biashara kwa Shughuli za Kiuchumi...55

Jedwali 21: Mwenendo wa amana katika benki za biashara ............... 56

Jedwali 22: Viwango vya wastani vya riba (asilimia) ......................... 56

Jedwali 23: Mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali................. 66

Jedwali 24: Mgawanyo wa Matumizi ya Serikali kwa huduma za Serikali (Sh. Milioni) .................................................. 68

Jedwali 25: Thamani ya Bidhaa za biashara baina ya Tanzania na nchi za nje (Sh. Milioni) ............................................. 82

Jedwali 26: Kiasi na thamani ya bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh. Milioni) .......................................................... 83

Jedwali 27: Kiasi na thamani ya bidhaa za asilia na zisizo asilia zilizouzwa nchi za nje ............................................. 84

Jedwali 28: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh./tani)......................................................... 89

Jedwali 29: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (US $/tani)...................................................... 90

Jedwali 31: Aina na thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za nje (Sh. Milioni).................................................... 92

Jedwali 32: Mizania ya malipo na nchi za nje (US$ milioni) ............... 93

Jedwali 33: Idadi ya watu nchini Tanzania kimkoa (2010-2018)....... 102

Jedwali34: Kituo cha Uwekezaji Tanzania(TIC): Miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa .................................................. 111

Jedwali 35: Uzalishaji wa miwa na sukari nchini................................145

Jedwali 36: Pamba iliyonunuliwa na mauzo nchini............................ 146

Jedwali 37: Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana.................................................................. 147

Jedwali 38: Kahawa iliyonunuliwa na mauzo nchini .......................... 148

Jedwali 39: Eneo lililopandwa mkonge na katani iliyopatikana.......... 149

Jedwali 40: Tumbaku iliyonunuliwa na mauzo nchini ........................ 150

Jedwali 41: Maua ya pareto yaliyonunuliwa na mauzo ya bidhaa za pareto nchini.................................................... 151

Jedwali 42: Korosho zilizonunuliwa na mauzo nchini. ....................... 152

Jedwali 43: Muhtasari wa kiasi cha mazao muhimu ya biashara yaliyonunuliwa ................................................................ 153

Jedwali 45: Idadi ya wageni waliotembelea Hifadhi za Taifa na mapato yaliopatikana........................................................ 162

Jedwali 47: Mauzo ya bidhaa za misitu katika masoko ya nje ............ 163

Jedwali 48: Idadi na mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii.......... 164

Jedwali 50: Uzalishaji katika sekta ya uvuvi (2000-2018) ................. 165

Jedwali 51: Mauzo ya mazao ya uvuvi nchi za nje............................. 166

Jedwali 51A: Muhtasari wa Mauzo ya Mazao ya Uvuvi Nchi za Nje.... 167

Jedwali 51B: Mwelekeo wa Mauzo ya Sangara Nje ya Nchi ............... 167

Jedwali 52: Mwenendo wa Biashara ya Utalii .................................. 168

Jedwali 53: Idadi ya watalii walioingia nchini na kiasi cha fedha kilichopatikana....................................................... 169

Jedwali 54 Watalii waliotembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro katika mwaka 2009 - 2018...............................................169

Jedwali 55: Idadi ya wageni waliotembelea Vituo vya Utalii ............ 170

Jedwali 56: Uchimbaji wa madini: Kiasi kilichopatikana .................. 174

Jedwali 57: Madini yaliyouzwa nchi za nje (2014-2018).................... 175

Jedwali 58: Matumizi ya saruji nchini................................................ 182

Jedwali 59: Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani................. 183

Jedwali 60: Viwanda - Idadi ya Watu walioajiriwa............................ 184

Jedwali 61: Viwanda - Gharama za kazi ............................................ 185

Jedwali 62: Viwanda - Muhtasari wa Matokeo .................................. 186

Jedwali 63: Viwanda - Muhtasari wa Matokeo Kimkoa ..................... 187

Jedwali 65: Vigezo vya Ufanisi katika Sekta ya Viwanda ................. 188

Jedwali 67: Shirika la Reli Tanzania (TRL) ....................................... 217

Jedwali 68: Reli ya Uhuru (TAZARA)............................................... 218

Jedwali 69: Usafirishaji kwa Meli ...................................................... 219

Jedwali 70: Huduma za Posta ............................................................ 222

Jedwali 71: Idadi ya Wanaotumia Simu za Mezani na Viganjani........223

Jedwali 73: Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ................................ 224

Jedwali 74: Uwezo wa Mitambo ya Umeme na Kiasi cha Umeme Uliotengenezwa kwa Vituo………………………………226

Jedwali 75: Mauzo ya Umeme kwa Watumiaji Mbalimbali .............. 227

Jedwali 76: Mauzo ya Umeme kwa Mikoa ........................................ 228

Jedwali 77: Uzalishaji wa maji na mapato yatokanayo na maji Mijini..239

Jedwali 78: Mahitaji na Upatikanaji wa Maji katika Miji ...................240

Jedwali 80: Shule za sekondari za Serikali - Idadi ya wanafunzi kwa kidato ............................................ ........... ..........246

Jedwali 81: Shule za sekondari za binafsi - Idadi ya wanafunzi kwa kidato ...................................................................... 250

Jedwali 84: Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma za afya nchini ........ 260

Jedwali 85: Huduma za Afya: Waliofaulu Mafunzo ya Afya ............ 261

Jedwali 86: Idadi ya Wagonjwa katika Vituo vya Afya...................... 262

Jedwali 87: Idadi ya Vitanda katika Hospitali zote Nchini...................263

## KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

| | | |
|---|---|---|
| ASDP | - | Agricultural Sector Development Programme (Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo) |
| AfDB | - | African Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Afrika) |
| RVs | - | Anti-retrovirals ( Dawa za Kupunguza Makali ya UKIMWI) |
| ATCL | - | Air Tanzania Company Limited (Kampuni ya Ndege Tanzania) |
| AU | - | African Union (Umoja wa Afrika) |
| BoT | - | Bank of Tanzania (Benki Kuu ya Tanzania) |
| CCM | - | Chama cha Mapinduzi |
| Cif | - | Cost, insurance and freight (Thamani ya bidhaa ikijumuisha gharama za usafiri na bima) |
| CPI | - | Consumer Price Index (Fahirisi ya Bei za Walaji) |
| COMESA | - | Common Market for Eastern and Southern Africa |
| CHF | - | Community Health Fund (Mfuko wa Jamii wa Afya) |
| CUHAS | - | Catholic University of Health and Allied Sciences (Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba) |
| CFTA | - | Afican Continental Free Trade Areas (Eneo Huru la Biashara kwa Umoja wa Afrika) |
| DSE | - | Dar es Salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar Es Salaam) |
| ECA | - | Economic Commission for Africa (Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika) |
| EAC | - | East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| EPOCA | - | Electronic and Postal Communications (Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta) |
| EPZ | - | Export Processing Zones (Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje) |
| EWURA | - | Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati) |
| EFD | - | Electronic Fiscal Divices Machines (Mashine za Kielektroniki) |
| f.o.b | - | free on board (Thamani ya Bidhaa bila Kujumuisha Gharama za Usafiri na Bima) |
| FDI | - | Foreign Direct Investment (Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni) |
| GEPF | - | Government Employees Provident Fund (Mfuko wa Mafao ya Kustaafu) |
| GBS | - | General Budget Support (Misaada na Mikopo ya Bajeti) |
| GePG | - | Government e-Payment Gateway (Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali wa Ukusanyaji wa Mapato) |
| GDP | - | Gross Domestic Product (Pato la Taifa) |
| GIS | - | Geographic Information System (Mfumo wa Kijiografia ) |
| HBS | - | Household Budget Survey (Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya) |
| HDI | - | Human Development Index (Fahirisi ya Maendeleo ya Watu) |
| IFMS | - | Integrated Financial Management System (Mfumo Tungamanishi wa Usimamizi wa Fedha) |
| IHI | - | Ifakara Health Institute (Taasisi ya Afya Ifakara) |
| IMF | - | International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa) |

| | | |
|---|---|---|
| LAPF | - | Local Authorities Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa) |
| $M_1$ | - | Narrow Money Supply (Ujazi wa fedha kwa Tafsiri Finyu) |
| $M_2$ | - | Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana) |
| $M_3$ | - | Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi) |
| ILO | - | International Labour Organisation ( Shirika la Kazi Duniani) |
| KCMUCo | - | Kilimanjaro Christian Medical University College ( Chuo cha Matibabu Kilimanjaro) |
| MUHAS | - | Muhimbili University of Health and Allied Sciences ( Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili) |
| MKUKUTA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania |
| MKURABITA | - | Mpango wa Kurasimisha Biashara na Mali za Wanyonge Tanzania |
| MSCL | - | Marine Services Company Ltd (Kampuni ya Huduma za Meli) |
| MSD | - | Medical Stores Department (Bohari Kuu ya Dawa) |
| MW | - | Mega Watts |
| NIMR | - | National Institute for Medical Research (Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu) |
| NSSF | - | National Social Security Fund (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) |
| NGO's | - | Non-Governmental Organisations (Asasi Zisizo ya Kiserikali) |
| NHIF | - | National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya) |
| NIC | - | National Insurance Corporation (Shirika la Bima la Taifa) |
| NIDA | - | National Identification Authority (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) |
| NMB | - | National Microfinance Bank (Benki ya Taifa ya Mikopo Midogo) |
| NICOL | - | National Investments Company Limited (Kampuni ya Usimamizi wa Uwekezaji ) |
| PSSSF | - | Public Service Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ) |
| PPF | - | Parastatal Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma) |
| RITA | - | Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) |
| SIDO | - | Small Industries Development Organization (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) |
| SAGCOT | - | Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania |
| SACCOS | - | Savings and Credit Cooperative Societies (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo) |
| SGR | - | Standard Gauge Railway (Reli kwa Kiwango cha Kimataifa ) |
| SADC | - | Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika) |
| SELF | - | Small Enterpreneurs Loan Facility (Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogondogo) |
| SSRA | - | Social Security Reguratory Authority (Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii) |
| SUMATRA | - | Surface and Marine Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini) |
| TAA | - | Tanzania Airpots Authority (Mamlaka ya Viwanja vya Ndege) |

| | | |
|---|---|---|
| TEMESA | - | Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency (Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania) |
| TARI | - | Tanzania Agricultural Research Institute (Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ) |
| TaESA | - | Tanzania Employment Service Agency (Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania) |
| TANESCO | - | Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Umeme Tanzania) |
| TANROAD | - | Tanzania Roads Agency (Mamlaka ya Barabara Tanzania) |
| TAWA | - | Tanzania Wildlife Authority (Mamlaka ya Uhifadhi Wanyamapori) |
| TAZARA | - | Tanzania Zambia Railways Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia) |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TIRA | - | Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania) |
| TICTS | - | Tanzania International Container Terminal Services (Kampuni ya Kupakua Makontena katika Bandari ya Dar es Salaam) |
| TEUs | - | Twenty Equivalent Units |
| TCAA | - | Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania) |
| TCRA | - | Tanzania Communications Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania) |
| TCCIA | - | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo) |
| TDHS | - | Tanzania Demographic and Health Survey (Utafiti wa Afya na Demografia Tanzania) |
| TMA | - | Tanzania Meteorology Agency (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania) |
| TMRC | - | Tanzania Mortgage Refinance Company ( Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania) |
| TPA | - | Tanzania Ports Authority ( Mamlaka ya Bandari Tanzania) |
| TRL | - | Tanzania Railways Company Limited (Kampuni ya Reli Tanzania) |
| TTCL | - | Tanzania Telecomunications Company Limited (Kampuni ya Simu Tanzania) |
| TPB | - | Tanzania Postal Bank (Benki ya TPB) |
| UAE | - | United Arab Emirates (Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu) |
| UNDP | - | United Nations Development Programme (Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo) |
| UNIDO | - | United Nations Industrial Development Organization (Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda) |
| UKIMWI | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UTT | - | Unit Trust of Tanzania |
| VVU | - | Virusi Vya Ukimwi |
| WCF | - | Workers Compensation Fund (Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi) |
| WHC | - | Watumishi Housing Company |
| WEO | - | World Economic Organisation (Shirika la Kiuchumi Duniani) |
| WTO | - | World Trade Organisation (Shirika la Biashara Duniani) |

## MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2018

| TAREHE | MWEZI | MATUKIO |
|---|---|---|
| 14 | Machi | Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli aweka jiwe la msingi katika sehemu ya pili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (Standard Gauge) |
| 4 | Aprili | Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli azindua ujenzi wa ukuta wa Mererani kudhibiti uchimbaji wa madini ya Tanzanite. |
| 5 | Mei | Uzinduzi wa Miradi ya Kimkakati kuziwezesha Halmashauri kujitegemea kimapato. |
| 27 | Septemba | Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli alizindua daraja la juu la Mfugale, TAZARA. |
| 25 | Novemba | Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli alizindua Kampasi ya Mloganzila Kibamba. |
| 27 | Novemba | Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli alizindua maktaba ya kisasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. |
| 12 | Desemba | Utiaji saini mkataba wa utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Mto Rufiji ulifanyika. |

**TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA**

**Jedwali Na. A**

| Maelezo | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018p | 2017/18 Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watu (Milioni) | 43.6 | 44.8 | 46.1 | 47.4 | 48.7 | 51.0 | 52.6 | 3.1 |
| Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. Milioni) | 62,318,659 | 72,977,200 | 82,603,388 | 94,349,316 | 108,362,324 | 118,744,498 | 129,364,353 | 8.9 |
| Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2015 (Sh. Milioni) | 77,979,847 | 83,268,117 | 88,874,111 | 94,349,316 | 100,828,393 | 107,657,405 | 115,140,194 | 7.0 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.) | 1,429,327 | 1,628,955 | 1,793,387 | 1,990,492 | 2,225,099 | 2,328,323 | 2,459,398 | 5.6 |
| Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2007 (Sh.) | 1,788,529 | 1,858,663 | 1,929,529 | 1,990,492 | 2,070,398 | 2,110,930 | 2,188,977 | 3.7 |
| Kasi ya Upandaji Bei (asilimia) | 16.0 | 7.9 | 6.1 | 5.6 | 5.2 | 5.3 | 3.5 | -34.0 |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni) | -4429.9 | -5771.1 | -5723.7 | -4526.3 | -3513.9 | -3027.80 | -3793.50 | 25.3 |
| Urari wa Bidhaa,Huduma na Uhamisho wa Mali (US$ milioni) | -3768.9 | -4988.5 | -5028.2 | -3987.4 | -2664.7 | -1880.70 | -2344.50 | 24.7 |
| Saruji Iliyotumika (Tani '000) | 3,425,991 | 3,433,791 | 4,082,681 | 4,404,187 | 6,028,794 | 4,359,163 | 4,577,960 | 5.0 |
| Umeme Uliouzwa (GWH) | 4,401.4 | 4,806.7 | 5,051.5 | 5,297.1 | 5,871.5 | 5,956.2 | 6,290.7 | 5.6 |
| Utalii (Mapato US$ milioni) | 1,712.8 | 1,853.3 | 1,983.0 | 1,901.9 | 2,131.6 | 2,199.8 | 2,432.9 | 10.6 |
| Reli: Uchukuzi Mizigo (Tani '000) | 413.0 | 430.0 | 160.0 | 363.6 | 198.0 | 341.0 | 625.0 | 83.3 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) * | 8247.2 | 8231.9 | 8222.7 | 8298.3 | 8639.2 | 9317.8 | 10,112 | 8.5 |
| Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) * | 1884.3 | 1804.1 | 1947.3 | 1774.4 | 1807.0 | 1908.9 | 2,149 | 12.6 |
| Hospitali: Idadi ya Vitanda | 47,484 | 70,906 | 50,670 | - | 59,757 | 60,952 | 62,203 | 2.1 |
| **Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (Mil. US$)** | | | | | | | | |
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | |
| Kahawa | 186.60 | 171.00 | 121.50 | 162.20 | 153.69 | 126.29 | 147.94 | 17.1 |
| Pamba | 164.90 | 111.70 | 54.70 | 30.20 | 46.76 | 36.76 | 68.39 | 86.0 |
| Katani | 18.40 | 16.90 | 16.80 | 26.50 | 17.23 | 28.73 | 33.22 | 15.6 |
| Chai | 56.10 | 56.90 | 45.70 | 44.00 | 44.79 | 49.13 | 45.95 | -6.5 |
| Tumbaku | 350.10 | 307.00 | 315.00 | 287.60 | 339.20 | 195.81 | 270.30 | 38.0 |
| Korosho | 142.60 | 162.40 | 222.20 | 218.80 | 320.24 | 529.60 | 196.47 | -62.9 |
| Karafuu | 38.10 | 43.00 | 52.90 | 24.10 | 39.28 | 54.40 | 10.53 | -80.7 |
| **Bidhaa zisizo Asilia** | | | | | | | | |
| Madini | 2197.80 | 1782.10 | 1469.20 | 1285.40 | 1930.02 | 1694.48 | 1615.25 | -4.7 |
| Bidhaa za Viwanda | 1037.30 | 1072.10 | 1239.60 | 1364.50 | 1092.10 | 693.73 | 794.56 | 14.5 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | 160.60 | 130.60 | 195.00 | 173.50 | 142.50 | 193.01 | 158.40 | -17.9 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 31.30 | 28.10 | 30.50 | 24.40 | 24.80 | 27.16 | 33.04 | 21.6 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (Re-export) | 181.70 | 172.80 | 177.00 | 385.80 | 480.00 | 126.49 | 175.58 | 38.8 |
| Bidhaa nyinginezo | 557.70 | 517.60 | 687.20 | 884.30 | 972.20 | 357.06 | 432.50 | 21.1 |
| **Ujazi wa Fedha** | | | | | | | | |
| Ujazi wa Fedha-M3 (Sh. bilioni) [1] | 14,647.1 | 16,106.8 | 18,614.2 | 22,115.3 | 22,877.8 | 24,714.3 | 25,823.5 | 4.5 |
| Karadha (Sh. bilioni) | 13,719.0 | 16,293.0 | 18,863.7 | 22,505.5 | 23,775.8 | 24,977.2 | 26,249.3 | 5.1 |
| **Fedha za serikali** | **2012/13** | **2013/14** | **2014/15** | **2015/16p** | **2016/17** | **2017/18** | **2018/19p** | **2018/19** |
| Mapato ya Ndani ya Serikali (Sh. milioni) | 8,442,610.8 | 10,182,454.7 | 10,957,765.3 | 14,048,034.0 | 16,639,831.5 | 17,944,887.0 | 20,894,578.1 | 16.4 |
| Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. milioni) | 9,043,323.0 | 10,032,119.7 | 10,893,486.1 | 13,420,045.1 | 11,625,865.8 | 12,852,304.0 | 14,199,023.1 | 10.5 |
| Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. milioni) | 4,499,695.2 | 3,926,042.2 | 3,710,228.2 | 4,339,552.9 | 7,272,824.3 | 7,615,768.3 | 12,007,273.5 | 57.7 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

* Kwa shule za Serikali na binafsi

[1] Kwa tafsiri pana (M3)

\- Takwimu hazikupatikana

[P] Takwimu za Awali

## JEDWALI B: MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI MKUU NA BAJETI

| Mwaka wa Kalenda | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PATO LA TAIFA** | | | | | | | |
| Ukuaji halisi wa Pato la Taifa (mp) | 4.5% | 6.8% | 6.7% | 6.2% | 6.9% | 6.8% | 7.0% |
| Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika (mp) | 15.5% | 17.1% | 13.2% | 14.2% | 14.9% | 9.6% | 8.1% |
| Uwiano wa Uwekezaji na Pato la Taifa (Investment/GDP) | 30.1% | 29.6% | 31.4% | 33.2% | 32.3% | 22.5% | 23.8% |
| Uwiano wa Akiba kwenye Benki na Pato la Taifa (Savings/GDP) | 12.2% | 8.0% | 14.7% | 17.1% | 15.0% | 17.7% | 20.9% |
| **MWENENDO WA BEI NA VIWANGO VYA RIBA** | | | | | | | |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (mwisho wa kipindi) | 12.1% | 5.6% | 4.8% | 6.8% | 6.5% | 4.0% | 3.3% |
| Kasi ya Upandaji wa Bei (wastani wa mwaka) | 16.1% | 7.9% | 6.1% | 5.6% | 5.2% | 5.3% | 3.5% |
| GDP deflator Inflation (bp) | 9.8% | 10.7% | 4.8% | 6.1% | 7.1% | 2.5% | 1.8% |
| GDP deflator Inflation (MP) | 10.5% | 9.7% | 6.1% | 7.6% | 7.5% | 2.6% | 1.8% |
| Riba za Mikopo (mwaka mmoja) | 14.2% | 14.0% | 14.7% | 14.2% | 13.7% | 18.3% | 18.2% |
| Riba za Amana za muda maalum (miezi 12) | 11.3% | 11.6% | 10.8% | 10.8% | 11.5% | 11.7% | 8.8% |
| Tofauti ya riba za amana na za mikopo (mwaka) | 2.9% | 2.4% | 3.9% | 3.4% | 2.2% | 6.6% | 9.4% |
| Thamani ya Tsh/Dola (wastani wa mwaka) | 1,571.7 | 1,598.7 | 1,652.5 | 1,985.4 | 2,177.1 | 2,228.9 | 2,255.8 |
| **UJAZI WA FEDHA** | | | | | | | |
| Kiwango cha ukuaji wa M3 | 12.5% | 10.0% | 15.6% | 18.8% | 3.4% | 8.0% | 4.5% |
| Kiwango cha ukuaji wa M2 | 16.0% | 10.9% | 17.0% | 13.4% | 5.3% | 10.4% | 3.8% |
| Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi | 18.2% | 15.3% | 19.4% | 24.8% | 7.2% | 1.7% | 4.9% |
| **UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | |
| Bidhaa zilizouzwa nje | 14.9% | 11.5% | 10.4% | 11.2% | 9.8% | 8.5% | 7.7% |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 21.9% | 18.5% | 17.2% | 18.4% | 17.0% | 15.7% | 14.8% |
| Bidhaa zilizonunuliwa kutoka nje | 26.0% | 24.2% | 21.9% | 20.6% | 17.0% | 14.2% | 14.4% |
| Bidhaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 32.0% | 29.6% | 27.2% | 26.2% | 21.4% | 18.0% | 18.2% |
| Urari wa malipo ya kawaida | -9.5% | -10.9% | -10.0% | -8.3% | -5.5% | -3.5% | -4.8% |
| Akiba ya fedha za kigeni (miezi) | **3.9** | **4.2** | **4.2** | **4.6** | **5.4** | **6.8** | **4.9** |
| **UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA** | | | | | | | |
| **Mwaka wa fedha** | **2011/12** | **2012/13** | **2013/14** | **2014/15** | **2015/16** | **2016/17** | **2017/18** |
| Mapato ya ndani | 12.4% | 12.5% | 13.1% | 12.4% | 13.9% | 14.7% | 14.7% |
| Mapato ya kodi | 11.1% | 11.4% | 11.9% | 11.2% | 12.2% | 12.4% | 12.3% |
| Matumizi (Bila rollover) | 18.5% | 18.8% | 17.9% | 16.5% | 17.5% | 16.6% | 17.3% |
| Matumizi ya kawaida | 12.0% | 13.4% | 12.9% | 12.3% | 13.2% | 10.2% | 11.1% |
| Matumizi ya maendeleo | 6.5% | 5.4% | 5.0% | 4.2% | 4.3% | 6.4% | 6.2% |
| Misaada | 3.2% | 2.0% | 2.0% | 1.2% | 0.5% | 1.0% | 0.8% |
| Nakisi (kabla ya misaada) | -6.7% | -6.2% | -5.3% | -4.3% | -3.9% | -2.4% | -2.6% |
| Nakisi (baada ya misaada) | -3.5% | -4.1% | -3.2% | -3.2% | -3.4% | -1.4% | -1.9% |
| Mikopo ya nje | 3.0% | 2.6% | 2.9% | 2.3% | 1.1% | 1.5% | 1.4% |
| Mikopo ya ndani (kutoka benki) | 0.0% | 1.0% | 1.2% | 0.6% | 1.5% | -0.9% | -0.3% |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

# SEHEMU YA KWANZA

# MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA


## SURA YA I

## HALI YA UCHUMI WA TAIFA

### Ukuaji wa Uchumi

1. Mwaka 2018, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia mwaka 2015 kama mwaka wa kizio kutoka mwaka wa kizio wa 2007. Kufuatia maboresho hayo, mabadiliko kadhaa yalijitokeza ikiwemo mfumo na ukubwa wa Pato la Taifa; viwango vya ukuaji na mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa; na uwiano wa viashiria mbalimbali kwa Pato la Taifa. Maelezo ya kina kuhusu maboresho hayo yako katika sura ya kumi. Kutokana na zoezi hilo, kuanzia toleo hili takwimu zitakazotumika zitakuwa za mwaka wa kizio wa 2015. Kwa mujibu wa takwimu mpya za mwaka wa kizio wa 2015, Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 7.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2017. Ukuaji huu ulichochewa zaidi na kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika miundombinu kama vile ujenzi wa barabara, reli, na viwanja vya ndege; kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; na hali nzuri ya hewa kwa ajili ya kilimo. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na: sanaa na burudani iliyokua kwa asilimia 13.7; ujenzi (asilimia 12.9); uchukuzi na uhifadhi mizigo (asilimia 11.8); na habari na mawasiliano (asilimia 9.1).

**Kielelezo Na. 1.1 Mwenendo wa Ukuaji kwa Baadhi ya Sekta (Asilimia)**



2. Miongoni mwa matokeo ya maboresho ya takwimu za Pato la Taifa ni kuongezeka kwa Pato la Wastani la kila mtu. Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika lilikuwa shilingi milioni 129,364,353 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi milioni 118,744,498 mwaka 2017. Aidha, mwaka 2018, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 52,619,314 ambapo Pato la wastani la kila mtu lilifikia shilingi 2,458,496 kutoka shilingi 2,327,395 mwaka 2017, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 5.6. Kiasi hicho cha Pato la wastani kwa kila mtu kwa mwaka 2018 ni sawa na dola za Marekani 1,090 ikilinganishwa na dola za Marekani 1,044 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.4.

3. Mwaka 2018, shughuli za kiuchumi za kilimo ambazo zinajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu, uvuvi na huduma za ughani zilikua kwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.9 mwaka 2017 kwa takwimu zilizoboreshwa. Ukuaji huu ulitokana na kupatikana kwa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wa mazao na upatikanaji wa maji na malisho ya kutosha kwa ajili ya mifugo. Shughuli ndogo za uzalishaji mazao zilikua kwa asilimia 5.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2017 na zilichangia asilimia 16.2 katika Pato la Taifa. Aidha, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za mifugo kilibaki kuwa asilimia 4.9 kama ilivyokuwa mwaka 2017 na kilichangia asilimia 7.6 katika Pato la Taifa mwaka 2018.

4. Shughuli ndogo za kiuchumi za misitu zilikua kwa asilimia 4.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2017. Shughuli hizi za misitu zilichangia asilimia 2.7 katika Pato la Taifa mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kwa shughuli ndogo za kiuchumi za uvuvi kilifikia asilimia 9.2 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.4 mwaka 2017. Kiwango kikubwa cha ukuaji kilitokana na utunzaji mzuri wa mazalia ya samaki yakiwemo mabwawa ya watu binafsi sambamba na kuongezeka kwa mahitaji katika soko la ndani na nje. Shughuli za uvuvi zilichangia asilimia 1.7 katika Pato la Taifa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2017. Kwa upande mwingine, huduma za ughani katika shughuli za kilimo zilikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 5.5 mwaka 2017. Hizi ni shughuli ambazo hapo awali kabla ya maboresho ya mwaka wa kizio zilikuwa zikijumuishwa katika kilimo cha mazao, mifugo na misitu.

5. Shughuli za kilimo sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 5.3 mwaka 2018 wakati sehemu isiyouzika zilikua kwa asilimia 4.9. Kiwango cha ukuaji wa shughuli ndogo za kiuchumi za uvuvi na misitu sehemu inayouzika kiliongezeka kufikia asilimia 9.2 na asilimia 5.2 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.4 na asilimia 4.9 mwaka 2017 kwa mtiririko huo. Hata hivyo, kasi ya ukuaji kwa shughuli ndogo za kiuchumi za mazao na mifugo sehemu inayouzika ilipungua na kuwa asilimia 5.4 na asilimia 4.2 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.9 na asilimia 5.2 mwaka 2017 mtawalia. Kwa upande wa sehemu isiyouzika, viwango vya ukuaji wa shughuli ndogo za kiuchumi za mifugo na uvuvi viliongezeka mwaka 2018 wakati ambapo ukuaji wa shughuli za mazao na misitu ulipungua ikilinganishwa na mwaka 2017. Mchango wa shughuli za kilimo katika Pato la Taifa kwa ujumla wake ulipungua kufikia asilimia 28.2 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 28.8 mwaka 2017.

6. Uchimbaji madini na mawe unahusisha ukusanyaji wa madini yabisi yanayopatikana kwenye uso wa dunia (kama vile makaa ya mawe na chuma), vimiminika, na gesi asilia. Shughuli za kiuchumi za uchimbaji madini na mawe zilikua kwa asilimia 1.5 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa almasi, makaa ya mawe na gesi asilia. Uzalishaji wa makaa ya mawe uliongezeka kufuatia kuimarika kwa soko la ndani kutokana na Serikali kuzuia uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi. Aidha, uzalishaji wa gesi asilia uliongezeka kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya umeme na matumizi mengine katika viwanda. Uzalishaji wa dhahabu ulipungua kutokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kudhibiti uchimbaji na uuzaji holela wa madini ili kuhakikisha kuwa madini hayo yanawanufaisha Watanzania na Taifa kwa ujumla. Licha ya kupungua kwa kiwango cha ukuaji, mchango wa shughuli za uchimbaji madini na mawe katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 5.1 mwaka 2018 kutoka asilimia 4.4 mwaka 2017.

**Jedwali Na.1.1: Uzalishaji kwa Baadhi ya Madini**

| Aina ya Madini | Kipimo | 2017 | 2018 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Almasi | Karati | 304,456 | 381,302 | 25.2 |
| Gesi Asilia | Mita za Ujazo (Milioni) | 47,457 | 59,142 | 24.6 |
| Makaa ya Mawe | Tani | 558,553 | 627,652 | 12.4 |
| Dhahabu | Kilogramu | 43,489 | 39,304 | -9.6 |

**Chanzo:** Wizara ya Madini

7. Mwaka 2018, kasi ya ukuaji wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani ilikuwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2017. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa baadhi ya bidhaa zikiwemo bidhaa za vyakula, vinywaji baridi, saruji, unga wa ngano, chuma, na rangi sambamba na kuongezeka kwa hamasa ya matumizi ya bidhaa za ndani. Mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka na kuwa asilimia 8.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 7.7 mwaka 2017.

8. Mwaka 2018, shughuli za uzalishaji na usambazaji umeme zilikua kwa asilimia 5.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.0 mwaka 2017. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji umeme kwa kutumia mitambo ya Kinyerezi II kutoka MW 55.94 mwaka 2017 hadi MW 248.22 mwaka 2018. Takribani theluthi mbili ya umeme uliozalishwa katika gridi ya Taifa ulitokana na gesi asilia. Ufuaji umeme kutoka vyanzo mbalimbali kwa ujumla uliongezeka kwa asilimia 3.4 kufikia saa za gigawati 7,354.59 mwaka 2018. Shughuli za usambazaji umeme zilichangia asilimia 0.3 katika Pato la Taifa mwaka 2018 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 0.4 mwaka 2017.

9. Mwaka 2018, shughuli za usambazaji maji na udhibiti maji taka zilikua kwa asilimia 7.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.4 mwaka 2017. Ukuaji huu unatokana na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuimarisha miundombinu ya maji safi na maji taka na azma ya kusogeza huduma ya maji karibu na makazi ya watu. Mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa uliendelea kubaki asilimia 0.4 kama ilivyokuwa mwaka 2017. Shughuli za usambazaji maji na udhibiti wa maji taka sehemu inayouzika zilikua kwa

asilimia 5.6 na sehemu isiyouzika ilikua kwa asilimia 14.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 7.1 na asilimia 4.0 mwaka 2017 mtawalia.

10. Shughuli za kiuchumi za ujenzi kwa mwaka 2018 zilikua kwa asilimia 12.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.1 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kwa ujenzi wa nyumba za biashara, makazi na ofisi za Serikali na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo ya nishati, maji na uchukuzi (barabara, madaraja, viwanja vya ndege, na reli). Aidha, shughuli za ujenzi sehemu inayouzika zilikua kwa asilimia 13.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 14.8 wakati ambapo sehemu isiyouzika zilikua kwa asilimia 11.8 mwaka 2018. Shughuli za kiuchumi za ujenzi zilichangia asilimia 13.0 katika Pato la Taifa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 12.2 mwaka 2017.

11. Shughuli za biashara na matengenezo zilikua kwa asilimia 5.8 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2017. Pamoja na kupungua kwa kasi ukuaji, hii imeendelea kuwa ni miongoni mwa sekta zinazotoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa. Sekta hii ni ya tatu kwa ukubwa ikitanguliwa na kilimo na ujenzi na katika miaka mitatu mfululizo imekuwa ikichangia wastani wa asilimia 9.1 katika Pato la Taifa.

12. Shughuli za malazi na huduma ya chakula zilikua kwa asilimia 5.2 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa idadi na matumizi ya wageni wa ndani na nje waliopata huduma za malazi, chakula na vinywaji nchini. Aidha, sekta hii ilichangia asilimia 1.3 katika Pato la Taifa mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2017.

13. Shughuli za uchukuzi na uhifadhi mizigo zilikua kwa asilimia 11.8 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2017. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa usafirishwaji wa gesi asilia kwa asilimia 25.3 kutoka futi za ujazo milioni 46,471 mwaka 2017 hadi futi za ujazo milioni 58,215 mwaka 2018. Aidha, idadi ya mizigo na abiria iliyosafirishwa kwa njia ya anga, reli na barabara pia iliongezeka kufuatia kuimarika kwa huduma katika maeneo hayo. Mwaka 2018, mchango wa huduma za uchukuzi na uhifadhi mizigo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 6.5 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2017.

14. Shughuli za kiuchumi za huduma za habari na mawasiliano ambazo zinajumuisha huduma za utayarishaji, uchapishaji na usambazaji wa taarifa mbalimbali kupitia vyombo vya habari kama vile radio, magazeti, luninga, tovuti pamoja na huduma za mawasiliano kwa njia ya simu zilikua kwa kiwango cha asilimia 9.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.2 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya huduma za simu za viganjani, muda wa maongezi, utangazaji na huduma ya intaneti nchini. Mchango wa shughuli za huduma za habari na mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.5 mwaka 2018 kama ilivyokuwa mwaka 2017.

15. Mwaka 2018, shughuli za kiuchumi katika huduma za fedha na bima zilianza kuimarika japo bado zilikuwa na kiwango hasi cha ukuaji wa asilimia 0.5 ikilinganisshwa na ukuaji hasi wa asilimia 2.8 mwaka 2017. Hali hii ilitokana na kasi ndogo ya kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi kufuatia tahadhari iliyochukuliwa na benki za biashara kuepuka ongezeko la mikopo chechefu. Mchango wa shughuli za huduma za fedha na bima katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 4.0 mwaka 2017 hadi asilimia 3.7 mwaka 2018.

16. Mwaka 2018, shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba zilikua kwa kiwango cha asilimia 4.4 kama ilivyokuwa mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba kwa ajili ya makazi, biashara na ofisi, hususan maeneo ya mijini. Aidha, ukuaji wa shughuli za upangishaji wa nyumba sehemu inayouzika ulipungua kufikia asilimia 4.3 mwaka 2018 kutoka asilimia 4.5 mwaka 2017. Hata hivyo, hali ilikuwa tofauti kwa upande wa sehemu isiyouzika ambayo ilikuwa na ongezeko la ukuaji uliofikia asilimia 9.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.8 mwaka 2017. Mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma za upangishaji nyumba katika Pato la Taifa ulipungua kidogo kufikia asilimia 2.7 mwaka 2018 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2017.

17. Mwaka 2018, kiwango cha ukuaji wa shughuli za utoaji huduma za afya na ustawi wa jamii kilifikia asilimia 8.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.6 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuboresha sekta hii ikiwa ni pamoja na kujenga na kukarabati zahanati na vituo vya afya; kuhakikisha upatikanaji wa dawa, wataalamu wa afya, na vifaa tiba; na kuongezeka kwa huduma za bima ya afya. Mchango wa

shughuli za utoaji huduma za afya na ustawi wa jamii katika Pato la Taifa uliendelea kuwa wa wastani wa asilimia 1.4 kama ilivyokuwa mwaka 2017.

18. Shughuli za utoaji huduma za elimu zilikua kwa asilimia 6.6 mwaka 2018 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.3 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa wanafunzi waliodahiliwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu. Aidha, utekelezaji wa Sera ya elimumsingi bila ada na ongezeko la mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu umeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la udahili wa wanafunzi. Mchango wa shughuli za huduma za elimu katika Pato la Taifa uliendelea kubakia asilimia 2.4 kama ilivyokuwa mwaka 2017.

19. Mwaka 2018, shughuli za kiuchumi za sanaa na burudani ndizo zilizokuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji wa asilimia 13.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.9 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa hamasa ya mahitaji ya huduma za sanaa na burudani sambamba na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kuboresha na kurasimisha tasnia hii. Hata hivyo, sekta hii bado ina mchango mdogo katika Pato la Taifa wa wastani wa asilimia 0.3.

20. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kaya binafsi katika kuajiri kilikuwa asilimia 3.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2017. Shughuli za kaya binafsi katika kuajiri hujumuisha shughuli zinazofanywa na wafanyakazi walioajiriwa katika kaya binafsi hususan walinzi, wapishi, wahudumu wa ndani, na madereva. Shughuli hizi zinachangia wastani wa asilimia 0.2 katika Pato la Taifa.


21. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiufundi, kitaalam, na kisayansi kilikuwa asilimia 9.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 14.5 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na ongezeko dogo la shughuli za utafiti na maendeleo, na huduma za ushauri wa kitaalam, kisheria, kihasibu na kiufundi. Shughuli hizi za kiufundi, kitaalam na kisayansi zinachangia wastani wa asilimia 0.6 katika Pato la Taifa.

22. Shughuli za utawala na ulinzi zinajumuisha shughuli zinazofanywa na Serikali kwa maana ya sekta ya umma, shughuli za mahakama, uhamiaji, mambo ya nje, ulinzi na usalama, na usimamizi wa programu za Serikali. Shughuli za kiuchumi za utawala na ulinzi zilikua kwa asilimia 3.1 mwaka 2018

ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.4 mwaka 2017. Ongezeko la ukuaji lilitokana na kuimarika kwa huduma za mahakama na uhamiaji pamoja na utekelezaji madhubuti wa programu za Serikali. Mchango wa shughuli hizi katika Pato la Taifa ulipungua na kufikia asilimia 4.0 mwaka 2018 kutoka asilimia 4.2 mwaka 2017.

23. Kiwango cha ukuaji wa shughuli nyingine za kiutawala na huduma kilipungua kutoka asilimia 10.8 mwaka 2017 hadi asilimia 5.6 mwaka 2018. Shughuli hizi zinajumuisha ukodishaji wa vifaa, mashine na mitambo, utafutaji wa ajira, huduma za utalii, ulinzi wa mali na watu, utoaji huduma ofisini, na haki ya kutumia matokeo ya kitaaluma. Aidha, mchango wa shughuli hizi uliendelea kubakia asilimia 2.6 kama ilivyokuwa mwaka 2017.

**Kielelezo Na.1.2: Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa**




## Mwenendo wa Bei

24. Mwaka 2018, mfumuko wa bei uliendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja na kufikia kiwango cha chini kabisa kuwahi kutokea katika kipindi cha miaka 40 iliyopita. Mfumuko wa bei ulipungua kutoka wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2017 hadi wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2018. Kiwango cha chini cha mfumuko wa bei kilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo:

(i) Kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani. Uzalishaji wa chakula nchini uliofikia tani milioni 15.9

ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3 kwa kipindi hicho, hivyo kuwa na utoshelevu wa chakula kwa asilimia 120;

(ii) Utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti; na

(iii) Kuimarika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu nyingine duniani.

25. Uchambuzi wa mwenendo wa bei kwa makundi makuu ya bidhaa na huduma unaonesha kuwa yapo makundi yaliyokuwa na ongezeko dogo la bei na mengine yalikuwa na ongezeko kubwa kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2017. Makundi ambayo mfumuko wa bei uliongezeka mwaka 2018 ni pamoja na nishati, maji na malazi; usafirishaji; elimu; na hoteli na migahawa. Hata hivyo, tofauti na makundi mengine yote, kundi la mawasiliano liliendelea kuwa na mwenendo wa kupungua kwa kasi ya upandaji bei kwa mwaka wa tatu mfululizo ambapo mwaka 2018 ulipungua kwa asilimia 1.6 ikilinganishwa na asilimia 0.9 mwaka 2017. Hii ilitokana na kubadilika kwa mwenendo wa matumizi ya wateja wa huduma hii sambamba na jitihada za watoa huduma kupunguza bei za huduma za mawasiliano ama kutoa motisha kwa wateja ikiwemo vifurushi vya gharama nafuu ili kuvutia wateja na kukabiliana na ushindani. Mwenendo wa bei za bidhaa na huduma mbalimbali ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.2**.

**Jedwali Na. 1.2: Fahirisi na Mfumuko wa Bei ya Bidhaa na Huduma Zitumiwazo na Wakazi wa Mijini - Tanzania Bara (2001=100)**

| Mwaka | | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2013 | FAHIRISI YA BEI | 82.9 | 90.4 | 91.7 | 89.7 | 94.9 | 91.6 | 95.8 | 98.8 | 96.1 | 91.9 | 92.3 | 90.1 | 87.3 |
| 2014 | | 89.1 | 95.8 | 94.5 | 99.3 | 96.7 | 95.0 | 99.4 | 99.6 | 96.8 | 96.8 | 94.7 | 95.6 | 92.7 |
| 2015 | | 96.8 | 99.2 | 98.4 | 100.9 | 98.2 | 97.9 | 98.8 | 99.8 | 98.4 | 99.6 | 99.1 | 98.4 | 97.9 |
| 2026 | | 103.8 | 103.2 | 102.2 | 107.3 | 101.7 | 103.4 | 99.5 | 99.1 | 101.1 | 102.3 | 103.1 | 101.7 | 102.9 |
| 2017 | | 113.3 | 106.6 | 105.8 | 115.4 | 104.7 | 106.0 | 99.9 | 98.2 | 102.3 | 103.2 | 104.4 | 105.0 | 108.4 |
| 2018 | | 116.6 | 108.4 | 108.9 | 129.2 | 107.4 | 107.4 | 102.5 | 96.6 | 102.8 | 105.8 | 105.7 | 106.7 | 112.2 |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 2014 | MWENENDO WA BEI | 7.4% | 5.9% | 3.0% | 10.7% | 1.9% | 3.6% | 3.8% | 0.7% | 0.7% | 5.3% | 2.7% | 6.1% | 6.1% |
| 2015 | | 8.7% | 3.6% | 4.1% | 1.6% | 1.6% | 3.0% | -0.6% | 0.3% | 1.6% | 2.9% | 4.6% | 2.9% | 5.6% |
| 2016 | | 7.2% | 4.0% | 3.9% | 6.3% | 3.6% | 5.6% | 0.6% | -0.7% | 2.7% | 2.7% | 4.1% | 3.4% | 5.2% |
| 2017 | | 9.1% | 3.3% | 3.5% | 7.6% | 2.9% | 2.6% | 0.5% | -0.9% | 1.3% | 0.9% | 1.2% | 3.2% | 5.3% |
| 2018 | | 3.0% | 1.6% | 2.9% | 12.0% | 2.5% | 1.3% | 2.5% | -1.6% | 0.5% | 2.4% | 1.3% | 1.6% | 3.5% |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

26. Uchambuzi wa mwenendo wa bei kwa makundi mengine maalum unaonesha kuwa wastani wa ongezeko la bei ya chakula kinachojumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na hotelini ulikuwa asilimia 3.7 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.6 mwaka 2017. Hii ilitokana na kuimarika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika soko la ndani na nchi jirani kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula. Aidha, wastani wa kasi ya upandaji bei kwa bidhaa zisizokuwa za chakula uliongezeka kufikia asilimia 4.3 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2017. Mwenendo wa bei ya nishati nao uliongezeka kufikia asilimia 17.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 10.5 mwaka 2017. Mfumuko wa bei ambao haujumuishi chakula na nishati (core inflation) ulikuwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 2.0 mwaka 2017 kufuatia utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti. Kundi hili limechangia asilimia 54.3 katika kapu la walaji na ndilo ambalo linaweza kudhibitiwa kwa kutumia nyenzo za sera za fedha.

27. Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma kwa makundi ya watu wa tabaka la kipato cha chini na juu iliongezeka mwaka 2018 kufikia asilimia 2.0 na asilimia 4.7 ikilinganishwa na asilimia 1.9 na asilimia 4.2 mwaka 2017 kwa mtiririko huo. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wastani wa bei za bidhaa na huduma zinazotumiwa kwa wingi na makundi hayo zikiwemo nishati, maji na malazi; na mavazi ya nguo na viatu. Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma kwa kundi la watu wa tabaka la kipato cha kati ilipungua na kufikia asilimia 1.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2017. Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma nyingine ilikuwa na mwenendo unaoendana na mahitaji ya kundi husika kimapato kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.3.** Aidha, **Majedwali Na. 8 – 16** yanaonesha mwenendo wa fahirisi ya bei kwa makundi na sehemu mbalimbali.

## Jedwali Na. 1.3: Mfumuko wa Bei za Bidhaa na Huduma Zitumiwazo Na Walaji Kulingana na Tabaka la Kipato

| Mwaka | Tabaka la Kipato | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2014 | KIPATO CHA JUU | 6.7% | 8.1% | 2.1% | 7.5% | 1.3% | 2.4% | 5.3% | 0.0% | 3.8% | 15.9% | 4.5% | 3.2% | 6.0% |
| 2015 | | 8.8% | 6.5% | 0.9% | 7.1% | 0.7% | 1.2% | 3.6% | 2.9% | 0.8% | 2.1% | 8.4% | -0.7% | 6.5% |
| 2026 | | 8.6% | 3.3% | 1.8% | 8.8% | 3.3% | 14.1% | -2.3% | 2.4% | 1.1% | -1.6% | 5.1% | 3.5% | 4.8% |
| 2017 | | 9.2% | 2.1% | 1.8% | 1.3% | 5.4% | 2.5% | 4.9% | 0.6% | -1.2% | -0.1% | 0.8% | 3.2% | 4.2% |
| 2018 | | 7.0% | 0.2% | 2.5% | 5.6% | 1.1% | 0.1% | 6.4% | 0.4% | 0.8% | 7.8% | 1.0% | 0.6% | 4.7% |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 2014 | KIPATO CHA KATI | 3.9% | 8.1% | 2.1% | 13.9% | 5.1% | 5.2% | 12.5% | 0.7% | 3.7% | 11.0% | 7.1% | 6.2% | 6.2% |
| 2015 | | 2.9% | 7.4% | 2.1% | 14.6% | 4.5% | 3.1% | 4.4% | 0.5% | 3.9% | 5.5% | 11.4% | 5.0% | 5.6% |
| 2016 | | 3.3% | 2.5% | 1.1% | 12.4% | 1.4% | 13.4% | 0.3% | 0.6% | 2.9% | -2.3% | 8.3% | 5.4% | 4.5% |
| 2017 | | 4.6% | 2.3% | 1.4% | 2.2% | 3.3% | 2.4% | 0.7% | 0.5% | 0.5% | -0.1% | 1.2% | 1.1% | 2.6% |
| 2018 | | 7.0% | -0.5% | 2.1% | 4.1% | 1.3% | 0.3% | -18.8% | -0.1% | 0.1% | 8.6% | -0.5% | 1.5% | 1.9% |
| | | | | | | | | | | | | | | |
| 2014 | KIPATO CHA CHINI | 7.3% | 8.4% | 9.2% | 7.0% | 4.0% | 0.7% | 15.9% | 0.0% | 4.3% | 0.0% | 7.8% | 11.5% | 7.7% |
| 2015 | | 5.9% | 14.2% | 9.0% | 3.4% | 6.0% | 5.6% | -0.2% | 0.0% | 5.6% | -0.3% | 7.1% | 2.7% | 5.4% |
| 2026 | | 3.6% | 8.2% | -2.4% | 7.1% | 2.7% | 12.1% | 0.9% | 0.6% | 1.2% | -5.2% | 6.8% | 6.0% | 4.3% |
| 2017 | | 3.4% | 2.9% | 1.3% | 0.9% | 3.1% | 1.6% | -0.1% | 0.4% | 1.7% | 3.9% | 0.5% | 0.9% | 1.9% |
| 2018 | | 4.5% | 0.0% | 3.1% | 5.7% | 1.9% | 0.1% | -12.5% | -0.1% | 1.1% | 5.5% | 0.1% | 1.6% | 2.0% |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### Ukuzaji Rasilimali

28. Ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika kwa mwaka 2018 ulifikia shilingi bilioni 50,383.14, ikiwa ni ongezeko la asilimia 24.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 40,427.43 mwaka 2017. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka mpya wa kizio wa 2015 uliongezeka kwa asilimia 18.3 kufikia shilingi bilioni 45,360.12 mwaka 2018 kutoka shilingi bilioni 38,338.12 mwaka 2017. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika uliongezeka kufikia asilimia 38.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 34.0 mwaka 2017.

29. Ukuzaji rasilimali za kudumu unaojumuisha majengo; vifaa vya usafiri; mitambo na vifaa; mitambo na vifaa vingine; rasilimali za mazao ya mifugo; na haki za umiliki, utafiti na maendeleo na huduma za kitaalam ulifikia shilingi bilioni 46,636.42 mwaka 2018 kutoka shilingi bilioni 40,376.86 mwaka 2017 kwa bei za mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za miaka husika nao uliongezeka kwa asilimia 19.4 kutoka shilingi bilioni 42,141.92 mwaka 2017 hadi shilingi bilioni 50,316.24 mwaka 2018. Thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka 2015 ilipungua kwa shilingi bilioni 1,276.3 mwaka 2018 ikilinganishwa na punguzo la shilingi bilioni 2,038.74 mwaka 2017. Hata hivyo, thamani ya limbikizo la rasilimali

kwa bei za miaka husika iliongezeka kwa shilingi bilioni 66.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na punguzo la shilingi bilioni 1,714.49 mwaka 2017.

30. Ukuzaji rasilimali katika shughuli za ujenzi wa majengo kwa bei za mwaka 2015 uliongezeka kwa asilimia 16.3 kufikia shilingi bilioni 38,191.16 mwaka 2018 kutoka shilingi bilioni 32,836.68 mwaka 2017. Vile vile, ukuzaji rasilimali katika shughuli za ujenzi wa majengo kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 22.0 kufikia shilingi bilioni 41,330.86 mwaka 2018. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ujenzi wa nyumba za makazi na za biashara. Thamani ya uagizaji wa vifaa vya usafiri kwa bei za mwaka 2015 iliongezeka kwa asilimia 64.0 kufikia shilingi bilioni 1,924.37 wakati ambapo kwa bei za miaka husika iliongezeka kwa asilimia 29.6 kufikia shilingi bilioni 1,832.64 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, thamani ya ununuzi wa mitambo na vifaa vingine kwa ujumla wake kwa bei za miaka husika ilipungua kwa asilimia 2.4 kufikia shilingi bilioni 5,319.82 na kwa bei za mwaka 2015 thamani iliongezeka kwa asilimia 0.8 kufikia shilingi bilioni 4,845.93 mwaka 2018.

31. Ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma inayojumuisha Serikali kuu, mashirika na taasisi za Serikali ulifikia shilingi bilioni 15,265.61 mwaka 2018 kwa bei za miaka husika ikilinganishwa na shilingi bilioni 13,021.85 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 17.2. Aidha, ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi ulifikia shilingi bilioni 35,050.63 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 29,120.07 mwaka 2017 kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 20.4. Sekta ya umma ilichangia asilimia 30.3 katika rasilimali za kudumu wakati ambapo sekta binafsi ilichangia asilimia 69.7 mwaka 2018.

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO**
**(KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Jedwali NA.1** Shs.Milioni

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **16,546,181** | **19,551,225** | **21,313,803** | **25,234,560** | **29,739,111** | **34,154,594** | **36,539,300** |
| | Kilimo cha Mazao | 8,797,362 | 10,500,528 | 11,562,090 | 13,279,392 | 16,474,729 | 19,703,004 | 20,969,477 |
| | Mifugo | 4,633,266 | 5,579,312 | 5,585,211 | 7,158,457 | 8,205,007 | 8,857,939 | 9,850,934 |
| | Misitu | 1,736,757 | 2,069,113 | 2,477,897 | 2,920,425 | 3,094,767 | 3,310,076 | 3,459,581 |
| | Uvuvi | 1,353,297 | 1,375,790 | 1,658,605 | 1,843,401 | 1,929,747 | 2,245,558 | 2,218,731 |
| | Agriculture support services | 25,499 | 26,483 | 30,000 | 32,886 | 34,861 | 38,017 | 40,577 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **15,828,627** | **18,570,322** | **20,767,734** | **23,103,647** | **26,937,139** | **29,735,584** | **34,732,007** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 3,071,558 | 3,125,480 | 3,097,933 | 4,055,619 | 5,299,362 | 5,206,217 | 6,573,059 |
| C | Viwanda | 5,881,780 | 6,648,876 | 7,533,519 | 7,411,672 | 8,467,126 | 9,102,282 | 10,418,295 |
| D | Umeme | 522,829 | 550,300 | 818,693 | 798,801 | 472,868 | 413,351 | 348,527 |
| E | Maji safi na Maji taka | 279,326 | 324,028 | 371,581 | 390,758 | 433,132 | 519,909 | 566,562 |
| F | Ujenzi | 6,073,134 | 7,921,637 | 8,946,007 | 10,446,797 | 12,264,650 | 14,493,826 | 16,825,564 |
| | **Huduma** | **25,308,528** | **29,384,671** | **34,111,643** | **38,146,529** | **42,747,407** | **45,066,596** | **47,923,308** |
| G | Biashara na Matengenezo | 6,448,378 | 7,063,673 | 8,045,702 | 8,747,862 | 9,861,678 | 10,843,499 | 11,792,072 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 3,747,784 | 5,246,333 | 6,167,366 | 6,929,895 | 7,549,484 | 7,897,993 | 8,381,276 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,253,970 | 1,317,191 | 1,330,371 | 1,421,916 | 1,523,035 | 1,602,543 | 1,653,792 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,282,255 | 1,433,179 | 1,598,597 | 1,681,098 | 1,739,556 | 1,829,360 | 1,948,116 |
| K | Fedha na Bima | 2,561,997 | 2,541,198 | 3,614,991 | 4,189,021 | 5,268,866 | 4,789,632 | 4,823,650 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,308,221 | 2,551,029 | 2,721,061 | 2,949,598 | 3,162,290 | 3,334,171 | 3,553,630 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 282,744 | 353,038 | 433,939 | 518,123 | 617,914 | 726,707 | 817,442 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 1,243,365 | 1,522,884 | 1,914,456 | 2,183,917 | 2,661,978 | 3,027,384 | 3,306,554 |
| O | Utawala na Ulinzi | 2,882,065 | 3,615,292 | 3,973,787 | 4,548,604 | 4,846,491 | 4,986,287 | 5,124,667 |
| P | Elimu | 1,498,868 | 1,728,376 | 2,027,225 | 2,413,306 | 2,673,289 | 2,864,290 | 3,081,718 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,011,197 | 1,113,563 | 1,233,077 | 1,419,090 | 1,540,484 | 1,681,353 | 1,812,292 |
| R | Sanaa na Burudani | 174,358 | 194,938 | 223,468 | 248,510 | 285,626 | 322,353 | 374,924 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 474,340 | 555,957 | 661,939 | 717,898 | 831,216 | 959,152 | 1,037,612 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 138,986 | 148,022 | 165,666 | 177,691 | 185,501 | 201,872 | 215,564 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **57,683,336** | **67,506,219** | **76,193,180** | **86,484,736** | **99,423,658** | **108,956,774** | **119,194,615** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 4,635,323 | 5,470,981 | 6,410,208 | 7,864,579 | 8,938,667 | 9,787,724 | 10,169,738 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **62,318,659** | **72,977,200** | **82,603,388** | **94,349,316** | **108,362,324** | **118,744,498** | **129,364,353** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA (GDP) KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA BEI ZA SOKO- SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA**
**(KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Jedwali Na. 1A** Shs.Milioni

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A:SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **55,171,372** | **64,901,865** | **73,572,807** | **84,275,963** | **97,295,383** | **106,025,246** | **114,392,270** |
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **9,873,083** | **12,100,550** | **13,008,318** | **16,020,386** | **19,628,661** | **22,561,096** | **22,832,457** |
| | Kilimo cha Mazao | 4,157,753 | 5,416,553 | 5,828,361 | 7,176,326 | 9,729,649 | 11,822,710 | 11,332,130 |
| | Mifugo | 3,177,749 | 3,944,325 | 3,866,240 | 5,160,608 | 6,322,457 | 6,877,739 | 7,101,644 |
| | Misitu | 1,194,105 | 1,388,640 | 1,685,505 | 1,882,033 | 1,706,926 | 1,680,599 | 2,229,486 |
| | Uvuvi | 1,317,977 | 1,324,549 | 1,598,212 | 1,768,534 | 1,834,769 | 2,142,032 | 2,128,621 |
| | Agriculture support services | 25,499 | 26,483 | 30,000 | 32,886 | 34,861 | 38,017 | 40,577 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **15,486,501** | **18,096,470** | **20,188,806** | **22,361,768** | **26,111,436** | **28,749,158** | **33,608,087** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 3,071,558 | 3,125,480 | 3,097,933 | 4,055,619 | 5,299,362 | 5,206,217 | 6,573,059 |
| C | Viwanda | 5,881,780 | 6,648,876 | 7,533,519 | 7,411,672 | 8,467,126 | 9,102,282 | 10,418,295 |
| D | Umeme | 522,829 | 550,300 | 818,693 | 798,801 | 472,868 | 413,351 | 348,527 |
| E | Maji safi na Maji taka | 194,157 | 222,978 | 261,504 | 272,990 | 301,821 | 372,032 | 395,810 |
| F | Ujenzi | 5,816,176 | 7,548,836 | 8,477,157 | 9,822,685 | 11,570,259 | 13,655,276 | 15,872,398 |
| | **Huduma** | **25,176,466** | **29,233,864** | **33,965,476** | **38,029,229** | **42,616,618** | **44,927,268** | **47,781,987** |
| G | Biashara na Matengenezo | 6,448,378 | 7,063,673 | 8,045,702 | 8,747,862 | 9,861,678 | 10,843,499 | 11,792,072 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 3,747,784 | 5,246,333 | 6,167,366 | 6,929,895 | 7,549,484 | 7,897,993 | 8,381,276 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,253,970 | 1,317,191 | 1,330,371 | 1,421,916 | 1,523,035 | 1,602,543 | 1,653,792 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,282,255 | 1,433,179 | 1,598,597 | 1,681,098 | 1,739,556 | 1,829,360 | 1,948,116 |
| K | Fedha na Bima | 2,561,997 | 2,541,198 | 3,614,991 | 4,189,021 | 5,268,866 | 4,789,632 | 4,823,650 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,176,159 | 2,400,221 | 2,574,893 | 2,832,298 | 3,031,501 | 3,194,842 | 3,412,309 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 282,744 | 353,038 | 433,939 | 518,123 | 617,914 | 726,707 | 817,442 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 1,243,365 | 1,522,884 | 1,914,456 | 2,183,917 | 2,661,978 | 3,027,384 | 3,306,554 |
| O | Utawala na Ulinzi | 2,882,065 | 3,615,292 | 3,973,787 | 4,548,604 | 4,846,491 | 4,986,287 | 5,124,667 |
| P | Elimu | 1,498,868 | 1,728,376 | 2,027,225 | 2,413,306 | 2,673,289 | 2,864,290 | 3,081,718 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,011,197 | 1,113,563 | 1,233,077 | 1,419,090 | 1,540,484 | 1,681,353 | 1,812,292 |
| R | Sanaa na Burudani | 174,358 | 194,938 | 223,468 | 248,510 | 285,626 | 322,353 | 374,924 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 474,340 | 555,957 | 661,939 | 717,898 | 831,216 | 959,152 | 1,037,612 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 138,986 | 148,022 | 165,666 | 177,691 | 185,501 | 201,872 | 215,564 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **50,536,049** | **59,430,884** | **67,162,600** | **76,411,383** | **88,356,716** | **96,237,522** | **104,222,532** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 4,635,323 | 5,470,981 | 6,410,208 | 7,864,579 | 8,938,667 | 9,787,724 | 10,169,738 |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **7,147,287** | **8,075,334** | **9,030,580** | **10,073,353** | **11,066,941** | **12,719,252** | **14,972,083** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | **6,673,099** | **7,450,675** | **8,305,485** | **9,214,174** | **10,110,449** | **11,593,497** | **13,706,843** |
| | Mazao | 4,639,609 | 5,083,974 | 5,733,729 | 6,103,066 | 6,745,080 | 7,880,294 | 9,637,347 |
| | Mifugo | 1,455,518 | 1,634,987 | 1,718,971 | 1,997,848 | 1,882,549 | 1,980,200 | 2,749,290 |
| | Misitu | 542,652 | 680,473 | 792,392 | 1,038,392 | 1,387,841 | 1,629,477 | 1,230,096 |
| | Uvuvi | 35,320 | 51,240 | 60,393 | 74,867 | 94,978 | 103,526 | 90,110 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **342,126** | **473,852** | **578,928** | **741,880** | **825,703** | **986,427** | **1,123,919** |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 85,168 | 101,050 | 110,077 | 117,768 | 131,311 | 147,877 | 170,752 |
| F | Ujenzi | 256,958 | 372,802 | 468,851 | 624,112 | 694,392 | 838,550 | 953,167 |
| | **Huduma** | **132,062** | **150,808** | **146,168** | **117,300** | **130,789** | **139,328** | **141,321** |
| L | Upangishaji Majengo | 132,062 | 150,808 | 146,168 | 117,300 | 130,789 | 139,328 | 141,321 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **62,318,659** | **72,977,200** | **82,603,388** | **94,349,316** | **108,362,324** | **118,744,498** | **129,364,353** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**MCHANGO WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO**
**(KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Jedwali Na.2** Asilimia

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | ***26.55*** | ***26.79*** | ***25.80*** | ***26.75*** | ***27.44*** | ***28.76*** | ***28.25*** |
| | Kilimo cha Mazao | 14.12 | 14.39 | 14.00 | 14.07 | 15.20 | 16.59 | 16.21 |
| | Mifugo | 7.43 | 7.65 | 6.76 | 7.59 | 7.57 | 7.46 | 7.61 |
| | Misitu | 2.79 | 2.84 | 3.00 | 3.10 | 2.86 | 2.79 | 2.67 |
| | Uvuvi | 2.17 | 1.89 | 2.01 | 1.95 | 1.78 | 1.89 | 1.72 |
| | Agriculture support services | 0.04 | 0.04 | 0.04 | 0.03 | 0.03 | 0.03 | 0.03 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4.93 | 4.28 | 3.75 | 4.30 | 4.89 | 4.38 | 5.08 |
| C | Viwanda | 9.44 | 9.11 | 9.12 | 7.86 | 7.81 | 7.67 | 8.05 |
| D | Umeme | 0.84 | 0.75 | 0.99 | 0.85 | 0.44 | 0.35 | 0.27 |
| E | Maji safi na Maji taka | 0.45 | 0.44 | 0.45 | 0.41 | 0.40 | 0.44 | 0.44 |
| F | Ujenzi | 9.75 | 10.85 | 10.83 | 11.07 | 11.32 | 12.21 | 13.01 |
| G | Biashara na Matengenezo | 10.35 | 9.68 | 9.74 | 9.27 | 9.10 | 9.13 | 9.12 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 6.01 | 7.19 | 7.47 | 7.34 | 6.97 | 6.65 | 6.48 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 2.01 | 1.80 | 1.61 | 1.51 | 1.41 | 1.35 | 1.28 |
| J | Habari na Mawasiliano | 2.06 | 1.96 | 1.94 | 1.78 | 1.61 | 1.54 | 1.51 |
| K | Fedha na Bima | 4.11 | 3.48 | 4.38 | 4.44 | 4.86 | 4.03 | 3.73 |
| L | Upangishaji Majengo | 3.70 | 3.50 | 3.29 | 3.13 | 2.92 | 2.81 | 2.75 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.45 | 0.48 | 0.53 | 0.55 | 0.57 | 0.61 | 0.63 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.00 | 2.09 | 2.32 | 2.31 | 2.46 | 2.55 | 2.56 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4.62 | 4.95 | 4.81 | 4.82 | 4.47 | 4.20 | 3.96 |
| P | Elimu | 2.41 | 2.37 | 2.45 | 2.56 | 2.47 | 2.41 | 2.38 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1.62 | 1.53 | 1.49 | 1.50 | 1.42 | 1.42 | 1.40 |
| R | Sanaa na Burudani | 0.28 | 0.27 | 0.27 | 0.26 | 0.26 | 0.27 | 0.29 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 0.76 | 0.76 | 0.80 | 0.76 | 0.77 | 0.81 | 0.80 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.22 | 0.20 | 0.20 | 0.19 | 0.17 | 0.17 | 0.17 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **92.6** | **92.5** | **92.2** | **91.7** | **91.8** | **91.8** | **92.1** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 7.4 | 7.5 | 7.8 | 8.3 | 8.2 | 8.2 | 7.9 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**MCHANGO WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI KWA PATO LA TAIFA KWA BEI ZA SOKO- SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA**
**(KWA BEI ZA MIAKA INAYOHUSIKA)**

**Jedwali Na. 2A** Asilimia

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A:SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | | | | | | | |
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **15.8** | **16.6** | **15.7** | **17.0** | **18.1** | **19.0** | **17.6** |
| | Kilimo cha Mazao | 6.7 | 7.4 | 7.1 | 7.6 | 9.0 | 10.0 | 8.8 |
| | Mifugo | 5.1 | 5.4 | 4.7 | 5.5 | 5.8 | 5.8 | 5.5 |
| | Misitu | 1.9 | 1.9 | 2.0 | 2.0 | 1.6 | 1.4 | 1.7 |
| | Uvuvi | 2.1 | 1.8 | 1.9 | 1.9 | 1.7 | 1.8 | 1.6 |
| | Agriculture support services | 0.04 | 0.04 | 0.04 | 0.03 | 0.03 | 0.03 | 0.03 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4.9 | 4.3 | 3.8 | 4.3 | 4.9 | 4.4 | 5.1 |
| C | Viwanda | 9.4 | 9.1 | 9.1 | 7.9 | 7.8 | 7.7 | 8.1 |
| D | Umeme | 0.8 | 0.8 | 1.0 | 0.8 | 0.4 | 0.3 | 0.3 |
| E | Maji safi na Maji taka | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| F | Ujenzi | 9.3 | 10.3 | 10.3 | 10.4 | 10.7 | 11.5 | 12.3 |
| G | Biashara na Matengenezo | 10.3 | 9.7 | 9.7 | 9.3 | 9.1 | 9.1 | 9.1 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 6.0 | 7.2 | 7.5 | 7.3 | 7.0 | 6.7 | 6.5 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 2.0 | 1.8 | 1.6 | 1.5 | 1.4 | 1.3 | 1.3 |
| J | Habari na Mawasiliano | 2.1 | 2.0 | 1.9 | 1.8 | 1.6 | 1.5 | 1.5 |
| K | Fedha na Bima | 4.1 | 3.5 | 4.4 | 4.4 | 4.9 | 4.0 | 3.7 |
| L | Upangishaji Majengo | 3.5 | 3.3 | 3.1 | 3.0 | 2.8 | 2.7 | 2.6 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.6 | 0.6 | 0.6 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 2.0 | 2.1 | 2.3 | 2.3 | 2.5 | 2.5 | 2.6 |
| O | Utawala na Ulinzi | 4.6 | 5.0 | 4.8 | 4.8 | 4.5 | 4.2 | 4.0 |
| P | Elimu | 2.4 | 2.4 | 2.5 | 2.6 | 2.5 | 2.4 | 2.4 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1.6 | 1.5 | 1.5 | 1.5 | 1.4 | 1.4 | 1.4 |
| R | Sanaa na Burudani | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 | 0.3 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 | 0.8 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.2 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **81.1** | **81.4** | **81.3** | **81.0** | **81.5** | **81.0** | **80.6** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 7.4 | 7.5 | 7.8 | 8.3 | 8.2 | 8.2 | 7.9 |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **11.5** | **11.1** | **10.9** | **10.7** | **10.2** | **10.7** | **11.6** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | 10.7 | 10.2 | 10.1 | 9.8 | 9.3 | 9.8 | 10.6 |
| | Mazao | 7.4 | 7.0 | 6.9 | 6.5 | 6.2 | 6.6 | 7.4 |
| | Mifugo | 2.3 | 2.2 | 2.1 | 2.1 | 1.7 | 1.7 | 2.1 |
| | Misitu | 0.9 | 0.9 | 1.0 | 1.1 | 1.3 | 1.4 | 1.0 |
| | Uvuvi | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| F | Ujenzi | 0.4 | 0.5 | 0.6 | 0.7 | 0.6 | 0.7 | 0.7 |
| L | Upangishaji Majengo | 0.2 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 0.1 | 0.1 | 0.1 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

| ıtumizi | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **fa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **62,318,659** | **72,977,200** | **82,603,388** | **94,349,317** | **108,362,324** | **118,744,498** | **129,364,353** |
| **'a Mwisho(Final consumption)** | **48,841,250** | **56,171,499** | **62,297,764** | **69,619,572** | **74,761,715** | **81,577,249** | **88,207,317** |
| | 6,497,975 | 7,330,733 | 8,151,130 | 9,366,334 | 9,824,677 | 10,097,404 | 10,467,841 |
| | 42,196,070 | 48,675,221 | 53,954,463 | 60,047,089 | 64,699,505 | 71,211,545 | 77,442,970 |
| nafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 147,205 | 165,545 | 192,171 | 206,149 | 237,532 | 268,299 | 296,506 |
| **silimali** | **21,714,587** | **27,344,522** | **31,103,452** | **30,907,602** | **34,865,346** | **40,427,427** | **50,383,140** |
| za kudumu | 20,543,461 | 24,780,897 | 27,399,832 | 30,070,195 | 35,492,828 | 42,141,921 | 50,316,239 |
| › la limbikizo la Vito vya Thamani *(changes in Valuables)* | 806,021 | 766,581 | 756,477 | 903,043 | 1,105,406 | 1,006,179 | 1,215,104 |
| › la limbikizo (changes in Inventories) | 365,106 | 1,797,044 | 2,947,143 | -65,636 | -1,732,887 | -2,720,674 | -1,148,203 |
| | **13,941,974** | **13,874,574** | **14,925,779** | **16,138,367** | **17,717,213** | **17,993,324** | **17,799,492** |
| b | 9,256,365 | 8,403,257 | 8,441,487 | 8,708,690 | 9,177,377 | 8,924,522 | 8,265,768 |
| | 4,685,609 | 5,471,317 | 6,484,292 | 7,429,677 | 8,539,835 | 9,068,803 | 9,533,723 |
| | **19,940,424** | **21,614,687** | **22,539,832** | **22,316,226** | **20,665,232** | **20,320,749** | **22,522,249** |
| b | 16,227,332 | 17,628,319 | 18,054,008 | 16,955,419 | 15,602,694 | 15,816,338 | 17,625,266 |
| | 3,713,092 | 3,986,369 | 4,485,823 | 5,360,807 | 5,062,538 | 4,504,411 | 4,896,983 |
| Mapungufu | -2,238,729 | -2,798,709 | -3,183,776 | 0 | 1,683,283 | -932,752 | -4,503,347 |

isi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**
**(KWA BEI ZA MWAKA 2015)**

**Jedwali NA.3** Shs.Milioni

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **21,807,030** | **22,408,192** | **23,952,077** | **25,234,560** | **26,436,338** | **28,008,976** | **29,482,834** |
| | Kilimo cha Mazao | 10,806,678 | 11,283,264 | 12,344,014 | 13,279,392 | 13,996,348 | 14,895,622 | 15,638,612 |
| | Mifugo | 6,204,980 | 6,503,187 | 6,820,846 | 7,158,457 | 7,506,593 | 7,876,592 | 8,266,049 |
| | Misitu | 2,578,779 | 2,695,825 | 2,825,341 | 2,920,425 | 3,034,569 | 3,180,379 | 3,334,791 |
| | Uvuvi | 2,187,669 | 1,896,254 | 1,930,394 | 1,843,401 | 1,864,627 | 2,020,292 | 2,205,459 |
| | Agriculture support services | 28,925 | 29,661 | 31,482 | 32,886 | 34,201 | 36,091 | 37,923 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **17,987,423** | **19,872,086** | **21,057,206** | **23,103,647** | **25,817,955** | **28,565,774** | **31,235,045** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 3,314,742 | 3,464,721 | 3,687,273 | 4,055,619 | 4,356,709 | 4,588,624 | 4,659,195 |
| C | Viwanda | 6,066,989 | 6,292,514 | 6,919,794 | 7,411,672 | 8,213,364 | 8,889,818 | 9,623,501 |
| D | Umeme | 669,069 | 723,608 | 815,297 | 798,801 | 869,262 | 877,667 | 928,174 |
| E | Maji safi na Maji taka | 358,361 | 367,890 | 381,760 | 390,758 | 417,899 | 444,660 | 477,510 |
| F | Ujenzi | 7,578,263 | 9,023,353 | 9,253,082 | 10,446,797 | 11,960,720 | 13,765,005 | 15,546,664 |
| | **Huduma** | **31,223,623** | **32,808,710** | **35,863,739** | **38,146,529** | **40,549,564** | **42,689,011** | **45,358,029** |
| G | Biashara na Matengenezo | 7,371,411 | 7,682,286 | 8,444,243 | 8,747,862 | 9,260,703 | 9,821,248 | 10,395,783 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 5,710,466 | 6,050,976 | 6,577,706 | 6,929,895 | 7,324,856 | 7,815,845 | 8,736,561 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,343,924 | 1,356,204 | 1,397,782 | 1,421,916 | 1,480,052 | 1,525,619 | 1,604,391 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,266,747 | 1,414,116 | 1,560,064 | 1,681,098 | 1,718,548 | 1,824,471 | 1,989,829 |
| K | Fedha na Bima | 3,444,161 | 3,405,940 | 3,764,113 | 4,189,021 | 4,235,515 | 4,115,393 | 4,094,972 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,606,439 | 2,714,775 | 2,828,970 | 2,949,598 | 3,077,086 | 3,211,895 | 3,354,518 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 322,260 | 385,090 | 447,921 | 518,123 | 606,207 | 694,291 | 763,332 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 1,417,467 | 1,660,994 | 1,976,260 | 2,183,917 | 2,611,498 | 2,892,463 | 3,054,288 |
| O | Utawala na Ulinzi | 3,623,123 | 3,974,206 | 4,242,164 | 4,548,604 | 4,793,820 | 4,907,113 | 5,058,292 |
| P | Elimu | 1,922,643 | 1,927,633 | 2,186,260 | 2,413,306 | 2,665,336 | 2,859,171 | 3,046,789 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,284,594 | 1,245,030 | 1,349,941 | 1,419,090 | 1,497,896 | 1,611,999 | 1,742,444 |
| R | Sanaa na Burudani | 198,470 | 212,502 | 230,652 | 248,510 | 280,131 | 307,907 | 350,027 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 550,177 | 612,079 | 685,475 | 717,898 | 814,529 | 912,404 | 971,690 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 161,741 | 166,880 | 172,190 | 177,691 | 183,387 | 189,193 | 195,113 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **71,018,076** | **75,088,988** | **80,873,021** | **86,484,736** | **92,803,857** | **99,263,761** | **106,075,908** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 6,961,771 | 8,179,129 | 8,001,090 | 7,864,579 | 8,024,535 | 8,393,644 | 9,064,286 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **77,979,847** | **83,268,117** | **88,874,111** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,140,194** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO - SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA**
**(KWA BEI ZA MWAKA 2015)**

**Jedwali Na.3A** Shs. Milioni

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2,012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | **67,184,948** | **71,115,822** | **76,759,835** | **82,398,098** | **88,440,032** | **94,635,626** | **101,148,176** |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **74,146,719** | **79,294,951** | **84,760,925** | **90,262,677** | **96,464,568** | **103,029,270** | **110,217,961** |
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **18,560,733** | **19,105,967** | **20,538,538** | **21,953,873** | **22,914,869** | **24,357,439** | **25,652,991** |
| | Kilimo cha Mazao | 8,857,547 | 9,308,881 | 10,267,229 | 11,330,959 | 11,852,633 | 12,666,159 | 13,344,020 |
| | Mifugo | 5,184,319 | 5,465,006 | 5,788,062 | 6,131,537 | 6,458,453 | 6,797,008 | 7,080,239 |
| | Misitu | 2,316,438 | 2,421,026 | 2,536,530 | 2,629,474 | 2,720,412 | 2,853,656 | 3,002,559 |
| | Uvuvi | 2,173,504 | 1,881,393 | 1,915,235 | 1,829,018 | 1,849,169 | 2,004,525 | 2,188,251 |
| | Huduma za shughuli za kilimo | 28,925 | 29,661 | 31,482 | 32,886 | 34,201 | 36,091 | 37,923 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **17,491,788** | **19,292,729** | **20,449,621** | **22,391,185** | **25,070,677** | **27,685,960** | **30,248,978** |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 3,314,742 | 3,464,721 | 3,687,273 | 4,055,619 | 4,356,709 | 4,588,624 | 4,659,195 |
| C | Viwanda | 6,066,989 | 6,292,514 | 6,919,794 | 7,411,672 | 8,213,364 | 8,889,818 | 9,623,501 |
| D | Umeme | 669,069 | 723,608 | 815,297 | 798,801 | 869,262 | 877,667 | 928,174 |
| E | Maji safi na Maji taka | 278,139 | 285,538 | 296,333 | 302,407 | 326,898 | 350,019 | 369,545 |
| F | Ujenzi | 7,162,850 | 8,526,348 | 8,730,924 | 9,822,685 | 11,304,444 | 12,979,833 | 14,668,563 |
| | **Huduma** | **31,132,427** | **32,717,125** | **35,771,676** | **38,053,040** | **40,454,486** | **42,592,227** | **45,251,706** |
| G | Biashara na Matengenezo | 7,371,411 | 7,682,286 | 8,444,243 | 8,747,862 | 9,260,703 | 9,821,248 | 10,395,783 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 5,710,466 | 6,050,976 | 6,577,706 | 6,929,895 | 7,324,856 | 7,815,845 | 8,736,561 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1,343,924 | 1,356,204 | 1,397,782 | 1,421,916 | 1,480,052 | 1,525,619 | 1,604,391 |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,266,747 | 1,414,116 | 1,560,064 | 1,681,098 | 1,718,548 | 1,824,471 | 1,989,829 |
| K | Fedha na Bima | 3,444,161 | 3,405,940 | 3,764,113 | 4,189,021 | 4,235,515 | 4,115,393 | 4,094,972 |
| L | Upangishaji Majengo | 2,515,243 | 2,623,190 | 2,736,907 | 2,856,109 | 2,982,008 | 3,115,112 | 3,248,194 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 322,260 | 385,090 | 447,921 | 518,123 | 606,207 | 694,291 | 763,332 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 1,417,467 | 1,660,994 | 1,976,260 | 2,183,917 | 2,611,498 | 2,892,463 | 3,054,288 |
| O | Utawala na Ulinzi | 3,623,123 | 3,974,206 | 4,242,164 | 4,548,604 | 4,793,820 | 4,907,113 | 5,058,292 |
| P | Elimu | 1,922,643 | 1,927,633 | 2,186,260 | 2,413,306 | 2,665,336 | 2,859,171 | 3,046,789 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | 1,284,594 | 1,245,030 | 1,349,941 | 1,419,090 | 1,497,896 | 1,611,999 | 1,742,444 |
| R | Sanaa na Burudani | 198,470 | 212,502 | 230,652 | 248,510 | 280,131 | 307,907 | 350,027 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 550,177 | 612,079 | 685,475 | 717,898 | 814,529 | 912,404 | 971,690 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 161,741 | 166,880 | 172,190 | 177,691 | 183,387 | 189,193 | 195,113 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **67,184,948** | **71,115,822** | **76,759,835** | **82,398,098** | **88,440,032** | **94,635,626** | **101,153,675** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 6,961,771 | 8,179,129 | 8,001,090 | 7,864,579 | 8,024,535 | 8,393,644 | 9,064,286 |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **3,833,129** | **3,973,166** | **4,113,187** | **4,086,638** | **4,363,825** | **4,628,135** | **4,922,233** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | 3,246,297 | 3,302,224 | 3,413,539 | 3,280,687 | 3,521,469 | 3,651,537 | 3,829,843 |
| | Mazao | 1,949,130 | 1,974,383 | 2,076,785 | 1,948,433 | 2,143,714 | 2,229,463 | 2,294,592 |
| | Mifugo | 1,020,661 | 1,038,181 | 1,032,784 | 1,026,920 | 1,048,140 | 1,079,584 | 1,185,810 |
| | Misitu | 262,340 | 274,799 | 288,811 | 290,951 | 314,157 | 326,723 | 332,233 |
| | Uvuvi | 14,165 | 14,861 | 15,159 | 14,383 | 15,458 | 15,767 | 17,208 |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **495,636** | **579,357** | **607,585** | **712,462** | **747,278** | **879,814** | **986,067** |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 80,222 | 82,352 | 85,427 | 88,351 | 91,001 | 94,641 | 107,966 |
| F | Ujenzi | 415,413 | 497,005 | 522,159 | 624,112 | 656,276 | 785,173 | 878,101 |
| | **Huduma** | **91,196** | **91,585** | **92,063** | **93,489** | **95,078** | **96,783** | **106,323** |
| L | Upangishaji Majengo | 91,196 | 91,585 | 92,063 | 93,489 | 95,078 | 96,783 | 106,323 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **77,979,847** | **83,268,117** | **88,874,111** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,140,194** |


**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI**
**(Kwa Bei za Mwaka 2015)**

**Jedwali NA.4** **Asilimia**

| | **SHUGHULI YA KIUCHUMI** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **2.8** | **6.9** | **5.4** | **4.8** | **5.9** | **5.3** |
| | Kilimo cha Mazao | 4.4 | 9.4 | 7.6 | 5.4 | 6.4 | 5.0 |
| | Mifugo | 4.8 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.9 |
| | Misitu | 4.5 | 4.8 | 3.4 | 3.9 | 4.8 | 4.9 |
| | Uvuvi | -13.3 | 1.8 | -4.5 | 1.2 | 8.4 | 9.2 |
| | Agriculture support services | 2.5 | 6.1 | 4.5 | 4.0 | 5.5 | 5.1 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4.5 | 6.4 | 10.0 | 7.4 | 5.3 | 1.5 |
| C | Viwanda | 3.7 | 10.0 | 7.1 | 10.8 | 8.2 | 8.3 |
| D | Umeme | 8.2 | 12.7 | -2.0 | 8.8 | 1.0 | 5.8 |
| E | Maji safi na Maji taka | 2.7 | 3.8 | 2.4 | 6.9 | 6.4 | 7.4 |
| F | Ujenzi | 19.1 | 2.5 | 12.9 | 14.5 | 15.1 | 12.9 |
| G | Biashara na Matengenezo | 4.2 | 9.9 | 3.6 | 5.9 | 6.1 | 5.8 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 6.0 | 8.7 | 5.4 | 5.7 | 6.7 | 11.8 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 0.9 | 3.1 | 1.7 | 4.1 | 3.1 | 5.2 |
| J | Habari na Mawasiliano | 11.6 | 10.3 | 7.8 | 2.2 | 6.2 | 9.1 |
| K | Fedha na Bima | -1.1 | 10.5 | 11.3 | 1.1 | -2.8 | -0.5 |
| L | Upangishaji Majengo | 4.2 | 4.2 | 4.3 | 4.3 | 4.4 | 4.4 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 19.5 | 16.3 | 15.7 | 17.0 | 14.5 | 9.9 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 17.2 | 19.0 | 10.5 | 19.6 | 10.8 | 5.6 |
| O | Utawala na Ulinzi | 9.7 | 6.7 | 7.2 | 5.4 | 2.4 | 3.1 |
| P | Elimu | 0.3 | 13.4 | 10.4 | 10.4 | 7.3 | 6.6 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | -3.1 | 8.4 | 5.1 | 5.6 | 7.6 | 8.1 |
| R | Sanaa na Burudani | 7.1 | 8.5 | 7.7 | 12.7 | 9.9 | 13.7 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 11.3 | 12.0 | 4.7 | 13.5 | 12.0 | 6.5 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.1 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **5.7** | **7.7** | **6.9** | **7.3** | **7.0** | **6.9** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 17.5 | -2.2 | -1.7 | 2.0 | 4.6 | 8.0 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **6.8** | **6.7** | **6.2** | **6.9** | **6.8** | **7.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu


UKUAJI HALISI WA PATO LA TAIFA - Kwa bei za mwaka 2015
Asilimia
7.2
7.0
6.8
6.6
6.4
6.2
6.0
5.8
5.6
6.8
6.7
6.2
6.9
6.8
7.0
2013
2014
2015
2016
2017
2018
Miaka

**PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI, KWA BEI ZA SOKO -SEHEMU INAYOUZIKA NA ISIYOUZIKA**
**(KWA BEI ZA MWAK 2015)**

**Jedwali Na.4A** Asilimia

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **A: SEHEMU INAYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | | | | | | |
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **2.9** | **7.5** | **6.9** | **4.4** | **6.3** | **5.3** |
| | Kilimo cha Mazao | 5.1 | 10.3 | 10.4 | 4.6 | 6.9 | 5.4 |
| | Mifugo | 5.4 | 5.9 | 5.9 | 5.3 | 5.2 | 4.2 |
| | Misitu | 4.5 | 4.8 | 3.7 | 3.5 | 4.9 | 5.2 |
| | Uvuvi | -13.4 | 1.8 | -4.5 | 1.1 | 8.4 | 9.2 |
| | Agriculture support services | 2.5 | 6.1 | 4.5 | 4.0 | 5.5 | 5.1 |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4.5 | 6.4 | 10.0 | 7.4 | 5.3 | 1.5 |
| C | Viwanda | 3.7 | 10.0 | 7.1 | 10.8 | 8.2 | 8.3 |
| D | Umeme | 8.2 | 12.7 | -2.0 | 8.8 | 1.0 | 5.8 |
| E | Maji safi na Maji taka | 2.7 | 3.8 | 2.0 | 8.1 | 7.1 | 5.6 |
| F | Ujenzi | 19.0 | 2.4 | 12.5 | 15.1 | 14.8 | 13.0 |
| G | Biashara na Matengenezo | 4.2 | 9.9 | 3.6 | 5.9 | 6.1 | 5.8 |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 6.0 | 8.7 | 5.4 | 5.7 | 6.7 | 11.8 |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 0.9 | 3.1 | 1.7 | 4.1 | 3.1 | 5.2 |
| J | Habari na Mawasiliano | 11.6 | 10.3 | 7.8 | 2.2 | 6.2 | 9.1 |
| K | Fedha na Bima | -1.1 | 10.5 | 11.3 | 1.1 | -2.8 | -0.5 |
| L | Upangishaji Majengo | 4.3 | 4.3 | 4.4 | 4.4 | 4.5 | 4.3 |
| M | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | 19.5 | 16.3 | 15.7 | 17.0 | 14.5 | 9.9 |
| N | Huduma zinazohusiana na Utawala | 17.2 | 19.0 | 10.5 | 19.6 | 10.8 | 5.6 |
| O | Utawala na Ulinzi | 9.7 | 6.7 | 7.2 | 5.4 | 2.4 | 3.1 |
| P | Elimu | 0.3 | 13.4 | 10.4 | 10.4 | 7.3 | 6.6 |
| Q | Afya na Huduma za Jamii | -3.1 | 8.4 | 5.1 | 5.6 | 7.6 | 8.1 |
| R | Sanaa na Burudani | 7.1 | 8.5 | 7.7 | 12.7 | 9.9 | 13.7 |
| S | Huduma nyingine za Kijamii | 11.3 | 12.0 | 4.7 | 13.5 | 12.0 | 6.5 |
| T | Shughuli za Kaya katika kuajiri | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.1 |
| | **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **5.9** | **7.9** | **7.3** | **7.3** | **7.0** | **6.9** |
| | Ongeza kodi katika bidhaa | 17.5 | -2.2 | -1.7 | 2.0 | 4.5 | 8.0 |
| | **B: SEHEMU ISIYOUZIKA** | | | | | | |
| | **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **3.7** | **3.5** | **-0.6** | **6.8** | **6.1** | **6.3** |
| A | Kilimo, Misitu na Uvuvi | 1.7 | 3.4 | -3.9 | 7.3 | 3.7 | 4.9 |
| | Mazao | 1.3 | 5.2 | -6.2 | 10.0 | 4.0 | 2.9 |
| | Mifugo | 1.7 | -0.5 | -0.6 | 2.1 | 3.0 | 9.8 |
| | Misitu | 4.7 | 5.1 | 0.7 | 8.0 | 4.0 | 1.7 |
| | Uvuvi | 4.9 | 2.0 | -5.1 | 7.5 | 2.0 | 9.1 |
| E | Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 2.7 | 3.7 | 3.4 | 3.0 | 4.0 | 14.1 |
| F | Ujenzi | 19.6 | 5.1 | 19.5 | 5.2 | 19.6 | 11.8 |
| L | Upangishaji Majengo | 0.4 | 0.5 | 1.5 | 1.7 | 1.8 | 9.9 |
| | **Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko** | **6.8** | **6.7** | **6.2** | **6.9** | **6.8** | **7.0** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**PATO LA TAIFA NA MATUMIZI YAKE KWA BEI ZA SOKO (BEI ZA MWAKA 2015)**

**Jedwali Na. 4B** Shs.Milioni

| Aina ya Matumizi | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pato la Taifa kwa Gharama zake (GDPbp)** | **71,018,076** | **75,088,988** | **80,873,021** | **86,484,736** | **92,803,857** | **99,263,761** | **106,075,908** |
| Kodi za uzalishaji | 6,961,771 | 8,179,129 | 8,001,090 | 7,864,579 | 8,024,535 | 8,393,644 | 9,064,286 |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **77,979,847** | **83,268,117** | **88,874,111** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,140,194** |
| **MATUMIZI YA PATO LA TAIFA** | | | | | | | |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko(GDPmp)** | **77,979,847** | **83,268,117** | **88,874,111** | **94,349,316** | **100,828,393** | **107,657,405** | **115,140,194** |
| **Matumizi ya Mwisho(Final consumption)** | **59,307,279** | **61,881,807** | **65,250,580** | **69,619,572** | **70,594,782** | **73,603,189** | **77,820,838** |
| Serikali | 7,770,261 | 8,058,996 | 8,548,398 | 9,366,334 | 9,667,251 | 9,771,806 | 9,968,648 |
| Binafsi | 51,370,798 | 53,641,790 | 56,500,911 | 60,047,089 | 60,697,766 | 63,578,381 | 67,577,020 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za kijamii | 166,220 | 181,021 | 201,271 | 206,149 | 229,766 | 253,003 | 275,169 |
| **Ukuzaji rasilimali** | **23,424,588** | **29,019,243** | **31,803,806** | **30,907,602** | **33,795,169** | **38,338,123** | **45,360,124** |
| Rasilimali za kudumu | 22,298,479 | 26,190,461 | 28,081,728 | 30,070,195 | 34,878,462 | 40,376,858 | 46,636,421 |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani *(*changes in Valuables*)* | 769,674 | 775,566 | 820,886 | 903,043 | 902,490 | 858,566 | 776,123 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 356,435 | 2,053,216 | 2,901,191 | -65,636 | -1,985,783 | -2,897,301 | -2,052,420 |
| **Mauzo nje** | **15,183,222** | **14,674,503** | **15,923,654** | **16,138,367** | **16,137,713** | **15,480,491** | **14,170,138** |
| Bidhaa-fob | 9,657,332 | 8,406,652 | 8,815,465 | 8,708,690 | 8,060,826 | 7,805,507 | 6,247,664 |
| Huduma | 5,525,891 | 6,267,851 | 7,108,189 | 7,429,677 | 8,076,886 | 7,674,984 | 7,922,474 |
| **Uagizaji** | **20,548,434** | **22,796,325** | **23,545,813** | **22,316,226** | **20,331,252** | **18,879,441** | **21,296,466** |
| Bidhaa-fob | 15,864,267 | 17,946,005 | 18,354,816 | 16,955,419 | 15,631,116 | 15,311,240 | 17,434,678 |
| Huduma | 4,684,167 | 4,850,319 | 5,190,997 | 5,360,807 | 4,700,136 | 3,568,202 | 3,861,788 |
| Makosa na Mapungufu | 613,191 | 488,889 | -558,115 | 0 | 631,981 | -884,958 | -914,439 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Kwa bei za miaka inayohusika)**

**Jedwali Na. 5** Shs. Milioni

| **Aina** | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 13,307,923 | 17,908,862 | 19,195,447 | 22,807,556 | 27,721,670 | 33,872,241 | 41,330,856 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,428,849 | 1,395,037 | 1,828,607 | 1,663,027 | 1,514,772 | 1,413,888 | 1,832,641 |
| Mitambo na Vifaa | 4,198,642 | 3,599,450 | 4,154,298 | 3,194,486 | 3,430,297 | 3,756,643 | 3,561,018 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 875,770 | 987,752 | 1,156,588 | 1,172,391 | 1,366,982 | 1,441,018 | 1,758,799 |
| Raslimali za Mazao ya Mifugo | 254,212 | 297,937 | 330,525 | 375,399 | 425,361 | 461,511 | 508,945 |
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, na Huduma za Kitaalamu | 478,066 | 591,860 | 734,368 | 857,335 | 1,033,744 | 1,196,620 | 1,323,980 |
| **Rasilimali za Kudumu** | **20,543,461** | **24,780,897** | **27,399,832** | **30,070,195** | **35,492,828** | **42,141,921** | **50,316,239** |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 806,021 | 766,581 | 756,477 | 903,043 | 1,105,406 | 1,006,179 | 1,215,104 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 365,106 | 1,797,044 | 2,947,143 | -65636 | -1732887 | -2720674 | -1148203 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **21,714,587** | **27,344,522** | **31,103,452** | **30,907,602** | **34,865,346** | **40,427,427** | **50,383,140** |

**Chanzo:**Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Bei za Mwaka 2015)**

**Jedwali Na.6** Shs.Milioni

| Aina | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 14,855,881 | 19,218,436 | 19,485,103 | 22,807,556 | 27,512,753 | 32,836,681 | 38,191,158 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,336,722 | 1,218,733 | 2,044,517 | 1,663,027 | 1,373,682 | 1,173,050 | 1,924,369 |
| Mitambo na Vifaa | 4,280,352 | 3,713,748 | 4,229,095 | 3,194,486 | 3,268,709 | 3,473,892 | 3,276,373 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 990,971 | 1,061,609 | 1,200,328 | 1,172,391 | 1,323,953 | 1,335,724 | 1,569,555 |
| Raslimali za Mazao ya Mifugo | 290,292 | 332,936 | 364,963 | 375,399 | 385,150 | 414,428 | 434,330 |
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, na Huduma za Kitaalamu | 544,261 | 645,000 | 757,723 | 857,335 | 1,014,215 | 1,143,083 | 1,240,636 |
| **Rasilimali za Kudumu** | **22,298,479** | **26,190,461** | **28,081,728** | **30,070,195** | **34,878,462** | **40,376,858** | **46,636,421** |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 769,674 | 775,566 | 820,886 | 903,043 | 902,490 | 858,566 | 776,123 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 356,435 | 2,053,216 | 2,901,191 | -65636 | -1985783 | -2897301 | -2052420 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **23,424,588** | **29,019,243** | **31,803,806** | **30,907,602** | **33,795,169** | **38,338,123** | **45,360,124** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**MCHANGO KATIKA UKUZAJI RASILIMALI KWA AINA YA SHUGHULI (Kwa bei za miaka inayohusika)**

**Jedwali Na. 7a** Asilimia

| Aina | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 61.3 | 65.5 | 61.7 | 73.8 | 79.5 | 83.8 | 82.0 |
| Vifaa vya Usafiri | 6.6 | 5.1 | 5.9 | 5.4 | 4.3 | 3.5 | 3.6 |
| Mitambo na Vifaa | 19.3 | 13.2 | 13.4 | 10.3 | 9.8 | 9.3 | 7.1 |
| Mitambo na Vifaa vingine | 4.0 | 3.6 | 3.7 | 3.8 | 3.9 | 3.6 | 3.5 |
| Raslimali za Mazao ya Mifugo | 1.2 | 1.1 | 1.1 | 1.2 | 1.2 | 1.1 | 1.0 |
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, na Huduma za Kitaalamu | 2.2 | 2.2 | 2.4 | 2.8 | 3.0 | 3.0 | 2.6 |
| **Rasilimali za Kudumu** | **94.6** | **90.6** | **88.1** | **97.3** | **101.8** | **104.2** | **99.9** |
| Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables) | 3.7 | 2.8 | 2.4 | 2.9 | 3.2 | 2.5 | 2.4 |
| Ongezeko la limbikizo (changes in Inventories) | 1.7 | 6.6 | 9.5 | -0.2 | -5.0 | -6.7 | -2.3 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **100.0** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** |

**Chanzo:**Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**UKUZAJI WA RASILIMALI KATIKA SEHEMU ZA UCHUMI WA KITAIFA NA BINAFSI (Kwa bei za miaka inayohusika)**

**Jedwali Na.7b** Shs. Milioni

| Sekta | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A. Rasilimali za Kudumu** | **20,543,461** | **24,780,897** | **27,399,832** | **30,070,195** | **35,492,828** | **42,141,921** | **50,316,239** |
| 1. Serikali kuu | 4,930,430 | 5,451,797 | 6,549,213 | 7,219,843 | 8,944,186 | 10,914,757 | 13,106,326 |
| 2. Mashirika | 534,130 | 545,180 | 534,350 | 589,169 | 745,349 | 1,011,406 | 1,104,748 |
| 3. Taasisi | 554,673 | 545,180 | 586,415 | 812,232 | 851,827 | 1,095,690 | 1,054,532 |
| 4. Sekta binafsi | 14,524,227 | 18,238,741 | 19,729,853 | 21,448,950 | 24,951,465 | 29,120,067 | 35,050,634 |
| **B: Ongezeko la limbikizo la Vito vya Thamani (changes in Valuables)** | **806,021** | **766,581** | **756,477** | **903,043** | **1,105,406** | **1,006,179** | **1,215,104** |
| **C. Ongezeko la Limbikizo** | **365,106** | **1,797,044** | **2,947,143** | **-65636** | **-1732887** | **-2720674** | **-1148203** |
| **D. Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **21,714,587** | **27,344,522** | **31,103,452** | **30,907,602** | **34,865,346** | **40,427,427** | **50,383,140** |

**Chanzo**:Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**FAHIRISI ZA BEI ZA REJAREJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR-ES-SALAAM (Des.2015=100)**

Jedwali Na.8

| MWAKA | BIDHAA ZOTE | | CHAKULA | |
|---|---|---|---|---|
| | FAHIRISI | BADILIKO ASILIMIA | FAHIRISI | BADILIKO ASILIMIA |
| 2000 | 23.8 | 1.7 | 22.0 | -2.0 |
| 2001 | 25.9 | 8.5 | 24.0 | 8.9 |
| 2002 | 26.9 | 3.8 | 24.9 | 4.0 |
| 2003 | 28.4 | 5.8 | 26.3 | 5.4 |
| 2004 | 30.2 | 6.4 | 28.1 | 6.8 |
| 2005 | 32.7 | 8.3 | 30.1 | 7.3 |
| 2006 | 36.49 | 11.5 | 33.24 | 10.3 |
| 2007 | 39.89 | 9.3 | 36.34 | 9.3 |
| 2008 | 46.80 | 17.3 | 41.87 | 15.2 |
| 2009 | 54.66 | 16.8 | 50.01 | 19.4 |
| 2010 | 61.89 | 13.2 | 58.99 | 18.0 |
| 2011 | 66.48 | 7.4 | 63.16 | 7.1 |
| 2012 | 78.96 | 18.8 | 77.83 | 23.2 |
| 2013 | 86.34 | 9.3 | 85.98 | 10.5 |
| 2014 | 92.95 | 7.7 | 92.22 | 7.3 |
| 2015* | 97.97 | 5.4 | 97.67 | 5.9 |
| 2016 | 102.21 | 4.3 | 101.19 | 3.6 |
| 2017 | 104.10 | 1.9 | 104.67 | 3.4 |
| 2018 | 106.15 | 2.0 | 109.36 | 4.5 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

**FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIKAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (2001= 100)**

Jedwali Na.9

| Mwaka | Chakula | Vinywaji na Sigara | Kodi ya Nyumba | Umeme, Mafuta ya Taa, Maji | Nguo na Viatu | Fenicha, Vyombo Vya Nyumbani | Huduma Mahitaji ya Nyumbani | Huduma za Afya | Michezo na Starehe | Usafiri | Elimu | Vinginevyo | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2003 | 114.2 | 120.0 | 100.0 | 123.1 | 87.9 | 114.6 | 74.3 | 71.9 | 96.2 | 104.8 | 180.2 | 150.3 | 112.7 |
| 2004 | 123.5 | 122.9 | 100.0 | 142.0 | 97.2 | 137.4 | 80.5 | 85.1 | 99.4 | 104.1 | 191.1 | 123.0 | 121.9 |
| 2005 | 125.7 | 120.0 | 113.6 | 162.3 | 108.7 | 115.7 | 110.0 | 113.6 | 110.4 | 109.8 | 115.0 | 121.1 | 126.5 |
| 2006 | 138.6 | 141.8 | 132.8 | 193.7 | 108.0 | 115.4 | 109.6 | 118.8 | 113.5 | 134.0 | 93.3 | 139.3 | 141.1 |
| 2007 | 151.5 | 159.5 | 146.1 | 209.1 | 124.1 | 131.7 | 119.1 | 114.8 | 148.5 | 114.9 | 104.0 | 128.4 | 154.2 |
| 2008 | 174.6 | 175.1 | 199.3 | 269.8 | 139.3 | 160.5 | 138.4 | 134.0 | 110.8 | 179.5 | 99.2 | 137.2 | 180.9 |
| 2009 | 208.5 | 210.8 | 206.6 | 276.6 | 152.8 | 173.3 | 167.1 | 163.8 | 124.7 | 225.9 | 111.3 | 147.7 | 211.3 |
| **FAHIRISI ZA BEI ZA REJA REJA ZA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI DAR ES SALAAM (Des. 2015 = 100)** | | | | | | | | | | | | | |
| | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
| 2010 | 58.99 | 58.09 | 58.47 | 68.80 | 77.22 | 79.73 | 63.60 | 99.68 | 68.72 | 102.48 | 63.66 | 63.22 | 61.89 |
| 2011 | 63.16 | 61.31 | 68.58 | 73.79 | 83.74 | 82.85 | 73.17 | 99.72 | 68.03 | 102.59 | 67.21 | 69.09 | 66.48 |
| 2012 | 77.83 | 66.34 | 75.61 | 86.46 | 86.26 | 88.38 | 83.22 | 100.00 | 81.74 | 103.20 | 73.61 | 76.41 | 78.96 |
| 2013 | 85.98 | 75.34 | 85.60 | 88.69 | 88.81 | 90.62 | 86.32 | 100.00 | 90.84 | 102.73 | 85.16 | 84.36 | 86.34 |
| 2014 | 92.22 | 81.64 | 93.45 | 94.93 | 92.39 | 91.24 | 100.08 | 100.00 | 94.70 | 102.72 | 91.76 | 94.05 | 92.95 |
| 2015* | 97.67 | 93.26 | 101.90 | 98.12 | 97.91 | 96.35 | 99.91 | 100.00 | 100.00 | 102.40 | 98.24 | 96.61 | 97.97 |
| 2016 | 101.19 | 100.89 | 99.41 | 105.13 | 100.55 | 108.05 | 100.84 | 100.57 | 101.22 | 97.07 | 104.92 | 102.41 | 102.21 |
| 2017 | 104.67 | 103.85 | 100.71 | 106.08 | 103.70 | 109.73 | 100.74 | 100.95 | 102.92 | 100.84 | 105.48 | 103.38 | 104.10 |
| 2018 | 109.36 | 103.85 | 103.87 | 112.15 | 105.67 | 109.80 | 88.19 | 100.86 | 104.08 | 106.36 | 105.60 | 105.01 | 106.15 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

NB. Wastani (Average) wa mwaka (kuanzia mwaka 2003, Fahirisi (Index) imekuwa ikitolewa kila mwezi katika miezi yote 12 ya mwaka

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya

Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI - DAR-ES-SALAAM (Des.2015 =100)**

Jedwali Na. 10

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2000 | 27.0 | 28.1 | 27.2 | 29.4 | 27.9 | 2.5 |
| 2001 | 30.5 | 28.9 | 28.7 | 28.4 | 29.1 | 4.5 |
| 2002 | 30.0 | 30.0 | 30.2 | 30.4 | 30.2 | 3.5 |
| 2003 | 30.4 | 30.4 | 30.9 | 31.7 | 30.8 | 2.3 |
| 2004 | 32.8 | 33.1 | 33.5 | 34.2 | 33.4 | 8.2 |
| 2005 | 34.9 | 35.3 | 36.7 | 37.3 | 36.0 | 7.9 |
| 2006 | 38.3 | 39.4 | 39.5 | 40.2 | 39.3 | 9.2 |
| 2007 | 41.7 | 43.3 | 44.4 | 46.0 | 43.9 | 11.5 |
| 2008 | 48.5 | 49.9 | 51.2 | 52.7 | 50.6 | 15.3 |
| 2009 | 55.7 | 57.3 | 60.3 | 62.3 | 58.9 | 16.4 |
| 2010 | 63.9 | 64.6 | 65.1 | 65.6 | 64.8 | 10.0 |
| 2011 | 67.9 | 69.3 | 70.3 | 72.1 | 69.9 | 7.9 |
| 2012 | 78.4 | 81.6 | 82.7 | 83.4 | 81.5 | 16.6 |
| 2013 | 87.6 | 88.6 | 88.5 | 88.4 | 88.3 | 8.3 |
| 2014 | 92.8 | 94.2 | 94.5 | 93.5 | 93.7 | 6.2 |
| 2015* | 96.5 | 98.9 | 100.6 | 100.0 | 99.0 | 5.6 |
| 2016 | 102.05 | 104.35 | 103.81 | 103.79 | 103.50 | 4.5 |
| 2017 | 104.48 | 106.72 | 106.65 | 107.02 | 106.22 | 2.6 |
| 2018 | 105.75 | 108.50 | 108.73 | 109.82 | 108.20 | 1.9 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

**FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI DAR ES SALAAM (DES. 2015=100)**

Jedwali Na.11

| FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI DAR ES SALAAM (DES. 2015 = 100) | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
| 2010 Robo ya kwanza | 64.9 | 67.0 | 70.8 | 49.0 | 75.0 | 77.1 | 68.2 | 96.9 | 73.3 | 67.4 | 68.5 | 69.7 | 63.9 |
| Robo ya pili | 66.0 | 66.2 | 71.4 | 49.6 | 74.5 | 77.1 | 68.2 | 96.8 | 73.0 | 67.4 | 68.6 | 69.4 | 64.6 |
| Robo ya tatu | 66.3 | 67.3 | 71.8 | 50.8 | 75.4 | 77.1 | 68.4 | 97.3 | 75.4 | 67.4 | 69.2 | 69.5 | 65.1 |
| Robo ya nne | 66.7 | 68.9 | 72.1 | 51.7 | 75.9 | 77.1 | 68.8 | 97.3 | 75.2 | 67.4 | 69.4 | 69.1 | 65.6 |
| 2011 Robo ya kwanza | 69.8 | 69.5 | 74.0 | 54.2 | 78.8 | 79.0 | 70.2 | 97.3 | 75.8 | 67.1 | 68.6 | 70.9 | 67.9 |
| Robo ya pili | 70.9 | 70.1 | 75.9 | 56.5 | 81.3 | 80.6 | 71.0 | 97.3 | 76.8 | 67.0 | 69.5 | 73.4 | 69.3 |
| Robo ya tatu | 72.1 | 71.3 | 75.9 | 57.6 | 82.0 | 80.8 | 71.1 | 97.4 | 77.0 | 67.2 | 70.0 | 75.1 | 70.3 |
| Robo ya nne | 75.1 | 72.0 | 76.3 | 58.1 | 82.5 | 80.8 | 71.6 | 97.6 | 77.7 | 67.3 | 70.0 | 75.9 | 72.1 |
| 2012 Robo ya kwanza | 82.9 | 76.0 | 84.8 | 64.1 | 83.8 | 83.0 | 73.6 | 97.9 | 81.3 | 73.8 | 74.4 | 79.5 | 78.4 |
| Robo ya pili | 85.9 | 78.7 | 87.6 | 67.5 | 87.9 | 87.0 | 78.2 | 98.3 | 86.3 | 79.1 | 77.0 | 81.9 | 81.6 |
| Robo ya tatu | 87.1 | 81.2 | 89.5 | 68.4 | 89.0 | 87.9 | 78.5 | 98.4 | 89.2 | 81.3 | 78.6 | 83.1 | 82.7 |
| Robo ya nne | 87.6 | 82.2 | 91.9 | 69.4 | 89.6 | 88.8 | 78.1 | 98.5 | 89.4 | 82.7 | 79.5 | 84.6 | 83.4 |
| 2013 Robo ya kwanza | 94.6 | 82.5 | 94.0 | 70.7 | 90.1 | 90.0 | 78.0 | 98.7 | 90.0 | 83.5 | 80.0 | 85.4 | 87.6 |
| Robo ya pili | 94.6 | 83.5 | 94.7 | 73.7 | 90.4 | 90.1 | 83.6 | 99.0 | 90.8 | 84.2 | 80.7 | 86.0 | 88.6 |
| Robo ya tatu | 92.7 | 86.2 | 95.6 | 76.2 | 90.8 | 91.3 | 88.0 | 99.2 | 91.5 | 85.9 | 81.6 | 88.2 | 88.5 |
| Robo ya nne | 91.7 | 88.0 | 95.7 | 77.5 | 91.3 | 91.7 | 89.5 | 99.2 | 92.2 | 86.8 | 82.5 | 88.8 | 88.4 |
| 2014 Robo ya kwanza | 98.1 | 88.8 | 96.0 | 80.3 | 92.1 | 92.2 | 93.5 | 99.3 | 92.6 | 91.8 | 83.5 | 90.2 | 92.8 |
| Robo ya pili | 99.1 | 89.0 | 96.6 | 82.8 | 93.2 | 94.8 | 94.2 | 99.5 | 93.2 | 94.3 | 85.8 | 90.6 | 94.2 |
| Robo ya tatu | 97.3 | 92.9 | 97.3 | 86.8 | 96.7 | 97.0 | 96.3 | 100.0 | 95.0 | 95.9 | 88.0 | 93.6 | 94.5 |
| Robo ya nne | 93.7 | 97.0 | 98.0 | 89.6 | 99.0 | 97.8 | 97.7 | 100.0 | 97.2 | 95.9 | 90.5 | 95.7 | 93.5 |
| 2015* Robo ya kwanza | 97.3 | 97.9 | 98.5 | 93.4 | 99.6 | 97.8 | 98.6 | 100.2 | 97.2 | 99.0 | 93.8 | 96.0 | 96.5 |
| Robo ya pili | 100.1 | 98.1 | 98.9 | 96.7 | 99.3 | 97.8 | 99.3 | 100.3 | 97.3 | 99.9 | 96.4 | 96.6 | 98.9 |
| Robo ya tatu | 101.8 | 98.9 | 99.0 | 99.4 | 99.4 | 98.4 | 100.5 | 100.2 | 98.2 | 100.0 | 98.0 | 96.7 | 100.6 |
| Robo ya nne | 100.4 | 100.0 | 99.8 | 99.5 | 99.9 | 99.6 | 100.1 | 100.0 | 100.1 | 100.0 | 99.0 | 99.2 | 100.0 |
| 2016 Robo ya kwanza | 101.81 | 100.94 | 99.84 | 108.37 | 99.89 | 106.44 | 99.44 | 100.00 | 100.34 | 97.77 | 100.70 | 101.37 | 102.05 |
| Robo ya pili | 104.35 | 100.23 | 100.67 | 111.35 | 101.13 | 111.18 | 99.79 | 100.65 | 100.98 | 97.34 | 105.93 | 102.20 | 104.35 |
| Robo ya tatu | 103.90 | 101.28 | 99.83 | 107.36 | 100.24 | 113.92 | 100.57 | 101.22 | 101.05 | 97.34 | 106.92 | 102.16 | 103.81 |
| Robo ya nne | 102.52 | 102.55 | 100.25 | 110.34 | 102.43 | 114.81 | 99.94 | 101.34 | 101.94 | 97.34 | 105.83 | 103.52 | 103.79 |
| 2017 Robo ya kwanza | 105.73 | 103.07 | 100.93 | 105.30 | 104.32 | 114.49 | 101.20 | 101.35 | 101.16 | 97.34 | 106.10 | 102.99 | 104.48 |
| Robo ya pili | 110.22 | 103.61 | 101.49 | 108.85 | 104.02 | 114.00 | 102.03 | 101.35 | 101.70 | 97.34 | 105.91 | 103.44 | 106.72 |
| Robo ya tatu | 107.86 | 103.86 | 101.84 | 115.20 | 104.13 | 114.10 | 99.40 | 101.34 | 101.41 | 97.34 | 106.27 | 103.89 | 106.65 |
| Robo ya nne | 107.75 | 103.85 | 101.95 | 117.53 | 104.36 | 114.48 | 99.98 | 101.28 | 101.91 | 97.34 | 106.27 | 103.25 | 107.02 |
| 2018 Robo ya kwanza | 111.38 | 103.06 | 101.58 | 112.37 | 104.56 | 114.41 | 80.57 | 101.28 | 101.05 | 105.74 | 104.96 | 103.43 | 105.75 |
| Robo ya pili | 117.46 | 103.06 | 102.80 | 114.81 | 105.34 | 114.57 | 80.87 | 101.18 | 101.75 | 105.74 | 104.97 | 104.92 | 108.50 |
| Robo ya tatu | 116.84 | 103.06 | 104.34 | 116.35 | 105.73 | 114.65 | 81.26 | 101.12 | 101.55 | 105.74 | 105.55 | 105.35 | 108.73 |
| Robo ya nne | 115.96 | 103.21 | 106.12 | 121.73 | 106.68 | 114.80 | 84.15 | 101.17 | 102.12 | 105.74 | 106.91 | 106.24 | 109.82 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Des. 2015=100)**

Jedwali Na.12

**FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Des. 2015=100)**

| Mwaka | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamaduni na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2010 Robo ya kwanza | 54.8 | 68.9 | 75.2 | 63.9 | 82.3 | 84.4 | 67.3 | 94.3 | 82.5 | 82.1 | 65.4 | 83.0 | 63.4 |
| Robo ya pili | 57.0 | 72.3 | 74.7 | 65.1 | 82.8 | 84.4 | 67.8 | 94.7 | 84.8 | 82.1 | 65.7 | 85.2 | 64.9 |
| Robo ya tatu | 56.8 | 72.4 | 78.6 | 68.2 | 85.5 | 84.4 | 68.5 | 94.9 | 87.1 | 82.1 | 66.3 | 86.7 | 65.8 |
| Robo ya nne | 57.7 | 72.6 | 81.1 | 67.7 | 84.6 | 84.4 | 69.1 | 94.9 | 88.2 | 82.1 | 65.9 | 87.1 | 66.3 |
| 2011 Robo ya kwanza | 61.1 | 73.8 | 80.7 | 70.9 | 86.7 | 85.2 | 70.8 | 94.9 | 89.3 | 82.1 | 67.5 | 83.9 | 68.7 |
| Robo ya pili | 62.4 | 74.8 | 83.8 | 72.0 | 89.5 | 87.7 | 77.2 | 94.9 | 91.2 | 82.1 | 72.2 | 85.6 | 70.8 |
| Robo ya tatu | 64.5 | 76.7 | 84.2 | 74.4 | 88.9 | 87.7 | 80.5 | 95.2 | 91.8 | 82.5 | 76.4 | 86.9 | 72.8 |
| Robo ya nne | 68.8 | 77.3 | 85.7 | 76.4 | 90.3 | 89.5 | 82.9 | 95.4 | 92.0 | 82.7 | 77.2 | 88.4 | 75.7 |
| 2012 Robo ya kwanza | 72.8 | 78.2 | 88.7 | 77.3 | 92.9 | 91.5 | 82.4 | 95.4 | 92.8 | 82.7 | 78.7 | 91.3 | 78.0 |
| Robo ya pili | 74.2 | 78.6 | 89.2 | 79.8 | 94.2 | 91.9 | 83.3 | 95.4 | 93.0 | 82.7 | 79.6 | 95.4 | 79.5 |
| Robo ya tatu | 74.9 | 80.5 | 91.0 | 81.8 | 95.0 | 92.0 | 83.3 | 95.5 | 93.3 | 82.7 | 81.5 | 95.7 | 80.4 |
| Robo ya nne | 77.3 | 81.4 | 93.0 | 83.1 | 95.7 | 93.3 | 85.2 | 95.6 | 93.4 | 82.7 | 82.9 | 96.1 | 82.2 |
| 2013 Robo ya kwanza | 83.1 | 81.4 | 93.8 | 83.9 | 96.1 | 94.8 | 86.4 | 95.5 | 93.9 | 84.4 | 84.9 | 96.4 | 85.5 |
| Robo ya pili | 81.7 | 82.1 | 95.2 | 83.4 | 96.3 | 94.8 | 94.1 | 95.7 | 96.1 | 84.4 | 85.3 | 96.8 | 85.6 |
| Robo ya tatu | 82.8 | 87.7 | 96.3 | 84.3 | 97.1 | 94.8 | 95.6 | 95.7 | 96.3 | 84.4 | 85.8 | 97.2 | 86.6 |
| Robo ya nne | 84.2 | 90.4 | 96.4 | 86.4 | 97.7 | 94.8 | 96.2 | 95.7 | 96.0 | 84.7 | 87.4 | 97.2 | 87.9 |
| 2014Robo ya kwanza | 88.5 | 90.4 | 97.5 | 87.6 | 97.7 | 95.5 | 96.6 | 95.7 | 98.8 | 95.7 | 87.9 | 99.0 | 90.6 |
| Robo ya pili | 87.9 | 90.4 | 97.6 | 88.1 | 98.5 | 97.7 | 97.6 | 95.7 | 98.9 | 98.6 | 88.0 | 99.8 | 90.7 |
| Robo ya tatu | 88.0 | 92.9 | 97.5 | 92.7 | 97.8 | 97.5 | 98.7 | 95.7 | 99.3 | 98.6 | 90.4 | 101.2 | 91.8 |
| Robo ya nne | 89.7 | 95.6 | 97.3 | 95.1 | 98.2 | 97.3 | 99.3 | 95.6 | 99.8 | 98.6 | 92.5 | 99.9 | 93.3 |
| 2015*Robo ya kwanza | 92.5 | 96.7 | 97.8 | 95.2 | 98.3 | 97.5 | 101.2 | 97.6 | 99.7 | 100.0 | 95.4 | 100.2 | 95.1 |
| Robo ya pili | 95.1 | 98.1 | 97.8 | 96.0 | 98.2 | 97.5 | 102.5 | 97.7 | 100.0 | 100.0 | 97.5 | 98.6 | 96.8 |
| Robo ya tatu | 97.6 | 99.0 | 98.5 | 97.1 | 98.7 | 98.4 | 102.6 | 98.5 | 100.2 | 100.0 | 97.5 | 98.7 | 98.3 |
| Robo ya nne | 100.0 | 99.6 | 99.3 | 101.1 | 99.6 | 99.3 | 99.9 | 100.0 | 100.1 | 100.0 | 98.4 | 99.6 | 100.0 |
| 2016Robo ya kwanza | 102.6 | 100.4 | 99.8 | 105.2 | 100.2 | 107.3 | 98.6 | 100.0 | 100.4 | 98.6 | 100.4 | 101.4 | 101.0 |
| Robo ya pili | 105.3 | 100.9 | 100.7 | 107.2 | 103.0 | 111.9 | 98.9 | 100.6 | 101.3 | 98.4 | 103.1 | 102.0 | 102.5 |
| Robo ya tatu | 106.0 | 102.3 | 99.7 | 104.3 | 100.1 | 114.0 | 99.7 | 101.2 | 101.0 | 98.4 | 102.9 | 102.7 | 102.4 |
| Robo ya nne | 104.4 | 102.8 | 100.2 | 106.9 | 104.4 | 115.0 | 99.8 | 101.3 | 101.9 | 98.4 | 102.4 | 105.0 | 102.8 |
| 2017 Robo ya kwanza | 107.4 | 102.9 | 101.3 | 105.5 | 107.3 | 115.2 | 101.7 | 101.3 | 100.1 | 98.4 | 102.5 | 105.3 | 104.0 |
| Robo ya pili | 112.6 | 103.8 | 102.0 | 105.8 | 107.7 | 114.7 | 103.2 | 101.3 | 100.6 | 98.4 | 103.1 | 105.4 | 105.8 |
| Robo ya tatu | 116.9 | 104.1 | 102.1 | 107.7 | 107.3 | 114.2 | 104.8 | 101.3 | 99.4 | 98.4 | 103.4 | 106.3 | 107.4 |
| Robo ya nne | 119.9 | 104.1 | 102.4 | 110.0 | 107.2 | 115.2 | 106.8 | 101.5 | 99.8 | 98.4 | 103.0 | 107.3 | 108.9 |
| 2018 Robo ya kwanza | 120.6 | 104.1 | 102.8 | 110.4 | 107.6 | 115.1 | 107.8 | 101.7 | 100.4 | 101.4 | 103.0 | 105.2 | 109.5 |
| Robo ya pili | 121.9 | 104.1 | 103.9 | 112.9 | 108.6 | 115.1 | 110.4 | 101.8 | 100.9 | 107.6 | 103.2 | 106.6 | 111.2 |
| Robo ya tatu | 123.3 | 103.8 | 105.2 | 113.8 | 108.9 | 115.0 | 111.6 | 101.8 | 101.3 | 107.6 | 103.9 | 107.5 | 112.1 |
| Robo ya nne | 122.9 | 103.8 | 105.9 | 115.9 | 109.2 | 114.9 | 113.4 | 101.8 | 100.7 | 107.6 | 106.1 | 107.7 | 113.0 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Des. 2015=100)**

Jedwali Na. 13

| Mwaka | M I E Z I | | | | Wastani | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Machi | Juni | Sept. | Desemba | | Asilimia |
| 2000 | 24.18 | 24.18 | 25.27 | 25.83 | 24.87 | 6.2 |
| 2001 | 30.87 | 28.15 | 27.03 | 25.83 | 27.97 | 12.5 |
| 2002 | 28.96 | 28.88 | 28.93 | 28.89 | 28.91 | 6.6 |
| 2003 | 29.92 | 30.22 | 30.19 | 30.24 | 30.14 | 4.2 |
| 2004 | 30.98 | 31.77 | 32.30 | 33.02 | 32.02 | 6.2 |
| 2005 | 33.62 | 33.88 | 34.76 | 36.80 | 34.77 | 8.6 |
| 2006 | 37.88 | 38.51 | 38.90 | 40.13 | 38.86 | 11.8 |
| 2007 | 42.19 | 43.45 | 44.68 | 45.76 | 44.02 | 13.3 |
| 2008 | 48.86 | 50.13 | 53.91 | 55.41 | 52.08 | 18.3 |
| 2009 | 57.72 | 58.40 | 61.62 | 63.21 | 60.24 | 15.7 |
| 2010 | 63.41 | 64.89 | 65.82 | 66.29 | 65.10 | 8.1 |
| 2011 | 68.73 | 70.77 | 72.83 | 75.67 | 72.00 | 10.6 |
| 2012 | 78.04 | 79.50 | 80.40 | 82.20 | 80.04 | 11.2 |
| 2013 | 85.48 | 85.58 | 86.64 | 87.93 | 86.41 | 8.0 |
| 2014 | 90.61 | 90.68 | 91.84 | 93.27 | 91.60 | 6.0 |
| 2015* | 95.14 | 96.78 | 98.27 | 100.00 | 97.55 | 6.5 |
| 2016 | 101.02 | 102.52 | 102.43 | 102.81 | 102.20 | 4.8 |
| 2017 | 104.01 | 105.76 | 107.37 | 108.93 | 106.52 | 4.2 |
| 2018 | 109.52 | 111.24 | 112.15 | 113.00 | 111.48 | 4.7 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Des. 2015=100)**

Jedwali Na.14

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Des. 2015=100)**

| Mwaka | | Vyakula na vinywaji baridi | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | Mavazi ya nguo na viatu | Nishati, Maji na Makazi | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | Gharama za Afya | Usafirishaji | Mawasiliano | Utamadun i na Burudani | Elimu | Hoteli na Migahawa | Bidhaa na huduma nyinginezo | FAHIRISI BIDHAA ZOTE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2010 | Robo ya kwanza | 54.4 | 66.1 | 68.2 | 54.3 | 72.0 | 84.6 | 79.4 | 101.3 | 81.7 | 83.4 | 69.5 | 72.4 | 61.3 |
| | Robo ya pili | 55.2 | 64.8 | 68.4 | 57.2 | 72.9 | 84.8 | 79.2 | 102.0 | 82.7 | 83.4 | 69.5 | 72.9 | 62.1 |
| | Robo ya tatu | 54.2 | 66.2 | 70.2 | 58.1 | 74.1 | 84.9 | 78.9 | 102.2 | 84.2 | 81.9 | 69.8 | 74.6 | 61.9 |
| | Robo ya nne | 54.9 | 66.6 | 71.7 | 58.1 | 74.8 | 84.6 | 78.9 | 102.3 | 83.9 | 81.3 | 68.9 | 74.5 | 62.4 |
| 2011 | Robo ya kwanza | 59.0 | 67.7 | 73.6 | 61.9 | 80.5 | 85.7 | 80.4 | 100.2 | 84.7 | 85.6 | 72.4 | 74.6 | 65.8 |
| | Robo ya pili | 61.2 | 68.7 | 75.0 | 66.2 | 83.1 | 86.2 | 84.5 | 99.9 | 85.2 | 85.9 | 73.9 | 75.4 | 68.2 |
| | Robo ya tatu | 64.4 | 69.7 | 76.9 | 70.3 | 84.6 | 86.5 | 86.6 | 100.7 | 86.1 | 85.9 | 75.9 | 77.9 | 71.0 |
| | Robo ya nne | 69.0 | 70.3 | 79.5 | 71.8 | 86.1 | 87.6 | 88.1 | 100.7 | 86.3 | 85.9 | 78.0 | 80.3 | 74.2 |
| 2012 | Robo ya kwanza | 74.7 | 73.1 | 83.8 | 73.4 | 88.9 | 88.2 | 88.8 | 99.6 | 90.9 | 89.2 | 83.7 | 82.9 | 78.6 |
| | Robo ya pili | 76.3 | 75.5 | 86.5 | 76.3 | 90.7 | 89.0 | 90.4 | 99.1 | 93.7 | 90.0 | 87.3 | 85.2 | 80.5 |
| | Robo ya tatu | 76.3 | 83.3 | 87.8 | 80.4 | 91.8 | 89.4 | 90.5 | 99.1 | 96.0 | 90.0 | 88.5 | 85.9 | 81.4 |
| | Robo ya nne | 78.5 | 85.4 | 89.0 | 84.1 | 93.1 | 90.1 | 90.5 | 98.9 | 95.7 | 90.0 | 90.5 | 87.1 | 83.4 |
| 2013 | Robo ya kwanza | 83.4 | 87.6 | 90.5 | 86.1 | 94.4 | 91.0 | 90.7 | 98.7 | 95.6 | 91.7 | 91.8 | 88.6 | 86.7 |
| | Robo ya pili | 82.9 | 88.3 | 91.2 | 90.1 | 94.6 | 91.7 | 96.1 | 98.5 | 96.0 | 91.9 | 92.2 | 89.4 | 87.3 |
| | Robo ya tatu | 81.6 | 92.4 | 92.3 | 90.7 | 95.0 | 91.9 | 97.8 | 99.0 | 96.4 | 92.1 | 92.3 | 90.9 | 86.9 |
| | Robo ya nne | 83.7 | 93.5 | 92.8 | 92.0 | 95.6 | 92.0 | 98.4 | 99.1 | 96.4 | 92.1 | 92.9 | 91.7 | 88.4 |
| 2014 | Robo ya kwanza | 88.9 | 93.8 | 93.8 | 96.8 | 96.1 | 92.8 | 98.8 | 99.2 | 96.6 | 96.8 | 93.3 | 92.6 | 91.9 |
| | Robo ya pili | 89.7 | 93.8 | 94.1 | 98.7 | 96.8 | 95.2 | 99.4 | 99.5 | 96.7 | 96.8 | 94.5 | 96.6 | 92.9 |
| | Robo ya tatu | 88.6 | 96.8 | 94.5 | 100.5 | 96.9 | 95.8 | 100.0 | 99.9 | 96.9 | 96.8 | 95.2 | 96.6 | 92.7 |
| | Robo ya nne | 89.2 | 98.6 | 95.5 | 101.1 | 96.9 | 96.2 | 99.6 | 99.7 | 97.0 | 96.8 | 96.1 | 96.7 | 93.3 |
| 2015* | Robo ya kwanza | 93.5 | 98.8 | 97.0 | 101.6 | 97.4 | 96.6 | 97.5 | 99.8 | 97.1 | 98.6 | 97.6 | 97.4 | 95.7 |
| | Robo ya pili | 97.3 | 98.8 | 97.8 | 99.8 | 97.4 | 97.1 | 97.6 | 99.8 | 97.5 | 100.0 | 98.9 | 97.8 | 97.8 |
| | Robo ya tatu | 97.5 | 99.4 | 99.1 | 101.1 | 98.7 | 98.4 | 100.3 | 99.7 | 98.9 | 100.0 | 99.8 | 98.5 | 98.5 |
| | Robo ya nne | 98.9 | 99.8 | 99.7 | 100.9 | 99.3 | 99.5 | 99.8 | 100.0 | 100.1 | 100.0 | 100.0 | 99.8 | 99.4 |
| 2016 | Robo ya kwanza | 102.1 | 100.4 | 101.0 | 103.8 | 100.5 | 101.6 | 99.1 | 99.5 | 100.4 | 101.8 | 100.5 | 100.8 | 101.4 |
| | Robo ya pili | 104.2 | 103.2 | 101.9 | 107.3 | 101.5 | 103.2 | 98.9 | 98.8 | 100.9 | 102.3 | 103.6 | 101.4 | 103.0 |
| | Robo ya tatu | 103.9 | 104.4 | 102.8 | 107.8 | 101.9 | 104.0 | 99.8 | 99.1 | 101.2 | 102.6 | 104.4 | 101.9 | 103.3 |
| | Robo ya nne | 105.1 | 104.9 | 103.3 | 110.1 | 103.1 | 104.6 | 100.0 | 99.1 | 101.7 | 102.6 | 104.1 | 102.6 | 104.2 |
| 2017 | Robo ya kwanza | 111.4 | 105.5 | 104.4 | 112.5 | 104.2 | 105.3 | 100.0 | 98.7 | 101.5 | 102.9 | 104.3 | 103.4 | 107.1 |
| | Robo ya pili | 115.7 | 106.5 | 105.8 | 113.6 | 104.7 | 105.8 | 100.1 | 98.1 | 102.0 | 103.1 | 104.4 | 105.5 | 109.1 |
| | Robo ya tatu | 113.2 | 107.0 | 106.4 | 116.7 | 104.8 | 106.2 | 99.5 | 98.1 | 102.7 | 103.4 | 104.4 | 105.7 | 108.6 |
| | Robo ya nne | 112.9 | 107.5 | 106.5 | 118.8 | 105.1 | 106.7 | 100.1 | 98.1 | 103.2 | 103.5 | 104.5 | 105.4 | 108.9 |
| 2018 | Robo ya kwanza | 117.4 | 107.9 | 107.6 | 122.3 | 106.1 | 107.0 | 101.2 | 98.2 | 103.1 | 105.5 | 105.2 | 105.7 | 111.4 |
| | Robo ya pili | 119.4 | 107.6 | 108.3 | 128.7 | 107.1 | 107.3 | 101.9 | 97.3 | 102.8 | 105.6 | 105.3 | 106.8 | 113.1 |
| | Robo ya tatu | 115.9 | 108.4 | 109.4 | 131.4 | 107.8 | 107.5 | 102.4 | 95.5 | 102.7 | 106.0 | 105.7 | 107.0 | 112.2 |
| | Robo ya nne | 113.9 | 109.6 | 110.2 | 134.4 | 108.5 | 107.7 | 104.5 | 95.5 | 102.6 | 106.0 | 106.7 | 107.5 | 112.3 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP


**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Des 2015=100)**

Jedwali Na.15

| Mwaka | Robo ya Mwaka | | | | Wastani wa Fahirisi | Badiliko Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | | |
| 2000 | 33.2 | 33.0 | 31.8 | 32.3 | 32.6 | 6.0 |
| 2001 | 35.0 | 34.7 | 33.4 | 33.8 | 34.2 | 5.1 |
| 2002 | 35.4 | 35.6 | 35.5 | 36.3 | 35.7 | 4.3 |
| 2003 | 37.1 | 37.6 | 37.4 | 38.3 | 37.6 | 5.3 |
| 2004 | 39.0 | 39.0 | 39.1 | 40.4 | 39.4 | 4.7 |
| 2005 | 40.6 | 41.2 | 41.3 | 42.4 | 41.4 | 5.0 |
| 2006 | 43.8 | 44.9 | 43.7 | 45.1 | 44.4 | 7.3 |
| 2007 | 46.9 | 47.5 | 47.4 | 48.2 | 47.5 | 7.0 |
| 2008 | 51.1 | 51.9 | 52.3 | 54.2 | 52.4 | 10.3 |
| 2009 | 57.7 | 57.8 | 58.4 | 61.0 | 58.7 | 12.1 |
| 2010 | 61.3 | 62.1 | 61.9 | 62.4 | 61.9 | 5.5 |
| 2011 | 65.8 | 68.2 | 71.0 | 74.2 | 69.8 | 12.7 |
| 2012 | 78.6 | 80.5 | 81.4 | 83.4 | 81.0 | 16.0 |
| 2013 | 86.7 | 87.3 | 86.9 | 88.4 | 87.3 | 7.9 |
| 2014 | 91.9 | 92.9 | 92.7 | 93.3 | 92.7 | 6.1 |
| 2015* | 95.7 | 97.8 | 98.5 | 99.4 | 97.9 | 5.6 |
| 2016 | 101.4 | 103.0 | 103.3 | 104.2 | 102.9 | 5.2 |
| 2017 | 107.1 | 109.1 | 108.6 | 108.9 | 108.4 | 5.3 |
| 2018 | 111.4 | 113.1 | 112.2 | 112.3 | 112.2 | 3.5 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100


MWENENDO WA KASI YA UPANDAJI BEI - Tanzania Bara
Asilimia
18.0
16.0
14.0
12.0
10.0
8.0
6.0
4.0
2.0
0.0
16.0
7.9
6.1
5.6
5.2
5.3
3.5
2012
2013
2014
2015
2016
2017
2018

**FAHIRISI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA ( Des.2015=100)**

Jedwali Na.16

| Mwaka | F A H I R I S I | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA | B A D I L I K O % | | | WAKAZI MIJINI TANZ. BARA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | K I P A T O C H A | | | | K I P A T O C H A | | | |
| | CHINI | KATI | JUU | | CHINI | KATI | JUU | |
| 2000 | 23.8 | 27.9 | 24.9 | 32.6 | 1.7 | 2.5 | 6.2 | 6.0 |
| 2001 | 25.9 | 29.1 | 28.0 | 34.2 | 8.5 | 4.5 | 12.5 | 5.1 |
| 2002 | 26.9 | 30.2 | 28.9 | 35.7 | 3.8 | 3.5 | 3.3 | 4.3 |
| 2003 | 28.4 | 30.8 | 30.1 | 37.6 | 5.8 | 2.3 | 4.3 | 5.3 |
| 2004 | 30.2 | 33.4 | 32.0 | 39.4 | 6.4 | 8.2 | 6.2 | 4.7 |
| 2005 | 32.7 | 36.0 | 34.8 | 41.4 | 8.3 | 7.9 | 8.6 | 5.0 |
| 2006 | 36.5 | 39.3 | 38.9 | 44.4 | 11.5 | 9.2 | 11.8 | 7.3 |
| 2007 | 39.9 | 43.9 | 44.0 | 47.5 | 9.3 | 11.5 | 13.3 | 7.0 |
| 2008 | 46.8 | 50.6 | 52.1 | 52.4 | 17.3 | 15.3 | 18.3 | 10.3 |
| 2009 | 54.7 | 58.9 | 60.2 | 58.7 | 16.8 | 16.4 | 15.7 | 12.1 |
| 2010* | 61.9 | 64.8 | 65.1 | 61.9 | 13.2 | 10.0 | 8.1 | 5.5 |
| 2011 | 66.5 | 69.9 | 72.0 | 69.8 | 7.4 | 7.9 | 10.6 | 12.7 |
| 2012 | 79.0 | 81.5 | 80.0 | 81.0 | 18.8 | 16.6 | 11.2 | 16.0 |
| 2013 | 86.3 | 88.3 | 86.4 | 87.3 | 9.3 | 8.3 | 8.0 | 7.9 |
| 2014 | 93.0 | 93.7 | 91.6 | 92.7 | 7.7 | 6.2 | 6.0 | 6.1 |
| 2015* | 98.0 | 99.0 | 97.5 | 97.9 | 5.4 | 5.6 | 6.5 | 5.6 |
| 2016 | 102.2 | 103.5 | 102.2 | 102.9 | 4.3 | 4.5 | 4.8 | 5.2 |
| 2017 | 104.1 | 106.2 | 106.5 | 108.4 | 1.9 | 2.6 | 4.2 | 5.3 |
| 2018 | 106.1 | 108.2 | 111.5 | 112.2 | 2.0 | 1.9 | 4.7 | 3.5 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Des. 2015=100

## SURA YA 2

## FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

**Ujazi wa Fedha**

32. Mwaka 2018, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuna kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye uchumi kinachoendana na malengo mapana ya kiuchumi ya utulivu wa bei na kiwango cha juu cha ukuaji uchumi. Katika kipindi hicho, Benki Kuu iliendelea kufuatilia kwa ukaribu amana za benki zilizopo Benki Kuu ili kuhakikisha benki za biashara zina ukwasi wa kutosha kusaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kiuchumi. Aidha, Benki Kuu ilitumia njia mbalimbali kuongeza ukwasi kwenye uchumi ikiwemo kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki, kushusha kiwango cha riba ya mikopo kwa benki na kununua fedha za kigeni kutoka katika benki za biashara na taasisi za Serikali.

33. Hadi Desemba 2018, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka kwa asilimia 5.1 na kufikia shilingi bilioni 11,723.7 kutoka shilingi bilioni 11,155.3 Desemba 2017. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikuwa shilingi bilioni 19,040.4 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 18,349.9 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kutoka shilingi bilioni 24,714.3 mwaka 2017 hadi shilingi bilioni 25,823.5 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Ukuaji wa ujazi wa fedha ulibaki chini ya tarakimu moja kutokana na kupungua kwa rasilimali fedha za kigeni kwa asilimia 8.3 mwaka 2018. Kupungua kwa rasilimali fedha za kigeni kulichangiwa zaidi na kupungua kwa rasilimali za nje za Benki Kuu kutokana na ongezeko la malipo ya nje ya Serikali kufuatia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, malipo ya madeni ya nje na mauzo katika soko la jumla la fedha za kigeni.

**Mwenendo wa Mikopo kwa Serikali Kuu na Sekta Binafsi**

34. Mwaka 2018, mikopo kwa Serikali Kuu kutoka sekta ya benki iliongezeka kwa asilimia 36.8 kutokana na kuongezeka kwa mikopo kutoka Benki Kuu pamoja na matumizi ya amana za Serikali zilizoko Benki Kuu kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kutoka

shilingi bilioni 16,895.4 mwaka 2017 hadi shilingi bilioni 17,726.6 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 4.9 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 1.7 mwaka 2017. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kulichangiwa na jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya biashara, usimamizi thabiti wa sera ya fedha pamoja na kupungua kwa mikopo chechefu kwenye benki za biashara kulikotokana na matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji katika kuidhinisha mikopo. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli za watu binafsi ikifuatiwa na shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 27.2 na asilimia 18.2 ya mikopo yote kwa mtiririko huo.

**Amana Katika Benki za Biashara**

35. Mwaka 2018, amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 2.6 na kufikia shilingi bilioni 20,921.3 kutoka shilingi bilioni 20,385.1 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za benki za biashara kuhimiza wananchi kuweka fedha benki kwa kutumia vivutio mbalimbali vya akaunti, kuongeza matawi ya benki pamoja na matumizi ya wakala wa benki. Aidha, sekta binafsi ilikuwa na jumla ya shilingi bilioni 20,562.8, sawa na asilimia 98.3 ya amana zote. Katika kipindi hicho, uwiano wa amana za fedha za kigeni ukilinganishwa na amana zote uliongezeka kutoka asilimia 29.9 mwaka 2017 hadi asilimia 30.5 mwaka 2018.

**Mwenendo wa Viwango vya Riba**

36. Riba za mikopo kwa ujumla zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 17.42 mwaka 2018 kutoka wastani wa asilimia 17.77 kwa mwaka 2017. Katika kipindi hicho, riba za mikopo ya mwaka mmoja zilipungua hadi wastani wa asilimia 17.83 kutoka asilimia 18.54 mwaka 2017. Riba za amana za muda maalum zilifikia wastani wa asilimia 8.24 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 10.04 mwaka 2017. Aidha, riba za amana za mwaka mmoja zilipungua hadi wastani wa asilimia 8.78 kutoka asilimia 11.66 mwaka 2017. Kupungua kwa riba za mikopo kulitokana na jitihada mbalimbali za Serikali kupitia Benki Kuu kupunguza mikopo chechefu pamoja na kuhakikisha kuna ukwasi wa kutosha katika benki. Kufuatia mwenendo huo, tofauti ya viwango vya riba ya kukopa na ya amana ya mwaka mmoja iliongezeka na kufikia nukta ya asilimia 9.05 mwaka 2018 kutoka asilimia 6.88 mwaka 2017. Kwa upande mwingine, riba baina ya benki ilipungua hadi asilimia 2.21 mwaka 2018 kutoka asilimia 6.0

mwaka 2017. Vile vile, riba za dhamana za Serikali zilipungua hadi wastani wa asilimia 6.43 mwaka 2018 kutoka wastani wa asilimia 11.10 mwaka 2017.

## MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA

### Huduma za Benki

37. Katika kurahisisha upatikanaji wa huduma za kibenki nchini, benki za biashara ziliongeza matawi yake kufikia 878 hadi Desemba 2018 kutoka matawi 821 Desemba 2017. Mwaka 2018, hali ya ukwasi katika sekta ya benki iliendelea kuwa juu ya ukomo unaokubalika kisheria. Uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi ulipungua hadi asilimia 35.6 Desemba 2018 kutoka asilimia 40.3 Desemba 2017, kiasi ambacho ni zaidi ya uwiano wa chini wa asilimia 20 unaohitajika kisheria. Aidha, uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki ulipungua hadi asilimia 18.2 Desemba 2018 kutoka asilimia 18.9 Desemba 2017, kiasi ambacho ni zaidi ya uwiano wa chini unaohitajika kisheria ambao ni asilimia 10.

38. Hadi kufikia Desemba 2018, benki 17 zilitoa huduma kwa njia ya uwakala ikilinganishwa na benki 16 mwaka 2017. Mawakala wa benki waliongezeka na kufikia 18,827 Desemba 2018 kutoka mawakala 10,665 Desemba 2017, sawa na ongezeko la asilimia 76.5 . Aidha, miamala ya kuweka amana kupitia huduma za benki kwa njia ya uwakala iliongezeka kutoka 9,911,695 yenye thamani ya shilingi bilioni 4,638.6 Desemba 2017 hadi miamala 18,034,023 yenye thamani ya shilingi bilioni 10,278.30 Desemba 2018, sawa na ongezeko la miamala la asilimia 81.9. Katika kipindi hicho, miamala ya kutoa fedha ilikuwa 9,784,192 yenye thamani ya shilingi bilioni 3,070.48 ikilinganishwa na miamala 4,075,195 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,106.40 Desemba 2017.

### Maendeleo ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

39. Hadi Desemba 2018, kampuni 28 ziliorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ikilinganishwa na kampuni 26 Desemba 2017. Hii ilitokana na kuorodheshwa kwa Kampuni ya Usimamizi wa Uwekezaji (National Investment Company Limited - NICOL) na Kampuni ya uwekezaji ya Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA Investment Limited). Kati ya kampuni ziliorodheshwa, 21 zilikuwa za ndani na kampuni 7 zilikuwa za nje. Hadi kufikia Desemba 2018, idadi ya wawekezaji katika soko la mitaji iliongezeka na kufikia 672,209 kutoka wawekezaji 524,277 mwaka 2017, sawa

na ongezeko la asilimia 28.2. Ongezeko hilo, lilitokana na kuongezeka kwa fursa za kununua hisa kwenye soko  na kuorodheshwa kwa kampuni za *NICOL* na *TCCIA.*

40. Mwaka 2018, hisa 304,215,411 zenye thamani ya shilingi bilioni 504.82 ziliuzwa na kununuliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ikilinganishwa na hisa 328,552,495 zenye thamani ya shilingi bilioni 418.96 mwaka 2017, sawa na ongezeko la thamani la asilimia 20.5. Aidha, hatifungani za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 1,221.24 zilinunuliwa na kuuzwa katika soko la upili ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 683.17 zilizouzwa na kununuliwa katika kipindi kilichoishia Desemba 2017, sawa na ongezeko la asilimia 78.8. Vile vile,  Soko liliorodhesha hatifungani zenye thamani ya shilingi trilioni 9.11 ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi trilioni 7.71 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 18.2. Kwa upande wa hatifungani za kampuni, katika kipindi kilichoishia Desemba 2018, hatifungani za kampuni zenye thamani ya shilingi bilioni 134.88 ziliorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 98.1 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 37.5. Ongezeko hilo lilitokana na kuorodheshwa kwa toleo la kwanza la hatifungani ya Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Tanzania, (TMRC).

41. Mwaka 2018, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilikuwa shilingi milioni 281,668.39 ikilinganishwa na shilingi milioni 256,480.40 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mifuko ya Ukwasi kwa asilimia 153.0 na Umoja asilimia 1.9. Hata hivyo, thamani ya mfuko wa uwekezaji wa Jikimu ilipungua kutoka shilingi milioni 21,687.04 mwaka 2017 hadi shilingi milioni 20,280.46 mwaka 2018 , sawa na upungufu wa asilimia 6.5. Kupungua kwa thamani ya mfuko huu kulitokana na kushuka kwa thamani ya hisa za Kampuni ambazo mfuko  uliwekeza. Aidha, thamani ya mfuko wa Wekeza Maisha ilipungua kutoka shilingi milioni 1,488.96 mwaka 2017 hadi shilingi milioni 1,193.82 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 19.8. Upungufu huo ulitokana na Mfuko kufikia ukomo wake wa miaka kumi na hivyo, kuvunjwa kama taratibu za mfuko zinavyoelekeza. Thamani ya Mfuko wa Watoto ilipungua na kufikia shilingi milioni 3,154.30 mwaka 2018 kutoka shilingi milioni 3,532.13 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 10.7. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa thamani ya hisa za kampuni ambazo Mfuko uliwekeza. Mchanganuo wa

thamani ya Uwekezaji wa Pamoja ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.1.**

**Jedwali Na.2.1:Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (Shs. Milioni)**

| Aina ya Uwekezaji | 2016 | 2017 | 2018 | Ukuaji (%) |
|---|---|---|---|---|
| Umoja | 210,443.15 | 214,658.83 | 218,809.27 | 1.9 |
| Jikimu | 25,451.02 | 21,687.04 | 20,280.46 | -6.5 |
| Wekeza | 3,671.93 | 1,488.96 | 1,193.82 | -19.8 |
| Watoto | 3,301.31 | 3,532.13 | 3,154.30 | -10.7 |
| Ukwasi | 8,155.95 | 15,113.44 | 38,230.54 | 153.0 |
| **Jumla** | **251,023.36** | **256,480.40** | **281,668.39** | **9.8** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

**Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)**

42. Mwaka 2017/18, wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii waliongezeka hadi kufikia 1,351,517 kutoka wanachama 1,322,206 mwaka 2016/17. Katika kipindi hicho, thamani ya mali za mifuko ya hifadhi ya jamii ilikuwa shilingi trilioni 12.84 ikilinganishwa na shilingi trilioni 11.68 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 9.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kupanda kwa thamani ya uwekezaji. Aidha, idadi ya wastaafu waliopokea pensheni ya kila mwezi ilikuwa 152,605. Mapato yaliyotokana na michango ya wanachama yalipungua kufikia shilingi trilioni 2.67 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.72 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 1.8. Upungufu huu ulitokana na baadhi ya waajiri kutowasilisha michango ya wanachama kwa wakati.

43. Mifuko ya hifadhi ya jamii iliendelea kuwekeza katika miradi mikubwa ya kimkakati ambapo kufikia mwaka 2017/18 uwekezaji wa miradi ya kimkakati ulifikia shilingi bilioni 51.59. Miradi hiyo ni pamoja na kiwanda cha sukari cha Mkulazi mkoani Morogoro, kiwanda cha ngozi cha karanga mkoani Kilimanjaro, kiwanda cha kusindika nyama cha Nguru Ranch mkoani Morogoro na kiwanda cha viwatilifu Kibaha.

44. Mwaka 2018, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (The Public Service Social Security Fund Act). Sheria hii, iliiunganisha Mifuko minne ya

Pensheni ambayo ni Mfuko wa Pensheni wa PSPF, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa LAPF, Mfuko wa Pensheni wa PPF, na Mfuko wa Mafao ya Kustaafu GEPF na kuunda Mfuko mmoja wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (Public Service Social Security Fund - PSSSF). Aidha, Sheria hii ilihusisha maboresho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Sura ya 50 na kuufanya Mfuko huo kuwa Mfuko wa wafanyakazi wa sekta binafsi pamoja na sekta isiyo rasmi. Uamuzi wa kuunganisha Mifuko ulilenga kutatua changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na: ushindani usiokuwa na tija baina ya mifuko iliyokuwepo; gharama kubwa za uendeshaji; na mifuko kuwa chini ya mamlaka za wizara tofauti.

**Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)**

45. Mwaka 2018, Serikali ilianzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwa Sheria Na.2 ya Mwaka 2018. Mfuko huu ulitokana na kuunganishwa kwa mifuko ya PSPF, PPF, LAPF na GEPF na ulianza kufanya kazi rasmi tarehe 1 Agosti 2018. Kazi zilizofanywa na Mfuko katika kipindi hicho zililenga katika kutekeleza malengo makuu yaliyoainishwa kwenye sheria iliyoanzisha Mfuko yakiwemo kuandikisha wanachama, kukusanya michango, uwekezaji na kulipa mafao kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyounda Mfuko. Hadi Desemba 2018, Mfuko ulisajili wanachama wapya 6,705 na kukusanya shilingi bilioni 588.51 kutokana na michango ya wanachama. Aidha, Mfuko ulilipa shilingi bilioni 888.40 kwa wastaafu na wategemezi 9,971 waliorithiwa kutoka katika mifuko iliyounganishwa. Katika kipindi hicho, Mfuko uliendelea kulipa mafao kwa mujibu wa sheria ambapo mafao yenye thamani ya shilingi bilioni 321.39 yalilipwa kwa wanachama 12,124.

46. Mwaka 2018, Mfuko ulipata shilingi bilioni 186.70 kutokana na uwekezaji. Shughuli za uwekezaji katika Mfuko zilifanywa kwa mujibu wa Sheria ya PSSSF na Sera ya Uwekezaji ya Mfuko ambayo inaratibiwa na Benki Kuu ya Tanzania na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii (SSRA). Hadi Julai 2018, thamani ya rasilimali na uwekezaji wa Mfuko ilikuwa shilingi trilioni 5.8.

**Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

47. Mwaka 2017/18, wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii waliongezeka kwa asilimia 19.1 na kufikia jumla ya wanachama 1,297,299

kutoka wanachama 1,087,229 mwaka 2016/17. Aidha, michango iliyokusanywa kutoka kwa wanachama wa Mfuko ilikuwa na thamani ya shilingi milioni 728,736.26 ikilinganishwa na shilingi milioni 736,405.01 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 1.04. Kupungua kwa michango kulitokana na wanachama 23,743 kujitoa na wanachama 17,350 kustaafu.

48. Mwaka 2017/18, mafao yenye thamani ya shilingi milioni 402,477.43 yalilipwa kwa wanachama ikilinganishwa na shilingi milioni 248,118.15 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 62.2. Aidha, wanachama waliolipwa mafao hayo walikuwa 48,388 ikilinganishwa na wanachama 45,143 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 7.2.

49. Thamani ya uwekezaji katika vitega-uchumi ilikuwa shilingi bilioni 2,418.77 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,333.98 mwaka 2016/17. Aidha, thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali ilikuwa shilingi bilioni 340.48 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 311.21 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Vile vile, mapato yaliyotokana na uwekezaji katika vitega uchumi yalikuwa shilingi bilioni 193.75 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 207.12 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 6.5. Kwa upande mwingine, rasilimali za Mfuko zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 3,433.25 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3,408.58 mwaka 2016/17. Aidha, rasilimali halisi za Mfuko zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 3,192.32 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3,119.62 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 2.3

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)**

50. Hadi kufikia Desemba 2018, waajiri 17,845 kutoka katika sekta binafsi na umma walisajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ikilinganishwa na waajiri 12,282 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 45.3. Ongezeko hilo, lilichangiwa na utoaji elimu kwa waajiri, wafanyakazi na wadau mbalimbali pamoja na kufanya kaguzi. Kutokana na ongezeko hilo la waajiri, michango iliongezeka kutoka shilingi bilioni 81.80 mwaka 2017 hadi shilingi bilioni 100.92 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 23.4. Katika kipindi hicho, Mfuko ulitumia shilingi bilioni 2.21 kulipia matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia ama kufariki wakiwa kazini ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.76

mwaka 2017, sawa na ongezeko la asimilia 25.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa madai ya wafanyakazi walioumia, kuugua ama kufariki wakiwa kazini.

51. Mwaka 2018, Mfuko uliwekeza shilingi bilioni 91.72 ikilinganishwa na shilingi bilioni 70.46 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 30.2. Ongezeko hilo lilitokana na uwepo wa ziada iliyotokana na michango iliyowasilishwa na waajiri. Aidha, Mfuko uliendelea kuwekeza kwenye dhamana za Serikali, amana za benki na Soko la Hisa. Hadi kufikia Desemba 2018, shilingi bilioni 21.39 zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya uwekezaji wa Mfuko ikilinganishwa na shilingi bilioni 16.35 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Vile vile, thamani ya rasilimali halisi za Mfuko ilikuwa shilingi bilioni 259.57 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 138.16 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 87.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa makusanyo ya michango na mapato ya uwekezaji.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

52. Mwaka 2017/18, wanachama wachangiaji kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya walikuwa 858,446 ikilinganishwa na wanachama 753,832 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 13.9. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za Mfuko kuyafikia makundi mbalimbali katika jamii kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya bima ya afya kwa wote. Katika kipindi hicho, kaya 2,251,055 ziliandikishwa kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ikilinganishwa na kaya 2,030,666 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 10.9.

53. Mwaka 2017/18, Mfuko ulihudumia wanufaika 17,425,329 ikilinganishwa na wanufaika 15,675,396 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 11.2. Idadi hiyo ya wanufaika ni sawa na asilimia 33 ya wananchi wote Tanzania bara. Kati ya hao, wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya walikuwa 3,918,999 na wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii walikuwa 13,506,330 . Katika kipindi hicho, shilingi milioni 371,043.00 zililipwa kwa watoa huduma ikilinganishwa na shilingi milioni 303,818.99 zilizolipwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 22.1. Ongezeko hilo lilitokana na Mfuko kuboresha mafao yanayotolewa kwa wanachama pamoja na kuongezeka kwa huduma za upasuaji hasa wa moyo ambazo ni ghali zaidi.

54. Mwaka 2017/18, mapato ya Mfuko yalikuwa shilingi milioni 488,595.90 ikilinganishwa na shilingi milioni 478,971.38 mwaka 2016/17, sawa na

ongezeko la asilimia 2.0. Kati ya mapato hayo, michango ya wanachama ilikuwa shilingi milioni 383,562.36 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi milioni 367,634.47 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Aidha, michango ya wanachama ilikuwa asilimia 78.5 ya mapato yote ikifuatiwa na mapato ya vitega uchumi asilimia 21.3 na mapato mengineyo asilimia 0.2. Hadi mwaka 2017/18, rasilimali halisi za Mfuko zilifikia shilingi bilioni 1,307.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,300.4 mwaka 2016/17. Kwa upande mwingine, vituo vya afya vilivyosajiliwa na Mfuko vilifikia 7,465 ikilinganishwa na vituo 7,140 mwaka 2016/17, sawa na ongezekao la asilimia 4.6.

**Jedwali Na 2.2: Mchanganuo Vituo vya Afya Vilivyosajiliwa na Mfuko mwaka 2017/18**

| Aina ya Vituo | Serikali | Mashirika ya Dini | Binafsi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Hospitali za Taifa | 13 | 3 | 3 | 19 |
| Hospitali za Rufaa Kikanda | 2 | 5 | 6 | 13 |
| Hospitali za Mikoa | 27 | 15 | 15 | 57 |
| Hospitali za Wilaya | 91 | 20 | 96 | 207 |
| Vituo vya Afya | 485 | 101 | 170 | 756 |
| Zahanati | 4,934 | 329 | 407 | 5,670 |
| Maduka ya Madawa | 13 | 395 | 8 | 416 |
| ADDO | - | 207 | - | 207 |
| Kliniki Maalum | - | 101 | 10 | 11 |
| Vituo vya uchunguzi wa Magonjwa | - | 7 | 1 | 8 |
| *Evacuating facility* | - | 1 | - | 1 |
| **Jumla** | **5,565** | **1,184** | **716** | **7,465** |

**Chanzo:** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

**Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA)**

55. Mwaka 2018, kampuni zilizoandikishwa kufanya biashara ya bima nchini zilikuwa 31 ikijumuisha kampuni moja ya bima mtawanyo. Aidha, madalali 109, mawakala wa bima 614 na wakadiriaji hasara za bima 54 waliandikishwa kufanya biashara ya bima ikilinganishwa na madalali 152, mawakala 596 na wakadiriaji hasara 55 mwaka 2017. Vile vile, hati za bima zilizotolewa na

kampuni za bima kwa wananchi ziliongezeka na kufikia 2,745,584 mwaka 2018 ikilinganishwa na hati 2,548,553 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.7.

56. Mwaka 2018, mauzo ya soko la bima yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 691.06 ikilinganishwa na shilingi bilioni 637.14 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Katika kipindi hicho, bima za kawaida zilichangia asilimia 84.91 ya mauzo yote ya bima na bima za maisha zilichangia asilimia 15.09. Aidha, mauzo ya bima za kawaida yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 586.76 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 556.30 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Vile vile, mauzo ya bima za maisha yalikuwa shilingi bilioni 104.30 mwaka 2018, ikilinganishwa na shilingi bilioni 80.84 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 29.0. Ongezeko hilo lilitokana na kutolewa kwa elimu ya bima kwa umma pamoja na kutumia mfumo wa kielekroniki wa kuhakiki bima ya vyombo vya moto.

**Jedwali Na. 2.3: Mwenendo wa Mauzo ya Bima (Shilingi milioni)**

| Mauzo | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mauzo - Bima za Kawaida** | 493,981 | 550,168 | 585,789 | 556,298 | 586,762 |
| Ukuaji (Asilimia) | 18.3 | 11.4 | 6.5 | -5.0 | 5.5 |
| Mchango kwa Jumla (Asilimia ) | 89.1 | 88.9 | 88.7 | 87.3 | 84.9 |
| **Mauzo - Bima za Maisha** | 60,420 | 68,691 | 74,909 | 80,843 | 104,297 |
| Ukuaji (Asilimia) | 7.1 | 13.7 | 9.1 | 7.9 | 29.0 |
| Mchango kwa Jumla (Asilimia) | 10.9 | 11.1 | 11.3 | 12.7 | 15.1 |
| **Jumla ya Mauzo** | 554,401 | 618,859 | 660,698 | 637,141 | 691,059 |
| Ukuaji (Asilimia) | 16.94 | 11.63 | 6.76 | -3.57 | 8.46 |

**Chanzo**: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

57. Mwaka 2018, kampuni za bima za kawaida zilipata faida yenye thamani ya shilingi bilioni 20.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.8 mwaka 2017. Kuongezeka kwa faida kulitokana na kupanda kwa ada za bima. Katika kipindi hicho, thamani ya mali za kampuni za bima ilikuwa shilingi bilioni 920.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 862.6 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 6.7. Aidha, madeni ya kampuni za bima yalifikia shilingi bilioni 631.2 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 586.5 mwaka 2017, sawa na

ongezeko la asilimia 7.6. Tofauti kati ya mali na madeni ya kampuni za bima ilikuwa shilingi bilioni 289.6 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 276.1 mwaka 2017.

**Jedwali Na. 2.4**: **Thamani ya Mali na Madeni ya Kampuni za Bima (Shilingi Milioni)**

| Mali na Madeni | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Mali | 619,979 | 729,025 | 824,290 | 862,618 | 920,816 |
| Ukuaji (asilimia) | 19 | 18 | 13 | 5 | 7 |
| Jumla ya Madeni | 401,665 | 484,059 | 559,128 | 586,480 | 631,151 |
| Ukuaji (asilimia) | 17 | 21 | 16 | 5 | 8 |
| Ziada ya Mali (Networth) | 218,314 | 244,966 | 265,162 | 276,138 | 289,665 |
| Ukuaji (asilimia ) | 25 | 12 | 8 | 4 | 5 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

**Mwenendo wa Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania**

58. Mwaka 2018, mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi bilioni 421.07 ilitolewa na sekta ya benki na taasisi za fedha ikilinganishwa na shilingi bilioni 344 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 22.4. Ongezeko hilo lilitokana na matokeo chanya ya utekelezaji wa sera ya fedha na matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji. Mikopo hiyo ilitolewa kwa riba ya kuanzia asilimia 15 hadi 19 mwaka 2018 ikilinganishwa na riba ya kuanzia asilimia 22 hadi 24 mwaka 2010. Katika kipindi hicho, benki na taasisi za fedha 32 zilitoa mikopo ya nyumba ikilinganishwa na benki na taasisi za fedha 31 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na Benki ya Maendeleo Plc kuingia kwenye soko la mikopo ya nyumba. Aidha, asilimia 70.1 ya soko la mikopo ya nyumba ilimilikiwa na; CRDB Bank Plc (asilimia 40.9), Stanbic Bank (asilimia 14.2), Azania Bank (asilimia 6.8), Commercial Bank of Africa (asilimia 4.4) na First National Bank Tanzania Ltd (asilimia 3.8).

**Jedwali Na. 2.5: Mchanganuo wa Utoaji wa Mikopo ya Nyumba hadi Desemba 2018**

| Mkopeshaji | Idadi ya Wateja | Thamani ya Mikopo (Shs.Bilioni) | Miliki ya Soko (%) |
|---|---|---|---|
| CRDB Bank Plc | 1,461 | 172.28 | 40.92 |
| Stanbic Bank (T) Ltd | 188 | 59.78 | 14.20 |
| Azania Bank Limited | 491 | 28.71 | 6.82 |
| Commercial Bank of Africa (T) Limited | 107 | 18.53 | 4.40 |
| First National Bank Tanzania Limited | 92 | 15.89 | 3.77 |
| NMB Bank Plc. | 119 | 15.33 | 3.64 |
| DCB Commercial Bank Plc | 662 | 9.28 | 2.20 |
| Bank of Africa Tanzania Limited | 105 | 9.23 | 2.19 |
| Bank M Tanzania Public Limited Company | 7 | 8.40 | 1.99 |
| Letshego Bank (T) Limited | 161 | 8.21 | 1.95 |
| Amana Bank Limited | 118 | 7.98 | 1.90 |
| Barclays Bank (T) Limited | 57 | 7.93 | 1.88 |
| NIC Bank Tanzania Limited | 18 | 7.52 | 1.79 |
| NBC Limited | 53 | 6.05 | 1.44 |
| I & M Bank Tanzania Limited | 35 | 5.59 | 1.33 |
| KCB Bank Tanzania Limited | 49 | 5.18 | 1.23 |
| Peoples Bank Of Zanzibar | 23 | 5.11 | 1.21 |
| Equity Bank Tanzania Limited | 14 | 4.67 | 1.11 |
| African Banking Corporation (T) Ltd | 39 | 4.59 | 1.09 |
| Standard Chartered Bank (T) Ltd | 21 | 4.44 | 1.05 |
| Exim Bank Tanzania Limited | 40 | 3.01 | 0.71 |
| Yetu Microfinance Plc | 513 | 2.03 | 0.48 |
| Akiba Commercial Bank Ltd | 314 | 1.91 | 0.45 |
| Diamond Trust Bank (T) Ltd. | 7 | 1.76 | 0.42 |
| TIB Corporate Bank Limited | 14 | 1.72 | 0.41 |
| Efc M.F.B Tanzania Limited | 80 | 1.71 | 0.40 |
| Citibank Tanzania Limited | 8 | 1.08 | 0.26 |
| TIB Development Bank Limited | 9 | 1.01 | 0.24 |
| 1st Housing Finance | 6 | 0.83 | 0.20 |
| Mucoba Bank Plc | 144 | 0.72 | 0.17 |
| International Commercial Bank (T) Ltd. | 2 | 0.38 | 0.09 |
| Maendeleo Bank Plc | 39 | 0.23 | 0.06 |
| **Jumla** | **4,996** | **421.07** | **100.00** |

**Chanzo:** Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Nchini

59. Mwaka 2018, Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Nchini ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 102.1 kwa benki 11 ambazo ni wanachama na benki nne ambazo sio wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 91.1 mwaka 2017,

sawa na ongezeko la asilimia 12.1. Mikopo iliyotolewa ilikuwa ni asilimia 24 ya jumla ya mikopo yote ya nyumba nchini ikilinganishwa na asilimia 26.4 mwaka 2017. Aidha, mikopo iliyotolewa kupitia Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba ulio chini ya Kampuni ya Mikopo ya Nyumba ilikuwa shilingi bilioni 17.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.5 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 55.7.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB)**

60. Mwaka 2018, Benki ya Maendeleo ya KilimoTanzania ilikuwa na mtaji wa shilingi bilioni 67.09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 67.53 mwaka 2017. Aidha, Benki ilipata faida ya shilingi bilioni 1.93 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.79 mwaka 2017. Vile vile, mikopo iliyotolewa na benki mwaka 2018 ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 284.57 na hivyo kufanya mikopo iliyotolewa kufikia shilingi bilioni 295.04 tangu kuanza kwa utoaji wa mikopo mwaka 2016. Ongezeko la utoaji wa mikopo lilitokana na Benki kuongeza wigo wa huduma zake kwa kufungua ofisi mbili za kanda. Ofisi ya Kanda ya Ziwa inayohudumia mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu, Shinyanga na Geita na ofisi ya Kanda ya Kati inayohudumia mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida. Kati ya mikopo iliyotolewa, kiwango kikubwa kilielekezwa katika ununuzi wa zao la kahawa na korosho. Mikopo hiyo iliwanufaisha wakulima 1,994,726 ikilinganishwa na wakulima 2,202 mwaka 2017. Kati ya mikopo iliyotolewa, shilingi bilioni 8.68 zilielekezwa kwenye miradi 6 ya umwagiliaji wa mazao ya mahindi, mpunga, na mbogamboga iliyofanywa na vyama vya wakulima wadogo katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Tanga pamoja na mradi mkubwa wa mazao ya nafaka uliopo Kagera.

**Jedwali Na. 2.6 Mchanganuo wa Mikopo (Shs. Bilioni)**

| **Mwaka** | **kiasi kilichoidhinishwa** | **Kiasi kilichotolewa** |
|---|---|---|
| 2016 | 6.5 | 2.64 |
| 2017 | 24.5 | 7.83 |
| 2018 | 324.5 | 284.57 |
| **Jumla** | **355.5** | **295.04** |

**Chanzo -** Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania

61. Mwaka 2018, Benki ilifanikiwa kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo, wafugaji na wavuvi wapatao 7,469 katika mikoa mbalimbali na kufanya jumla ya wakulima waliopatiwa mafunzo kufikia 20,399 tangu benki ilipoanza kutoa huduma za mafunzo kwa wakulima mwaka 2016. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga kuwajengea uwezo wakulima katika usimamizi wa fedha, kuratibu vikundi na vyama, utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa miradi inayokidhi masharti ya mikopo kutoka benki na taasisi za fedha.

62. Mwaka 2018, Benki iliendelea kuratibu upatikanaji wa fedha za uwekezaji kwenye sekta ya kilimo kwa kusaini mkataba na Serikali pamoja na Programu ya MIVARF. Mikataba hiyo iliiwezesha Benki kupata ridhaa ya kusimamia miradi miwili mikubwa ya kilimo ambayo ni Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (Smallholder Farmers Credit Guarantee Scheme - SCGS) na Mfuko wa Kuwezesha Ubunifu Vijijini (Rural Innovation Fund - RIF). Hadi Desemba 2018, Mfuko wa SCGS ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.3 kupitia benki za NMB na TPB. Kwa upande mwingine, Mfuko wa RIF, ulipokea maombi 117 ya ufadhili yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 90 ambayo yameshafanyiwa uchambuzi na yanasubiri uundwaji wa Kamati ya Utendaji wa Mfuko ili yafanyiwe maamuzi.

**Benki ya TPB**

63. Mwaka 2018, matawi ya Benki ya TPB yaliongezeka na kufikia 36 kutoka matawi 30 mwaka 2017. Aidha, matawi madogo ya benki yaliongezeka na kufikia 40 kutoka matawi 36 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Ongezeko hilo lilichangiwa na benki kuendelea kutoa huduma kupitia ofisi za Shirika la Posta Tanzania ili kupanua wigo wa biashara na kupeleka huduma jirani na wananchi. Aidha, Benki iliendelea kutoa huduma zake kupitia mashine 304 za ATM ikilinganishwa na mashine 238 za ATM mwaka 2017. Kati ya hizo, ATM 72 zilikuwa mali ya Benki ya Posta ikilinganishwa na ATM 51 mwaka 2017.

64. Mwaka 2018, amana za wateja ziliongezeka na kufikia shilingi milioni 446,111 kutoka shilingi milioni 382,558 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 16.6. Aidha, idadi ya wateja ilifikia 576,264 Desemba 2018 ambapo wateja wapya walikuwa 65,240. Kuongezeka kwa wateja wapya kulitokana na

benki kuwafuata wananchi katika maeneo ya vyuo, shule na vikundi vya kuweka na kukopa na kuwaingiza katika mfumo wa kuweka amana na kupata mikopo midogo midogo.

65. Mwaka 2018, uwekezaji wa Benki katika dhamana za Serikali ulikuwa shilingi milioni 56,819 ikilinganishwa na shilingi milioni 61,764 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 8.0. Upungufu huo ulitokana na ongezeko kubwa la mahitaji ya mikopo sambamba na ukuaji mdogo wa amana za wateja. Katika kipindi hicho, Benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 408,459 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 336,802 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 21.3. Ongezeko hilo lilitokana na Benki ya Twiga na Benki ya Wanawake Tanzania kuunganishwa na Benki ya Posta. Katika kipindi hicho, kiwango cha mikopo chechefu kiliongezeka na kufikia asilimia 6.9 kutoka asilimia 6.1 mwaka 2017. Ongezeko la mikopo chechefu lilitokana na Benki ya TPB kuunganishwa na Benki ya Twiga na Benki ya Wanawake zilizokuwa zimeathiriwa vibaya na mikopo chechefu. Kwa upande mwingine, kuungana kwa Benki ya TPB na Benki ya Twiga pamoja na Benki ya Wanawake kulichangia mtaji kuongezeka hadi shilingi bilioni 76 mwaka 2018 kutoka shilingi bilioni 60 mwaka 2017.

66. Mwaka 2018, Benki ilizalisha pato ghafi la shilingi milioni 117,400 ikilinganishwa na shilingi milioni 107,964 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Ongezeko hilo lilitokana na uongozi wa Benki kuendelea kusimamia kwa uangalifu matumizi katika shughuli zake, kuongezeka kwa uwekezaji katika mikopo pamoja na kukua kwa wigo wa huduma na bidhaa zinazozalisha mapato.

**Mfuko wa SELF**

67. Mwaka 2017/18, Mfuko wa SELF ulikuwa na mtaji wa shilingi bilioni 60.63 ikilinganishwa na shilingi bilioni 58.94 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Aidha, Mfuko uliendelea kutoa huduma ya mikopo yenye masharti nafuu pamoja na mafunzo kwa wajasiriamali wadogo hususan vijijini. Kwa upande mwingine, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 20.36 ilitolewa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na shilingi billion 13.10 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 55.4. Ongezeko hilo lilitokana na Mfuko kufanya kazi na asasi zenye mitandao mikubwa ya kuwafikia wananchi wengi waishio mijini na vijijini. Vile vile, wajasiriamali 15,276 walinufaika na mikopo

kutoka Mfuko wa SELF ikilinganishwa na wajasilimali 11,653 mwaka 2016/17. Kati ya wanufaika hao, wanawake walikuwa 8,613 sawa na asilimia 56 na wanaume walikuwa 6,663. Kiwango cha urejeshaji mikopo kiliongezeka na kufikia asilimia 93 ikilinganishwa na asilimia 88 mwaka 2016/17. Ongezeko hilo lilitokana na utoaji wa mikopo kwa wakopaji wenye sifa stahiki, ufuatiliaji wa kina na kuhakikisha kila mkopo uliotolewa una dhamana.

**Jedwali Na. 2.7: Mchanganuo wa Mtaji wa Mfuko wa SELF (Shilingi Bilioni)**

| Eneo la Uwekezaji | 2016/17 | 2017/18 | Ukuaji (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Fedha Taslimu Benki | 0.93 | 11.99 | 1189.24 |
| Kasma ya mikopo | 11.33 | 18.24 | 60.98 |
| Uwekezaji katika Amana za Serikali | 46.68 | 30.40 | (34.87) |
| **Jumla** | **58.94** | **60.63** | **2.86** |

**Chanzo:** Mfuko wa SELF

68. Mwaka 2017/18, Mfuko uliendelea kuwekeza kwenye vyanzo mbalimbali vikiwemo mikopo na uwekezaji katika dhamana za Serikali. Aidha, Mfuko ulikuwa na mapato ya shilingi bilioni 5.19 ikilinganishwa na shilingi bilioni 7.47 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 30.5. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa riba za dhamana za Serikali.

**Jedwali Na. 2.8: Vyanzo vya Mapato ya Mfuko wa SELF (Shilingi Bilioni)**

| Vyanzo vya Mapato | 2016/17 | 2017/18 | Ukuaji (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Mikopo | 1.48 | 1.96 | 32.43 |
| Uwekezaji katika Amana za Serikali | 5.73 | 2.90 | (49.38) |
| Mapato mengineyo | 0.26 | 0.33 | 26.92 |
| Ruzuku kutoka Serikalini | - | - | - |
| **Jumla** | **7.47** | **5.19** | **(30.53)** |

**Chanzo:** Mfuko wa SELF

**MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

Jedwali Na. 17 **Sh. Bilioni**

| | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba | | | | | | | Badiliko 2016/17 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Kiasi | % |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **4,525.6** | **5,027.8** | **5,909.5** | **6,833.1** | **6,854.4** | **6,954.4** | **6,992.9** | **38.5** | 0.6 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **6,538.6** | **7,218.1** | **8,284.2** | **9,575.7** | **10,083.8** | **11,155.3** | **11,723.7** | **568.4** | 5.1 |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 4,186.0 | 4,672.4 | 5,632.9 | 6,204.4 | 6,536.5 | 7,194.6 | 7,316.7 | 122.1 | 1.7 |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **10,724.5** | **11,890.6** | **13,917.0** | **15,780.1** | **16,620.3** | **18,349.9** | **19,040.4** | 690.5 | 3.8 |
| Amana za fedha za kigeni | 3,922.6 | 4,216.2 | 4,697.1 | 6,335.2 | 6257.5 | 6364.4 | 6783.1 | 418.7 | 6.6 |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **14,647.1** | **16,106.8** | **18,614.2** | **22,115.3** | **22,877.8** | **24,714.3** | **25,823.5** | 1,109.2 | 4.5 |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **6,396.0** | **6,576.3** | **6,551.5** | **8,244.0** | **8186.3** | **11596.1** | **10629.8** | **-966.3** | -8.3 |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **8,251.1** | **9,530.4** | **12,062.6** | **13,871.3** | **14,691.6** | **13,118.2** | **15,193.7** | 2,075.5 | 15.8 |
| Karadha Nchini | 13,719.0 | 16,293.0 | 18,863.7 | 22,505.5 | 23,775.8 | 24,977.2 | 26,249.3 | 1,272.1 | 5.1 |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 2,019.4 | 2,554.6 | 3,651.6 | 4,881.6 | 4,282.0 | 3,275.7 | 4,481.6 | 1,205.9 | 36.8 |
| Mikopo kwa serikali kuu | 4,708.6 | 5,900.4 | 6,451.5 | 7,012.8 | 7,166.9 | 8,081.8 | 8,522.5 | 440.7 | 5.5 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 9,010.4 | 10,392.7 | 12,412.3 | 15,492.7 | 16608.9 | 16895.4 | 17726.8 | 831.4 | 4.9 |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 2689.2 | 3345.8 | 2799.8 | 2131.1 | 2,884.9 | 4,806.1 | 4,040.9 | -765.2 | -15.9 |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -2,778.7 | -3,416.8 | -4,001.3 | -6,503.1 | -6,199.3 | -7,052.9 | -7,014.7 | 38.2 | -0.5 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA**

Jedwali Na. 18

| | Kipindi kinachoishia mwezi Desemba | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| **Fedha ya msingi (M0)** | **102.4%** | **11.1%** | **17.5%** | **15.6%** | **0.3%** | **1.5%** | **0.6%** |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)** | **17.3%** | **10.4%** | **14.8%** | **15.6%** | **5.3%** | **10.6%** | **5.1%** |
| Amana za Akiba na za muda maalum | 13.9% | 11.6% | 20.6% | 10.1% | 5.4% | 10.1% | 1.7% |
| **Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)** | **16.0%** | **10.9%** | **17.0%** | **13.4%** | **5.3%** | **10.4%** | **3.8%** |
| Amana za fedha za kigeni | 4.0% | 7.5% | 11.4% | 34.9% | -1.2% | 1.7% | 6.6% |
| **Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)** | **12.5%** | **10.0%** | **15.6%** | **18.8%** | **3.4%** | **8.0%** | **4.5%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)** | **2.0%** | **2.8%** | **-0.4%** | **25.8%** | **-0.7%** | **41.7%** | **-8.3%** |
| **Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)** | **22.3%** | **15.5%** | **26.6%** | **15.0%** | **5.9%** | **-10.7%** | **15.8%** |
| Karadha Nchini | 25.2% | 18.8% | 15.8% | 19.3% | 5.6% | 5.1% | 5.1% |
| Madai halisi kwa serikali kuu | 37.3% | 26.5% | 42.9% | 33.7% | -12.3% | -23.5% | 36.8% |
| Mikopo kwa serikali kuu | 41.2% | 25.3% | 9.3% | 8.7% | 2.2% | 12.8% | 5.5% |
| Mikopo kwa sekta Binafsi | 18.2% | 15.3% | 19.4% | 24.8% | 7.2% | 1.7% | 4.9% |
| Amana za Serikali zilizopo Benki Kuu na Benki za Biashara | 44.2% | 24.4% | -16.3% | -23.9% | 35.4% | 66.6% | -15.9% |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | 18.5% | 23.0% | 17.1% | 62.5% | -4.7% | 13.8% | -0.5% |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na.19

| | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Shs/Dola mwisho wa mwaka | 1,453.54 | 1,605.35 | 1,578.41 | 1603.20667 | 1,723.69 | 2,148.52 | 2172.62 | 2230.07 | 2281.23 |
| Badiliko la thamani ya shilingi (%) | -9.6 | -9.5 | 1.7 | -1.5 | -7.0 | -19.8 | -1.1 | -2.6 | -2.2 |
| Shs/Dola wastani wa mwaka | 1,401.79 | 1,557.43 | 1,571.71 | 1598.66 | 1,652.51 | 1985.39 | 2177.07 | 2228.86 | 2263.78 |
| Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%) | 7.2 | -10.0 | -0.9 | -1.7 | -3.3 | -16.8 | -8.8 | -2.3 | -1.5 |

## MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Jedwali Na. 20

| **Aina ya Shughuli** | **Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Billioni)** | | | | | | | Ukuaji (%) | Mchango (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2012** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | | |
| Uzalishaji katika Kilimo | 938.9 | 965.1 | 1057.3 | 1174.2 | 1107.6 | 1134.8 | 952.9 | -16.0 | 5.4 |
| Huduma za Kifedha | 231.3 | 251.3 | 310.7 | 404.6 | 388.7 | 292.1 | 172.9 | -40.8 | 1.0 |
| Madini na Uchimbaji Mawe | 55.2 | 96.7 | 166.3 | 275.2 | 328.6 | 292.6 | 375.2 | 28.2 | 2.1 |
| Viwanda | 991.8 | 1160.6 | 1386.2 | 1695.8 | 1627.8 | 1777.6 | 2087.9 | 17.5 | 11.8 |
| Majengo na Ujenzi | 410.7 | 514.4 | 660.1 | 741.4 | 740.7 | 837.2 | 643.3 | -23.2 | 3.6 |
| Uchukuzi na Mawasiliano | 610.1 | 727.5 | 925.7 | 1231.8 | 1180.9 | 975.6 | 1221.7 | 25.2 | 6.9 |
| Biashara | 1843.2 | 2162.2 | 2652.1 | 3077.7 | 3349.3 | 3306.9 | 3228.9 | -2.4 | 18.2 |
| Utalii | 60.2 | 113.4 | 129.5 | 176.6 | 198.5 | 176.3 | 138.8 | -21.3 | 0.8 |
| Mahoteli na Migahawa | 363.0 | 371.0 | 436.1 | 514.6 | 526.4 | 595.0 | 587.3 | -1.3 | 3.3 |
| Umeme | 338.0 | 403.0 | 440.9 | 439.8 | 429.9 | 335.2 | 358.1 | 6.8 | 2.0 |
| Watu Binafsi | 1778.7 | 1745.0 | 2104.5 | 2731.7 | 2981.7 | 3258.7 | 4819.5 | 47.9 | 27.2 |
| Sekta Nyinginezo | 1389.2 | 1882.4 | 2142.8 | 3029.2 | 3748.6 | 3913.4 | 3140.4 | -19.8 | 17.7 |
| **Jumla** | **9010.4** | **10392.7** | **12412.3** | **15492.7** | **16608.9** | **16895.4** | **17726.8** | 4.9 | 100.0 |

**MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA**

Jedwali Na.21 **Sh. Bilioni**

| | Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba | | | | | | Badiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2017/18 ( %)** |
| **Amana za Sekta Binafsi** | | | | | | | |
| Amana za Hundi/Zinazaohamishika | 4,454.2 | 5,039.4 | 5,897.2 | 5,941.5 | 6,685.3 | 7,031.7 | 5.2 |
| Amana za Akiba na za Muda Maalum | 4,672.4 | 5,632.9 | 6,204.4 | 6,415.6 | 7,052.2 | 7,154.7 | 1.5 |
| Amana za fedha za kigeni | 4,216.0 | 4,697.1 | 6,335.2 | 5,831.5 | 6,087.1 | 6,376.3 | 4.8 |
| **Jumla** | **13,342.6** | **15,369.4** | **18,436.8** | **18,188.7** | **19,824.6** | **20,562.8** | 3.7 |
| Amana za Serikali | 791.8 | 808.4 | 856.9 | 577.8 | 560.6 | 358.5 | -36.0 |
| **Jumla za Amana zote** | **14,134.4** | **16,177.8** | **19,293.7** | **18,766.5** | **20,385.1** | **20,921.3** | 2.6 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA**

Jedwali Na. 22 Asilimia

| Aina ya Riba | Wastani wa mwaka | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** |
| Riba ya Benki kuu (Discount rate) | 12.33 | 16.00 | 16.00 | 16.00 | 11.42 | 8.17 |
| Riba katika soko la fedha kati ya benki za biashara kwa ujumla | 7.92 | 9.12 | 11.23 | 13.47 | 6.00 | 2.21 |
| Riba za dhamana za serikali kwa ujumla | 14.22 | 13.56 | 12.91 | 16.17 | 11.10 | 6.43 |
| Siku 91 | 12.34 | 12.08 | 8.80 | 7.85 | 5.49 | 2.89 |
| Siku 182 | 14.37 | 13.66 | 13.04 | 15.84 | 10.01 | 4.13 |
| Siku 364 | 14.77 | 13.98 | 13.92 | 16.56 | 11.79 | 7.08 |
| Riba za amana | | | | | | |
| Amana za akiba | 3.09 | 3.13 | 3.45 | 3.35 | 3.03 | 2.52 |
| Amana za muda maalum kwa ujumla | 8.94 | 8.44 | 8.89 | 9.19 | 10.04 | 8.24 |
| Mwaka mmoja | 11.58 | 10.85 | 10.80 | 11.47 | 11.66 | 8.78 |
| Riba za mikopo | | | | | | |
| Mikopo kwa ujumla | 15.86 | 16.29 | 16.10 | 15.96 | 17.77 | 17.42 |
| Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja | 17.98 | 18.19 | 18.68 | 18.20 | 18.54 | 17.83 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## SURA YA 3

## FEDHA ZA SERIKALI

**Utangulizi**

69. Bajeti ya mwaka 2018/19 iliandaliwa kwa kuzingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Ilani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020. Malengo makuu ni kuondokana na umaskini na kuibadilisha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda na kuingia kwenye kundi la nchi zenye kipato cha kati (Middle Income Countries) ifikapo mwaka 2025. Kama ilivyokuwa mwaka 2017/18, dhima ya bajeti ya mwaka 2018/19 kwa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa ni **"kujenga uchumi wa viwanda utakao chochea ajira na ustawi endelevu wa jamii'.**

70. Katika bajeti ya mwaka 2018/19, Serikali ililenga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko, kuimarisha upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo, kupanua huduma za ughani, kuboresha mfumo wa utafiti na utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wananchi, na uendelezaji wa sekta ndogo za uvuvi na mifugo; kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi hususan viwanda vya nguo, ngozi na nyama, samaki, mafuta ya kula, madawa na vifaa tiba, vyakula vya binadamu na mifugo, na katika sekta ya madini; kuongeza upatikanaji na usambazaji wa maji safi hasa vijijini na uondoshaji wa majitaka, uchimbaji wa visima katika maeneo kame nchini na ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati; Kugharamia elimu msingi bila ada, kuongeza idadi ya wataalam katika fani adimu kwenye maeneo ya madini, mafuta na gesi, madaktari bingwa (moyo na figo) pamoja na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; kuongeza usambazaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na uboreshaji wa huduma katika vituo vya afya, zahanati na hospitali za rufaa; na Kujenga na kukarabati miundombinu wezeshi hususan kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali.

71. Shabaha za bajeti ya mwaka 2018/19 zililenga kuwa na ukuaji wa Pato halisi la Taifa wa asilimia 7.2 mwaka 2018; kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei katika wigo wa tarakimu moja; mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri kuwa asilimia 15.8 ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia

asilimia 13.6 ya Pato la Taifa; matumizi ya Serikali kufikia asilimia 24.5 ya Pato la Taifa; na nakisi ya bajeti kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa.

72. Mwaka 2018/19, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 32,476.0 kutoka vyanzo vya ndani na nje. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalitarajiwa kuwa shilingi bilioni 20,894.6, sawa na asilimia 64.3 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo ya ndani, mapato ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 18,000.2, sawa na asilimia 13.6 ya Pato la Taifa. Mapato yasiyo ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 2,158.8 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 735.6.

**Mwenendo wa Mapato**

**Mapato ya Ndani**

73. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, makusanyo ya ndani ikijumuisha mapato ya halmashauri yalifikia shilingi bilioni 14,064.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 13,479.5 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2017/18, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia shilingi bilioni 11,722.1 sawa na asilimia 88 ya lengo la kipindi hicho na ongezeko la asilimia 2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11,546.9 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18.

74. Hadi Machi 2019, makusanyo ya maduhuli yalifikia shilingi bilioni 1,872.8 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 1,522.6 sawa na asilimia 123 ya lengo la kipindi hicho. Mwenendo huu mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli ulitokana na kuimarika kwa matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji wa maduhuli kwenye taasisi za Serikali kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali wa Ukusanyaji wa Mapato –GePG.

75. Kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya kodi kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo: mwamko mdogo wa wafanyabiashara na wananchi katika matumizi ya mashine za kielektroniki za kutolea risiti.

**Misaada na Mikopo Nafuu**

76. Hadi Machi 2019, kiasi cha shilingi bilioni 1,703.4 kilipokelewa kama misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 85.6 ya ahadi za shilingi bilioni 1,991.1 kwa kipindi hicho. Kati ya

kiasi hicho, shilingi bilioni 125.4 zilipokelewa kama misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, sawa na asilimia 34.2 ya makadirio ya kipindi hicho ya shilingi bilioni 366.9; mifuko ya kisekta shilingi bilioni 170.2 ambayo ni asilimia 141.3 ya makadirio ya shilingi bilioni 120.4; na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,407.9 ikiwa ni asilimia 93.6 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,503.8.

77. Mwenendo wa upokeaji wa misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya Washirika wa Maendeleo kutotimiza ahadi zao kama walivyoahidi kwenye bajeti, hivyo kwenda kinyume na misingi ya makubaliano kama ilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania (Development Cooperation Framework- DCF).

**Mikopo ya Ndani**

78. Hadi kufikia Machi 2018, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 2,827.4 kutoka soko la ndani sawa na asilimia 64.6 ya kiasi kilichopangwa kukopwa kwa kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,594.1 zilikopwa kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva, na shilingi bilioni 233.3 zilikopwa ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

**Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara**

79. Mwaka 2018/19, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 3,111.1 ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi Machi 2019, Serikali iliweza kukopa kiasi cha shilingi bilioni 455.5. Aidha, Serikali haikuweza kukopa kiasi kilichopangwa kwa wakati kutoka kwenye chanzo hiki kutokana na hali ya soko la fedha la kimataifa kutokuwa nzuri. Hata hivyo, Serikali inaendelea kufanya majadiliano na taasisi mbalimbali za fedha ili kuweza kukopa kiasi kilichosalia.

**Matumizi**

80. Mwaka 2018/19, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa fedha zinaelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele ili kutekeleza kikamilifu Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2018/19. Katika kutekeleza azma hiyo, Sera za matumizi zililenga: kudhibiti nakisi ya bajeti isizidi asilimia 3.2 ya Pato la Taifa; kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele na yenye tija ili kuchochea ukuaji wa kilimo na viwanda, kupanua fursa za ajira, kujenga na kuboresha miundombinu ya uchumi na kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za jamii; kusimamia nidhamu ya

matumizi ya fedha za umma na kuendelea kupunguza matumizi yasiyo ya lazima; na kudhibiti ulimbikizaji wa madai.

81. Mwaka 2018/19, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 32,476.0. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20,468.7 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 7,410.0 za mishahara na shilingi bilioni 10,004.5 kwa ajili ya kulipia deni la Serikali na huduma nyinginezo. Aidha, matumizi ya maendeleo yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 12,007.3, ambapo shilingi bilioni 9,876.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 2,130.9 ni fedha za nje.

82. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, Serikali imetoa ridhaa za matumizi zenye jumla ya shilingi bilioni 19,051.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 13,836.7 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha shilingi bilioni 5,186.6 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa umma, shilingi bilioni 2,100.5 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 6,549.6 kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali na mahitaji mengine ya Mfuko Mkuu. Shilingi bilioni 5,215.2 zilitolewa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 4,879.7 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 335.5 ni fedha za nje.

83. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje yalifikia shilingi bilioni 1,453.6 ambayo ni asilimia 82 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,780.3 kwa kipindi hicho. Aidha, malipo ya mtaji yalifikia shilingi bilioni 3,954.8 ikiwa ni asilimia 80 ya lengo la shilingi bilioni 4,931.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,260.1 zilikuwa malipo ya mtaji kwa mkopo wa nje sawa na asilimia 95 ya lengo la kulipa shilingi bilioni 1,326.4. Aidha, shilingi bilioni 2,694.7 zilikuwa ni malipo ya dhamana na hati fungani za Serikali zilizoiva ikiwa ni asilimia 75 ya lengo la shilingi bilioni 3,605.3 kwa kipindi hicho. Matumizi mengine ya Mfuko Mkuu (CFS Others) yalikuwa shilingi bilioni 1,141.2 ikiwa ni asilimia 93 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,231.4 ya kipindi hicho.

84. Hadi Machi 2019, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali yalikuwa shilingi bilioni 5,186.7 sawa na asilimia 93.7 ya lengo la shilingi bilioni 5,537.9. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,618.6 zililipwa kwa watumishi wa Serikali

Kuu, shilingi bilioni 82.1 zililipwa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 2,565.6 kwa watumishi wa halmashauri za majiji, manispaa, miji na wilaya. Aidha, Serikali ililipa mishahara ya taasisi na mashirika ya umma jumla ya shilingi bilioni 716.3.

85. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 8,420.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, ambapo shilingi bilioni 6,796.5 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 1,624.2 fedha za nje. Hadi Machi, 2019, ridhaa ya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 5,215.3 sawa na asilimia 61.9 ya makadirio zilitolewa. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 4,879.7 zilikuwa fedha za ndani sawa na asilimia 71.8 na shilingi bilioni 335.6 fedha za nje sawa na asilimia 22.7.


86. Baadhi ya mahitaji yaliyopewa kipaumbele zaidi katika utoaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo katika kipindi cha Julai 2018 hadi Machi 2019 ni pamoja na: kuendeleza elimumsingi bila malipo na kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, shilingi bilioni 533.6; kuendelea kulipa mishahara ya watumishi kila mwezi na kwa wakati shilingi bilioni 5,186.7; kugharamia shughuli za uendeshaji wa ofisi shilingi bilioni 2,100.5; kulipwa kwa malimbikizo ya madai yaliyohakikiwa shilingi bilioni 468.4; kuendeleza ujenzi wa reli kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) shilingi bilioni 167.5; kukamilisha ununuzi wa ndege mpya mbili aina ya Airbus A220 – 300 na ndege moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner; kulipa sehemu ya gharama za ununuzi wa ndege moja aina ya Boeing 787-8 Dreamliner; na kuanza taratibu za ununuzi wa ndege moja mpya aina ya Bombadier Q400 shilingi bilioni 166.8; mradi wa kufua umeme utokanao na nguvu za maji katika Mto Rufiji shilingi bilioni 1,183.2; awamu ya tatu ya mradi wa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) shilingi bilioni 242.4; na kuendeleza ujenzi wa meli mpya katika Ziwa Victoria shilingi bilioni 30.6.

**Deni la Serikali**

87. Deni la Serikali liliongezeka kutoka shilingi bilioni 49,728.03 Machi 2018 na kufikia shilingi bilioni 50,772.27 Machi 2019, ongezeko hilo ni sawa na asilimia 2.1. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 13,133.05 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 37,639.22. Ongezeko la deni lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo

ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa, madaraja ya juu na miradi ya barabara. **Kielelezo Na. 3.1** kinaonesha mwenendo wa Deni la Serikali.

**Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Deni la Serikali kwa kipindi cha Machi 2011 - Machi 2019 (Shs Bilioni)**




**Deni la Nje**

88. Deni la Serikali la nje liliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 15,811.30 Machi 2018 na kufikia dola milioni 16,358.55 Machi 2019, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 3.5. Ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, mchanganuo wa deni la nje unaonesha kuwa, mashirika ya fedha ya kimataifa yalichangia asilimia 58.2 ya deni la nje ikilinganishwa na asilimia 56.8 Machi 2018, mikopo yenye masharti ya kibiashara ilichangia asilimia 29.9 na mikopo kutoka Nchi Wahisani ilichangia asilimia 11.9 ya mikopo yote ya nje. Aidha, Serikali imedhamiria kuendelea kukopa kutoka kwenye vyanzo nafuu na kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inatumika kugharamia miradi ya maendeleo inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

**Jedwali Na.3.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Wakopeshaji**


| Taasisi | Machi 2016 | Mchango kwa % | Machi 2017 | Mchango kwa % | Machi 2018 | Machi 2019 | Mchango kwa % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mashirika ya Fedha | 7,084.0 | 55.3 | 7,834.4 | 56.8 | 9,305.80 | 9,558.60 | 58.2 |
| Washirika wa Maendeleo | 1,732.0 | 13.5 | 1,905.3 | 13.8 | 1,876.60 | 1,927.50 | 11.9 |
| Benki za Kibiashara | 3,998.4 | 31.2 | 4,044.2 | 29.3 | 4,460.50 | 4,862.50 | 29.9 |
| **Jumla** | **12,814.4** | **100** | **13,783.9** | **100** | **15,811.30** | **16,348.60** | **100** |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango

### Deni la Ndani

89. Hadi Machi 2019, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 13,133.05 ikilinganishwa na shilingi bilioni 14,158.63 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Sehemu kubwa ya deni la ndani ilikuwa ni mikopo ya hati fungani ambayo ilikuwa ni asilimia 68.7 ya deni lote la ndani ikifuatiwa na dhamana za Serikali za muda mfupi asilimia 21.4 hati fungani maalum asilimia 9.7 na madeni mengine asilimia 0.1. Aidha, Serikali inaendelea kukopa kutoka kwenye soko la ndani ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na kulipia mikopo ya ndani iliyoiva. **Kielelezo Na. 3.2** kinaonesha mwenendo wa madeni ya ndani.

**Kielelezo Na. 3.2: Mwenendo wa Deni la Ndani**



90. Hadi kufikia Machi 2019, benki za biashara zilikuwa zinaongoza kwa kuhodhi asilimia 42.4 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimi 48.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni ya pili kwa kuhodhi asilimia 32.92 ikifuatiwa na kampuni za bima asilimia 11.4.

**Jedwali Na. 3.2: Deni la Ndani kwa Wakopeshaji hadi Machi 2018**

| Taasisi | Machi 2016 | Mchango kwa % | Machi 2017 | Mchango kwa % | Machi 2018 | Mchango kwa % | Machi 2018 | Mchango kwa % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Benki za Biashara | 4,859.48 | 64.6 | 4,578.83 | 49.1 | 5,417.34 | 48.7 | 4,866.29 | 42.4 |
| Taasisi za Fedha | 117.63 | 1.6 | 145.75 | 1.6 | 128.10 | 1.2 | 139.04 | 1.2 |
| Mifuko ya Jamii | 1,383.98 | 18.4 | 2995.30 | 32.1 | 3,805.40 | 34.2 | 3,782.05 | 32.9 |
| Kampuni za Bima | 798.75 | 10.6 | 1105.75 | 11.9 | 1,123.77 | 10.1 | 1310.64 | 11.41 |
| Taasisi za Kigeni | - | - | - | - | - | - | 502.40 | 4.37 |
| Mashirika Madogo | 187.13 | 2.5 | 193.83 | 2.1 | 245.82 | 2.2 | 230.32 | 2.0 |
| Watu Binafsi | 175.55 | 2.3 | 297.70 | 3.2 | 397.92 | 3.6 | 656.88 | 5.7 |
| **Jumla** | **7,522.52** | **100.00** | **9,317.16** | **100.0** | **11,118.35** | **100.0** | **11,487.63** | **100.0** |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

### Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

91. Tathmini ya Uhimilivu wa Deni ilifanyika mwezi Desemba 2018 kwa kuzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa, uwiano wa deni halisi kwa mauzo ya nje na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa iliyofanyika Desemba, 2018, ilionesha kuwa deni la Taifa ni himilivu. Viashiria vya deni vinaonesha kuwa: mwaka 2018/19, thamani ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 15.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimi 55; thamani ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 112.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 240 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 15.0 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 22. Matokeo haya yanaonesha kuwa nchi ina uwezo wa kukopa ndani na nje, na kulipa mikopo hiyo bila kuwa na athari hasi kwenye ukuaji wa uchumi na msukosuko wa kifedha. Aidha, katika kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu, Serikali itaendelea kukopa na kuelekeza mikopo hiyo kwenye miradi ambayo itachochea ukuaji wa uchumi.

**Jedwali Na.3.3: Tathmini ya Viashiria vya Deni la Taifa**

| **VIASHIRIA VYA DENI LA NJE** | **Ukomo** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2028/29** | **2038/39** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni (PV[1] ) /Pato la Taifa | 55 | 15.9 | 15.0 | 1404 | 13.6 | 12.8 | 8.6 | 4.7 |
| Deni (PV) / uuzaji wa bidhaa nje | 240 | 112.4 | 105.9 | 101.4 | 95.8 | 85.4 | 56.4 | 30.4 |
| Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje | 23 | 15.0 | 12.6 | 10.7 | 10.4 | 8.8 | 6.8 | 4.8 |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | 22 | 15.0 | 12.3 | 10.4 | 10.4 | 9.1 | 6.4 | 3.7 |
| **VIASHIRIA VYA DENI LA NJE NA LA NDANI** | **Ukomo** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2028/29** | **2038/39** |
| Deni (PV) /Pato la Taifa | 70 | 27.2 | 26.0 | 25.2 | 24.3 | 23.2 | 16.3 | 10.7 |
| Deni (PV) / Mapato ya ndani | N/A | 182.5 | 170.6 | 165.1 | 162.0 | 152.7 | 97.2 | 52.8 |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | N/A | 49.6 | 38.1 | 31.8 | 30.0 | 30.9 | 19.4 | 16.5 |


**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

**MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI**

Jedwali Na. 23 — Sh.milioni

| | 2014/15 Halisi | 2015/16 Halisi | 2016/17 Halisi | 2017/18 Halisi | 2018/19 Bajeti | 2018/19 Matokeo Hadi Machi | 2018/19 Matarajio hadi Juni |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri) | 10,957,765 | 14,048,034 | 16,639,831 | 17,944,887 | 20,894,578 | 14,064,884 | 19,040,651 |
| MAPATO YA NDANI | 10,597,681 | 13,622,182 | 16,128,113 | 17,403,388 | 20,158,989 | 13,594,894 | 18,378,621 |
| 1. Mapato yatokanayo na Kodi | 9,891,680 | 12,410,951 | 14,055,173 | 15,191,421 | 18,000,219 | 11,722,081 | 16,219,851 |
| Ushuru wa Forodha na Excise Duty | 2,495,082 | 3,090,110 | 3,116,298 | 3,313,671 | 3,789,755 | 2,673,564 | 3,606,445 |
| Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) | 3,031,828 | 3,553,637 | 3,979,473 | 4,478,851 | 5,573,892 | 3,595,998 | 4,927,037 |
| Bidhaa toka nje | 1,519,939 | 1,717,902 | 1,803,667 | 2,054,675 | 2,397,484 | 1,671,770 | 2,269,439 |
| Bidhaa za ndani | 1,511,889 | 1,835,735 | 2,175,806 | 2,424,175 | 3,176,408 | 1,924,228 | 2,657,597 |
| Kodi ya Mapato | 3,727,934 | 4,608,245 | 4,832,759 | 5,157,886 | 6,130,785 | 3,883,683 | 5,447,204 |
| Kodi nyingine | 1,278,648 | 1,921,459 | 2,216,357 | 2,299,242 | 2,564,260 | 1,598,069 | 2,297,638 |
| Marejesho (Refunds Accounts) | (641,811) | (762,499) | (89,714) | (58,229) | (58,473) | (29,233) | (58,473) |
| 2. Mapato yasiyotokana na Kodi | 706,001 | 1,211,231 | 2,072,941 | 2,211,967 | 2,158,770 | 1,872,813 | 2,158,770 |
| 3. Mapato ya Halmashauri | 360,084 | 425,852 | 511,718 | 541,499 | 735,589 | 469,990 | 662,030 |
| B. JUMLA YA MATUMIZI | 14,603,714 | 17,759,598 | 18,898,690 | 20,468,072 | 26,206,297 | 15,269,905 | 23,721,576 |
| 1. Matumizi ya Kawaida | 10,893,486 | 13,420,045 | 11,625,866 | 12852304 | 14,199,023 | 8,938,622 | 13,261,195 |
| 2. Matumizi ya Maendeleo | 3,710,228 | 4,339,553 | 7,272,824 | 7615768 | 12,007,273 | 6,331,284 | 10,460,381 |
| Fedha za ndani | 2,264,506 | 2,904,530 | 5,141,451 | 5397034 | 9,876,393 | 4,753,231 | 8,329,501 |
| Fedha za nje | 1,445,722 | 1,435,023 | 2,131,374 | 2218735 | 2,130,880 | 1,578,053 | 2,130,880 |
| C. NAKISI/SALIO (A-B) | (3,645,949) | (3,711,564) | (2,258,859) | (2,523,185) | (5,311,719) | (1,205,021) | (4,680,925) |
| D. KUZIBA NAKISI | 3,645,949 | 3,711,564 | 2,258,859 | 2,523,185 | 5,311,719 | 1,205,021 | 4,680,925 |
| 1. Fedha kutoka nje | 3,030,875 | 3,982,100 | 2,797,488 | 2,632,731 | 4,118,050 | 964,154 | 2,397,336 |
| Ruzuku | 896,496 | 1,349,799 | 923,512 | 813,483 | 989,245 | 226,091 | 752,982 |
| Basket support | 127,637 | 81,073 | 168,984 | 117,165 | 92,163 | 152,756 | 92,163 |
| Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL | 537,881 | 546,846 | 257,473 | 71,078 | 343,202 | 142,793 | 388,358 |
| Mikopo ya miradi | 640,724 | 344,800 | 1,124,190 | 1,464,294 | 1,252,035 | 1,181,809 | 1,252,035 |
| Mikopo ya masharti ya kibiashara | 1,054,803 | 2,142,469 | 1,226,760 | 1,474,282 | 3,111,058 | 455,521 | 1,581,452 |
| Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign) | (226,667) | (482,887) | (903,431) | (1,307,571) | (1,669,653) | (1,194,816) | (1,669,653) |
| 2. Fedha za Ndani | 615,075 | (270,536) | (538,629) | (109,545) | 1,193,669 | 240,868 | 2,283,589 |
| Mikopo isiyo ya mabenki | - | 776,945 | 989,283 | -343326 | 119367 | 442041 | 119367 |
| Mikopo ya mabenki | 799,776 | 1,522,207 | (1,100,145) | 941973 | 1074302 | 24164 | 1074302 |
| Mikopo ya ndani (Rollover) | 2,064,756 | 2,600,000 | 4,615,670 | 4835199 | 4600000 | 2594102 | 4600000 |
| Mapato ya Ubinafsishaji | - | - | - | - | - | - | - |
| Marekebisho (Adjustment to Cash) | 62,959 | (2,500,270) | (368,120) | (636,425) | | (215,094) | 1,089,921 |
| Kulipia madeni ya ndani (amortization) | (2,064,756) | (2,600,000) | (4,615,670) | (4,835,199) | (4,600,000) | (2,594,102) | (4,600,000) |
| Expenditure float | (247,661) | (69,418) | (59,647) | (71,768) | - | (10,243) | - |

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango


MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI
Sh. milioni
30000000
25000000
20000000
15000000
10000000
5000000
0
-5000000
-10000000
2012/13
2013/14
2014/15
2015/16
2016/17
2017/18
2018/19
MAPATO YA NDANI
B. JUMLA YA MATUMIZI
C. NAKISI/SALIO (A-B)

**MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI**

**Jedwali Na. 24**

Shs. Milioni

| Fungu | Maelezo | 2017/18 (Halisi) | | | 2018/19 (Bajeti) | | | 2019/20 (Makadirio) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **701** | **Huduma za Kawaida** | **14,296,414.9** | **1,627,967.8** | **15,924,382.6** | **12,230,832.7** | **392,882.4** | **12,623,715.1** | **12,883,436.3** | **2,020,850.2** | **14,904,286.5** |
| 70111 | Utawala na Shughuli za Bunge | 777,915.7 | 22,791.0 | 800,706.8 | 693,979.8 | 4,010.7 | 697,990.5 | 688,458.9 | 26,801.8 | 715,260.7 |
| 70112 | Fedha na Masuala ya Kodi | 308,879.9 | 762,833.7 | 1,071,713.5 | 364,756.3 | 7,889.8 | 372,646.0 | 1,062,488.0 | 770,723.4 | 1,833,211.4 |
| 70113 | Mambo ya Nje | 99,337.9 | 0.0 | 99,337.9 | 137,336.6 | 0.0 | 137,336.6 | 148,664.9 | 0.0 | 148,664.9 |
| 70121 | Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70122 | Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa | 371.2 | 0.0 | 371.2 | 697.2 | 0.0 | 697.2 | 784.3 | 0.0 | 784.3 |
| 70131 | Huduma za Umma | 115,472.5 | 1,965.0 | 117,437.5 | 139,473.6 | 4,928.5 | 144,402.0 | 131,231.6 | 6,893.5 | 138,125.0 |
| 70132 | Huduma za Mipango na Takwimu | 83,471.4 | 374,616.0 | 458,087.4 | 152,434.2 | 282,403.0 | 434,837.2 | 148,599.9 | 657,019.0 | 805,618.9 |
| 70133 | Huduma nyingine za Kawaida | 3,475,274.6 | 452,443.5 | 3,927,718.2 | 698,591.2 | 86,109.2 | 784,700.4 | 941,483.4 | 538,552.7 | 1,480,036.1 |
| 70140 | Utafiti wa Msingi | 19.2 | 0.0 | 19.2 | 32.9 | 0.0 | 32.9 | 66.0 | 0.0 | 66.0 |
| 70150 | Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma | 257.5 | 0.0 | 257.5 | 349.1 | 0.0 | 349.1 | 327.5 | 0.0 | 327.5 |
| 70160 | Huduma za Umma zisizotajwa hapo Juu | 31,217.7 | 13,223.8 | 44,441.4 | 25,875.7 | 0.0 | 25,875.7 | 24,609.5 | 13,223.8 | 37,833.3 |
| 70170 | Deni la Taifa | 9,402,210.1 | 84.8 | 9,402,294.9 | 10,013,706.1 | 312.4 | 10,014,018.5 | 9,733,231.0 | 397.2 | 9,733,628.1 |
| 70180 | Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali | 1,987.2 | 10.0 | 1,997.2 | 3,600.0 | 7,228.9 | 10,828.8 | 3,491.4 | 7,238.9 | 10,730.3 |
| **702** | **Ulinzi** | **1,108,518.9** | **127,600.0** | **1,236,118.9** | **1,674,994.8** | **0.0** | **1,674,994.8** | **1,724,221.0** | **127,600.0** | **1,851,821.0** |
| 70210 | Huduma za Ulinzi wa Kijeshi | 1,107,874.9 | 127,600.0 | 1,235,474.9 | 1,674,068.2 | 0.0 | 1,674,068.2 | 1,723,525.4 | 127,600.0 | 1,851,125.4 |
| 70220 | Huduma za Ulinzi wa Kiraia | 213.5 | 0.0 | 213.5 | 239.0 | 0.0 | 239.0 | 255.8 | 0.0 | 255.8 |
| 70230 | Misaada ya Nje ya Ulinzi | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70240 | Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi | 430.5 | 0.0 | 430.5 | 687.6 | 0.0 | 687.6 | 439.8 | 0.0 | 439.8 |
| 70250 | Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo Juu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **703** | **Usalama wa Raia** | **777,119.4** | **22,910.0** | **800,029.4** | **797,971.0** | **17,781.2** | **815,752.2** | **806,070.6** | **40,691.2** | **846,761.8** |
| 70310 | Huduma za Polisi | 674,612.6 | 6,500.0 | 681,112.6 | 668,297.5 | 792.9 | 669,090.4 | 665,882.5 | 7,292.9 | 0.7 |
| 70320 | Huduma za Zimamoto | 9,497.8 | 0.0 | 9,497.8 | 13,274.2 | 0.0 | 13,274.2 | 15,167.7 | 0.0 | 0.0 |
| 70330 | Mahakama | 43,747.4 | 1,410.0 | 45,157.4 | 69,720.0 | 7,342.7 | 77,062.8 | 78,392.3 | 8,752.7 | 0.1 |
| 70340 | Magereza | 31,609.8 | 5,000.0 | 36,609.8 | 32,394.6 | 0.0 | 32,394.6 | 31,824.2 | 5,000.0 | 0.0 |
| 70350 | Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 166.4 | 0.0 | 0.0 |
| 70360 | Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu | 17,651.8 | 10,000.0 | 27,651.8 | 14,284.7 | 9,645.5 | 23,930.2 | 14,637.6 | 19,645.5 | 0.0 |
| **704** | **Shughuli za Kiuchumi** | **548,645.5** | **6,396,150.4** | **6,944,796** | **679,365.4** | **1,057,750.4** | **1,737,116** | **668,992.9** | **7,453,900.8** | **8,122,894** |
| 70411 | Shughuli za Kiuchumi na Biashara | 20,552.4 | 7,800.0 | 28,352 | 20,363.0 | 288.9 | 20,652 | 22,323.5 | 8,088.9 | 30,412 |
| 70412 | Masuala ya Kazi | 12,611.1 | 18,000.0 | 30,611 | 17,349.5 | 595.2 | 17,945 | 18,132.9 | 18,595.2 | 36,728 |
| 70421 | Kilimo | 193,008.5 | 92,201.6 | 285,210 | 255,653.4 | 95,194.9 | 350,848 | 253,881.4 | 187,396.5 | 441,278 |
| 70422 | Misitu | 21,500.3 | 200.0 | 21,700 | 42,176.5 | 13,330.8 | 55,507 | 21,782.5 | 13,530.8 | 35,313 |
| 70423 | Uvuvi na Uwindaji | 14,345.4 | 2,848.0 | 17,193 | 13,966.4 | 11,347.5 | 25,314 | 26,902.4 | 14,195.5 | 41,098 |
| 70431 | Makaa ya Mawe na Nishati nyingine | 5,059.9 | 37,160.0 | 42,220 | 4,988.5 | 0.0 | 4,989 | 6,595.6 | 37,160.0 | 43,756 |
| 70432 | Petroli na Gesi Asilia | 0.0 | 23,350.0 | 23,350 | 17,495.7 | 15,728.3 | 33,224 | 16,059.1 | 39,078.3 | 55,137 |
| 70433 | Nishati ya Nyukilia | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70434 | Nishati nyingine | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70435 | Umeme | 13,630.4 | 1,928,772.0 | 1,942,402 | 2,534.7 | 144,353.7 | 146,888 | 2,105.1 | 2,073,125.7 | 2,075,231 |
| 70436 | Nishati isiyo ya umeme | 6,748.2 | 2,400.0 | 9,148 | 2,205.8 | 0.0 | 2,206 | 3,034.7 | 2,400.0 | 5,435 |
| 70441 | Uchimbaji Madini yasiyo Nishati | 21,900.0 | 7,039.8 | 28,940 | 32,236.5 | 3,119.9 | 35,356 | 36,151.9 | 10,159.7 | 46,312 |
| 70442 | Uzalishaji Viwandani | 159.8 | 0.0 | 160 | 267.5 | 0.0 | 268 | 323.3 | 0.0 | 323 |
| 70443 | Ujenzi | 26,322.3 | 95,043.9 | 121,366 | 70,505.2 | 182,278.6 | 252,784 | 57,800.9 | 277,322.5 | 335,123 |
| 70451 | Usafiri wa Barabara | 128,643.1 | 1,374,808.0 | 1,503,451 | 96,531.0 | 241,859.2 | 338,390 | 96,240.2 | 1,616,667.2 | 1,712,907 |
| 70452 | Usafiri wa Majini | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70453 | Usafiri wa Reli | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70454 | Usafiri wa Anga | 206.3 | 2,771,716.6 | 2,771,923 | 1,520.9 | 278,198.0 | 279,719 | 1,603.1 | 3,049,914.6 | 3,051,518 |
| 70455 | Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri | 212.9 | 0.0 | 213 | 701.9 | 0.0 | 702 | 726.4 | 0.0 | 726 |
| 70460 | Mawasiliano | 8,246.0 | 1,085.5 | 9,331 | 16,067.2 | 619.1 | 16,686 | 15,754.1 | 1,704.6 | 17,459 |
| 70471 | Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo | 20,969.4 | 11,000.0 | 31,969 | 23,033.6 | 6,284.5 | 29,318 | 25,072.0 | 17,284.5 | 42,356 |
| 70472 | Hoteli na Migahawa | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70473 | Utalii | 12,090.3 | 300.0 | 12,390 | 13,115.0 | 20,000.0 | 33,115 | 10,426.5 | 20,300.0 | 30,726 |
| 70474 | Miradi ya Maendeleo | 37,228.2 | 19,324.7 | 56,553 | 40,728.9 | 44,551.9 | 85,281 | 46,529.2 | 63,876.6 | 110,406 |
| 70481 | Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi | 16.3 | 0.0 | 16 | 59.3 | 0.0 | 59 | 59.3 | 0.0 | 59 |
| 70482 | Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na U | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70483 | Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70484 | Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji Viwandani na Ujenzi | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70485 | Utafiti na Maendeleo ya Usafiri | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70486 | Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70487 | Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0 |
| 70490 | Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu | 5,194.4 | 3,100.3 | 8,295 | 7,864.9 | 0.0 | 7,865 | 7,489.0 | 3,100.3 | 10,589 |

*Jedwali linaendelea ukurasa unaofuata*

*Jedwali Na. 24 linaendelea*

| Fungu | Maelezo | 2017/18 (Halisi) | | | 2018/19 (Bajeti) | | | 2019/20 (Makadirio) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla | Matumizi ya kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
| **705** | **Hifadhi ya Mazingira** | **25,544.9** | **5,400.0** | **30,945** | **29,139.1** | **32,778.1** | **61,917.1** | **26,193.2** | **38,178.1** | **64,371.2** |
| 70510 | Hifadhi ya Taka | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70520 | Hifadhi ya Maji Taka | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70530 | Kupunguza Uharibifu wa Mazingira | 0.0 | 0.0 | 0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70540 | Hifadhi ya Viumbehai na Mazingira | 21,344.6 | 3,500.0 | 24,845 | 23,007.5 | 14,559.1 | 37,566.7 | 19,757.5 | 18,059.1 | 37,816.6 |
| 70550 | Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira | 298.6 | 1,800.0 | 2,099 | 369.6 | 0.0 | 369.6 | 331.0 | 1,800.0 | 2,131.0 |
| 70560 | Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu | 3,901.7 | 100.0 | 4,002 | 5,761.9 | 18,218.9 | 23,980.9 | 6,104.7 | 18,318.9 | 24,423.6 |
| **706** | **Nyumba na Huduma za Jamii** | **57,795.5** | **367,151.1** | **424,946.6** | **105,305.0** | **256,395.6** | **361,700.7** | **85,111.3** | **623,546.7** | **708,658.0** |
| 70610 | Maendeleo ya Nyumba | 16,052.2 | 1,100.0 | 17,152.2 | 20,319.3 | 0.0 | 20,319.3 | 14,731.0 | 1,100.0 | 15,831.0 |
| 70620 | Maendeleo ya Jamii | 14,559.0 | 21,032.1 | 35,591.1 | 29,652.3 | 2,359.5 | 32,011.8 | 22,932.7 | 23,391.6 | 46,324.3 |
| 70630 | Usambazaji Maji | 26,511.1 | 345,019.0 | 371,530.1 | 54,571.1 | 254,036.1 | 308,607.2 | 46,707.7 | 599,055.1 | 645,762.8 |
| 70640 | Taa za Barabarani | 673.2 | 0.0 | 673.2 | 762.3 | 0.0 | 762.3 | 739.9 | 0.0 | 739.9 |
| 70650 | Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70660 | Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **707** | **Afya** | **371,317.4** | **340,877.4** | **712,194.7** | **1,004,967.6** | **411,369.9** | **1,416,337.5** | **1,018,191.9** | **752,247.3** | **1,770,439.2** |
| 70711 | Madawa | 70.2 | 200,000.0 | 200,070.2 | 185.5 | 0.0 | 185.5 | 385.1 | 200,000.0 | 200,385.1 |
| 70712 | Bidhaa nyingine za madawa | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70713 | Huduma za Tiba na Vifaa vya Tiba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70721 | Huduma za Tiba za Jumla | 192,283.5 | 42,097.5 | 234,381.0 | 393,382.0 | 11,910.5 | 405,292.6 | 394,505.4 | 54,008.0 | 448,513.4 |
| 70722 | Huduma Maalumu za Tiba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70723 | Huduma za Meno | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70724 | Huduma za Wakunga Wasaidizi | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70731 | Huduma za Hospitali | 31,998.6 | 10.0 | 32,008.6 | 28,311.5 | 130.6 | 28,442.1 | 3,351.1 | 140.6 | 3,491.7 |
| 70732 | Huduma za Hospitali Maalumu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 17,263.0 | 0.0 | 17,263.0 | 111,086.5 | 0.0 | 111,086.5 |
| 70733 | Huduma za Vifaa vya Kujifungulia Wajawazito | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70734 | Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jadi | 248.4 | 0.0 | 248.4 | 390.2 | 0.0 | 390.2 | 552.9 | 0.0 | 552.9 |
| 70740 | Huduma za Afya | 65,872.6 | 98,636.9 | 164,509.5 | 515,214.3 | 395,245.4 | 910,459.7 | 492,047.8 | 493,882.3 | 985,930.1 |
| 70750 | Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70760 | Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu | 80,844.0 | 133.0 | 80,977.0 | 50,221.0 | 4,083.4 | 54,304.5 | 16,263.2 | 4,216.4 | 20,479.6 |
| **708** | **Burudani, Utamaduni na Dini** | **17,247.1** | **7,000.0** | **24,247.1** | **19,768.8** | **772.0** | **20,540.7** | **23,673.4** | **7,772.0** | **31,445.4** |
| 70810 | Huduma za Burudani na Michezo | 1,200.4 | 0.0 | 1,200.4 | 2,253.5 | 0.0 | 2,253.5 | 1,846.6 | 0.0 | 1,846.6 |
| 70820 | Huduma za Utamaduni | 3,499.4 | 0.0 | 3,499.4 | 4,152.9 | 0.0 | 4,152.9 | 7,267.5 | 0.0 | 7,267.5 |
| 70830 | Huduma za Utangazaji na Uchapishaji | 12,002.9 | 6,000.0 | 18,002.9 | 13,012.4 | 0.0 | 13,012.4 | 13,647.1 | 6,000.0 | 19,647.1 |
| 70840 | Dini na Huduma nyingine za Kijamii | 544.4 | 1,000.0 | 1,544.4 | 350.0 | 772.0 | 1,122.0 | 912.3 | 1,772.0 | 2,684.2 |
| 70850 | Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70860 | Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| **709** | **Elimu** | **821,475.6** | **842,682.2** | **1,664,157.9** | **3,749,973.7** | **340,670.4** | **4,090,644.1** | **3,466,947.5** | **1,183,352.6** | **4,650,300.1** |
| 70911 | Elimu ya Awali | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70912 | Elimu ya Msingi | 17,134.9 | 157,468.7 | 174,603.5 | 2,001,233.9 | 147,276.6 | 2,148,510.5 | 1,767,366.7 | 304,745.3 | 2,072,111.9 |
| 70921 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV) | 352.1 | 162,759.9 | 163,112.0 | 931,624.6 | 0.0 | 931,624.6 | 837,815.0 | 162,759.9 | 1,000,574.9 |
| 70922 | Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI) | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70930 | Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu | 458.6 | 0.0 | 458.6 | 480.7 | 0.0 | 480.7 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70941 | Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70942 | Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu | 1,549.2 | 0.0 | 1,549.2 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 70950 | Elimu isiyopambanuliwa | 396,295.9 | 29,953.6 | 426,249.6 | 362,585.7 | 22,894.9 | 385,480.6 | 395,232.9 | 52,848.5 | 448,081.4 |
| 70960 | Huduma za Ziada kwa Elimu | 381,258.1 | 492,500.0 | 873,758.1 | 433,418.8 | 170,248.9 | 603,667.7 | 443,135.1 | 662,748.9 | 1,105,884.0 |
| 70970 | Utafiti na Maendeleo ya Elimu | 9,508.5 | 0.0 | 9,508.5 | 12,515.3 | 0.0 | 12,515.3 | 15,313.3 | 0.0 | 15,313.3 |
| 70980 | Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu | 14,918.3 | 0.0 | 14,918.3 | 8,114.7 | 250.0 | 8,364.7 | 8,084.5 | 250.0 | 8,334.5 |
| **710** | **Kinga ya Jamii** | **185,602.5** | **0.0** | **185,602.5** | **176,357.8** | **463.5** | **176,821.3** | **153,969.6** | **463.5** | **154,433.0** |
| 71011 | Ugonjwa | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71012 | Ulemavu | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 1,139.9 | 0.0 | 1,139.9 |
| 71020 | Wazee | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71030 | Waathirika | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71040 | Familia na Watoto | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71050 | Ukosefu wa Ajira | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71060 | Nyumba | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| 71070 | Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu | 582.6 | 0.0 | 582.6 | 904.3 | 0.0 | 904.3 | 739.5 | 0.0 | 739.5 |
| 71080 | Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 315.4 | 0.0 | 315.4 |
| 71090 | Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu | 185,020.0 | 0.0 | 185,020.0 | 175,453.5 | 463.5 | 175,916.9 | 151,774.7 | 463.5 | 152,238.2 |
| | **JUMLA** | **18,209,681.8** | **9,737,738.8** | **27,947,420.6** | **20,468,676.0** | **2,510,863.5** | **22,979,539.5** | **20,856,807.5** | **12,248,602.3** | **33,105,409.8** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

CS: Huduma za umma zinazotolewa na Serikali na wanufaika ni watu wote

IS: Huduma za umma zinazotolewa na Serikali na wanufaika ni wanakaya

# SURA YA 4

## SEKTA YA NJE

### Bidhaa Zilizouzwa Nje

92. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 4,380.3 ikilinganishwa na dola milioni 4,523.9 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 3.2. Upungufu wa mauzo ulitokana na kupungua kwa mapato yatokanayo na bidhaa asilia. Bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 80.6 ya mauzo ya bidhaa nje wakati mauzo ya bidhaa asilia yalichangia asilimia 19.4.

### Bidhaa Asilia

93. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia ilipungua hadi kufikia dola za Marekani milioni 772.8 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 1,020.7 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 24.3. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa bei katika soko la dunia kwa mazao ya kahawa, pamba, katani, chai na tumbaku, na kupungua kwa mauzo ya korosho katika soko la dunia.

### Kahawa

94. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya kahawa nje iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 147.9 kutoka dola milioni 126.3 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 17.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya kahawa nje ambapo tani 56,600 ziliuzwa mwaka 2018 ikilinganishwa na tani 41,800 mwaka 2017. Hata hivyo, wastani wa bei ya kahawa katika soko la dunia ulipungua kwa asilimia 13.5 mwaka 2018.

### Pamba

95. Mwaka 2018, thamani ya pamba iliyouzwa nje ilikuwa dola za Marekani milioni 68.4 ikilinganishwa na dola milioni 36.8 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 85.9. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha pamba kilichouzwa nje kutoka tani 25,300 mwaka 2017 hadi tani 47,400 mwaka 2018. Aidha, wastani wa bei ya pamba kwa tani katika soko la dunia ulipungua na kufikia dola 1,444.2 mwaka 2018 kutoka dola za Marekani 1,450.3 mwaka 2017.

**Katani**

96. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya katani nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 33.2 ikilinganishwa na dola milioni 28.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha katani kilichouzwa nje kutoka tani 17,000 mwaka 2017 hadi tani 20,400 mwaka 2018. Aidha, wastani wa bei ya katani katika soko la dunia ulipungua kwa asilimia 3.5 hadi kufikia dola za Marekani 1,627.0 kwa tani mwaka 2018 kutoka dola 1,686.7 kwa tani mwaka 2017.

**Chai**

97. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya chai nje ilikuwa dola za Marekani milioni 45.9 ikilinganishwa na dola milioni 49.1 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 6.5. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa bei ya chai katika soko la dunia kwa asilimia 4.5 kutoka dola za Marekani 1,783.6 kwa tani mwaka 2017 hadi dola 1,707.4 kwa tani mwaka 2018. Aidha, kiasi cha chai kilichouzwa nje kilipungua kutoka tani 27,500 mwaka 2017 hadi tani 26,900 mwaka 2018.

**Tumbaku**

98. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya tumbaku iliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 270.3 ikilinganishwa na dola milioni 195.8 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 38.0. Hii ilitokana na kuongezeka kiasi cha tumbaku kilichouzwa nje kutoka tani 48,300 mwaka 2017 hadi tani 72,200 mwaka 2018. Aidha, wastani wa bei ya tumbaku kwa tani katika soko la dunia ulipungua kutoka dola za Marekani 4,055.6 mwaka 2017 hadi dola 3,741.9 mwaka 2018, sawa na upungufu wa asilimia 7.7.

**Korosho**

99. Thamani ya mauzo ya korosho nje ilikuwa dola za Marekani milioni 196.5 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 529.6 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 62.9. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa kiasi cha korosho kilichouzwa nje kwa asilimia 63.5 kutoka tani 329,400 mwaka 2017 hadi tani 120,200 mwaka 2018. Aidha, bei ya korosho kwa tani katika soko la dunia ilipanda kwa asilimia 1.6 kutoka dola za Marekani 1,607.7 mwaka 2017 hadi dola za Marekani 1,634.2 mwaka 2018.

**Bidhaa Zisizo Asilia**

100. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 3,209.3 kutoka dola milioni 3,091.9 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani, mazao ya mboga na maua pamoja na bidhaa nyinginezo.

**Madini**

101. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya madini nje ilipungua kwa asilimia 4.8 kufikia dola za Marekani milioni 1,615.3 ikilinganishwa na dola milioni 1,694.5 mwaka 2017. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa mauzo ya dhahabu iliyouzwa nje pamoja na madini mengine. Aidha, thamani ya mauzo ya dhahabu ilikuwa dola za Marekani milioni 1,524.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 1,541.1 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 1.1. Mapato ya mauzo ya madini yalichangia asilimia 50.3 ya mapato yote ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2018.

**Bidhaa za Viwandani**

102. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 794.6 kutoka dola milioni 693.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani nchi za nje hususan, marumaru, vifaa vya plastiki na alumini (aluminium products). Aidha, mapato ya mauzo ya bidhaa za viwandani yalichangia asilimia 24.8 ya mapato yote ya bidhaa zisizo asilia mwaka 2018.

**Samaki na Mazao ya Samaki**

103. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya samaki na mazao yake ilipungua hadi dola za Marekani milioni 158.4 kutoka dola milioni 193.0 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 17.9. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa kiasi cha samaki na mazao ya samaki kilichouzwa nje.

**Mazao ya Mboga na Maua**

104. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya mazao ya mboga na maua ilikuwa dola za Marekani milioni 33.0 ikilinganishwa na dola milioni 27.2 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 21.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mboga na maua na kuimarika kwa bei katika soko la dunia.

**Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje**

105. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya bidhaa nyinginezo zilizouzwa nje iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 432.5 kutoka dola milioni 357.1 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 21.1. Bidhaa zilizopo katika kundi hili ni pamoja na mbegu za mafuta, kakao, ngozi na nafaka, ambazo kwa pamoja zilichangia takriban asilimia 75 ya mauzo katika kundi hili.

**Jedwali Na. 4.1: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje**

| Bidhaa | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko, % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia** | | | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 186.6 | 171.0 | 121.5 | 162.2 | 153.7 | 126.3 | 147.9 | 17.1 |
| Kiasi ('000 tani) | 54.8 | 59.5 | 44.1 | 51.9 | 58.7 | 41.8 | 56.6 | 35.4 |
| Bei (US$ kwa tani) | 3,403.2 | 2,872.7 | 2,756.2 | 3,123.0 | 2,616.8 | 3,019.5 | 2,612.0 | -13.5 |
| **Pamba** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 164.9 | 111.7 | 54.7 | 30.2 | 46.8 | 36.8 | 68.4 | 86.0 |
| Kiasi ('000 tani) | 132.0 | 89.0 | 49.5 | 29.1 | 33.0 | 25.3 | 47.4 | 86.8 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,249.7 | 1,256.0 | 1,104.9 | 1,037.8 | 1,416.1 | 1,450.3 | 1,444.2 | -0.4 |
| **Katani** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 18.4 | 16.9 | 16.8 | 26.5 | 17.2 | 28.7 | 33.2 | 15.6 |
| Kiasi ('000 tani) | 13.5 | 12.6 | 11.5 | 15.2 | 8.6 | 17.0 | 20.4 | 19.8 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,357.1 | 1,341.6 | 1,459.7 | 1,748.8 | 2,002.1 | 1,686.7 | 1,627.0 | -3.5 |
| **Chai** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 56.1 | 56.9 | 45.7 | 44.0 | 44.8 | 49.1 | 45.9 | -6.5 |
| Kiasi ('000 tani) | 27.2 | 28.8 | 29.2 | 27.5 | 26.3 | 27.5 | 26.9 | -2.3 |
| Bei (US$ kwa tani) | 2,061.2 | 1,977.9 | 1,568.1 | 1,600.9 | 1,700.8 | 1,783.6 | 1,707.4 | -4.3 |
| **Tumbaku** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 350.1 | 307.0 | 315.0 | 287.6 | 339.2 | 195.8 | 270.3 | 38.0 |
| Kiasi ('000 tani) | 105.6 | 67.8 | 67.4 | 66.3 | 74.3 | 48.3 | 72.2 | 49.6 |
| Bei (US$ kwa tani) | 3,316.0 | 4,526.1 | 4,673.5 | 4,336.5 | 4,562.7 | 4,055.6 | 3,741.9 | -7.7 |
| **Korosho** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 142.6 | 162.4 | 222.2 | 218.8 | 320.2 | 529.6 | 196.5 | -62.9 |
| Kiasi ('000 tani) | 130.9 | 147.3 | 172.2 | 171.7 | 217.5 | 329.4 | 120.2 | -63.5 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,089.3 | 1,102.5 | 1,290.7 | 1,273.8 | 1,472.4 | 1,607.7 | 1,634.2 | 1.6 |
| **Karafuu** | | | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 38.1 | 43.0 | 52.9 | 24.1 | 39.3 | 54.4 | 10.5 | -80.7 |
| Kiasi ('000 tani) | 3.4 | 4.1 | 4.7 | 2.8 | 4.9 | 6.9 | 1.3 | -81.0 |
| Bei (US$ kwa tani) | 11,198.5 | 10,562.8 | 11,231.3 | 8,653.1 | 7,976.0 | 7,886.6 | 8,031.7 | 1.8 |
| **Jumla (Bidhaa Asilia)** | **956.7** | **868.9** | **828.8** | **793.3** | **961.2** | **1,020.7** | **772.8** | **-24.3** |
| **Bidhaa Zisizo Asilia (US$ millioni)** | | | | | | | | |
| **Madini** | **2,197.8** | **1,782.1** | **1,469.2** | **1,285.4** | **1,930.0** | **1,694.5** | **1,615.3** | **-4.7** |
| Dhahabu | 2,117.4 | 1,644.8 | 1,324.1 | 1,183.3 | 1,508.8 | 1,541.1 | 1,524.0 | -1.1 |
| Almasi | 30.2 | 48.8 | 78.2 | 53.2 | 38.9 | 64.4 | 81.8 | 26.9 |
| Madini mengine | 50.2 | 88.5 | 66.9 | 48.9 | 382.3 | 88.9 | 9.5 | -89.3 |
| **Bidhaa za Viwandani** | **1,037.3** | **1,072.1** | **1,239.6** | **1,277.0** | **714.2** | **693.7** | **794.6** | **14.5** |
| Nyuzi za Pamba | 5.8 | 10.9 | 10.8 | 11.9 | 16.8 | 16.1 | 16.8 | 3.9 |
| Kahawa iliyozalishwa | 1.0 | 1.1 | 1.2 | 0.3 | 0.5 | 1.2 | 2.0 | 69.3 |
| Tumbaku iliyozalishwa | 24.6 | 32.2 | 33.6 | 33.0 | 31.6 | 22.3 | 21.6 | -2.8 |
| Mazao ya Katani | 9.1 | 9.7 | 10.5 | 17.4 | 22.3 | 26.3 | 21.4 | -18.8 |
| Mazao mengine ya Viwandani | 996.8 | 1,018.2 | 1,183.4 | 1,214.4 | 643.1 | 627.9 | 732.8 | 16.7 |
| **Samaki na Mazao ya Samaki** | **160.6** | **130.6** | **195.0** | **173.5** | **143.7** | **193.0** | **158.4** | **-17.9** |
| **Mazao ya Mboga na Maua** | **31.3** | **28.1** | **30.5** | **24.4** | **24.8** | **27.2** | **33.0** | **21.6** |
| **Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)** | **181.7** | **172.8** | **177.0** | **385.8** | **187.7** | **126.5** | **175.6** | **38.8** |
| **Bidhaa nyinginezo** | **555.7** | **517.6** | **687.2** | **894.0** | **538.1** | **357.1** | **432.5** | **21.1** |
| **Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)** | **4,164.4** | **3,703.3** | **3,798.6** | **4,040.1** | **3,538.5** | **3,091.9** | **3,209.3** | **3.8** |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 768.2 | 685.8 | 566.8 | 483.3 | 450.0 | 411.3 | 398.2 | -3.2 |
| **JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)** | **5,889.2** | **5,258.1** | **5,194.1** | **5,316.8** | **4,949.7** | **4,523.9** | **4,380.3** | **-3.2** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

## Mapato ya Huduma

106. Mwaka 2018**,** mapato yatokanayo na biashara ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 4,014.7 ikilinganishwa na dola milioni 3,831.9 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za safari (hususan utalii), usafirishaji na mawasiliano. Katika kipindi hicho, mapato yatokanayo na huduma za safari za utalii yalikuwa dola za Marekani milioni 2,449.4 ikilinganishwa na dola milioni

2,250.3 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Hii ilitokana na juhudi za Serikali kutangaza vivutio vya utalii. Aidha, mapato yatokanayo na huduma ya usafirishaji yaliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,222.1 ikilinganishwa na dola milioni 1,137.4 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Hii ilitokana kuongezeka kwa usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani baada ya kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani na kuongezeka kwa ufanisi katika bandari ya Dar es Salaam. Vile vile, mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano yalikuwa dola za Marekani milioni 27.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 18.4 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 47.3.

**Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje**

107. Mwaka 2018, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 8,173.8 ikilinganishwa na dola milioni 7,551.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.2. Ongezeko hilo lilitokana na kupanda kwa thamani ya bidhaa za kukuza mitaji hususan bidhaa za majengo na ujenzi, vifaa vya usafirishaji pamoja na bidhaa za matumizi ya kati.

**Bidhaa za Kukuza Mitaji**

108. Mwaka 2018, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoingizwa nchini iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 3,187.3 ikilinganishwa na dola milioni 2,688.4 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 18.6. Ongezeko hilo lilitokana na kupanda kwa thamani ya vifaa vya usafirishaji, bidhaa za majengo na ujenzi, na mitambo iliyoagizwa kutoka nje. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa za majengo na ujenzi iliongezeka kwa asilimia 48.2, vifaa vya usafirishaji asilimia 26.9 na mitambo asilimia 2.3.

**Bidhaa za Kati**

109. Mwaka 2018, thamani ya bidhaa za kati zilizoingizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 3.8 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,807.2 kutoka dola milioni 2,704.4 mwaka 2017. Kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za kati kulitokana na kupanda kwa thamani ya bidhaa za mafuta ya petroli, mbolea na malighafi za viwandani. Thamani ya bidhaa za mafuta ya petroli zilizoagizwa iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,871.5 ikilinganishwa na dola milioni 1,850.6 mwaka 2017. Kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za mafuta ya petroli kulitokana na kupanda kwa wastani wa bei katika soko la dunia pamoja na kuongezeka kwa kiasi kilichoagizwa nje. Aidha,

thamani ya bidhaa za mbolea iliongezeka kwa asilimia 33.2 na kufikia dola za Marekani milioni 166.4 kutoka dola 124.9 mwaka 2017. Vile vile, thamani ya malighafi za viwandani zilizoagizwa iliongezeka kwa asilimia 5.5 na kufikia dola za Marekani milioni 769.2 kutoka na dola milioni 728.9 mwaka 2017.

### Bidhaa za Matumizi ya Kawaida

110. Mwaka 2018, thamani ya uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 2,177.1 kutoka dola milioni 2,156.7 mwaka 2017. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida zisizohusisha bidhaa za chakula. Uagizaji wa bidhaa za chakula ulipungua kutokana na kuimarika kwa uzalishaji ndani ya nchi.

### Malipo ya Huduma

111. Mwaka 2018, malipo ya huduma yalikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 2,163.4 ikilinganishwa na dola milioni 2,039.9 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya huduma za usafirishaji, bidhaa zilizoagizwa toka nje, huduma ya ujenzi, na huduma nyingine za biashara.

**Jedwali Na. 4.2: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje (Dola za Marekani)**


| Bidhaa | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko, % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa za Kukuza Mitaji** | **3,460.4** | **3,598.1** | **3,813.0** | **3,497.4** | **2,688.4** | **3,187.3** | **18.6** |
| Vifaa vya Usafirishaji | 1,160.2 | 1,214.8 | 1,096.5 | 907.7 | 694.2 | 880.6 | **26.9** |
| Majengo na Ujenzi | 959.8 | 1,032.4 | 908.0 | 817.2 | 581.8 | 862.4 | **48.2** |
| Mitambo | 1,340.5 | 1,351.0 | 1,808.4 | 1,772.5 | 1,412.5 | 1,444.3 | **2.3** |
| **Bidhaa za Kati** | **5,205.2** | **4,663.6** | **3,696.6** | **2,863.2** | **2,704.4** | **2,807.2** | **3.8** |
| Uagizaji Mafuta | 4,308.6 | 3,656.8 | 2,760.7 | 1,807.7 | 1,850.6 | 1,871.5 | **1.1** |
| Mbolea | 160.1 | 122.8 | 145.6 | 118.6 | 124.9 | 166.4 | **33.2** |
| Malighafi za Viwanda | 736.6 | 884.0 | 790.4 | 937.0 | 728.9 | 769.2 | **5.5** |
| **Bidhaa za Matumizi ya Kawaida** | **2,361.3** | **2,653.9** | **2,331.3** | **2,100.8** | **2,156.7** | **2,177.1** | **0.9** |
| Bidhaa za Vyakula | 646.4 | 632.6 | 541.7 | 445.5 | 405.3 | 262.0 | **-35.3** |
| Bidhaa Nyingine za Matumiza | 1,714.9 | 2,021.3 | 1,789.6 | 1,655.4 | 1,751.4 | 1,915.1 | **9.3** |
| **Jumla (FoB)** | **11,029.1** | **10,917.8** | **9,843.1** | **8,463.6** | **7,551.7** | **8,173.8** | **8.2** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

**Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali**

112. Mwaka 2018, nchi ambazo Tanzania iliagiza bidhaa zake kwa kiasi kikubwa zilikuwa Saudi Arabia, China, India, Umoja wa Falme za Kiarabu, Norway, Malaysia, Indonesia, Afrika Kusini, Uswisi, Uingereza, Marekani na Japani ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 50.1 ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje. Sehemu kubwa ya bidhaa zilizoagizwa ni mafuta ya petroli kutoka nchi za Saudi Arabia na Falme za Kiarabu pamoja na mitambo, matrekta na bidhaa za kielektroniki kutoka China. Aidha, bidhaa za magari na chuma ziliagizwa kutoka India, Japani, China na Afrika Kusini.

**Kielelezo Na. 1.4: Mchanganuo wa Vyanzo vya Bidhaa Zilizoingia Nchini mwaka 2018**





**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

113. Mwaka 2018, nchi ambazo Tanzania iliuza bidhaa zake kwa kiasi kikubwa zilikuwa ni Afrika Kusini, India, Uswisi, Ubelgiji, China, Japani na Vietnam ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 52.9 ya bidhaa zote zilizouzwa nje. Aidha, bidhaa zilizouzwa Ubelgiji, China, India, Japani na Vietnam ni pamoja na mbegu za mafuta, tumbaku, kahawa na korosho. Kwa upande mwingine,

bidhaa za mahindi, maharage, vyandarua, mboga mboga na nafaka ziliuzwa Kenya na dhahabu iliuzwa India na Uswisi.

**Kielelezo Na. 4.2: Mchanganuo wa Masoko ya Bidhaa za Tanzania Nje ya Nchi Mwaka 2018**




**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**Mizania ya Malipo na Nchi za Nje**

**Urari wa Malipo Yote**

114. Mwaka 2018, urari wa malipo yote ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 784.0 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 1,669.6 mwaka 2017. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma Nje**

115. Mwaka 2018, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,942.1 ikilinganishwa na nakisi ya dola milioni

1,235.8 mwaka 2017, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 57.2.Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kutoka dola za Marekani milioni 9,591.6 mwaka 2017 hadi dola milioni 10,337.1 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia kiasi cha dola za Marekani milioni 8,395.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 8,355.8 mwaka 2017.

**Urari wa Biashara ya Bidhaa**

116. Urari wa biashara ya bidhaa uliongezeka kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 3,027.8 mwaka 2017 hadi nakisi ya dola milioni 3,793.5 mwaka 2018, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 25.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje.

**Urari wa Biashara ya Huduma**

117. Mwaka 2018, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,851.3 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 1,792.0 mwaka 2017, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 3.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma hususan, katika biashara ya utalii na kupungua kwa malipo ya huduma za safari.

**Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi**

118. Mwaka 2018, urari wa mapato ya vitega uchumi ambayo yanajumuisha kiasi cha malipo yatokanayo na ajira kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 870.9 ikilinganishwa na nakisi ya dola milioni 1,046.9 mwaka 2017, sawa na upungufu wa nakisi ya asilimia 16.8. Kupungufu kwa nakisi kulitokana na kuongezeka kwa mapato ya uwekezaji.

**Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida**

119. Urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha unaofanywa na sekta binafsi, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 468.5 mwaka 2018 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 402.0 mwaka 2017, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 16.5. Ongezekola ziada lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na biashara ya huduma.

**Urari wa Malipo ya Kawaida**

120. Mwaka 2018, urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,498.7 ikilinganishwa na dola milioni 1,880.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 32.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa nakisi ya biashara ya bidhaa na huduma.

**Urari wa Uhamisho wa Mitaji**

121. Mwaka 2018, urari wa uhamisho wa mitaji, unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 480.1 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 376.8 mwaka 2017, sawa na ongezeko la ziada kwa asilimia 27.4. Kuongezeka kwa ziada ya urari wa uhamisho wa mitaji kulitokana na kuongezeka kwa misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

**Urari wa Rasilimali ya Kifedha**

122. Mwaka 2018, urari wa malipo katika rasilimali ya kifedha, unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,883.8 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 2,154.9 mwaka 2017, sawa na upungufu wa ziada kwa asilimia 12.6. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa uwekezaji wa mikopo ya fedha.

**Akiba ya Fedha za Kigeni**

123. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha na kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuongeza imani kwa wawekezaji. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2018, akiba ya fedha za kigeni (bila kujumuisha bidhaa na huduma ambazo zinalipiwa na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja) ilifikia dola za Marekani milioni 5,044.6 ikilinganishwa na dola milioni 5,906.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Kiasi hicho cha akiba ya fedha za kigeni kilikuwa kinatosheleza kulipia uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.9 ikilinganishwa na miezi 5.4 mwaka 2017. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, akiba ya fedha za kigeni za benki iliongezeka hadi

kufikia dola za Marekani milioni 966.7 kutoka dola milioni 726.6 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 33.0.

**Soko la Fedha za Kigeni kwa Mabenki**

124. Mwaka 2018, viwango vya ubadilishanaji wa fedha za kigeni viliendelea kuamuliwa na nguvu ya soko. Kiasi cha fedha kilichouzwa katika soko la fedha za kigeni kilikuwa dola za Marekani milioni 1,302.8 ikilinganishwa na dola milioni 2,081.2 mwaka 2017. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania iliuza jumla ya dola za Marekani milioni 528.6, sawa na asilimia 40.5 ya mauzo yote yaliyofanyika mwaka 2018 na kiasi kilichobaki kiliuzwa na benki za biashara.

**Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania**

125. Mwaka 2018, dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 2,263.8 ikilinganishwa na shilingi 2,228.9 mwaka 2017. Mwenendo huu wa thamani ya shilingi ulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuimarika kwa dola ya Marekani na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za kigeni kwa ajili ya bajeti ya Serikali. Aidha, dola moja ya Marekani iliuzwa kwa wastani wa shilingi 2,281.2 mwishoni mwa mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,230.1 mwishoni mwa mwaka 2017.

## THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na.25 Shs. Milioni

| Aina ya Bidhaa | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje | 5,343,693 | 7,331,020 | 8,653,372 | 8,223,206 | 7,434,928 | 8,656,231 | 9,716,889 | 9,081,599 | 8,727,419 |
| Bidhaa Halisi | 5,165,013 | 7,175,377 | 8,363,496 | 7,012,100 | 7,060,772 | 7,979,691 | 9,303,457 | 8,779,726 | 8,307,170 |
| Zilizouzwa Tena | 178,680 | 155,643 | 289,875 | 1,211,106 | 374,156 | 676,540 | 413,431 | 301,873 | 420,249 |
| Zilizoagizwa | 11,131,917 | 17,112,779 | 18,275,893 | 19,904,472 | 20,977,104 | 21,475,090 | 20,660,282 | 17,380,607 | 19,368,436 |
| **Jumla** | 16,475,610 | 24,443,799 | 26,929,265 | 28,127,678 | 28,412,032 | 30,131,321 | 30,377,171 | 26,462,206 | 28,095,855 |
| Urari | (5,788,224) | (9,781,759) | (9,622,521) | (11,681,266) | (13,542,176) | (12,818,859) | (10,943,393) | (8,299,008) | (10,641,017) |
| Thamani ya Fedha (Shs/US$) | 1,395.68 | 1,557.43 | 1,571.71 | 1,598.66 | 1,652.51 | 1,985.40 | 2,177.59 | 2,228.63 | 2,269.88 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya Forodha na Benki Kuu ya Tanzania

## KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 26

| Bidhaa | Kiasi(000" Tani) | | | | | | | Thamani(sh. Milioni) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko(%) 2017/18 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) 2017/18 |
| Kahawa | 59.5 | 44.1 | 51.9 | 58.7 | 41.8 | 56.6 | 35.4 | 259,132 | 204,301 | 315,921 | 335,629 | 282,427 | 337,459 | 19.5 |
| Pamba | 89.0 | 49.5 | 29.1 | 33.0 | 25.3 | 47.4 | 86.8 | 137,663 | 558,404 | 62,959 | 101,816 | 80,259 | 157,151 | 95.8 |
| Katani | 12.6 | 11.5 | 1.5 | 8.6 | 17.0 | 20.4 | 19.8 | 25,396 | 111,323 | 53,927 | 37,524 | 57,703 | 46,925 | -18.7 |
| Chai | 28.8 | 29.2 | 27.5 | 26.3 | 27.5 | 26.9 | -2.3 | 86,810 | 72,784 | 86,285 | 97,381 | 108,990 | 103,341 | -5.2 |
| Tumbaku | 67.8 | 67.4 | 66.3 | 74.3 | 48.3 | 72.2 | 49.6 | 159,454 | 319,295 | 568,812 | 680,453 | 434,456 | 609,677 | 40.3 |
| Korosho | 147.3 | 172.2 | 171.7 | 217.5 | 329.4 | 120.2 | -63.5 | 301,212 | 647,936 | 430,023 | 587,849 | 1,200,450 | 287,891 | -76.0 |
| Karafuu | 4.1 | 4.7 | 2.8 | 4.9 | 6.9 | 1.3 | -81.0 | 68,429 | 50,880 | 48,912 | 85,454 | 121,237 | 684 | -99.4 |
| Almasi (Carat) | 173,464 | 241,709 | 185,873 | 235,951 | 282,032 | 408,656 | 44.9 | 63,584 | 166,107 | 65,636 | 186,254 | 142,998 | 184,233 | 28.8 |
| Dhahabu(gms) | 35,100,000 | 41,813,100 | 48,394,953 | 81,561,000 | 54,660,377 | 60,784,383 | 11.2 | 2,768,481 | 2,812,561 | 2,717,187 | 3,072,728 | 3,418,902 | 3,435,639 | 0.5 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA


- Takwimu hazikupatikana


**KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 27


| Bidhaa | Kiasi (000" Tani) | | | | | | Badiliko(%) | Thamani (Milioni US$) | | | | | | | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2017/18 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2017/18 |
| Bidhaa Asilia: | | | | | | | | | | | | | | | |
| Kahawa | 59.5 | 44.1 | 51.9 | 58.7 | 41.8 | 56.6 | 35.4 | 186.6 | 171.0 | 121.5 | 162.2 | 153.7 | 126.3 | 147.9 | 17.1 |
| Pamba | 89.0 | 49.5 | 29.1 | 33.0 | 25.3 | 47.4 | 86.8 | 164.9 | 111.7 | 54.7 | 30.2 | 46.8 | 36.8 | 68.4 | 86.0 |
| Katani | 12.6 | 11.5 | 1.5 | 8.6 | 17.0 | 20.4 | 19.8 | 18.4 | 16.9 | 16.8 | 26.5 | 17.2 | 28.7 | 33.2 | 15.6 |
| Chai | 28.8 | 29.2 | 27.5 | 26.3 | 27.5 | 26.9 | (2.3) | 56.1 | 56.9 | 45.7 | 44.0 | 44.8 | 49.1 | 45.9 | -6.5 |
| Tumbaku | 67.8 | 67.4 | 66.3 | 74.3 | 48.3 | 72.2 | 49.6 | 350.1 | 307.0 | 315.0 | 287.6 | 339.2 | 195.8 | 270.3 | 38.0 |
| Korosho | 147.3 | 172.2 | 171.7 | 217.5 | 329.4 | 120.2 | (63.5) | 142.6 | 162.4 | 222.2 | 218.8 | 320.2 | 529.6 | 196.5 | -62.9 |
| Karafuu | 4.1 | 4.7 | 2.8 | 4.9 | 6.9 | 1.3 | (81.0) | 38.1 | 43.0 | 52.9 | 24.1 | 39.3 | 54.4 | 10.5 | -80.7 |
| **Jumla** | | | | | | | | **956.8** | **868.9** | **828.8** | **793.4** | **961.2** | **1020.7** | **772.8** | -24.3 |
| Bidhaa zisizo asilia: | | | | | | | | | | | | | | | |
| Madini | | | | | | | | 2197.8 | 1782.1 | 1469.2 | 1285.4 | 1930.0 | 1694.5 | 1615.3 | -4.7 |
| Bidhaa za Viwanda | | | | | | | | 1037.3 | 1072.1 | 1239.6 | 1364.5 | 1092.1 | 693.7 | 794.6 | 14.5 |
| Samaki na Mazao ya Samaki | | | | | | | | 160.6 | 130.6 | 195.0 | 173.5 | 142.5 | 193.0 | 158.4 | -17.9 |
| Mazao ya Mboga na Maua | | | | | | | | 31.3 | 28.1 | 30.5 | 24.4 | 24.8 | 27.2 | 33.0 | 21.6 |
| Bidhaa zilizouzwa tena | | | | | | | | 181.7 | 172.8 | 177.0 | 385.8 | 480.0 | 126.5 | 175.6 | 38.8 |
| Bidhaa nyinginezo | | | | | | | | 557.7 | 517.6 | 687.2 | 884.3 | 972.2 | 357.1 | 432.5 | 21.1 |
| **Jumla** | | | | | | | | **4166.4** | **3703.3** | **3798.5** | **4117.9** | **4641.6** | **3091.9** | **3209.3** | 3.8 |
| Bidhaa Zisizorekodiwa | | | | | | | | 768.2 | 685.8 | 694.1 | 491.1 | 0.0 | 517.2 | 398.1 | -23.0 |
| **JUMLA KUBWA** | | | | | | | | **5891.4** | **5258.0** | **5321.4** | **5402.4** | **5602.8** | **4629.8** | **4380.3** | -5.4 |


Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA


I: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE
(US$ Milioni)
US$ Milioni
4500.00
4000.00
3500.00
3000.00
2500.00
2000.00
1500.00
1000.00
500.00
0.00
2013
2014
2015
2016
2017
2018
Bidhaa asilia
Bidhaa zisizo asilia



II: PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE
(Kiasi kwa Tani '000)
'000 Tani
100.0
90.0
80.0
70.0
60.0
50.0
40.0
30.0
20.0
10.0
0.0
2013
2014
2015
2016
2017
2018
Kahawa
Pamba


IIIA: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2017
Bidhaa Zisizorekodiwa 11.2%
Bidhaa nyinginezo 7.7%
Kahawa 2.7%
Pamba 0.8%
Katani 0.6%
Chai 1.1%
Tumbaku 4.2%
Korosho 11.4%
Karafuu 1.2%
Bidhaa zilizouzwa tena 2.7%
Mboga na Maua 0.6%
Samaki na Mazao ya Samaki 4.2%
Bidha za Viwanda 15.0%
Madini 36.6%


IIIB: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2018
Bidhaa zilizouzwa tena
4.0%
Mboga na Maua
0.8%
Bidhaa Zisizorekodiwa
9.1%
Bidhaa nyinginezo
9.9%
Samaki na Mazao ya Samaki
3.6%
Kahawa
3.4%
Pamba
1.6%
Bidha za Viwanda
18.1%
Katani
0.8%
Chai
1.0%
Korosho
4.5%
Tumbaku
6.2%
Madini
36.9%
Karafuu
0.2%

**WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 28 Sh./Tani*

| Bidhaa | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 4,069,399 | 5,580,087 | 5,400,679 | 4,135,909 | 4,284,297 | 6,084,327 | 5,563,694 | 6,703,080 | 5,818,259 | -13.2 |
| Pamba | 1,775,008 | 1,431,997 | 1,724,164 | 2,016,331 | 4,196,444 | 2,164,592 | 3,080,982 | 3,210,269 | 3,099,629 | -3.4 |
| Katani | 1,986,211 | 2,091,121 | 2,102,332 | 2,129,059 | 2,052,892 | 3,554,124 | 2,473,086 | 3,539,730 | 3,910,441 | 10.5 |
| Chai | 2,501,897 | 2,664,933 | 3,144,333 | 3,392,989 | 2,617,376 | 3,139,968 | 3,543,747 | 3,956,329 | 3,841,655 | -2.9 |
| Tumbaku | 2,586,996 | 2,564,562 | 3,145,641 | 2,237,711 | 4,172,482 | 8,576,002 | 10,259,213 | 8,998,738 | 8,444,281 | -6.2 |
| Korosho | 1,284,308 | 1,636,560 | 1,695,963 | 1,943,340 | 3,255,142 | 2,503,867 | 3,422,830 | 3,625,943 | 3,733,995 | 3.0 |
| Karafuu | 4,390,290 | 20,972,246 | 9,783,616 | 16,735,615 | 17,997,878 | 17,576,080 | 17,439,592 | 17,570,634 | 11,525,538 | -34.4 |
| Almasi (kwa carat) | 38,695 | 40,709 | 99,809 | 353,966 | 317,548 | 353,123 | 789,375 | 507,027 | 205,594 | -59.5 |
| Dhahabu (kwa gramu) | 60,038 | 85,738 | 89,993 | 78,874 | 64,709 | 56,146 | 37,674 | 62,548 | 56,522 | -9.6 |

Chanzo:Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu


## WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 29 US$/Tani*

| Bidhaa | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko(%) 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 2,853 | 3,655 | 3,403 | 2,873 | 2,756 | 3,123 | 2,557 | 3,019 | 2,585 | -14.4 |
| Pamba | 1,242 | 1,529 | 1,250 | 1,256 | 1,105 | 1,038 | 1,416 | 1,438 | 1,371 | -4.7 |
| Katani | 940 | 1,224 | 1,357 | 3,142 | 1,460 | 1,749 | 2,002 | 1,579 | 1,735 | 9.9 |
| Chai | 1,840 | 1,740 | 2,061 | 1,978 | 1,568 | 1,601 | 1,696 | 1,777 | 1,708 | -3.9 |
| Tumbaku | 4,337 | 3,839 | 3,316 | 4,526 | 4,673 | 4,336 | 4,732 | 4,056 | 3,744 | -7.7 |
| Korosho | 963 | 1,110 | 1,089 | 1,103 | 1,291 | 1,274 | 1,599 | 1,636 | 1,674 | 2.3 |
| Karafuu | 3,450 | 13,163 | 11,189 | 10,563 | 11,231 | 8,653 | 7,976 | 7,884 | 5,111 | -35.2 |
| Almasi (kwa carat) | 3,028 | 2,395 | 2,188 | 208 | 187 | 178 | 361 | 228 | 200 | -12.0 |
| Dhahabu (kwa gramu) | 43 | 55 | 57 | 35 | 38 | 28 | 17 | 28 | 25 | -10.7 |

Chanzo: Idara ya forodha, TRA

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu


MWENENDO WA BEI YA PAMBA NA KAHAWA
ILIYOUZWA NCHI ZA NJE (US$/Tani)
3500.0
3000.0
2500.0
2000.0
1500.0
1000.0
500.0
0.0
Dola za M
arekani
2013
2014
2015
2016
2017

**AINA NA THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA TOKA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 31 Sh. Milioni

| Mwaka | Bidhaa za Matumizi ya Kawaida | Bidhaa za Kati | Bidhaa za Viwanda | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2001 | 468173 | 386317 | 648361 | 1502851 |
| 2002 | 499346 | 408872 | 697209 | 1605426 |
| 2003 | 654630 | 705729 | 846251 | 2206610 |
| 2004 | 917953 | 1024705 | 1029389 | 2972046 |
| 2005 | 937031 | 1451062 | 1341462 | 3729555 |
| 2006 | 1068550 | 1977695 | 1799855 | 4846100 |
| 2007 | 1393799 | 2441781 | 2186910 | 6022490 |
| 2008 | 1703932 | 3217747 | 3537543 | 8459222 |
| 2009 | 1836142 | 2471066 | 3319331 | 7626538 |
| 2010 | 2385447 | 3825823 | 3789528 | 10000799 |
| 2011 | 3314193 | 6446217 | 5545242 | 15305652 |
| 2012 | 3634506 | 6790046 | 5794109 | 16218662 |
| 2013 | 3774926 | 8321368 | 5532070 | 17628363 |
| 2014 | 4385587 | 7706629 | 5946049 | 18038265 |
| 2015 | 4628549 | 7339405 | 7570307 | 19538260 |
| 2016 | 4573589 | 6233387 | 7614215 | 18421191 |
| 2017 | 4806982 | 6027729 | 5992067 | 16826779 |
| 2018 | 4911102 | 6332482 | 7189911 | 18433495 |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*Angalia: Kuanzia mwaka 1990, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ni f.o.b. badala ya c.i.f.


**MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE**

Jedwali Na. 32 US $ milioni

| | 2010 Halisi | 2011 Halisi | 2012 Halisi | 2013 Halisi | 2014 Halisi | 2015 Halisi | 2016 Halisi | 2017 Halisi | 2018 Halisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Urari wa Biashara** | **-2841.2** | **-4729.6** | **-4429.9** | **-5771.1** | **-5723.7** | **-4526.3** | **-3513.9** | **-3027.8** | **-3793.5** |
| Zilizouzwa nje (fob) | 4324.3 | 5097.9 | 5889.2 | 5258.1 | 5194.1 | 5316.8 | 4949.7 | 4523.9 | 4380.3 |
| Zilizonunuliwa toka nje (fob)* | 7165.5 | 9827.5 | 10319.1 | 11029.1 | 10917.8 | 9843.1 | 8463.6 | 7551.7 | 8173.8 |
| Urari wa Huduma | 156.9 | 92.2 | 427.5 | 713.2 | 727.3 | 783.3 | 1422.9 | 1792.0 | 1851.3 |
| Mapato | 2045.7 | 2300.3 | 2786.4 | 3201.7 | 3396.0 | 3412.4 | 3599.3 | 3831.9 | 4014.7 |
| Malipo | 1888.9 | 2208.1 | 2358.9 | 2488.5 | 2668.7 | 2629.1 | 2176.4 | 2039.9 | 2163.4 |
| Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi | -577.6 | -645.8 | -574.0 | -705.7 | -529.5 | -724.3 | -955.1 | -1046.9 | -870.9 |
| Yaliyoingia | 160.1 | 184.2 | 131.1 | 130.1 | 118.4 | 110.3 | 98.5 | 125.3 | 154.9 |
| Yaliyotoka | 737.651 | 830.0 | 705.1 | 835.8 | 647.9 | 834.6 | 1053.6 | 1172.2 | 1025.8 |
| Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida | 1051.2 | 902.2 | 807.5 | 775.1 | 477.3 | 479.9 | 381.5 | 402.0 | 468.5 |
| Iliyoingia | 1130.2 | 994.9 | 913.0 | 836.9 | 535.5 | 560.1 | 452.7 | 485.2 | 535.8 |
| Serikalini | 798.1 | 609.7 | 544.3 | 485.2 | 177.9 | 194.8 | 81.1 | 121.8 | 170.3 |
| Sekta nyingine | 332.1 | 385.2 | 368.7 | 351.7 | 357.6 | 365.3 | 371.6 | 363.4 | 365.5 |
| Iliyotoka | 79.0 | 92.7 | 105.4 | 61.8 | 58.2 | 80.2 | 71.2 | 83.2 | 67.3 |
| **Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali** | **-2210.8** | **-4381.0** | **-3768.9** | **-4988.5** | **-5048.6** | **-3987.4** | **-2664.7** | **-1880.7** | **-2344.5** |
| Urari wa Uhamisho wa Mitaji | 537.9 | 690.9 | 777.2 | 684.5 | 547.9 | 380.1 | 446.2 | 376.8 | 480.1 |
| Iliyoingia | 537.9 | 690.9 | 777.2 | 684.5 | 547.9 | 380.1 | 446.2 | 376.8 | 480.1 |
| Iliyotoka | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Urari katika uwekezaji | 3063.7 | 2843.3 | 3879.6 | 4995.0 | 3218.1 | 2793.9 | 1794.8 | 2154.9 | 1883.8 |
| Uwekezaji katika miradi | 1813.2 | 1229.5 | 1799.6 | 2087.3 | 1416.1 | 1506.0 | 864.0 | 937.7 | 1106.0 |
| Uwekezaji katika hisa | 3.1 | 11.3 | 6.1 | 4.6 | 11.5 | 27.6 | -5.0 | 2.9 | -0.7 |
| Uwekezaji aina nyingine | 1247.4 | 1602.5 | 2073.9 | 2903.1 | 1790.5 | 1260.2 | 935.8 | 1214.2 | 778.6 |
| Makosa na Masahihisho | -1282.3 | -325.2 | -561.8 | -157.4 | 1035.1 | 640.0 | 755.0 | 1044.4 | -456.6 |
| **Urari wa Malipo yote** | **108.5** | **-1171.9** | **326.2** | **533.7** | **-247.5** | **-173.3** | **331.3** | **1695.4** | **-437.2** |

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia mwaka 2006 bidhaa zilizouzwa nje zinajumuisha pia zile zisizorekodiwa (Unrecorded trade)



MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE
3000.0
2000.0
1000.0
0.0
-1000.0
-2000.0
-3000.0
-4000.0
-5000.0
-6000.0
-7000.0
US $ milioni
2012
2013
2014
2015
2016
2017
2018
Urari wa Biashara
Huduma na Uhamisho Mali
Urari wa Malipo yote

# SURA YA 5

# HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

## HALI YA UCHUMI WA DUNIA

### Ukuaji wa Uchumi

126. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia mwaka 2018 iliendelea kusuasua na kutoridhisha kama ilivyokuwa katika miaka iliyotangulia. Uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2017. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na kushuka kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea na zinazoendelea.

127. Mwaka 2018, kasi ya ukuaji wa pato la nchi zilizoendelea ilipungua hadi kufikia asilimia 2.2 ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2017. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa na huduma kutoka nje, kutokuwa na uhakika wa sera za kibajeti, hali ya wasiwasi kuhusu kujitoa kwa Uingereza katika Jumuiya ya Ulaya (Brexit) na kushuka kwa kasi ya uwekezaji.

128. Mwaka 2018, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilipungua hadi kufikia asilimia 4.5 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 mwaka 2017. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na msuguano wa kibiashara baina ya China na Marekani, kudorora kwa soko la fedha kwa nchi za Argentina na Uturuki, na mvutano wa kisiasa Mashariki ya Kati. Kutokana na athari hizo, kasi ya ukuaji wa pato la nchi za Asia zinazoendelea ikijumuisha China na India ilishuka hadi asilimia 6.4 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 6.6 mwaka 2017.

**Jedwali Na 5.1: Pato la Dunia 2014 – 2018**

| | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Ukuaji** | | | | |
| Pato la Dunia | 3.4 | 3.2 | 3.1 | 3.8 | 3.6 |
| Nchi zilizoendelea | 1.9 | 2.1 | 1.6 | 2.4 | 2.2 |
| Nchi zinazoendelea | 4.6 | 4.1 | 4.1 | 4.8 | 4.5 |
| Nchi za Asia Zinazoendelea | 6.8 | 6.7 | 6.3 | 6.6 | 6.4 |
| Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara | 5.1 | 3.4 | 1.6 | 2.9 | 3.0 |

**Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO Aprili 2019

129. Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka hadi asilimia 3.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2017. Ukuaji huu ulitokana na kupanda kwa bei za bidhaa, marekebisho ya sera za kiuchumi pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa zinazozalishwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara katika soko la Dunia.

**Mwenendo wa Bei**

130. Mwaka 2018, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa uzalishaji viwandani hususan, katika nchi zinazoendelea, majanga ya asili na kulegezwa kwa sera za bajeti na fedha kwa baadhi ya nchi. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kufikia asilimia 2.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2017. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia uliongezeka hadi asilimia 2.6 ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta na chakula katika nchi za Cambodia, China, Thailand na Singapore. Mwaka 2018, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 8.5 kutoka wastani wa asilimia 11.0 mwaka 2017. Upungufu huo ulitokana na kuimarika kwa sera za fedha ikiwemo viwango imara vya kubadilisha fedha na kuimarika kwa sera za matumizi.

**Mwenendo wa Biashara Duniani**

131. Mwaka 2018, ukuaji wa shughuli za biashara duniani uliendelea kudhoofika ambapo kasi yake ilikuwa asilimia 3.0 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2017. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mvutano wa biashara baina ya China, Bara la Ulaya na Marekani, nchi nyingi kutokuwa na uhakika wa shughuli za kiuchumi, kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa dunia na hali tete katika masoko ya fedha na masharti magumu ya kifedha.

## USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA

### Jumuiya ya Afrika Mashariki

132. Mwaka 2018, Mkutano wa Kitaifa wa Kamati ya Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ulifanyika Dar es Salaam, Tanzania. Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ulikamilisha uandaaji wa bangokitita la kikanda lenye kuonesha utekelezaji wa maeneo yote ya msingi ya Soko la Pamoja la Jumuiya

ya Afrika Mashariki. Maeneo hayo ni pamoja na soko huru la bidhaa ndani ya Jumuiya; uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kusafiri ndani ya Jumuiya; uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kufanya kazi; uhuru wa kufanya biashara ya huduma; uhuru wa kuwekeza mitaji; haki ya kuanzisha na kuendesha shughuli za biashara na uchumi; na haki ya ukazi katika nchi yoyote. Aidha, mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Fedha na Masuala ya Uchumi ulifanyika mwezi Novemba 2018, jijini Arusha, Tanzania. Mkutano huo uliunda kikosi kazi cha kufanya mapitio ya Mkataba ulioanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki pamoja na kupitisha hadidu za rejea ili kuendana na Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

133. Mwaka 2018, Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifanyika Kampala, Uganda. Lengo la Mkutano huo lilikuwa kujadili maendeleo ya sekta ya miundombinu ya uchukuzi na nishati pamoja na uwekezaji katika sekta ya afya. Katika Mkutano huo, Wakuu wa Nchi walihimiza: ufikiwaji wa malengo ya Mkakati wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (2016/17 – 2020/21); Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; na Malengo Endelevu ya sekta za miundombinu na afya. Aidha, Wakuu wa Nchi waliidhinisha maeneo tisa ya kipaumbele ya uwekezaji katika sekta ya afya; na miradi 17 ya kielelezo (flagship projects) ambayo utekelezaji wake utasimamiwa katika ngazi ya Wakuu wa Nchi. Vile vile, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki liliagizwa kuendelea na mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

134. Mwaka 2018, maonesho ya 19 ya Juakali/Nguvukazi yalifanyika Mjini Eldoret, Kenya. Lengo la maonesho hayo lilikuwa ni kukuza ajira na biashara; kupanua wigo wa masoko ya wajasiriamali; na kuwezesha urasimishaji wa shughuli za sekta zisizo rasmi. Aidha, wajasiriamali walipata fursa ya kukutana na wajasiriamali wa nchi wanachama na kubadilishana taarifa za kibiashara, ujuzi pamoja na huduma. Katika maonesho hayo wajasiriamali 238 kutoka Tanzania walishiriki, ambapo washiriki 192 walitoka Tanzania Bara na washiriki 46 walitoka Zanzibar. Vile vile, wajasiriamali hao waliweza kuuza bidhaa zao na kukuza fursa za upatikanaji wa masoko ya bidhaa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika**

135. Mwaka 2018, Mkutano wa 19 wa Kikosi Kazi cha Mawaziri kuhusu Mtangamano wa Kiuchumi ulifanyika Pretoria, Afrika Kusini. Lengo la mkutano huo lilikuwa kupitia miradi ya miundombinu iliyowasilishwa katika Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ili kuombewa fedha kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) pamoja na washirika wengine wa maendeleo. SADC ilifikia makubaliano na AfDB kufadhili utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya miundombinu.

**Umoja wa Afrika**

136. Mwaka 2018, Mkutano wa 30 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika ulifanyika Addis Ababa. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huo ulijadili taarifa ya Rais wa Jamhuri ya Rwanda ambaye pia ni mwenyekiti wa Kamati ya Kuhuisha Mifumo ya Kitaasisi ya Umoja wa Afrika. Mkutano huo uliazimia kuwa nchi wanachama ziendelee na majadiliano ya namna bora ya kutekeleza mapendekezo ya mabadiliko ya kuhuisha mifumo ya kitaasisi ya Umoja wa Afrika ili kufikia muafaka kwa nchi zote. Aidha, Mkutano huo ulizindua soko moja la usafiri wa anga barani Afrika. Hadi Desemba 2018, nchi wanachama 21 zilisaini mkataba wa soko hilo unaotarajiwa kuchochea utalii na kuongeza ajira. Utekelezaji wa Mkataba huo utazisaidia nchi za Afrika kukua kiuchumi kwa kushiriki kwenye soko la pamoja.

# SURA YA 6

# RASILIMALI WATU

## Idadi ya Watu

137. Mwaka 2018, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 54,199,163 ikilinganishwa na watu 52,554,628 mwaka 2017. Kati ya hao, wanawake walikadiriwa kuwa 27,689,068 sawa na asilimia 51.1 ya watu wote na wanaume 26,510,095 sawa na asilimia 48.9. Aidha, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 52,619,314, sawa na asilimia 97.1 ya watu wote na Tanzania Zanzibar watu 1,579,849, sawa na asilimia 2.9. Makadirio haya yalitokana na maoteo ya idadi ya watu kwa kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na viashiria muhimu vya mabadiliko ya idadi ya watu vikijumuisha uzazi, vifo na uhamiaji.

## Mgawanyiko wa Watu Kimkoa

138. Mwaka 2018, mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na watu wengi zaidi wapatao 5,147,070 sawa na asilimia 9.8 ya watu wote Tanzania Bara ikilinganishwa na watu 5,017,294 mwaka 2017. Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es Salaam ilitokana na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na za kiuchumi na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohamia kutoka mikoa mingine. Mkoa wa Mwanza ulikadiriwa kuwa na watu 3,532,378 sawa na asilimia 6.7 na Kagera watu 3,022,037 sawa na asilimia 5.7. Aidha, mkoa wa Katavi ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu ikilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania Bara, ukikadiriwa kuwa na watu 738,237 sawa na asilimia 1.4, ukifuatiwa na mikoa ya Njombe na Lindi iliyokuwa na watu 803,299 na 983,738 mtawalia. Kwa upande wa Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na watu wengi zaidi ikilinganishwa na mikoa mingine, ukiwa na watu takribani 700,791, sawa na asilimia 44.4 ya watu wote Tanzania Zanzibar ukifuatiwa na mkoa wa Kaskazini Pemba uliokadiriwa kuwa na watu 271,594 sawa na asilimia 17.2 na mkoa wa Kusini Unguja ukiwa na idadi ndogo zaidi ya watu 133,767, sawa na asilimia 8.5.

139. Mwaka 2018, msongamano wa watu kwa Tanzania ulikuwa na wastani wa watu 61.2 kwa kila kilometa moja ya mraba. Aidha, kwa upande wa Tanzania Bara msongamano ulikuwa na wastani wa watu 59.6 kwa kila kilometa moja ya

mraba. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa zaidi wa watu, ukiwa na watu 3,695 kwa kila kilometa moja ya mraba, ukifuatiwa na Mwanza (watu 373.1), Kagera (watu 119.6), na Kilimanjaro (watu 104.7). Mkoa wa Lindi ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu kwa kila kilometa moja ya mraba ikiwa na wastani wa watu 14.9, ikifuatiwa na mikoa ya Katavi na Ruvuma iliyokuwa na wastani wa watu 16.1 na 24.8 kwa kila kilometa moja ya mraba mtawalia. Kwa upande wa Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 3,046.9 kwa kila kilometa moja ya mraba wakati Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na wastani wa watu 156.6 kwa kila kilometa moja ya mraba.

140. Mwaka 2018, watoto wenye umri chini ya miaka mitano walikuwa 9,408,347 sawa na asilimia 17.4 ya idadi ya watu wote Tanzania. Watu wenye umri kuanzia miaka 5 hadi 14 walikuwa 14,259,320, sawa na asilimia 26.3 ya watu wote Tanzania. Aidha, watu wenye umri wa miaka 15 hadi 24 walikuwa 10,675,520 sawa na asilimia 19.7 ya watu wote Tanzania. Vile vile, idadi ya watu wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 64 ilikuwa 18,148,819 sawa na asilimia 33.5 ya watu wote na wazee wenye umri zaidi ya miaka 64 walikuwa 1,707,157 sawa na asilimia 3.1 ya watu wote Tanzania. Katika kipindi hicho, watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ambao ni nguvukazi ya Taifa walikuwa 28,824,339, sawa na asilimia 53.2 ya watu wote Tanzania.

141. Mwaka 2018, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania ulisajili watafutakazi 21,684 ikilinganishwa na watafutakazi 1,344 mwaka 2017. Kuongezeka kwa usajili kulitokana na zoezi maalum lililofanywa na Wakala la kusajili watafutakazi wenye ujuzi unaohitajika katika mradi wa ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga. Aidha, katika kipindi hicho, watafutakazi 3,823 walipatiwa ushauri wa uchaguzi wa fani, mafunzo na kazi stahiki kulingana na sifa zao na mahitaji ya soko la ajira ili kuwawezesha kujiajiri na kuajirika.

142. Mwaka 2018, watafutakazi 607 waliunganishwa na waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi ikilinganishwa na watafutakazi 339 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 79.1. Aidha, watafutakazi 2,253 walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na watafutakazi 448 mwaka 2017. Vile vile, mafunzo hayo

yalitolewa kwa wanafunzi 1,052 wa vyuo mbalimbali vya elimu ya juu ikilinganishwa na wanafunzi 520 mwaka 2017. Katika kipindi hicho, Wakala ulitembelea waajiri na kuandikisha nafasi za kazi 395 zenye fursa za ajira 494 ikilinganishwa na nafasi za kazi 115 zenye fursa za ajira 315 mwaka 2017. Ongezeko la nafasi za kazi na fursa za ajira lilitokana na juhudi za Wakala kuwatembelea waajiri pamoja na kuongezeka kwa waajiri wanaotumia huduma za Wakala kufuatia uboreshwaji wa huduma.

143. Mwaka 2018, Wakala kwa kushirikiana na taasisi binafsi za ajira na Balozi za Tanzania katika nchi husika ulipitia na kuridhia mikataba ya Watanzania 237 kufanya kazi nje ya nchi hususan katika nchi za Oman, Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu. Aidha, Serikali ilifanya mapitio ya mfumo na utaratibu wa kuunganisha wafanyakazi na fursa za ajira nje ya nchi ili kuwezesha wananchi kunufaika na fursa na kuboresha mazingira ya kazi.

**IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2010-2018**

**Jedwali Na.33**

| Mkoa | 2010 | 2011 | 2012** | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 2111764 | 2163817 | 2083588 | 2127416 | 2172165 | 2217856 | 2264508 | 2419941 | 2492989 |
| Arusha | 1664780 | 1711624 | 1694310 | 1741396 | 1789791 | 1839531 | 1890653 | 1948219 | 1999907 |
| Kilimanjaro | 1635870 | 1669174 | 1640087 | 1669051 | 1698526 | 1728522 | 1759048 | 1823151 | 1864329 |
| Tanga | 1966908 | 2010480 | 2045205 | 2091341 | 2138517 | 2186757 | 2236086 | 2284712 | 2337053 |
| Morogoro | 2115275 | 2162197 | 2218492 | 2271310 | 2325386 | 2380750 | 2437431 | 2531268 | 2596287 |
| Pwani | 1062574 | 1086658 | 1098668 | 1122685 | 1147227 | 1172306 | 1197933 | 1236481 | 1265504 |
| Dar es Salaam | 3118132 | 3194903 | 4364541 | 4617000 | 4884061 | 5166570 | 5465420 | 5017294 | 5147070 |
| Lindi | 923607 | 941884 | 864652 | 872758 | 880939 | 889197 | 897533 | 963465 | 983738 |
| Mtwara | 1323568 | 1349235 | 1270854 | 1286501 | 1302340 | 1318374 | 1334606 | 1397723 | 1424083 |
| Ruvuma | 1375017 | 1412084 | 1376891 | 1406411 | 1436563 | 1467362 | 1498821 | 1543869 | 1579811 |
| Iringa | 1737382 | 1764285 | 941238 | 951964 | 962813 | 973784 | 984882 | 1068695 | 1095172 |
| Mbeya | 2662156 | 2743084 | 2707410 | 2781971 | 2858585 | 2937310 | 1883024 | 2006072 | 2070412 |
| Singida | 1367481 | 1404065 | 1370637 | 1402820 | 1435758 | 1469469 | 1503972 | 1569304 | 1612854 |
| Tabora | 2349374 | 2443049 | 2291623 | 2359642 | 2429679 | 2501796 | 2576053 | 2769093 | 2870522 |
| Rukwa | 1503184 | 1558200 | 1004539 | 1037259 | 1071044 | 1105931 | 1141953 | 1160568 | 1195550 |
| Kigoma | 1814158 | 1891173 | 2127930 | 2179598 | 2232520 | 2286727 | 2342250 | 2528708 | 2616200 |
| Shinyanga | 3841787 | 3998664 | 1534808 | 1566734 | 1599325 | 1632593 | 1666554 | 1816316 | 1874709 |
| Kagera | 2563870 | 2661671 | 2458023 | 2537021 | 2618558 | 2702715 | 2789577 | 2919942 | 3022037 |
| Mwanza | 3566263 | 3669380 | 2772509 | 2856258 | 2942537 | 3031422 | 3122992 | 3393620 | 3532378 |
| Mara | 1822866 | 1891907 | 1743830 | 1787279 | 1831810 | 1877451 | 1924230 | 2123683 | 2209143 |
| Manyara | 1388295 | 1441771 | 1425131 | 1471083 | 1518516 | 1567479 | 1618020 | 1692667 | 1750864 |
| Njombe | - | - | 702097 | 707698 | 713345 | 719036 | 724772 | 786347 | 803299 |
| Katavi | - | - | 564604 | 583160 | 602325 | 622121 | 642567 | 706472 | 738237 |
| Simiyu | - | - | 1584157 | 1613580 | 1643549 | 1674075 | 1705168 | 1998224 | 2094798 |
| Geita | - | - | 1739530 | 1785824 | 1833350 | 1882141 | 1932230 | 2148409 | 2239949 |
| Songwe | - | - | | | | | 1136415 | 1166094 | 1202419 |
| **Tanzania Bara** | **41914311** | **43169305** | **43625354** | **44827757** | **46069230** | **47351275** | **48676698** | **51020337** | **52619314** |
| | | | | | | | | | |
| Kaskazini Unguja | 177095 | 183209 | 187455 | 193551 | 199844 | 206343 | 213053 | 216697 | 222066 |
| Kusini Unguja | 112612 | 115035 | 115588 | 117923 | 120305 | 122736 | 125215 | 131162 | 133767 |
| Mjini Magharibi | 483205 | 495054 | 593678 | 619144 | 645701 | 673398 | 702283 | 683833 | 700791 |
| Kaskazini Pemba | 253999 | 264677 | 211732 | 214502 | 217309 | 220153 | 223033 | 260884 | 271594 |
| Kusini Pemba | 246601 | 257577 | 195116 | 197274 | 199456 | 201662 | 203893 | 241715 | 251631 |
| **Zanzibar** | **1273512** | **1315552** | **1303569** | **1342394** | **1382616** | **1424292** | **1467477** | **1534291** | **1579849** |
| **Tanzania** | **43187823** | **44484857** | **44928923** | **46170151** | **47451847** | **48775567** | **50144175** | **52554628** | **54199163** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2012

- Takwimu Hazipo, Mikoa Mipya

# SEHEMU YA PILI

# UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

# SURA YA 7

## UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

**Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini**

144. Mwaka 2018, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilisajili jumla ya miradi 215 ikilinganishwa na miradi 345 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 37.7. Upungufu huo ulitokana na kuondolewa kwa vivutio vya kifedha kwenye miradi ya upanuzi na bidhaa za msingi zisizo za mitaji. Kati ya miradi iliyosajiliwa, miradi 132 ilikuwa ya Watanzania, 69 ya wageni, 14 ya ubia kati ya Watanzania na wageni ikilinganishwa na miradi 84 ya Watanzania, 168 ya wageni na miradi 85 ya ubia mwaka 2017. Kwa upande mwingine, thamani ya miradi iliyosajiliwa ilipungua kwa asilimia 44.4 kutoka dola za Marekani bilioni 5.07 mwaka 2017 hadi dola bilioni 2.82 mwaka 2018. Aidha, miradi iliyosajiliwa mwaka 2018 ilitoa fursa za ajira 27,469 ikilinganishwa na fursa za ajira 30,728 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 10.6.

**Mgawanyiko wa Usajili wa Miradi Kisekta**

145. Mwaka 2018, sekta ya huduma za biashara iliongoza kwa kusajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.07 ikifuatiwa na uzalishaji viwandani dola bilioni 0.63; kilimo dola bilioni 0.50; majengo ya biashara dola bilioni 0.22; na usafirishaji mizigo dola bilioni 0.17. Aidha, sekta iliyosajili idadi kubwa ya miradi ilikuwa uzalishaji viwandani miradi 108 ikifuatiwa na majengo ya biashara miradi 26, huduma za kibiashara miradi 19, utalii miradi 18, usafirishaji mizigo miradi 16 na kilimo miradi 12.

**Jedwali Na. 7.1. Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa Mwaka 2018**

| Sekta | Miradi Mipya | Miradi ya Watanzania | Miradi ya wageni | Miradi ya Ubia | Ajira | Thamani (milioni) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo | 12 | 6 | 6 | 0 | 6,151 | 506.87 |
| Majengo ya Biashara | 26 | 13 | 13 | 0 | 2,580 | 244.55 |
| Nishati | 3 | 1 | 2 | 0 | 36 | 52.49 |
| Huduma za Fedha | 3 | 0 | 0 | 3 | 442 | 60.7 |
| Rasilimali Watu | 7 | 6 | 1 | 0 | 431 | 5.3 |
| Uzalishaji Viwandani | 108 | 68 | 38 | 2 | 10,893 | 639.18 |
| Maliasili | 4 | 2 | 1 | 1 | 157 | 1.61 |
| Utangazaji | 1 | 1 | 0 | 0 | 26 | 0.22 |
| Huduma za Biashara | 16 | 11 | 4 | 1 | 1,746 | 1,017.12 |
| Mawasiliano | 1 | 1 | 0 | 0 | 955 | 37.17 |
| Utalii | 18 | 11 | 1 | 6 | 1,817 | 91.3 |
| Usafirishaji Mizigo | 16 | 12 | 3 | 1 | 2,235 | 166.39 |
| **JUMLA** | **215** | **132** | **69** | **14** | **27,469** | **2,821.92** |

**Chanzo**: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

**Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa**

146. Mwaka 2018, mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuvutia miradi ya uwekezaji ambapo miradi 109 ilisajiliwa. Hii ilitokana na kuwepo kwa mazingira wezeshi ya uwekezaji hasa miundombinu bora ikilinganishwa na mikoa mingine. Aidha, mkoa wa Pwani ulisajili miradi 37, Arusha miradi 9, Kilimanjaro miradi 8 na Morogoro miradi 8. Mikoa ya Katavi, Kigoma, Lindi , Rukwa, Ruvuma, na Simiyu haikusajili mradi wowote mwaka 2018. Mchanganuo wa usajili wa miradi kimkoa ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 7.2**.

**Jedwali Na. 7.2: Mgawanyiko wa Miradi iliyosajiliwa Kimkoa Mwaka 2018**

| Mkoa/Sekta | Kilimo | Utangazaji | Kompyuta | Majengo ya Biashara | Miundo Mbinu | Nishati | Kifedha | Rasilimali Watu | Uzalishaji Viwandani | Maliasili | Huduma | Mawasiliano | Utalii | Usafirishaji | Madini | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | **9** |
| Pwani | 3 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 27 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **37** |
| Dar es Salaam | 0 | 0 | 0 | 18 | 0 | 1 | 3 | 4 | 49 | 0 | 14 | 1 | 8 | 11 | 0 | **109** |
| Dodoma | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **5** |
| Geita | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| Iringa | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **4** |
| Kagera | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| Katavi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Kigoma | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Kilimanjaro | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | **8** |
| Lindi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Manyara | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | **1** |
| Mbeya | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **1** |
| Morogoro | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | **8** |
| Mtwara | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **2** |
| Mwanza | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | **7** |
| Njombe | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **4** |
| Mara | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **3** |
| Rukwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ruvuma | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Shinyanga | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **4** |
| Simiyu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Singida | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **4** |
| Tabora | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | **3** |
| Tanga | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | **2** |
| **Jumla** | **12** | **1** | **0** | **26** | **0** | **3** | **3** | **7** | **107** | **4** | **16** | **1** | **18** | **16** | **1** | **215** |

**Chanzo:** Kituo cha Uwekezaji Tanzania

**Urahisi wa kuwekeza na Kufanya Biashara Nchini**

147. Taarifa ya Mazingira ya Biashara Duniani ya Mwaka 2019 ilionesha kuwa mwaka 2018, Tanzania ilishika nafasi ya 144 kati ya nchi 190 zilizofanyiwa tathmini ikilinganishwa na nafasi ya 137 mwaka 2017. Kushuka kwa nafasi ya Tanzania kulitokana na hatua mbalimbali za maboresho zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zenye lengo la kupunguza urasimu katika biashara. Hata hivyo,Tanzania imefanya vizuri katika viashiria vya urahisi wa kupata

mikopo nafasi ya 60, kuheshimu utekelezaji wa mikataba na ubora wa utatuzi wa migogoro ya kibiashara nafasi ya 64 na upatikanaji wa umeme nafasi 83. Aidha, viashiria ambavyo Tanzania haikufanya vizuri ni pamoja na wepesi wa kusafirisha bidhaa zinazopita bandarini kwenda nchi jirani nafasi ya 183, taratibu za kulipa kodi nafasi ya 167, na taratibu za kuanzisha na kuendesha biashara nafasi ya 163. Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa kutekeleza Mpango Kazi Jumuishi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini. Serikali inaendelea kutekeleza sera na mipango inayolenga kupunguza kodi, tozo na ucheleweshaji wa shughuli za kibiashara. Aidha, Serikali imeimarisha taratibu za uuzaji na uagizaji wa bidhaa nje na kuboresha miundombinu pamoja na kujenga kituo cha Pamoja cha Forodha mipakani kwa lengo la kupunguza urasimu na kuokoa muda.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

148. Mwaka 2018, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliendelea kutekeleza Sera na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Katika kipindi hicho, kupitia mifuko ya uwezeshaji, Watanzania 20,832 (wanawake 9,716 na wanaume 11,116) walipatiwa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya shilingi 82,550,000 katika vikundi 12 vya VICOBA kwa kushirikiana na benki na taasisi za kifedha. Benki na taasisi zilizotumika kutoa mikopo hiyo ni pamoja na Benki ya TPB na *UTT Microfinance*. Hadi Desemba 2018 Serikali kupitia Mpango wa Dhamana wa Uwezeshaji Wananchi ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 13.4 kwa vikundi 229 vya kifedha vya kijamii na vyama 57 vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na kunufaisha wajasiriamali 31,948. Mwaka 2018, Serikali iliandaa mfumo wa kutambua, kusajili na kutoa taarifa za vikundi vya kifedha vya kijamii pamoja na vikundi vingine vya kiuchumi ambapo hadi Aprili 2018, vikundi 22,944 vilisajiliwa na kupewa vyeti maalumu katika mikoa 15.

**Ushirikishwaji wa Watanzania katika Uwekezaji na Miradi ya Serikali**

149. Mwaka 2018, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliendelea kuhakikisha kuwa Watanzania wanashiriki na kunufaika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Katika kipindi hicho, mradi wa Uboreshaji wa Barabara za Juu Dar es Salaam (Mfugale Flyover) uliajiri watanzania 589 na wageni 27 pamoja na kushirikisha kampuni 24 za Kitanzania, tatu za kigeni na moja ya ubia katika manunuzi mbalimbali. Aidha, ujenzi wa

barabara za juu Ubungo uliajiri Watanzania 449 na wageni 53 pamoja na kushirikisha kampuni saba za Kitanzania  na moja ya kigeni katika kutoa huduma na bidhaa. Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa uliajiri Watanzania 3,526 na wageni 255. Vile vile, mradi wa TIRP (Tanzania Inter Modal and Rail Development Project) uliajiri Watanzania 1,129 na wageni 152 pamoja na kushirikisha kampuni 22 za Kitanzania katika kazi mbalimbali. Mradi wa Upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam uliajiri  Watanzania 997 na wageni 59; na Mradi wa Ujenzi wa Daraja la *New Salender* umeajiri Watanzania 33 na wageni tisa.

**Maendeleo ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**
150.  Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuibua na kuandaa miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kutoa mafunzo na ushauri na miongozo ya kutekeleza miradi ya ubia katika Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kupokea miradi inayokusudiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia. Miradi hiyo ni: Mradi wa Kujenga Hosteli za Wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara; Ujenzi wa Hospitali ya Taifa ya Saratani; Ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Ujenzi wa Jengo la Biashara katika Jengo la Abiria (*Terminal III*) katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

151. Serikali iliendelea kuchambua maandiko ya miradi iliyo katika hatua mbalimbali inayotarajiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia ambayo ni pamoja na: Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza; Mradi wa Kuzalisha dawa Muhimu na Vifaa Tiba wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD); Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, na Mtwara; Ujenzi wa Reli ya Mtwara-Mchuchuma/Liganga kwa kiwango cha kisasa(standard gauge); Ujenzi wa Reli ya Tanga-Arusha-Musoma kwa kiwango cha kisasa; na Mradi wa Kujenga na Kuendesha Vyuo 10 vya VETA.

**Uwekezaji  Binafsi Kutoka Nje**
152. Uwekezaji wa sekta binafsi ya nje ni muhimu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi nchini. Kuongezeka kwa  uwekezaji wa sekta  binafsi ya nje kunachangiwa zaidi na uwepo wa sera nzuri za uchumi, amani, utulivu, pamoja na kuimarika kwa mazingira ya biashara. Aidha, uwekezaji wa sekta ya nje

nchini unachangia ukuaji wa mitaji, upatikanaji wa ajira, kuongeza Pato la Taifa na kuvutia upatikanaji wa fedha za kigeni.

153. Kwa mujibu wa Ripoti ya Uwekezaji ya Mwaka 2018 (The Tanzania Investment Report, 2018), uwekezaji wa sekta binafsi ya nje ulifikia dola za Marekani milioni 15,392.9 kutoka dola 14,634.3 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Kati ya uwekezaji huo, fedha iliyowekezwa moja kwa moja ilikuwa dola za Marekani milioni 13,499.5 sawa na asilimia 87.7 ya uwekezaji wa sekta binafsi ya nje, uwekezaji wa hisa asilimia 0.5 na uwekezaji mwingine asilimia 11.8. Uwekezaji wa sekta binafsi ya nje uliongezeka kwa asilimia 5.7 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,052 mwaka 2017 kutoka dola milioni 995.5 mwaka 2016.

**Uwekezaji wa Moja kwa Moja na Hisa**

154. Ripoti ya Uwekezaji ya mwaka 2018 imebainisha kuwa, katika mwaka 2017, Tanzania ilivutia uwekezaji wa moja kwa moja wa dola za Marekani milioni 937.7 ikilinganishwa na dola milioni 755.0 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 24.2. Ongezeko hilo, lilichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji kwenye shughuli za kiuchumi za malazi na huduma za vyakula, uchimbaji madini na mawe, na huduma za fedha na bima ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 61.5 ya uwekezaji wa moja kwa moja mwaka 2017. Aidha, uwekezaji wa hisa ulikuwa dola za Marekani milioni 0.8 mwaka 2017 ikilinganishwa na dola milioni 2.8 mwaka 2016. Uwekezaji huu wa hisa unahusisha uwekezaji kwenye kampuni usiozidi asilimia kumi kwa wawekezaji wa kawaida.

**Uwekezaji Mwingine**

155. Uwekezaji mwingine huwakilisha mikopo ya muda mrefu na mfupi pamoja na mikopo ya kibiashara. Mwaka 2017, uwekezaji huu ulifikia dola za Marekani milioni 113.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 237.7 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 52.4. Mwaka 2017, uwekezaji katika eneo hili ulitokana na mikopo ya muda mrefu na mikopo ya kibiashara.

**Ajira kutokana na Uwekezaji wa Moja kwa Moja**

156. Uwekezaji wa moja kwa moja husaidia kupatikana kwa ajira na hivyo kuongeza ujuzi na utaalam ambavyo ni muhimu katika kuongeza uzalishaji. Mwaka 2017, ajira 105,364 zilipatikana kutokana na uwekezaji wa moja kwa

moja ikilinganishwa na ajira 108,330 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 2.74. Aidha, watu wenye taaluma walioajiriwa walikuwa asilimia 33 ya waajiriwa wote na wasiokuwa na taaluma maalum walikuwa asilimia 67. Katika kipindi hicho, sekta zilizochangia kutoa ajira nyingi zilikuwa uzalishaji viwandani, kilimo, fedha na bima, na huduma za utawala. Sekta hizi kwa pamoja zilichangia asilimia 65.0 ya watu wote walioajiriwa kutokana na uwekezaji wa moja kwa moja.

**Jedwali Na.7.3:Uwekezaji kutoka Sekta Binafsi ya Nje (**Dola za Marekani, Milioni)

| Aina ya Uwekezaji | Kiasi kilichowekezwa (Inflows) | | | | | Kiasi kilichowekezwa (Stock) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
| Uwekezaji wa Moja kwa Moja | 2,130.9 | 1,416.1 | 1,560.6 | 755.0 | 937.7 | 10,851.4 | 11,897.4 | 12,146.6 | 12,839.2 | 13,499.5 |
| Uwekezaji wa Hisa | 3.5 | 1.2 | 1.5 | 2.8 | 0.8 | 12.3 | 16.3 | 118 | 128 | 72.2 |
| Uwekezaji Mwingine | 47.4 | 106.1 | 2.7 | 237.7 | 113.2 | 1459.4 | 1509.5 | 1439.8 | 1667.1 | 1820.9 |
| **Jumla** | **2,181.8** | **1,523.4** | **1,564.8** | **995.5** | **1,051.7** | **12,323.1** | **13,423.2** | **13,704.4** | **14,634.3** | **15,392.6** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania

**KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA**

Jedwali Na.34

| Sekta | 2017 | | | | | | | | 2018 | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | B | C | D | E | F | G | H | A | B | C | D | E | F | G | H |
| Kilimo | 23 | 23 | 0 | 9 | 11 | 3 | 2535 | 371.64 | 12 | 12 | 0 | 6 | 6 | 0 | 6151 | 506.87 |
| Maliasili | 5 | 5 | 0 | 1 | 2 | 2 | 286 | 5.32 | 4 | 4 | 0 | 2 | 1 | 1 | 157 | 1.61 |
| Utafiti | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Uzalishaji Viwandani | 188 | 187 | 1 | 42 | 102 | 44 | 18389 | 2552.4 | 108 | 108 | 0 | 68 | 38 | 2 | 10893 | 639.18 |
| Majengo ya biashara | 27 | 27 | 0 | 5 | 13 | 9 | 2284 | 204.3 | 26 | 26 | 0 | 13 | 13 | 0 | 2580 | 244.55 |
| Usafirishaji Mizigo | 28 | 28 | 0 | 13 | 11 | 4 | 2953 | 1443.8 | 16 | 16 | 0 | 12 | 3 | 1 | 2235 | 166.39 |
| Huduma za Biashara | 19 | 19 | 0 | 3 | 12 | 4 | 1061 | 50.82 | 16 | 16 | 0 | 11 | 4 | 1 | 1746 | 1017.12 |
| Komputa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Taasisi za fedha | 6 | 6 | 0 | 0 | 2 | 4 | 520 | 40.05 | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 442 | 60.7 |
| Mawasiliano | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 18 | 4.08 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 955 | 37.17 |
| Nishati | 5 | 5 | 0 | 0 | 5 | 0 | 407 | 299.62 | 3 | 3 | 0 | 1 | 2 | 0 | 36 | 52.49 |
| Rasilimali watu | 3 | 3 | 0 | 1 | 1 | 1 | 202 | 4.45 | 7 | 7 | 0 | 6 | 1 | 0 | 431 | 5.3 |
| Utalii | 29 | 29 | 0 | 9 | 8 | 12 | 1581 | 64.41 | 18 | 18 | 0 | 11 | 1 | 6 | 1817 | 91.3 |
| miundombinu | 3 | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 | 492 | 30.63 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Utangazaji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 26 | 0.22 |
| **Jumla** | **337** | **336** | **1** | **84** | **168** | **85** | **30728** | **5071.5** | **215** | **215** | **0** | **132** | **69** | **14** | **27469** | **2822.9** |

**Chanzo:** Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa

B Miradi Mipya

C Miradi ya Upanuzi

D Miradi ya Wazawa

E Miradi ya Wageni

F Miradi ya Ubia

G Jumla ya Ajira

H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD. Milioni)

\- Takwimu Hazikupatikana

# SURA YA 8

## MASUALA MTAMBUKA

### UKIMWI

157. Mwaka 2018, Serikali iliendelea na jitihada za kupambana na ugonjwa wa UKIMWI kupitia Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI 2018/19 - 2022/23 ambao umeainisha malengo na shabaha za kuzuia maambukizi mapya na vifo vitokanavyo na UKIMWI nchini. Aidha, katika kutokomeza vifo vinavyotokana na UKIMWI, Serikali iliendelea kutoa huduma na tiba kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ambapo hadi kufikia Desemba, 2018 jumla ya watu 1,103,016 wanaoishi na VVU walikuwa wanatumia dawa za kufubaza VVU ikilinganishwa na watu 740,745 mwaka 2015. Juhudi hizi zimewezesha kufubaza virusi vya UKIMWI kwa asilimia 87 kwa wale walio katika mpango wa matibabu na matunzo.

158. Kwa upande mwingine, Serikali iliridhia malengo ya kimataifa ya kufikia Tisini Tatu (90-90-90) ifikapo mwaka 2020. Dhana hii ina maana kuwa asilimia 90 ya walioathirika na maambukizi ya VVU wajue hali zao kiafya, asilimia 90 ya watakaopimwa na kukutwa na VVU wapate dawa na asilimia 90 ya waliopo kwenye tiba wawe na kiwango kidogo cha virusi kwenye damu. Utekelezaji wa Tisini Tatu kulingana na matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI 2016/17 ulionesha kuwa: takriban asilimia 60.6 ya watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi wanatambua hali zao za maambukizo ya VVU ( asilimia 52.2 wanaume na asilimia 64.9 wanawake); asilimia 93.6 ya waliokuwa wanajua wana VVU, walikuwa wanatumia dawa za ARV (asilimia 89.6 wanaume na asilimia 95.3 wanawake); na asilimia 87 ya watu wanaotumia ARV virusi vimefubazwa (asilimia 83.2 wanaume na asilimia 88.6 wanawake).

### Mazingira

159. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuwahimiza wawekezaji kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika uwekezaji kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya kutekeleza miradi yao. Katika kipindi hicho, miradi 412 ilipata hati za TAM baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na miradi 425 mwaka 2017. Aidha, marekebisho ya Kanuni za TAM 2018 yalipunguza muda wa kupata cheti kwa miradi mikubwa kutoka siku 149 hadi 74. Kanuni hizo zilitoa fursa ya kupata cheti kwa miradi midogo katika hatua ya muhtasari wa mradi ambayo huainisha kazi zinazotekelezwa katika mradi; athari zinazoweza kutokea kwenye mazingira; na hatua zitakazochukuliwa kukabiliana

na athari hizo. Vile vile, miradi mikubwa saba ya viwanda ilisajiliwa na kupewa leseni za muda katika hatua ya *mobilization phase* wakati wanaendelea kuandaa taarifa nzima ya TAM.

160. Mwaka 2018, Serikali ilifanya ukaguzi kwa lengo la kupima uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Mazingira nchini, ambapo zaidi ya maeneo 4,853 yenye viwanda 1,627 yalikaguliwa. Ufuatiliaji na ukaguzi wa hali ya uharibifu wa mazingira ulifanyika katika maeneo ya migodi, vituo vya mafuta, machinjio, hoteli, majengo ya biashara na makazi, mabwawa ya kutibu maji taka, machimbo ya mchanga na vyanzo vya maji. Aidha, ukaguzi na ufuatiliaji huo ulifanyika katika mikoa ya Mara, Mwanza, Arusha, Kilimajaro, Tanga, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Morogoro, Mbeya, Rukwa, Iringa, Njombe, Katavi, Pwani, Tabora, Dodoma na Kigoma. Mwaka 2018, Serikali ilitoa vibali 77 vya ukusanyaji, usafirishaji na urejelezaji wa taka ngumu kwa lengo la kusimamia uwekezaji wa taka ngumu ili kutekeleza Mwongozo wa Uwekezaji wa Taka Ngumu wa mwaka 2017.

161. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kusimamia mazingira kwa lengo la kupunguza athari za uharibifu wa mazingira kwa binadamu ikiwa ni pamoja na kudhibiti athari za matumizi ya zebaki. Tathmini ya matumizi ya zebaki iliyofanyika mwaka 2018 inaonesha kuwa takribani asilimia 80 ya zebaki inayotumika nchini hutumiwa na wachimbaji wadogo wa dhahabu ambao wana uelewa mdogo kuhusu madhara yake kwa binadamu. Aidha, tathimini hiyo imeainisha kuwa asilimia 25 hadi asilimia 33 ya wachimbaji wadogo wa dhahabu wameathirika kwa kiasi na sumu itokanayo na zebaki. Katika kukabiliana na athari ya matumizi ya zebaki, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa elimu kuhusu madhara ya zebaki kwa binadamu na kuwezesha wachimbaji wadogo wa dhahabu kutumia nyenzo mbadala za uchenjuaji wa madini.

162. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kudhibiti uharibifu wa ardhi ikiwa ni pamoja na kukamilisha Tathmini ya hali ya uharibifu wa ardhi nchini. Tathmini hiyo inaonesha kuwa takribani asilimia 75 ya eneo la nchi linakabiliwa na upungufu wa rutuba na uharibifu wa ardhi. Aidha, Tathmini inapendekeza hatua za kuchukua ikiwa ni pamoja na: uhifadhi wa misitu ya miombo, ufugaji na kilimo endelevu hasa katika mikoa ya Magharibi ikiwemo Shinyanga, Simiyu na Tabora. Mapendekezo mengine ya Tathmini hii ni kuongoa maeneo ya ardhi yaliyoharibika sana; ufugaji na kilimo endelevu katika maeneo ya kanda ya kati

ikiwemo mkoa wa Dodoma; uhifadhi wa misitu na kilimo endelevu katika maeneo ya mikoa ya Kaskazini ikiwemo Kilimanjaro na Tanga; kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa mashamba ya miti ya biashara na kilimo endelevu katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini; na uhifadhi wa ekolojia ya Pwani na Bahari ikiwemo misitu ya mikoko katika mikoa ya Ukanda wa Pwani ikiwemo Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Tanga.

163. Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa Jamii za Pwani kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya pwani. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na: Ujenzi wa ukuta pembeni mwa mto Pangani kwa upande wa kaskazini kutoka mita 600 mwaka 2017 hadi mita 780 mwaka 2018; Ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua katika Shule za Sekondari Kingani na Matipwili katika Wilaya ya Bagamoyo ambapo takribani lita 265,000 za maji ya mvua huvunwa kwa msimu mmoja ili kukabiliana na ukosefu wa maji kutokana na kuingia maji ya bahari katika visima vya zamani (sea water intrusion); Upandaji mikoko katika eneo la hekta 208 katika *Delta* ya Rufiji ili kulikinga na athari za mabadiliko ya tabianchi.

164. Mwaka 2018, Serikali ilifanya tathmini ya kuongezeka kwa viumbe-vamizi (*invasive alien species),* vinavyojumuisha mimea na wanyama ambavyo vinaathiri bioanuwai na ikolojia nchini. Tathmini hiyo inaonesha kuwa Tanzania kuna takribani aina 198 ya viumbe-vamizi ikilinganishwa na nchi nyingine katika Afrika Mashariki na Kati. Mkakati na Mpango wa kushughulikia viumbe vamizi nchini wa mwaka 2019/2029 (National Invasive Species Strategy and Action Plan 2019-2029) umeandaliwa ili kukabiliana na viumbe -vamizi.

**Usalama wa Raia**

165. Mwaka 2018, jumla ya makosa makubwa ya jinai 60,108 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 67,140 yaliyoripotiwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 10.5. Makosa dhidi ya binadamu 11,759 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 12,578 yaliyoripotiwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 6.5. Makosa hayo yanahusisha mauaji, kulawiti, wizi wa watoto, kutupa watoto, kunajisi na usafirishaji wa binadamu. Makosa 29,596 ya kuwania mali yanayohusisha makosa kama unyanganyi, uvunjaji, wizi, kuchoma nyumba moto, kughushi na noti bandia yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 33,815 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 12.5. Aidha, makosa 18,753 dhidi ya maadili ya jamii yaliripotiwa mwaka 2018 ikilinganishwa na makosa

20,747 yaliyoripotiwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 9.6. Makosa hayo yalihusisha makosa ya kwenda kinyume na sheria, nyara za Serikali, silaha, risasi, pombe ya moshi, mazao ya misitu, rushwa, kupatikana na bangi pamoja na magendo.

166. Mwaka 2018, jumla ya matukio makubwa ya usalama barabarani 3,988 yaliripotiwa ikilinganishwa na matukio 6,022 yaliyoripotiwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 33.8. Ajali zilizosababisha vifo zilipungua kutoka 2,254 mwaka 2017 hadi ajali 1,449 mwaka 2018, sawa upungufu wa asilimia 35.7. Vifo kutokana na ajali hizo vilipungua hadi kufikia 1,912 mwaka 2018 ikilinganishwa na vifo 2,705 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 29.3. Aidha, kulikuwa na majeruhi 4,194 waliotokana na ajali za barabarani mwaka 2018 ikilinganishwa na majeruhi 6,169 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 32.

167. Mwaka 2018, idadi ya wafungwa na mahabusu katika magereza yote nchini ilikuwa 37,774 (wafungwa 18,661 na mahabusu 19,113) ikilinganishwa na wafungwa na mahabusu 38,300 (wafungwa 19,720 na mahabusu 18,580) mwaka 2017. Hatahivyo, idadi hiyo ya wafungwa na mahabusu ni kubwa ikilinganishwa na uwezo wa magereza wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Katika kupunguza msongamano magerezani, hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kutumia vikao vya Bodi ya Parole, vifungo vya nje pamoja na kukarabati baadhi ya mabweni yaliyochakaa na kuongeza mengine katika magereza ambayo bado kuna nafasi.

168. Mwaka 2018, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liliendelea kukabiliana na majanga ya moto na majanga mengine kwa lengo la kuokoa maisha na mali za watu. Katika kipindi hicho, jumla ya miito 1,633 ya matukio ya moto ilipokelewa ikilinganishwa na miito 1,532 mwaka 2017. Aidha, Jeshi limeshiriki kufanya uokoaji katika matukio 471 ikilinganishwa na matukio 410 mwaka 2017. Vile vile, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na jitihada za kutoa elimu kwa umma pamoja na ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwenye maeneo mbalimbali ambapo maeneo 62,675 yalikaguliwa mwaka 2018 ikilinganishwa na maeneo 74,893 mwaka 2017.

169. Mwaka 2018, wageni 1,376,228 waliingia nchini kwa vibali halali ikilinganishwa na wageni 1,327,148 waliongia mwaka 2017. Vile vile, wageni 1,555,273 waliondoka nchini ikilinganishwa na wageni 1,346,826 walioondoka mwaka 2017. Jumla ya vibali vya ukaazi 15,769 vilitolewa mwaka 2018,

ikilinganishwa na vibali 16,914 mwaka 2017. Kati ya vibali vya ukaazi vilivyotolewa mwaka 2018, vibali 1,565 vilikuwa vya daraja A; 8,333 daraja B; 3,633 daraja C na 2,238 vilitolewa kwa wanafunzi. Aidha, jumla ya hati za kusafiria 74,896 (kielektroniki 67,922 na za kawaida 6,974) zilitolewa kwa Watanzania ikilinganishwa na hati 64,621 zilizotolewa mwaka 2017. Vile vile, wahamiaji haramu 13,691 walikamatwa mwaka 2018 ikilinganishwa na wahamiaji haramu 15,068 mwaka 2017.

170. Mwaka 2018, Tanzania ilihifadhi wakimbizi 326,941 kutoka mataifa ya Burundi (241,976), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (84,346), Somalia (150) na wakimbizi 469 kutoka mataifa mengine (Rwanda, Uganda, Sudan ya Kusini na Ethiopia). Aidha, wakimbizi waliongia nchini mwaka 2018 walikuwa 7,748 ikilinganishwa na wakimbizi 63,296 waliongia mwaka 2017. Mwaka 2018, wakimbizi 44,789 walirejeshwa katika nchi zao kwa hiari kutokana na kuimarika kwa hali ya amani katika nchi hizo. Aidha, wakimbizi 3,448 walihamishiwa katika nchi ya tatu ilikinganishwa na wakimbizi 1,620 waliohamishiwa nchi ya tatu mwaka 2017. Nchi hizo ni Marekani, Australia, Ireland, Canada, Uingereza, Finland na Sweden.

**Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa**

171. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iliendelea na usajili na utambuzi wa wananchi wa mikoa yote nchini ambapo hadi kufikia Desemba 2018 jumla ya wananchi 19,648,857 walisajiliwa. Aidha, Mamlaka ilifanikiwa kuziunga Ofisi 117 za Usajili za Wilaya na huduma ya mtandao kupitia Mkongo wa Taifa chini ya TTCL ili kurahisisha usafirishaji wa taarifa baina ya ofisi hizo na Makao Makuu ya Mamlaka. Vile vile, Mamlaka iliunganisha mfumo wake wa utambuzi na taasisi 45 kwa lengo la kurahisisha utambuzi wa wananchi na wageni wakaazi katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii.

**Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini**

172. Mwaka 2018, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini ulisajili jumla ya vizazi 1,409,206; vifo 22,938; ndoa 24,490; talaka 3,923 na hati 32 za watoto wa kuasili ikilinganishwa na usajili wa vizazi 1,764,494; vifo 52,323; ndoa 23,444; talaka 109 na hati 37 za watoto wa kuasili mwaka 2017. Aidha, kupitia mpango wa usajili kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano, jumla ya watoto 836,790 walisajiliwa ikilinganishwa na watoto 1,132,566 waliosajiliwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 26.1.

173. Mwaka 2018, Serikali ilitumia Mfumo wa Usajili wa Kizazi-Toleo la Nne kusajili vizazi na vifo. Mfumo huo una lengo la kuboresha mifumo ya TEHAMA katika usajili wa vizazi na vifo kwa kuzingatia mahitaji ya Mkakati wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu. Hadi kufikia Desemba 2018 jumla ya vizazi 189,148 na vifo 4,290 vilisajiliwa katika vituo 142 nchini. Aidha, mfumo huu umesaidia kusogeza huduma za usajili wa vizazi na vifo katika ofisi za kata na vituo vya tiba (zahanati, vituo vya afya na hospitali).

174. Mwaka 2018, hati za miunganisho ya wadhamini 71 zilitolewa ikilinganishwa na hati 121 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 41.3. Aidha, elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuandika na kutunza wosia ilitolewa kupitia vipindi vya redio, runinga na makala katika magazeti kama sehemu ya kuepusha migogoro ya wanafamilia pindi mwenye mali anapofariki. Mwaka 2018, wosia 60 ziliandikwa na kuhifadhiwa ikilinganishwa na wosia 57 mwaka 2017, sawa na ongezeko la wosia tatu.

# SURA YA 9

# HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU

## Utangulizi

175. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kutekeleza Mipango na Sera mbalimbali kwa lengo la kuinua ubora wa maisha, ustawi wa jamii, na kupunguza umaskini wa kipato. Aidha, katika kufikia malengo ya kuwa nchi ya uchumi wa kati, Serikali iliendelea kuboresha utoaji wa huduma za msingi hasa za afya, elimu na maji kwa lengo la kuimarisha kiwango cha maendeleo ya watu. Katika kipindi hicho, Serikali iliendelea kutekeleza ajenda 2030 inayohusu kuondoa umaskini wa aina zote ikiwa ni pamoja na umaskini uliokithiri na kufikia maendeleo endelevu.

## Viwango vya Umaskini

176. Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18 umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18. Matokeo ya Utafiti yanaonesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi ni mkubwa kwa maeneo ya vijijini (asilimia 31.3) ikilinganishwa na maeneo ya mijini (asilimia15.8). Aidha, matokeo ya Utafiti huo yanaonesha kuwa mkoa wa Rukwa una kiwango kikubwa cha umaskini wa mahitaji ya msingi (asilimia 45.0) wakati mkoa wa Dar es Salaam una kiwango kidogo cha umaskini wa mahitaji ya msingi cha asilimia 8.0. Kwa upande mwingine, kiwango cha umaskini wa chakula kimepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 na kufikia asilimia 8.0 mwaka 2017/18. Umaskini wa chakula ni mkubwa maeneo ya vijijini (asilimia 9.7) ikilinganishwa na maeneo ya mijini (asilimia 4.4).

## Mgawanyo wa Watu Maskini

177. Mgawanyo wa watu maskini Tanzania Bara kwa kuzingatia umaskini wa mahitaji ya msingi unaonesha kuwa asilimia 81 ya watu maskini wanaishi maeneo ya vijijini ikilinganishwa na asilimia 84.1 mwaka 2011/12. Kwa upande wa maeneo mengine ya mijini, mgawanyo wa watu maskini ni asilimia 16.1 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 14.4 mwaka 2011/12. Aidha, asilimia 3.0 ya watu maskini wanaishi katika jiji la Dar es Salaam ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2011/12. Hata hivyo, kuna mabadiliko ya mgawanyo wa watu maskini kwa maeneo ambapo kiwango cha watu maskini kwa maeneo ya vijijini kimepungua kwa nukta za asilimia 3.1 na maeneo mengine ya mijini

kimeongezeka kwa nukta za asilimia 1.7. Kwa upande wa jiji la Dar es Salaam kiwango cha watu maskini kimeongezeka mara mbili.

**Kina cha Umaskini**

178. Kina cha umaskini (Depth of Poverty) huonesha wastani wa kiwango gani watu au kaya maskini zipo chini ya mstari wa umaskini. Matokeo ya Utafiti yanaonesha kuwa wastani wa kina cha umaskini wa mahitaji ya msingi katika ngazi ya Taifa ni asilimia 6.2 na wastani wa kina cha umaskini wa mahitaji ya chakula ni asilimia 1.4. Kina cha umaskini kimeonekana kuwa kikubwa katika maeneo ya vijijini (asilimia 7.4) ikilinganishwa na maeneo ya mijini (asilimia 3.5). Aidha, kina cha umaskini kwa kuzingatia tofauti ya kipato kati ya watu maskini (Squared Poverty Gap Index) kimeonekana kuwa asilimia 2.1 kitaifa ambapo maeneo ya vijijini kimekuwa kikubwa (asilimia 2.6) kuliko maeneo ya mijini (asilimia 1.2).

**Jedwali Na. 9.1: Viwango vya Umaskini Tanzania**

| Eneo | Umaskini wa Mahitaji ya Msingi | | | Umaskini wa Chakula | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiwango cha Umaskini | Kina cha Umaskinii | Kina cha Umaskini Kuzingatia tofauti ya Kipato | Kiwango cha Umaskini | Kina cha Umaskinii | Kina cha Umaskini Kuzingatia tofauti ya Kipato |
| **Sehemu** | | | | | | |
| Vijijini | 31.3 | 7.4 | 2.6 | 9.7 | 1.7 | 0.5 |
| Mjini | 15.8 | 3.5 | 1.2 | 4.4 | 0.7 | 0.2 |
| **Mkoa** | | | | | | |
| Dodoma | 23.2 | 4.1 | 1.2 | 3.7 | 0.7 | 0.2 |
| Arusha | 24.7 | 5.8 | 1.9 | 7.6 | 1.2 | 0.3 |
| Kilimanjaro | 10.5 | 1.7 | 0.4 | 2.1 | 0.2 | 0 |
| Tanga | 21 | 5.1 | 1.7 | 8 | 1 | 0.2 |
| Morogoro | 19.3 | 3.7 | 1.1 | 4.3 | 0.5 | 0.1 |
| Pwani | 27.9 | 8.7 | 3.7 | 12.1 | 3.1 | 1.1 |
| Dar es Salaam | 8 | 2 | 0.7 | 2.3 | 0.5 | 0.1 |
| Lindi | 38 | 9.6 | 3.3 | 15.3 | 2.2 | 0.5 |
| Mtwara | 29.1 | 5.9 | 2.1 | 9 | 1.6 | 0.4 |
| Ruvuma | 30.6 | 6.7 | 2.1 | 6.6 | 1 | 0.3 |
| Iringa | 24 | 5.6 | 1.9 | 8 | 1.1 | 0.3 |
| Mbeya | 21.4 | 5 | 1.8 | 7.7 | 1.2 | 0.3 |
| Singida | 34 | 7.4 | 2.3 | 9.3 | 1.3 | 0.3 |
| Tabora | 34.5 | 8.3 | 2.8 | 11.1 | 1.7 | 0.4 |
| Rukwa | 45 | 12.9 | 4.8 | 19.8 | 3.4 | 0.9 |
| Kigoma | 34.5 | 10.1 | 4.4 | 14.2 | 3.8 | 1.5 |
| Shinyanga | 31.9 | 6.7 | 2.1 | 8.2 | 1.2 | 0.3 |
| Kagera | 31.9 | 8.3 | 3.2 | 12 | 2.5 | 0.7 |
| Mwanza | 34.6 | 7.8 | 2.6 | 9.4 | 1.4 | 0.3 |
| Mara | 23.2 | 4.2 | 1.1 | 2.2 | 0.4 | 0.1 |
| Manyara | 30.5 | 6.5 | 2.1 | 8 | 1.2 | 0.4 |
| Njombe | 13.2 | 2.4 | 0.8 | 3.3 | 0.7 | 0.1 |
| Katavi | 29 | 6.7 | 2.1 | 9.2 | 1.1 | 0.2 |
| Simiyu | 39.2 | 8.2 | 2.3 | 7.5 | 0.9 | 0.2 |
| Geita | 37.5 | 9.9 | 3.8 | 14.5 | 2.9 | 0.9 |
| Songwe | 20.7 | 4.4 | 1.4 | 5.6 | 0.7 | 0.3 |
| **Tanzania Bara** | **26.4** | **6.2** | **2.1** | **8** | **1.4** | **0.4** |

**Chanzo:** Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18

**Umaskini wa Watoto**

179. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18 umeonesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi kwa watoto wenye umri wa miaka 0 – 17 ni asilimia 30.1 ambapo umaskini wa chakula ni asilimia 9.4. Umaskini wa mahitaji ya msingi kwa watoto umeonekana kuwa mkubwa katika maeneo ya vijijini (asilimia 34.5) ikilinganishwa na maeneo ya mijini (asilimia 11.0). Umaskini wa chakula kwa watoto wanaoishi maeneo ya vijijini umeonekana kuwa asilimia 11 ikilinganishwa na asilimia 5.4 maeneo ya mijini . Matokeo ya Utafiti yanaonesha kuwa kwa ujumla umaskini wa mtoto hauna uhusiano na jinsi ya mtoto ambapo umaskini wa mahitaji ya msingi ni asilimia 30.1 kwa wote. Aidha, umaskini wa chakula kwa watoto wa kiume umeonekana kuwa asilimia 9.5 na kwa watoto wa kike asilimia 9.4. Kwa upande wa mikoa, mkoa wa Rukwa umeonekana kuwa na kiwango kikubwa cha watoto wenye umaskini wa mahitaji ya msingi (asilimia 47.6) wakati mkoa wa Dar es Salaam una kiwango kidogo cha asilimia 9.6. Vile vile, mkoa wa Rukwa una kiwango kikubwa cha watoto wenye umaskini wa chakula (asilimia 21.2) na Mkoa wa Mara umeonekana kuwa na kiwango kidogo cha asilimia 1.9.

**Tofauti ya Kipato**

180. Tofauti ya kipato hupimwa kwa kutumia kipimo cha *Gini coefficient* ambacho huanzia sifuri (0) kama hakuna tofauti ya kipato mpaka moja (1) kama kuna tofauti kubwa ya kipato. Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2017/18 yanaonesha kuongezeka kwa kiwango cha tofauti ya kipato kutoka 0.34 mwaka 2011/12 hadi kufikia 0.38 mwaka 2017/18. Vile vile, tofauti ya kipato katika maeneo ya vijijini imeongezeka hadi 0.32 mwaka 2017/18 kutoka 0.29 mwaka 2011/12. Katika maeneo mengine ya mijini tofauti ya kipato imeongezeka hadi 0.38 mwaka 2017/18 kutoka 0.37 mwaka 2011/12. Katika mkoa wa Dar es Salaam, tofauti ya kipato imeongezeka kutoka 0.35 mwaka 2011/12 hadi 0.42 mwaka 2017/18.

**Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

181. Mwaka 2018, Serikali iliendelea na juhudi za kupunguza umaskini uliokithiri kupitia programu mbalimbali ukiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Mpango huu unajumuisha uhawilishaji fedha na mradi wa ajira za muda. Hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya kaya zinazonufaika na Mpango zilikuwa 1,118,752 zenye jumla ya wanufaika 5,259,503 ikilinganishwa na wanufaika 5,127,730 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3. Katika mwaka 2018, wanufaika walio shule (miaka 6-18) walikuwa asilimia 39.2 na

watoto wenye umri wa hadi miaka mitano (miaka 0-5) ambao wanatakiwa kuhudhuria kliniki walikuwa asilimia 16.7 ya wanufaika wote. Wanufaika wenye umri stahiki wa kushiriki katika uzalishaji (miaka 19 – 60) ambao walishiriki katika mradi wa ajira za muda (Public Works Programme - PWP) walikuwa asilimia 32.6 wakati wanufaika wenye umri wa zaidi ya miaka 60 walikuwa asilimia 11.5 ya wanufaika wote.Sehemu kubwa ya fedha za Mpango zilitumika kusaidia wale wanaoshiriki katika uzalishaji na wanaohudhuria shule na hatimaye kuchangia katika kujenga uwezo wa uzalishaji na kulinda mtaji - watu.

**Jedwali 9.2: Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini**

| Mwaka | Makundi | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Miaka 0-2 | Miaka 3-5 | Miaka 6-18 | Miaka 19-60 | Zaidi ya 60 | Jumla |
| 2017 | 343,558 | 487,134 | 1,994,687 | 1,697,279 | 605,072 | 5,127,730 |
| 2018 | 380,741 | 497,683 | 2,061,746 | 1,714,158 | 605,175 | 5,259,503 |

**Chanzo:** TASAF

182. Hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya shilingi bilioni 791.83 zilitolewa kupitia uhawilishaji fedha kwa wanufaika ikilinganishwa na shilingi bilioni 668.3 zilizotolewa kufikia Desemba 2017, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Vile vile, katika kipindi hicho, ujira wenye thamani ya shilingi bilioni 83.29 ulilipwa kama mshahara kwa kaya maskini zilizoshiriki katika utekelezaji wa mradi wa ajira za muda katika jamii zao ikilinganishwa na ujira wenye thamani ya shilingi bilioni 47.6 uliolipwa kufikia Desemba 2017, sawa na ongezeko la asilimia 75.0. Vile vile, jumla ya shilingi bilioni 35.79 zililipwa kama malipo yasiyo ya mshahara katika utekelezaji mradi wa ajira za muda kufikia mwaka 2018.

## MAENDELEO YA WATU

183. Mwaka 2018, Serikali iliendelea na juhudi za kuboresha maendeleo ya watu kwa kuimarisha utoaji wa huduma za msingi za afya, elimu na maji pamoja na kuinua viwango vya maisha ya Watanzania. Aidha, Serikali, iliendelea na juhudi za kuimarisha ustawi wa jamii na kuhakikisha kwamba ukuaji wa uchumi unaenda sambamba na maendeleo ya watu. Katika kutekeleza hilo, Serikali iliweka kipaumbele katika kuboresha huduma za afya na elimu ili kupata matokeo bora ya maendeleo ya watu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Maendeleo ya Watu ya mwaka 2018 (UNDP - Global Human Development

Indices and Indicators 2018), Tanzania ilikuwa nafasi 154 kati ya nchi 189 katika maendeleo ya watu mwaka 2017 ikilinganishwa na nafasi ya 154 kati ya nchi 188 mwaka 2016. Aidha, Fahirisi ya Maendeleo ya Watu (HDI) iliongezeka kutoka 0.533 mwaka 2016 hadi kufikia 0.538 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 0.94.

184. Rushwa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. Kwa kutambua hilo, mwaka 2018, Serikali iliendelea kupambana na vitendo vya rushwa hususan katika sekta ya umma. Jitihida hizi ziliifanya Tanzania kupata alama 36 ya fahirisi ya rushwa (Corruption Perception Index - CPI) katika kupambana na vitendo vya rushwa mwaka 2018 kama ilivyokuwa mwaka 2017. Kimataifa nafasi ya Tanzania katika kupambana na vitendo vya rushwa katika sekta ya umma iliimarika kwa nafasi 4 kufikia nafasi ya 99 kati ya nchi 183 ikilinganishwa na nafasi ya 103 kati ya nchi 180 mwaka 2017.

# SEHEMU YA TATU

# SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

## SURA YA 10

## MABORESHO YA MWAKA WA KIZIO KWA TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA

**Chimbuko**

185. Historia ya kutayarisha takwimu za Pato la Taifa Tanzania Bara ilianza mwaka 1954. Kuanzia kipindi hicho, yalifanyika maboresho katika wigo wa shughuli zote za kiuchumi kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa. Takwimu za Pato la Taifa za vipindi vilivyopita zilikuwa zikitayarishwa kwa kuzingatia dhana, tafsiri na miongozo ya kuanisha shughuli za kiuchumi kama ilivyoainishwa kwenye Mifumo ya Ukokotoaji wa Takwimu za Pato la Taifa (Systems of National Accounts) ya mwaka 1953, 1968 na 1993. Hadi sasa, yamefanyika maboresho katika awamu sita ya takwimu za Pato la Taifa kuanzia mwaka 1954. Awamu hizo ni: maboresho ya kwanza ambayo yalitumia mwaka wa kizio 1966 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1953; maboresho ya pili yalitumia mwaka wa kizio 1976 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1968; maboresho ya tatu yalitumia mwaka wa kizio 1992 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1968 na kwa sehemu ya Mfumo wa Mwaka 1993; maboresho ya nne yalitumia mwaka wa kizio 2001 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1993; maboresho ya tano yalitumia mwaka wa kizio 2007 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1993 na sehemu ya Mfumo wa Mwaka 2008; na maboresho ya sita yametumia mwaka wa kizio 2015 na yamezingatia Mfumo wa Mwaka 2008.

**Umuhimu wa Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa**

186. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa ni mchakato unaohusisha kubadilisha mwaka wa kizio uliopitwa na wakati na kutumia mwaka wa kizio wenye taarifa za karibuni. Mwaka wa kizio ni mwaka wa rejea unaotumika kukokotoa takwimu linganifu za Pato la Taifa za miaka mbalimbali. Maboresho hufanyika ili kuhakikisha kuwa ukokotoaji wa Pato la Taifa unaendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia. Aidha, Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa inapendekeza kuwa maboresho yafanyike kila baada ya miaka mitano ili kuwa na takwimu zinazoendana na wakati na zinazoakisi hali halisi ya mabadiliko katika mfumo wa uchumi. Kwa ujumla, maboresho ya takwimu za Pato la Taifa yanafanyika kwa sababu zifuatazo:

(i) Takwimu za mwaka wa kizio husika kupitwa na wakati na hivyo, kushindwa kutoa taswira halisi ya mabadiliko ya muundo wa

uchumi kwa wakati huo;

(ii) Kujumuisha mabadiliko yaliyojitokeza katika uchumi kwenye mfumo wa uzalishaji bidhaa, matumizi na uwekezaji;

(iii) Kuhuisha mabadiliko ya bei za bidhaa mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hicho;

(iv) Kuhuisha orodha ya bidhaa mpya zinazokuwa zimeingia kwenye soko kutokana na kukua kwa teknolojia na kuondoa bidhaa ambazo hazipo sokoni;

(v) Kujumuisha taarifa zote mpya kutoka katika taarifa za kiutawala, sensa na tafiti zilizofanyika miaka ya karibuni; na

(vi) Kuzingatia matakwa mapya ya Mfumo wa Kimataifa wa Kutayarisha takwimu za Pato la Taifa na miongozo ya kuainisha shughuli za kiuchumi.

187. Mchakato wa kubadilisha mwaka wa kizio unahusisha kufanya maboresho katika maeneo yafuatayo: mfumo wa uzalishaji bidhaa katika uchumi; mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali; mabadiliko ya bidhaa kutokana na kukua kwa teknolojia na ubunifu; na Mabadiliko upande wa mahitaji kama vile kubadilika kwa mwenendo wa matumizi na upatikanaji wa bidhaa za kukuza mitaji. Kadiri mwenendo wa matumizi na uzalishaji unavyobadilika, mfumo wa bei nao hubadilika hivyo, kuendelea kutumia mwaka wa kizio wa zamani unakuwa hauakisi hali halisi ya mwenendo wa uchumi. Kutokana na sababu hizo, kuna umuhimu wa kubadilisha mwaka wa kizio ili kuboresha makadirio ya kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa na kuendana na mabadiliko ya uchumi kwa ujumla

**Malengo na Mbinu Zilizotumika Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa kwa Mwaka wa Kizio 2015**

188. Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanya maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 kwa kuzingatia miongozo, kanuni, mbinu na mifumo inayokubalika Kimataifa hususan, Mfumo wa Kimataifa wa Mwaka 2008 na Mwongozo wa kuainisha shughuli mbalimbali za kiuchumi unaojulikana kama *International Standard Industrial Classification of all economic activities Revision 4* (ISIC Rev. 4). Maboresho hayo yalitumia mbinu ya Mizania ya Ugavi na Matumizi (Supply and Use Tables) ambayo iliwezesha kupatikana kwa takwimu za Pato la Taifa kwa njia za uzalishaji wa bidhaa na huduma (production approach), matumizi (expenditure approach) na mapato (income approach).

189. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 yalifanyika kwa malengo yafuatayo: kuboresha takwimu za Pato la Taifa ziweze kuakisi vyema shughuli za kiuchumi katika nchi ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi yaliyojitokeza katika kipindi cha hivi karibuni katika nyanja za kijamii, kiteknolojia na kimfumo; na kuhakikisha upatikanaji wa takwimu linganifu kimataifa kwa mujibu wa mfumo wa mwaka 2008.

**Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa**

190. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa hufanyika kila baada ya miaka mitano kulingana na upatikanaji wa takwimu mpya kutoka vyanzo mbalimbali. Vyanzo vya taarifa vilivyotumika kukokotoa takwimu za Pato la Taifa ni sensa, tafiti mbalimbali, taarifa za kiutawala na tafiti maalumu zenye lengo la kujazia takwimu pale ambapo vyanzo vingine havikuweza kutoa taarifa za kutosheleza. Aidha, taarifa zilizotumika katika kuandaa takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 kwa Tanzania Bara ni pamoja na:

(i) Sensa na tafiti mbalimbali: Utafiti wa Matumizi na Mapato wa Kaya Binafsi 2011/12, Tafiti ya Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi 2014, Utafiti wa Ajira na Mapato 2015, Sensa ya Kilimo 2007/08, Utafiti wa Kilimo 2014/15, Sensa ya Uzalishaji Viwandani 2013, Utafiti wa Kufuatilia Kaya 2014, na Utafiti wa Uzalishaji Viwandani wa mwaka 2015;

(ii) Tafiti maalum**:** Utafiti wa Shughuli za Biashara wa mwaka 2015 na Utafiti wa Asasi Zisizo za Kiserikali zinazohudumia Kaya Binafsi wa mwaka 2015; na

(iii) Vyanzo vingine**:** Taarifa za kiutawala za uuzaji na uagizaji wa bidhaa na huduma nje, takwimu za mapato na matumizi ya Serikali pamoja na takwimu za Kodi ya Ongezeko la Thamani.


191. Matumizi makubwa ya takwimu za Pato la Taifa ni: kutathmini hali ya ukuaji wa uchumi wa nchi katika kipindi husika; kupanga mipango ya maendeleo na kutoa maamuzi; kupima mchango wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na ukuaji wake katika kipindi husika; msingi wa utayarishaji wa bajeti ya Serikali; kulinganisha uchumi wa nchi na nchi nyingine; kutathimini mabadiliko yanayotokea katika uchumi; na hutumika kuwianisha viashiria mbalimbali.

192. Maboresho ya mwaka wa kizio wa 2015 wa takwimu za Pato la Taifa yamesababisha: kubadilika kwa mfumo na ukubwa wa Pato la Taifa; kubadilika kwa viwango vya ukuaji na mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa; na mabadiliko ya uwiano wa viashiria mbalimbali kwa Pato la Taifa. Kukamilika kwa maboresho ya mwaka wa kizio kumechangia kuleta mabadiliko ya mwenendo wa Pato la Taifa pamoja na viashiria vingine vya kiuchumi. Mabadiliko makubwa yamejitokeza katika maeneo yafuatayo.

**a) Thamani ya Pato Ghafi la Taifa**


193. Thamani ya Pato ghafi la Taifa kwa mwaka wa mapitio wa 2015 iliongezeka kwa asilimia 3.8 kutoka shilingi milioni 90,854,208 kwa kutumia mwaka wa kizio wa 2007 kufikia shilingi milioni 94,349,316 kwa mwaka wa kizio wa 2015. Kwa wastani, takwimu za Pato ghafi la Taifa zimeongezeka kwa asilimia 3.2 katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita (2008 – 2017) kwa kutumia mwaka wa kizio wa 2015 ikilinganishwa na takwimu za mwaka wa kizio wa 2007, kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 10.1**. Aidha, matokeo ya maboresho ya mwaka wa kizio 2015 yanaonesha ongezeko la thamani katika shughuli za kilimo, misitu na uvuvi limepungua wakati shughuli za viwanda na ujenzi pamoja na huduma limeongezeka ikilinganishwa na mwaka wa kizio 2007, kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 10.2.**

**Kielelezo Na. 10.1: Mwenendo wa Pato Ghafi la Taifa Kabla na Baada ya Maboresho ( Shilingi Bilioni)**



194. Tofauti zilizopo katika takwimu za Pato la Taifa kwa bei za miaka ya 2007 na 2015 zinatokana na kuboreshwa kwa mbinu za ukokotoaji na kuimarika kwa upatikanaji wa taarifa na takwimu husuan, kupitia matumizi ya TEHAMA. Kimsingi, tofauti hizo zilitokana na kujumuishwa kwa takwimu mpya zilizotokana na tafiti pamoja na vyanzo mbalimbali vikiwemo usafirishaji wa gesi asilia kupitia bomba la gesi na usafirishaji wa abiria kwa kutumia mabasi yaendayo haraka - Dar es Salaam. Ongezeko la Pato ghafi la Taifa linaashiria kuwepo kwa mabadiliko ya kimfumo katika uchumi, mabadiliko ya mwenendo wa uzalishaji, matumizi na uwekezaji na mabadiliko ya wastani wa bei za bidhaa na huduma.

**Kielelezo Na. 10.2: Ongezeko la Thamani kwa shughuli za kiuchumi mwaka 2015, kwa kutumia Takwimu za Mwaka kizio 2007 na 2015**




### b) Ongezeko la Thamani Kisekta

195. Maboresho ya mwaka wa kizio yamebadilisha kwa viwango tofauti thamani ya ongezeko la Pato kwa kila sekta. Pato ghafi la sekta za uzalishaji viwandani, malazi na uchukuzi liliongezeka kwa zaidi ya asilimia 50 na lilikuwa na ongezeko la mchango katika Pato la Taifa. Aidha, sekta ya huduma za fedha, afya, upangishaji majengo na madini zilikuwa na ongezeko kubwa la Pato ghafi, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali 10.1**. Ongezeko la thamani kisekta, lilitokana na maboresho yaliyofanywa katika ukokotoaji wa Pato la Taifa

ambayo yalizingatia hatua ya udhibiti wa shughuli za madini; kuongezeka kwa uwekezaji wa sekta ya umma na binafsi katika afya; na ujenzi wa nyumba za biashara na ofisi; na mageuzi katika shughuli za huduma za kifedha ikiwemo huduma za fedha kupitia mitandao ya simu.

**Jedwali Na. 10.1: Ongezeko la Thamani kwa Shughuli za Kiuchumi Kabla na Baada ya Maboresho kwa Mwaka 2015**

| | | Kabla ya Marekebisho | Baada ya Barekebisho | Badiliko |
|---|---|---|---|---|
| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | Shilingi Milioni | | Asilimia |
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | **26,346,673** | **25,234,560** | -4.2% |
| | Kilimo cha Mazao | 14,193,178 | 13,296,720 | -6.3% |
| | Mifugo | 7,135,172 | 7,167,798 | 0.5% |
| | Misitu | 3,146,646 | 2,924,236 | -7.1% |
| | Uvuvi | 1,871,677 | 1,845,806 | -1.4% |
| | **Viwanda na Ujenzi** | **22,093,974** | **23,103,647** | 4.6% |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 3,659,599 | 4,055,619 | 10.8% |
| C | Viwanda | 4,768,917 | 7,411,672 | 55.4% |
| D | Umeme | 898,712 | 798,801 | -11.1% |
| E | Maji safi na Maji taka | 392,557 | 390,758 | -0.5% |
| F | Ujenzi | 12,374,188 | 10,446,797 | -15.6% |
| | **Huduma** | **36,334,586** | **38,146,529** | 5.0% |
| G | Biashara na Matengenezo | 9,714,665 | 8,747,862 | -10.0% |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 3,864,156 | 6,929,895 | 79.3% |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 947,944 | 1,421,916 | 50.0% |
| J | Habari na Mawasiliano | 1,809,897 | 1,681,098 | -7.1% |
| K | Fedha na Bima | 3,254,440 | 4,189,021 | 28.7% |
| L | Upangishaji Majengo na Biashara | 4,035,613 | 5,651,637 | 40.0% |
| M | Utawala na Ulinzi | 8,012,812 | 4,548,604 | -43.2% |
| N | Elimu | 2,309,345 | 2,413,306 | 4.5% |
| O | Afya na Huduma za Jamii | 1,275,702 | 1,419,090 | 11.2% |
| P | Huduma nyingine | 1,110,013 | 1,144,099 | 3.1% |
| Q | Jumla ya Ongezeko la Thamani | **83,737,418** | **86,484,736** | 3.3% |
| R | Ongeza kodi katika bidhaa | 7,116,789 | 7864579.414 | 10.5% |
| S | Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | **90,854,208** | **94,349,316** | 3.8% |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

196. Maboresho ya mwaka wa kizio 2015 yamesababisha mabadiliko ya mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa kutokana na mabadiliko ya bei, bidhaa, teknolojia na mabadiliko ya tabia za walaji. Aidha, hakukuwa na mabadiliko makubwa katika muundo wa uchumi ambapo sekta za kilimo, biashara, ujenzi na uchukuzi zikiendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 50 kwa pamoja, wakati ambapo mchango wa sekta za madini, uzalishaji viwandani, huduma za fedha na bima, na

upangishaji majengo uliongezeka, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.10.2**.

**Jedwali Na. 10.2: Mabadiliko ya Mchango wa Shughuli za Uchumi Katika Pato la Taifa kwa Mwaka 2015**

| | SHUGHULI YA KIUCHUMI | Kabla ya Marekebisho | Baada ya Barekebisho | Badiliko |
|---|---|---|---|---|
| A | **Kilimo, Misitu na Uvuvi** | 29.0% | 26.7% | -7.8% |
| | Kilimo cha Mazao | 15.6% | 14.1% | -9.8% |
| | Mifugo | 7.9% | 7.6% | -3.3% |
| | Misitu | 3.5% | 3.1% | -10.5% |
| | Uvuvi | 2.1% | 2.0% | -5.0% |
| | **Viwanda na Ujenzi** | 24.3% | 24.5% | 0.7% |
| B | Uchimbaji Madini na Mawe | 4.0% | 4.3% | 6.7% |
| C | Viwanda | 5.2% | 7.9% | 49.7% |
| D | Umeme | 1.0% | 0.8% | -14.4% |
| E | Maji safi na Maji taka | 0.4% | 0.4% | -4.1% |
| F | Ujenzi | 13.6% | 11.1% | -18.7% |
| | **Huduma** | 40.0% | 40.4% | 1.1% |
| G | Biashara na Matengenezo | 10.7% | 9.3% | -13.3% |
| H | Uchukuzi na Uhifadhi mizigo | 4.3% | 7.3% | 72.7% |
| I | Malazi na Huduma ya chakula | 1.0% | 1.5% | 44.4% |
| J | Habari na Mawasiliano | 2.0% | 1.8% | -10.6% |
| K | Fedha na Bima | 3.6% | 4.4% | 23.9% |
| L | Upangishaji Majengo na Biashara | 4.4% | 6.0% | 34.9% |
| M | Utawala na Ulinzi | 8.8% | 4.8% | -45.3% |
| N | Elimu | 2.5% | 2.6% | 0.6% |
| O | Afya na Huduma za Jamii | 1.4% | 1.5% | 7.1% |
| P | Huduma nyingine | 1.2% | 1.2% | -0.7% |
| Q | Jumla ya Ongezeko la Thamani | 92.2% | 91.7% | -0.5% |
| R | Ongeza kodi katika bidhaa | 7.8% | 8.3% | 6.4% |
| S | Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 100.0% | 100.0% | 0.0% |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### c) Matokeo kwa Viashiria vya Kiuchumi


197. Matokeo ya maboresho ya mwaka wa kizio wa 2015 yamesababisha uwiano wa viashiria vingi kubadilika ambapo wastani wa Pato la kila mtu kwa mwaka wa mapitio wa 2015 uliongezeka kufikia shilingi 1,968,965 ikilinganishwa na shilingi 1,896,026 kwa kutumia mwaka wa kizio wa 2007. Aidha, uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa unaonekana kupungua na kuwa asilimia 13.9 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na asilimia 14.4 kwa takwimu za Pato la Taifa za mwaka wa kizio wa 2007. Vile vile, uwiano wa deni

la Serikali kwa Pato ghafi la Taifa umepungua kufikia asilimia 35.4 mwaka 2015/16 ikilinganishwa na uwiano wa asilimia 36.7 kwa mwaka wa kizio 2007.

**d) Viwango vya Ukuaji wa Uchumi**

198. Maboresho ya takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio wa 2015 yanaonesha kuwa uchumi wa Tanzania ni imara licha ya kwamba viwango vya ukuaji vimepungua ikilinganishwa na mwaka wa kizio wa 2007. Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.3 katika kipindi cha muongo mmoja uliopita baada ya maboresho ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.6 kabla ya maboresho. Kwa mwaka 2017, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.8 baada ya maboresho ya takwimu ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 mwaka 2016. Aidha, mwenendo wa ukuaji kisekta umekuwa na matokeo mchanganyiko ambapo baadhi ya sekta zimekuwa na ongezeko la viwango vya ukuaji na baadhi zikipungua kabla na baada ya maboresho. Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017, viwango vya ukuaji wa sekta za kilimo, uzalishaji viwandani na afya kabla ya maboresho vilikua kwa wastani wa asilimia 2.7, 7.1 na 5.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.4, 8.7, na 6.1 baada ya maboresho kwa mtiririko huo.

**Kielelezo Na. 10.3: Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa (2006 -2017)**



# SEHEMU YA NNE

## MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

## SURA YA 11
## KILIMO NA USHIRIKA

### KILIMO

**Uzalishaji wa Mazao ya Chakula**

199. Mwaka 2018, uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mchele, ngano, mihogo na ndizi uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017 kutokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa. Aidha, uzalishaji wa mazao ya mahindi, mtama, viazi, maharage na mikunde ulishuka kutokana na mashambulizi ya visumbufu kama vile, viwavijeshi vamizi, panya na kweleakwelea, **Jedwali Na. 11.1** linaonesha mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula.

**Jedwali Na. 11.1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula (Tani' 000)**

| Zao | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 5,104 | 5,288 | 6,734 | 5,908 | 6,149 | 6,681 | 6,273 | -6.1 |
| Mchele | 1,170 | 1,342 | 1,681 | 1,937 | 2,229 | 1,594 | 2,220 | 39.3 |
| Ngano | 109 | 102 | 167 | 72 | 76 | 50 | 57 | 14.0 |
| Mtama/Ulezi | 1,052 | 1,074 | 1,246 | 1,007 | 1,003 | 1,064 | 988 | -7.1 |
| Mihogo | 1,821 | 1,878 | 1,664 | 1,962 | 2,205 | 1,342 | 2,791 | 108.0 |
| Maharage/Mikunde | 1,827 | 1,871 | 1,697 | 1,808 | 1,959 | 2,318 | 1,823 | -21.4 |
| Ndizi | 842 | 1,317 | 1,064 | 1,195 | 1,061 | 845 | 1,132 | 34.0 |
| Viazi vitamu | 1,418 | 1,808 | 1,761 | 1,645 | 1,491 | 2,008 | 1,608 | -19.9 |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

200. Tathmini ya uzalishaji wa mazao ya chakula iliyofanyika Desemba 2018, ilionesha kuwa uzalishaji ulikuwa tani 16,891,974 (mazao ya nafaka tani 9, 537,857 na mazao yasiyo ya nafaka tani 7,354, 117) ikilinganishwa na mahitaji ya tani 13,569,285 za chakula mwaka 2018 ambapo mazao ya nafaka yalikuwa tani 8,627,273 na mazao yasiyo ya nafaka tani 4,942,012. Hii iliwezesha kuwa na ziada ya tani 3,322,689 na hivyo nchi kuwa na kiwango cha utoshelevu wa chakula kwa asilimia 124.

**Uzalishaji wa Mazao ya Biashara**

201. Mwaka 2018, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ulikuwa tani 967,184 ikilinganishwa na tani 901,641 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya pamba, chai, pareto, korosho, na mkonge. Hata hivyo, uzalishaji wa kahawa, tumbaku na sukari ulipungua kwa asilimia 6.4, 13.8 na 8.2 mtawalia. Kupungua kwa uzalishaji wa tumbaku kulitokana na kushuka kwa mahitaji katika soko la dunia

kulikosababisha kampuni za ununuzi kupunguza kiasi cha ununuzi wa tumbaku kwa wakulima. Vile vile, kupungua kwa uzalishaji wa sukari kulitokana na vipindi virefu vya mvua vilivyosababisha kushuka kwa viwango vya sukari kwenye miwa pamoja na kipindi kifupi cha uvunaji wa miwa. Uzalishaji wa kahawa ulishuka kutokana na msimu mfupi katika mzunguko wa uzalishaji na hali ya hewa kutokuwa nzuri. **Jedwali Na. 11.2** linaonesha mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya biashara.

**Jedwali Na. 11.2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani)**

| Zao | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 225,938 | 357,130 | 246,767 | 203,312 | 149,455 | 132,934 | 222,039 | 67.0 |
| Kahawa | 126,624 | 86,359 | 100,000 | 87,737 | 60,691 | 48,329 | 45,245 | -6.4 |
| Chai | 262,880 | 296,697 | 294,421 | 304,007 | 293,075 | 26,975 | 34,010 | 26.1 |
| Pareto | 32,810 | 33,700 | 33,000 | 35,750 | 32,629 | 2,150 | 2,400 | 11.6 |
| Tumbaku | 5,700 | 6,100 | 7,090 | 6,050 | 2,011 | 58,639 | 50,522 | -13.8 |
| Korosho | 33,219 | 71,200 | 47,301 | 41,674 | 60,921 | 265,238 | 313,826 | 18.3 |
| Mkonge | 25,690 | 34,875 | 37,571 | 39,204 | 42,314 | 36,533 | 40,635 | 11.2 |
| Sukari | 160,000 | 127,947 | 123,449 | 197,933 | 155,416 | 330,843 | 303,752 | -8.2 |
| **Jumla** | **872,861** | **1,014,008** | **889,599** | **915,667** | **796,512** | **901,641** | **967,184** | **7.3** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

**Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta**

202. Mwaka 2018, uzalishaji wa mazao ya mafuta ya alizeti, karanga, ufuta, michikichi na soya ulifikia tani 1,607,198 ikilinganishwa na tani 6,667,893 mwaka 2017, sawa na upungufu wa 75.9. Upungufu huo ulitokana na ukosefu wa soko la uhakika na bei ya kuridhisha kwa mazao hayo. Aidha, uzalishaji wa zao la soya uliongezeka kutokana na ongezeko la mahitaji yake na hivyo wakulima kuhamasika na kuzalisha kwa wingi. Uzalishaji wa mazao hayo ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.11.3**.

**Jedwali Na. 11.3: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta (Tani)**

| Zao | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | 1,125,000 | 2,625,000 | 2,755,000 | 2,878,500 | 2,995,500 | 3,112,500 | 768,188 | -75.3 |
| Karanga | 810,000 | 1,425,000 | 1,635,735 | 1,835,933 | 2,025,595 | 2,215,257 | 643,485 | -71.0 |
| Ufuta | 456,000 | 1,050,000 | 1,113,892 | 1,174,589 | 1,232,092 | 1,291,724 | 133,704 | -89.6 |
| Mawese | 24880 | 40500 | 41000 | 41475 | 41925 | 42277 | 40,500 | -4.2 |
| Soya | 5620 | 5830 | 6025 | 6030 | 6035 | 6135 | 21,321 | 247.5 |
| **Jumla** | **2,421,500** | **5,146,330** | **5,551,652** | **5,936,527** | **6,301,147** | **6,667,893** | **1,607,198** | **-75.9** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

**Uzalishaji wa Mazao ya Bustani**

203. Mwaka 2018, uzalishaji wa mazao ya bustani yakiwemo matunda, maua, mboga na viungo ulipungua hadi kufikia tani 5,333, 297 kutoka tani 6, 563,793 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 18.9. Upungufu huu ulitokana na ukosefu wa soko la uhakika wa mazao hayo. Hata hivyo uzalishaji wa mboga uliongezeka kwa asilimia 22.9 na maua asilimia 8.7. Mwenendo wa hali ya uzalishaji wa mazao ya bustani ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11.4.**

**Jedwali Na.11. 4: Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)**

| Zao | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Matunda | 3,938,730 | 4,096,280 | 4,416,690 | 4,574,240 | 4,711,000 | 5,243,343 | 3,703,124 | -29.4 |
| Mboga | 901,680 | 937,750 | 1,005,305 | 1,041,375 | 1,189,000 | 1,298,388 | 1,595,489 | 22.9 |
| Maua | 9,850 | 10,200 | 10,790 | 11,140 | 11,500 | 11,615 | 12,622 | 8.7 |
| Viungo | 7,370 | 8,125 | 8,377 | 8,609 | 20,400 | 22,062 | 22,062 | 0.0 |
| **Jumla** | **4,857,630** | **5,052,355** | **5,441,162** | **5,635,364** | **5,931,900** | **6,563,793** | **5,333,297** | **-18.9** |

**Chanzo:** Wizara ya Kilimo

**Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo**

204. Mwaka 2018, jumla ya matrekta makubwa 1,476 na madogo 380 yaliingizwa nchini ikilinganishwa na matrekta makubwa 1,604 na madogo 378 yaliyoingizwa mwaka 2017. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Taifa, Benki ya Maendeleo TIB, na Benki ya Maendeleo ya Kilimo, ilitoa mafunzo kwa madereva 76 wa matrekta kuhusu uendeshaji bora na matengenezo ya matrekta aina ya URSUS. Vile vile, viongozi 108 wa vyama vya msingi 53 vya mazao waliokopeshwa matrekta walipatiwa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa matrekta hayo. Kati ya hivyo, vyama 50 vilikuwa mkoa wa Mwanza na vitatu wilaya ya Bunda mkoa wa Mara. Katika kuendeleza matumizi ya kilimo hifadhi, Serikali kwa kushirikiana na *Conservation Farming Unit* na *Diocese of Central Tanganyika* ilitoa mafunzo ya matumizi ya kilimo hifadhi kwa wakulima viongozi 365 katika wilaya za Babati, Kiteto, Monduli, Same, Moshi Vijijini, Chamwino na Dodoma Mjini kwa lengo la kuhimiza umuhimu wa hifadhi ya chakula na kuongeza uzalishaji katika maeneo yanayokabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

**Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao ya Kilimo**

205. Mwaka 2018, mifumo ya masoko ya mazao ya kimkakati iliboreshwa kwa kufanya tafiti za mahitaji ya masoko, kuimarisha vyama vya ushirika, na

kusimamia mikataba baina ya wanunuzi na wakulima. Matokeo ya awali ya utekelezaji ya mifumo hiyo, yalionesha kuongezeka kwa tija, kuimarika kwa bei, upatikanaji wa takwimu na ubora wa mazao. Aidha, kupitia mfumo wa ushirika, wakulima waliweza kupata pembejeo kwa wakati kulingana na mahitaji yao. Katika kipindi hicho, bei ya zao la kahawa katika soko la ndani iliimarika ikilinganishwa na soko la nje. Bei ya kahawa ya Arabika katika soko la dunia ilikuwa dola za Marekani 107.04 ikilinganishwa na dola 112 katika soko la ndani kwa gunia la kilo 50 wakati bei ya kahawa ya Robusta katika soko la dunia ilikuwa dola 73.90 ikilinganishwa na dola 87.13 katika soko la ndani kwa gunia la kilo 50. Bei ya zao la ufuta ilikuwa shilingi 3,770 kwa kilo ikilinganishwa na shilingi 1,870 mwaka 2017. Bei ya korosho ghafi daraja la kwanza ilikuwa shilingi 3,300 kwa kilo na shilingi 2,640 kwa kilo ya korosho ghafi daraja la pili ikilinganishwa na shilingi 1,877 hadi 4,000 kwa kilo mwaka 2017.

**Huduma za Ughani**

206. Mwaka 2018, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iliendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kilimo bora kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija. Wakulima 420 walipatiwa mafunzo kwenye kilimo bora cha mboga na matunda, viazi mviringo, maharage na mahindi. Aidha, wakulima 179 walipatiwa mafunzo kuhusu kilimo cha umwagiliaji cha mpunga, utunzaji wa mpunga baada ya mavuno na masoko. Vile vile, mafunzo ya teknolojia ya kilimo shadidi cha mpunga yalitolewa kwa wakulima viongozi 168, maafisa ughani na mafundi sanifu umwagiliaji 70 kutoka skimu 40 za umwagiliaji, maafisa ughani 20 kutoka halmashauri sita na Sekretarieti ya mkoa wa Morogoro na wakulima 250 wa skimu za Kasela, Kazunzu, Luchili na Sukuma zilizopo katika Halmashauri ya Buchosa. Mashamba ya mfano 1,120 ya kilimo shadidi kwa zao la mpunga yalianzishwa kwenye skimu 40 za umwagiliaji katika halmashauri sita za mkoa wa Morogoro.

**Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo**

207. Mwaka 2018, vyuo 14 vya kilimo vilidahili wanafunzi 2,051 wanaofadhiliwa na Serikali kwenye mafunzo ya kilimo ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na wanafunzi 1,956 mwaka 2017. Mafunzo hayo yalitolewa katika vyuo vya Ilonga, Mlingano, Mtwara, Tumbi, Ukiriguru, Uyole, HORTI Tengeru, Mubondo, Maruku, KATC, Igurusi, KATRIN, Chuo cha Sukari Kidatu na Inyala. Aidha, wanafunzi 338 wanaojilipia wenyewe walidahiliwa katika ngazi ya astashahada na stashahada ikilinganishwa na

wanafunzi 246 mwaka 2017. Serikali kupitia vyuo vya kilimo kwa kushirikiana na taasisi binafsi iliendesha mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uwezo wakulima kuhusu teknolojia mbalimbali za kilimo yanayohusu kilimo cha korosho kwa wakulima 67 Mtwara; kilimo cha mahindi na maharage kwa wakulima 51 Ukiriguru; usindikaji wa mazao kwa wakulima vijana 56 Uyole; kilimo bora cha soya kwa wakulima 31, kilimo shadidi cha mpunga kwa maafisa ughani 33, kilimo bora cha alizeti kwa wakulima 25, na maafisa ughani watano na kilimo bora cha mpunga kwa wakulima 20 Ilonga.

208. Mwaka 2018, Serikali kwa kushirikiana na JICA kupitia mradi wa TANRICE2 ilitoa mafunzo kwa wakulima wa mpunga 1,964 ikilinganishwa na wakulima 4,781 mwaka 2017. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *Lutheran World Relief* kupitia mradi wa *Invest* ilifanya mapitio ya mitaala ya astashahada na stashahada ya kozi ya kilimo mseto ambapo wakufunzi 20 walijengewa uwezo. Vile vile, Serikali iliendelea kuwajengea uwezo wakufunzi wa kilimo 22 ambapo wakufunzi 10 walikuwa katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na 12 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi nchini India na China.

**Utafiti**

209. Mwaka 2018, Serikali iliidhinisha na kusambaza aina za mbegu bora 25 zilizogunduliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo -TARI na taasisi binafsi za kilimo ikilinganishwa na aina za mbegu bora 14 zilizogunduliwa mwaka 2017. Mbegu zilizogunduliwa zilikuwa za mazao ya pamba (2), maharage (9), mahindi (3), karanga (3), njugumawe (2), tumbaku (5) na mpunga (1). Aidha, Serikali kupitia vituo vya TARI, ilizalisha kilo 5,250 za mbegu mama kwa mazao ya pamba (kilo 4,200) na mpunga (kilo 1,050). Vile vile, kilo 94,600 za mbegu za awali zilizalishwa kwa mazao ya pamba kilo 23,240; viazi mviringo kilo 6,380; mpunga kilo 4,780; mahindi kilo 12,600; soya kilo 2,200; na maharage kilo 45,400; na jumla ya miche/vipando 6,769,260 kwa mazao ya migomba (1,750), matunda (3,400), mihogo (3,248,000) na viazi vitamu (3,516,110). Kwa upande mwingine, vituo vya utafiti, vilizalisha kwa njia ya tishu na kusambaza miche ya mananasi 22,000, mihogo 700, migomba 600 na viazi vitamu 150.

210. Matokeo ya utafiti wa udongo uliofanyika katika maeneo yanayolima mazao ya mahindi, mpunga na maharage katika kanda ya Ziwa, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, na Kanda ya Kusini yalifanikiwa kutoa aina mbili za mbolea mpya ya NPS na NPS Zinki.

Aidha, tathmini ya udongo kwa ajili ya kuzalisha zao la miwa ilifanyika katika mashamba makubwa ya miwa ya Mkulazi (hekta 60,000), Mbigiri (hekta 12,000) na Bagamoyo (hekta 10,000) na kuthibitishwa yanafaa kwa kilimo cha miwa. Vile vile, mapitio ya ramani za udongo kwa kutumia mfumo wa kijiografia (GIS) katika ukanda wa SAGCOT yalifanyika ili kurahisisha utambuzi wa maeneo yanayofaa kwa uwekezaji.

**Umwagiliaji**

211. Mwaka 2018, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliendeleza miundombinu ya umwagiliaji kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: kujenga na kukamilisha mifereji ya kutoa maji katika bwawa la Dongobesh (Hanang); kufanyika mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu katika skimu ya Gildahababerg (Hanang); na kukamilisha uchunguzi wa miamba katika skimu ya Lwanyo (Mbarali). Aidha, Tume ilikamilisha maandalizi ya zabuni za ujenzi wa skimu za Igenge (Bunda), Kirya (Mwanga), Endagaw (Mbulu) na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za Lupiro (Ulanga), Mwamkulu (Mpanda) na Muhongo (Ngara) pamoja na kuandaa Mpango wa Hifadhi ya Mazingira na Jamii katika skimu ya Madibira. Kupitia Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Mpunga, Tume ilitoa mafunzo ya uendeshaji na matunzo kwa wakulima 30 na maafisa ughani wawili katika skimu za Msolwa Ujamaa na Njage katika kanda ya umwagiliaji ya Morogoro iliyopo wilaya ya Kilombero.

**MIFUGO**

**Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake**

212. Mwaka 2018, idadi ya mifugo ilifikia ng'ombe milioni 30.5, mbuzi milioni 18.8, kondoo milioni 5.3 na nguruwe milioni 1.9 ikilinganishwa na ng'ombe milioni 28.4, mbuzi milioni 17.7 kondoo milioni 5.1 na nguruwe milioni 1.85 mwaka 2017. Aidha, kuku wa asili walifikia milioni 38.2 ikilinganishwa na kuku milioni 37.4 mwaka 2017.

213. Mwaka 2018, uzalishaji wa maziwa nchini uliongezeka hadi kufikia lita bilioni 2.40 ikinganishwa na lita bilioni 2.09 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 15. Kati ya kiasi kilichozalishwa, lita milioni 792.04 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita bilioni 1.61 zilitokana na ng'ombe wa asili. Kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kulitokana na ongezeko la idadi ya ng'ombe wa maziwa wa kisasa, ng'ombe wa asili na ng'ombe chotara kufuatia uhimilishaji unaoendelea nchini. Kiwango cha usindikaji wa maziwa kiliongezeka hadi kufika lita milioni 56.2 kwenye viwanda 76 mwaka 2018

ikilinganishwa na lita milioni 40.1 kwenye viwanda 65 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 40.1.

214. Mwaka 2018, uzalishaji wa nyama uliongezeka hadi kufikia tani 679,992 ikilinganishwa na tani 558,164 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 21.8. Kati ya tani hizo, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe ulikuwa tani 471,692; nyama ya mbuzi na kondoo tani 92,999; nyama ya kuku tani 78,110; na nyama ya nguruwe tani 37,191 ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani 394,604; nyama ya mbuzi na kondoo tani 81,064; nyama ya kuku tani 63,597; na nyama ya nguruwe tani 18,899 mwaka 2017. Ongezeko hili lilitokana na kukua kwa mahitaji ya nyama katika soko la ndani na nje ya nchi hususan soko maalum la kwenye migodi, mahoteli ya kitalii na mauzo ya nyama nje ya nchi

215. Mwaka 2018, uzalishaji wa mayai uliongezeka hadi kufikia mayai bilioni 3.2 ikilinganishwa na mayai bilioni 2.8 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 14.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika mashamba makubwa ya kuzalisha mayai. Aidha, uzalishaji wa vifaranga wa kuku wa mayai, wa nyama na chotara ulipungua kutoka vifaranga milioni 64.3 mwaka 2017 hadi vifaranga milioni 62.5 mwaka 2018.

**Jedwali Na.11.5: Uzalishaji wa Mazao Yatokanayo na Mifugo**

| **Aina ya Zao** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Uzalishaji wa Maziwa (Lita 000)** | | | | | | |
| Ng'ombe wa Asili | 1,339,613 | 1,381,451 | 1,381,451 | 1,423,288 | 1,460,900 | 1,608,099 |
| Ngombe wa Kisasa | 623,865 | 650,570 | 677,275 | 703,979 | 626,100 | 792,044 |
| **Jumla** | **1,963,478** | **2,032,021** | **2,058,726** | **2,127,267** | **2,087,000** | **2,400,134** |
| **Uzalishaji wa Nyama (Tani 000)** | | | | | | |
| Ng'ombe | 299,581 | 309,086 | 319,112 | 323,775 | 394,604 | 471,692 |
| Mbuzi/ Kondoo | 115,652 | 120,199 | 124,745 | 129,292 | 81,064 | 92,999 |
| Nguruwe | 50,814 | 74,174 | 54,360 | 91,451 | 18,899 | 37,191 |
| Kuku | 87,408 | 95,292 | 99,540 | 104,292 | 63,597 | 78,110 |
| **Jumla** | **553,455** | **598,751** | **597,757** | **648,810** | **558,164** | **679,992** |
| **Uzalishaji wa Mayai (Idadi 000)** | | | | | | |
| Mayai | 3,725,200 | 3,899,569 | 4,153,800 | 4,353,182 | 2,758,000 | 3,156,692 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Uzalishaji, Utengenezaji na Usindikaji wa Vyakula vya Mifugo**

216. Mwaka 2018, mbegu bora za aina mbalimbali za malisho zenye ujazo wa tani 10 zilizalishwa kutoka mashamba ya Serikali na sekta binafsi ikilinganishwa na tani 3.9 zilizozalishwa mwaka 2017. Aidha, uzalishaji wa majani ya hei uliongezeka kwa asilimia 1.9 na kufikia marobota 1,141,946 ikilinganishwa na marobota 1,120,246 yaliyozalishwa mwaka 2017. Kati ya kiasi hicho, marobota 482,246 yalizalishwa katika mashamba ya Serikali na marobota 659,700 yalizalishwa katika mashamba ya sekta binafsi na kuuzwa kwa wafugaji. Kuongezeka kwa uzalishaji kulitokana na mvua nyingi zilizonyesha katika maeneo ya uzalishaji wa malisho.

217. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuratibu utengenezaji wa vyakula vya mifugo na kusimamia ubora wake ambapo maeneo 72 ya vyakula vya mifugo yalikaguliwa. Kati ya hayo, maeneo 26 ya kutengeneza vyakula vya mifugo na maeneo matano ya kuhifadhia vyakula vya mifugo yalisajiliwa. Aidha, sekta binafsi ilizalisha tani 776,443 za vyakula vya mifugo ikilinganishwa na tani 1,100,000 zilizozalishwa mwaka 2017. Kupungua kwa kiasi cha vyakula vya mifugo vilivyotengenezwa kulitokana na kushuka kwa mahitaji ya vyakula vya mifugo kufuatia upungufu wa vifaranga vya kuku katika soko.

**Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

218. Mwaka 2018, mauzo ya mifugo hai yalikuwa na thamani ya shilingi trilioni 2.36 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.1 mwaka 2017. Mauzo hayo yalijumuisha ng’ombe 1,614,321; mbuzi 1,340,222; na kondoo 315,636 ikilinganishwa na ng’ombe 1,337,095; mbuzi 1,056,218; na kondoo 230,221 mwaka 2017. Aidha, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi ilipungua na kufikia ng’ombe 1,910, mbuzi 2,751 na kondoo 197 ambao kwa pamoja walikua na thamani ya shilingi bilioni 2.7 kutoka ng’ombe 3,421, mbuzi 23,465 na kondoo 1,710 wenye thamani ya shilingi bilioni 7.6 mwaka 2017. Kupungua kwa biashara ya mifugo hai nje ya nchi kulitokana na kuimarishwa kwa usimamizi wa biashara ya mifugo hai na kudhibiti utoroshwaji wa mifugo kwenda nje ya nchi kupitia doria maalum ya Nzagamba I.

219. Kwa upande wa mauzo ya nyama nje ya nchi, jumla ya tani 2,608.93 ziliuzwa katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, Iraq na Vietnam ambapo tani 1,248.14 zilikuwa za nyama ya mbuzi, tani 1,030.79 nyama ya ng’ombe, tani 50 nyama ya kondoo na tani 280 nyama ya punda. Aidha, tani 1,224.55 za

nyama ziliingizwa nchini kutoka Kenya, Afrika Kusini, na Uingereza ambapo tani 506.05 zilikuwa za nyama ya nguruwe, tani 711.03 nyama ya ng'ombe na tani 7.47 nyama ya kondoo.

220. Mwaka 2018, ukusanyaji wa ngozi uliongezeka na kufikia vipande 9,919,704 ambapo vipande vya ngozi za ng'ombe vilikuwa 2,896,796, vipande vya ngozi za mbuzi 5,508,811 na vipande vya ngozi za kondoo 1,514,097 ikilinganishwa na vipande 9,434,559 ambapo vipande vya ngozi za ng'ombe vilikuwa 2,790,561 vipande vya ngozi za mbuzi 4,824,204 na vipande vya ngozi za kondoo 1,819,794 vilivyokusanywa mwaka 2017. Aidha, jumla ya vipande vya ngozi 1,873,180 viliuzwa nje ya nchi ambapo vipande vya ngombe vilikuwa 828,079 na vipande vya mbuzi na kondoo vilikuwa 1,009,101 ikilinganishwa na vipande 2,143,145 vilivyouzwa nje mwaka 2017. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 3,650 za ngozi ghafi na tani 4,840 za ngozi iliyosindikwa kwa hatua ya *wet blue* ziliuzwa nje ikilinganishwa na tani 4,835 za ngozi ghafi na tani 6,482 za ngozi iliyosindikwa kwa hatua za *wet blue* zilizouzwa mwaka 2017.

**Jedwali Na. 11.6: Ukusanyaji na Uuzaji wa Vipande vya Ngozi Nje ya Nchi**

| A: UKUSANYAJI WA VIPANDE VYA NGOZI | | | |
|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Ngozi za Ng'ombe** | **Ngozi za Mbuzi na Kondoo** | **Jumla ya Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo** |
| 2003 | 2,437,100 | 6,437,790 | 8,874,890 |
| 2004 | 2,765,120 | 4,998,234 | 7,763,354 |
| 2005 | 1,937,215 | 2,789,230 | 4,726,445 |
| 2006 | 1,975,721 | 2,987,105 | 4,962,826 |
| 2007 | 2,168,000 | 5,995,305 | 8,163,305 |
| 2008 | 2,543,280 | 3,576,230 | 6,119,510 |
| 2009 | 1,223,668 | 6,983,998 | 8,207,666 |
| 2010 | 2,456,540 | 3,678,294 | 6,134,834 |
| 2011 | 2,378,235 | 4,978,000 | 7,356,235 |
| 2012 | 3,022,400 | 4,928,000 | 7,950,400 |
| 2013 | 2,567,340 | 6,325,525 | 8,892,865 |
| 2014 | 2,263,472 | 3,567,321 | 5,830,793 |
| 2015 | 2,543,914 | 5,983,210 | 8,527,124 |
| 2016 | 2,654,400 | 6,132,212 | 8,786,612 |
| 2017 | 2,790,561 | 6,643,998 | 9,434,559 |
| 2018 | 2,896,796 | 7,022,908 | 9,919,704 |

| B: UUZAJI WA VIPANDE VYA NGOZI NJE | | | |
|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Ngozi za Ng'ombe** | **Ngozi za Mbuzi /Kondoo** | **Jumla ya Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo** |
| 2003 | 1,300,000 | 900,000 | 2,200,000 |
| 2004 | 1,774,000 | 1,919,000 | 3,693,000 |
| 2005 | 1,400,000 | 1,797,155 | 3,197,155 |
| 2006 | 1,363,721 | 2,078,510 | 3,442,231 |
| 2007 | 1,700,000 | 1,980,530 | 3,680,530 |
| 2008 | 2,300,000 | 2,700,000 | 5,000,000 |
| 2009 | 982,668 | 3,469,936 | 4,452,604 |
| 2010 | 739,315 | 2,088,582 | 2,827,897 |
| 2011 | 1,719,506 | 1,561,000 | 3,280,506 |
| 2012 | 2,000,000 | 3,600,000 | 5,600,000 |
| 2013 | 1,269,060 | 2,582,525 | 3,851,585 |
| 2014 | 1,263,472 | 2,716,436 | 3,979,908 |
| 2015 | 1,388,139 | 1,020,000 | 2,408,139 |
| 2016 | 1,575,139 | 1,124,000 | 2,699,139 |
| 2017 | 1,215,030 | 928,115 | 2,143,145 |
| 2018 | 828,079 | 1,009,101 | 1,837,180 |

**Chanzo**: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Jedwali Na. 11.7: Mwenendo wa Mauzo ya Ngozi Nje**

| Mwaka | Ngozi ghafi | | Ngozi zilizoongezwa thamani | | Jumla ya Thamani (Shilingi milioni) | Ngozi zilizoongezwa thamani (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi kg ('000') | Thamani (shilingi Milioni) | Kiasi kg ('000') | Thamani (shilingi Milioni) | | |
| 2007 | 10,569 | 8,571 | 5,566 | 16,036 | 24,607 | 65.2 |
| 2008 | 5,482 | 5,107 | 6,749 | 12,093 | 17,200 | 70.3 |
| 2009 | 1,666 | 1,433 | 5,026 | 6,797 | 8,230 | 82.6 |
| 2010 | 3,241 | 2,438 | 7,217 | 8,672 | 11,110 | 78.1 |
| 2011 | 8,141 | 6,831 | 7,904 | 17,005 | 23,836 | 71.3 |
| 2012 | 2,887 | 3, 445 | 5,011 | 17,375 | 20,820 | 83.5 |
| 2013 | 2 | 3 | 7,061 | 22,686 | 22,689 | 99.9 |
| 2014 | 1,559 | 2,231 | 11,186 | 33,372 | 35,603 | 93.7 |
| 2015 | 372 | 1,185 | 6,594 | 20,878 | 22,063 | 94.6 |
| 2016 | 1,758 | 2,397 | 2,592 | 5,097 | 7,494 | 68.0 |
| 2017 | 4,835 | 6,592 | 6,482 | 9,452 | 16,044 | 58.9 |
| 2018 | 3,650 | 5,064 | 4,840 | 8,794 | 13,858 | 75.4 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania

**MAENDELEO YA USHIRIKA**

221. Mwaka 2018, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliendelea kutekeleza majukumu ya udhibiti, usimamizi na uhamasishaji wa ushirika ili kufikia mafanikio ya kiuchumi, kijamii na kupunguza umaskini. Vyama vya ushirika viliongezeka kutoka 10,990 mwaka 2017 hadi vyama 11,331 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, Tume ilihakiki vyama vya ushirika 8,804 ambapo vyama hai vilikuwa 7,615 na vyama sinzia 1,189. Ajira zilizotolewa na vyama hai zilikuwa 32,688, kati ya hizo 19,980 zilikuwa za mikataba na 12,708 zilikuwa ajira zisizokuwa za mikataba. Kupitia uhakiki huo, SACCOS 3,642 zilipangwa katika madaraja ambapo 32 zilipewa leseni, 365 zilipangwa kwenye daraja la kupewa leseni na 3,245 zilibaki kwenye daraja la SACCOS zilizosajiliwa. Hadi kufika Desemba 2018, mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.3 ilitolewa kwa wanachama wa SACCOS ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 1,007 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Aidha, amana za wanachama zilipungua hadi kufikia shilingi bilioni 37 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi bilioni 53 mwaka 2017.

222. Tume kwa kushirikiana na Bodi ya Leseni za Ghala iliendelea kuhamasisha wakulima wa mazao ya chai, kahawa, pamba, tumbaku, michikichi na kakao kuuza mazao kupitia vyama vya ushirika chini ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Matumizi ya Mfumo huo yaliongeza uzalishaji na ubora wa mazao, kuimarika kwa bei, kuongezeka kwa mapato na kupatikana kwa takwimu sahihi. Mwaka 2017/18, vyama vya ushirika vilikusanya na kuuza mazao ya chai tani 34,010 na tumbaku tani 60,552.

## UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

Jedwali Na. 35

| Msimu[1] | Miwa | | | | Sukari | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakulima | | | | | iliyotumika[3] | |
| | Umma (000 Tani) | Binafsi (000 Tani) | Jumla (000 Tani) | Bei[2] (Sh./Tani) | Iliyozalishwa Tani | Jumla Tani | Kilo kwa kila mtu[4] |
| 2000/01 | 1050 | 284 | 1334 | 14000.00 | 135534 | 122534 | 10.00 |
| 2001/02 | 1134 | 389 | 1523 | 14700.00 | 164498 | 142398 | 10.10 |
| 2002/03 | 1402 | 411 | 1813 | 15000.00 | 190120 | 167300 | 10.42 |
| 2003/04 | 1672 | 670 | 2342 | 16800.00 | 223839 | 290711 | 10.90 |
| 2004/05 | 1594 | 752 | 2346 | 20568.00 | 229617 | 328005 | 10.90 |
| 2005/06 | 1545 | 956 | 2501 | 22383.00 | 263317 | 343292 | 12.00 |
| 2006/07 | 1430 | 611 | 2041 | 29000.00 | 192095 | 366708 | 12.00 |
| 2007/08 | 1967 | 799 | 2766 | 32767.00 | 265434 | 382518 | 13.00 |
| 2008/09 | 2056 | 693 | 2749 | 32770.51 | 279850 | 396113 | 13.40 |
| 2009/10 | 1972 | 598 | 2570 | 42046.00 | 263461 | 398070 | 13.68 |
| 2010/11 | 2357 | 661 | 3018 | 43865.00 | 304135 | 410259 | 12.00 |
| 2011/12 | 2036 | 680 | 2716 | 48833.00 | 262879 | 439307 | 12.00 |
| 2012/13 | 2242 | 711 | 2953 | 52167.00 | 296698 | 468000 | 12.00 |
| 2013/14 | 2198 | 602 | 2800 | 50500.00 | 294300 | 434782 | 12.00 |
| 2014/15 | 2466 | 697 | 3163 | 51333.33 | 304007 | 511680 | 12.00 |
| 2015/16 | 2270 | 569 | 2839 | 59706.67 | 293075 | 525784 | 12.00 |
| 2016/17 | 2504 | 557 | 3061 | 72666.67 | 324930 | 456000 | 12.75 |
| 2017/18 | 2550 | 568 | 3118 | 72666.67 | 303752 | 515004 | 13.50 |
| Badiliko (%) | | | | | | | |
| 2016/17-2017/18 | 1.82 | 2.08 | 1.87 | 0.00 | -6.52 | 12.94 | 5.88 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | |
| 2000/01-2017/18 | 142.8 | 389.7 | 163.3 | 2776.9 | 156.2 | 142.3 | 127.7 |

Chanzo: Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni

2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10 za Sucrose

3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar

4 Ni kwa Tanzania bara

* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

## PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 36

| Msimu [1] | Pamba yenye mbegu | | | | | Pamba iliyoondolewa mbegu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uzalishaji Kiasi (tani) | | | Bei ya wastani (Shs/Kilo) | | Kiasi (tani) | | | Mauzo nchini | | |
| | | | | | | | | | Kiasi (tani) | Bei ya wastani (Shs/tani) | |
| | AR | BR | Jumla | AR | BR | AR | BR | Jumla | Jumla [2] | AR | BR |
| 2000/01 | 123558 | 0 | 123558 | 180.00 | .. | 41415 | .. | 41415 | .. | .. | .. |
| 2001/02 | 148180 | 0 | 148180 | 165.00 | .. | 49668 | .. | 49415 | .. | .. | .. |
| 2002/03 | 187908 | 781 | 188689 | 180.00 | 50 | 62983 | 262 | 63245 | .. | .. | .. |
| 2003/04 | 139756 | 213 | 139969 | 280.00 | 100 | 46843 | 72 | 46915 | .. | .. | .. |
| 2004/05 | 341589 | 0 | 341589 | 250.00 | 0 | 114496 | .. | 114496 | .. | .. | .. |
| 2005/06 | 376591 | 0 | 376591 | 220.00 | 0 | 126228 | .. | 126228 | .. | .. | .. |
| 2006/07 | 130585 | 0 | 130585 | 350.00 | 0 | 43770 | .. | 43770 | .. | .. | .. |
| 2007/08 | 200662 | 0 | 200662 | 450.00 | | 70773 | - | 70773 | 37488 | .. | .. |
| 2008/09 | 368697 | 0 | 368697 | 480.00 | 0 | 123582 | 0 | 123582 | 66554 | .. | .. |
| 2009/10 | 267644 | 0 | 267644 | 480.00 | 0 | 54851 | 0 | 54851 | .. | .. | .. |
| 2010/11 | 163518 | 0 | 163518 | 900.00 | 0 | 54809 | 0 | 54809 | .. | .. | .. |
| 2011/12 | 225938 | 0 | 225938 | 1000.00 | .. | 75731 | .. | 75731 | .. | .. | .. |
| 2012/13 | 351156 | 0 | 351156 | 660.00 | .. | 117702 | .. | 117702 | .. | .. | .. |
| 2013/14 | 245815 | 0 | 245815 | 700.00 | 0 | 82394 | 0 | 82394 | .. | .. | .. |
| 2014/15 | 202312 | 0 | 202312 | 750.00 | 0 | 67812 | 0 | 67812 | | | .. |
| 2015/16 | 149765 | 0 | 149765 | 800.00 | | 50199 | 0 | 50199 | 525784 | 12 | .. |
| 2016/17 | 132934 | 0 | 132934 | 1000.00 | 0 | 42203 | 0 | 42203 | | | |
| 2017/18 | 222039 | 0 | 222039 | 1200.00 | 0 | 47354 | 0 | 47354 | 585795 | 12 | .. |
| Badiliko (%) 2016/17-2017/18 | 67.03 | | 67.03 | 20.00 | | 12.21 | | 12.21 | | | |
| Ongezeko (%) 2000/01-2017/18 | 79.70 | | 79.70 | 566.67 | | 14.34 | | 14.34 | | | |

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Pamba

[1] Msimu ni kati ya Juni na Mei

[2] Ni jumla ya AR na BR

.. Takwimu hazikupatikana

Pamba ya Tanzania hainunuliwi wala kuuzwa katika madaraja kwa sasa

## ENEO LILILOPANDWA MICHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 37

| Msimu [1] | Eneo lililopandwa (hekta): mashamba | | | Majani Mabichi yaliyopatikana (tani) | | | | | | Bei kwa mkulima | Mauzo [2] Nchini |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kiumilikaji: mashamba | | | Kikanda: mashamba | | | | |
| | Makubwa | Madogo | Jumla | Makubwa | Madogo | Jumla | Kaskazini | Kusini | Jumla | (Shs/Kilo) | (tani) |
| 2000/01 | 10811 | 10364 | 21175 | 109007 | 9728 | 118735 | 29419 | 89316 | 118735 | 65.00 | 2386 |
| 2001/02 | 10811 | 10364 | 21175 | 97297 | 13999 | 111296 | 22794 | 88502 | 111296 | 80.00 | 2683 |
| 2002/03 | 11097 | 9762 | 20889 | 100677 | 31718 | 132395 | 28679 | 103716 | 132395 | 85.00 | 3158 |
| 2003/04 | 11485 | 10801 | 22286 | 95986 | 31993 | 127979 | 26384 | 101595 | 127979 | 86.00 | 3225 |
| 2004/05 | 11271 | 11442 | 22713 | 94172 | 39246 | 133418 | 20649 | 112769 | 133418 | 86.00 | 4004 |
| 2005/06 | 11310 | 10977 | 22287 | 91337 | 31881 | 123218 | 29046 | 94172 | 123218 | 93.00 | 3881 |
| 2006/07 | 11271 | 11956 | 23227 | 109632 | 49024 | 158656 | 39673 | 118983 | 158656 | 100.00 | 4737 |
| 2007/08 | 11272 | 11449 | 22722 | 97310 | 51160 | 148470 | 33456 | 115015 | 148471 | 111.00 | 4253 |
| 2008/09 | 11271 | 11449 | 22722 | 100644 | 41167 | 141811 | 31677 | 110134 | 141811 | 118.00 | 4464 |
| 2009/10 | 11272 | 11449 | 22722 | 106021 | 44716 | 150737 | 33309 | 117428 | 150737 | 124.00 | 5084 |
| 2010/11 | 11272 | 11449 | 22722 | 95511 | 47616 | 143127 | 112368 | 30759 | 143127 | 152.00 | 6065 |
| 2011/12 | 11272 | 11449 | 22722 | 88582 | 52359 | 140941 | 27009 | 113932 | 140941 | 200.00 | 4839 |
| 2012/13 | 11272 | 11449 | 22722 | 113628 | 54872 | 168500 | 30997 | 137503 | 168500 | 206.00 | 5498 |
| 2013/14 | 11272 | 11449 | 22722 | 101489 | 47001 | 148490 | 27935 | 120555 | 148490 | 225.00 | 5672 |
| 2014/15 | 11272 | 11449 | 22722 | 100018 | 52467 | 152485 | 23283 | 129202 | 152485 | 176.00 | 6302 |
| 2015/16 | 11272 | 11449 | 22721 | 96759 | 44605 | 141364 | 25413 | 115915 | 141328 | 230.00 | 10257 |
| 2016/17 | 11272 | 11449 | 22722 | 78929 | 41495 | 120424 | 20592 | 99832 | 120424 | 285.00 | 4648 |
| 2017/18 | 11322 | 11705 | 23028 | 97088 | 55426 | 152514 | 31489 | 121025 | 152514 | 312.00 | 5434 |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | | | |
| 2016/17-2017/18 | 0.4 | 2.2 | 1.3 | 23.0 | 33.6 | 26.6 | 52.9 | 21.2 | 26.6 | 9.5 | 16.9 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | | | | | |
| 2000/01-2017/18 | 4.7 | 12.9 | 8.7 | -10.9 | 469.8 | 28.4 | 7.0 | 35.5 | 28.4 | 380.0 | 127.7 |

Chanzo: Bodi ya Chai Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

.. Takwimu hazikupatikana

## KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 38

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (Tani) | | | | Bei (Sh./kilo) | | | Mauzo nchini[+] | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ARABICA | | ROBUSTA | JUMLA | ARABICA | | ROBUSTA | KIASI | THAMANI |
| | Laini | Ngumu | | | Laini | Ngumu | Maganda | (Tani) | (shs'000) |
| 2000/01 | 37176 | 3805 | 17007 | 57988 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 2001/02 | 38000 | 3500 | 12000 | 53500 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 2002/03 | 37294 | 4766 | 34368 | 76428 | .. | .. | .. | .. | .. |
| 2003/04 | 20716 | 1850 | 16138 | 38704 | 1800.00 | 1200.00 | 600.00 | 38704 | 46670 |
| 2004/05 | 23870 | 888 | 9133 | 33891 | 2593.50 | 1976.00 | 1235.00 | 33891 | 62566 |
| 2005/06 | 24116 | 1362 | 8856 | 34334 | 1200.00 | 420.00 | 270.00 | 33300 | 793042 |
| 2006/07 | 33345 | 2417 | 19076 | 54838 | 2840.00 | 1796.00 | 1616.00 | 548 | 129868 |
| 2007/08 | 26330 | 1588 | 15606 | 43524 | 2995.00 | 1875.00 | 1734.00 | 43523 | 89099 |
| 2008/09 | 37207 | 1727 | 29643 | 68577 | 2887.00 | 2172.00 | 1836.00 | 68577 | 165616 |
| 2009/10 | 22217 | 915 | 11467 | 34599 | 3988.00 | 2475.00 | 1563.00 | 34599 | 108741 |
| 2010/11 | 30309 | 2013 | 24348 | 56670 | 4500.00 | 1300.00 | 1200.00 | 56670 | 264144 |
| 2011/12 | 20775 | 941 | 11590 | 33306 | 8144.37 | 5436.40 | 3276.93 | 33306 | 212293 |
| 2012/13 | 33204 | 1655 | 36150 | 71009 | 4850.00 | 3600.00 | 3200.00 | 71009 | 281782 |
| 2013/14 | 28212 | 1115 | 18875 | 48202 | 4314.00 | 3272.94 | 3074.58 | 48202 | 183709 |
| 2014/15 | 26335 | 810 | 18788 | 45933 | 5848.00 | 4515.00 | 3848.50 | .. | .. |
| 2015/16 | 21517 | 460 | 17526 | 39503 | 7249.64 | 5943.40 | 4092.89 | 39503 | 105761 |
| 2016/17 | 27023 | 681 | 19989 | 47693 | 7636.00 | 6164.00 | 4347.00 | 47693 | 129428710 |
| 2017/18 | 30664 | 632 | 11897 | 43193 | 6877.00 | 4807.00 | 4577.00 | 43193 | 116587271 |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | |
| 2016/17-2017/18 | 13.47 | -7.20 | -40.48 | -9.44 | -9.94 | -22.01 | 5.29 | -9.44 | |
| Ongezeko (%) | | | | | | | | | |
| 2003/04-2017/18 | 48.0 | -65.8 | -26.3 | 11.6 | 282.1 | 300.6 | 662.8 | 11.6 | |

Chanzo: Bodi ya Kahawa Tanzania

- \+ Kahawa iliyosafishwa
- 1 Msimu ni kati ya Julai na Juni
- 2 Ni ya muda
- .. Takwimu hazikupatikana

## ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

Jedwali Na. 39

| Msimu[1] | Eneo (Hekta) | | | Katani iliyopatikana | | Mauzo nchini[+] | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Uliokomaa | Usiokomaa | Jumla | Kiasi (tani) | Bei kwa Mkulima (shs/tani) | Kiasi (tani) | Thamani (Sh. milioni) |
| 2000/01 | 34645 | 11473 | 46118 | 23542 | 368077 | 7569 | 2786.0 |
| 2001/02 | 34645 | 11473 | 46118 | 23641 | 337732 | 4947 | 1671.0 |
| 2002/03 | 39462 | 10611 | 50073 | 23280 | 450000 | 6300 | 2835.0 |
| 2003/04 | 29493 | 12204 | 41697 | 26758 | 540000 | 6370 | 4027.0 |
| 2004/05 | 45079 | 14500 | 59579 | 27794 | 617342 | 8213 | 5070.0 |
| 2005/06 | 26384 | 13264 | 39648 | 30934 | 810000 | 10767 | 8613.0 |
| 2006/07 | 28273 | 13608 | 41882 | 33327 | 975000 | 11010 | 10152.0 |
| 2007/08 | 28577 | 15622 | 44199 | 34057 | 1000000 | 16997 | 15800.0 |
| 2008/09 | 35751 | 18023 | 53774 | 25996 | 1000000 | 11496 | 10100.0 |
| 2009/10 | 30556 | 11849 | 42405 | 24092 | 1200000 | 12761 | 10375.0 |
| 2010/11 | 31117 | 12169 | 43286 | 25090 | 1300000 | 11617 | 13154.0 |
| 2011/12 | 32601 | 14302 | 46902 | 36600 | 1500000 | 11511 | 14390.0 |
| 2012/13 | 33649 | 11994 | 45643 | 34874 | 1600000 | 11466 | 16823.0 |
| 2013/14 | 35266 | 11044 | 46310 | 37805 | 1724864 | 9160 | 15.8 |
| 2014/15 | 35946 | 12494 | 48440 | 38872 | 2071446 | 8972 | 17513.0 |
| 2015/16 | 34723 | 13231 | 47954 | 41795 | 2700000 | 9075 | 20342.0 |
| 2016/17 | 41661 | 12850 | 54511 | 36533 | 2700000 | 9559 | 21540.9 |
| 2017/18 | 40635 | 14389 | 55024 | 43280 | 3000000 | 12111 | 30803.1 |
| Badiliko (%) | | | | | | | |
| 2016/17-2017/18 | -2.5 | 12.0 | 0.9 | 18.5 | 11.1 | 26.7 | 43.0 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | |
| 2000/01- 2017/18 | 17.29 | 25.41 | 19.31 | 83.84 | 715.05 | 60.01 | 1005.64 |

Chanzo: Bodi ya Katani

\+ Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

.. Takwimu hazikupatikana

## TUMBAKU ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 40

| Msimu[1] | Iliyonunuliwa (tani) | | | | Bei (shs/kg) | | | Mauzo Nchini[+] | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | Kiasi (tani) | | Thamani (shs.mil.) | |
| | Mvuke | Moshi | Hewa | Jumla | Mvuke | Moshi | Hewa | Mvuke | Moshi | Mvuke | Moshi |
| 2000/01 | 18231 | 6578 | - | 24809 | 543.00 | 556.00 | - | 2176 | 3392 | 5669.00 | - |
| 2001/02 | 25905 | 1799 | - | 27704 | 519.00 | 428.00 | - | 1595 | 348 | 4996.00 | - |
| 2002/03 | 23074 | 4798 | - | 27872 | 563.00 | 547.00 | - | 2325 | 45 | 5940.00 | - |
| 2003/04 | 30124 | 3422 | - | 43547 | 725.00 | 680.00 | - | 2245 | 136 | 6862.00 | - |
| 2004/05 | 41394 | 5983 | 74 | 47451 | 918.11 | 781.93 | 729.23 | 3144 | 252 | 6881.00 | 427.00 |
| 2005/06 | 50494 | 5228 | 741 | 56464 | 983.00 | 735.00 | 635.00 | 3486 | 168 | 9335.00 | 392.00 |
| 2006/07 | 49576 | 1038 | 170 | 50784 | 1264.00 | 881.00 | 960.00 | 3685 | 0 | 14302.00 | 0.00 |
| 2007/08 | 52597 | 2474 | 286 | 55357 | 1144.00 | 849.00 | 957.00 | 4057 | 231 | 15392.26 | 800.87 |
| 2008/09 | 56663 | 3641 | 437 | 60741 | 2741.47 | 1658.85 | 1698.48 | 5544 | 0 | 26167.09 | 0.00 |
| 2009/10 | 88808 | 4901 | 497 | 94202 | 2946.00 | 1691.00 | 1773.00 | 2210 | 148 | 9699.00 | 590.00 |
| 2010/11 | 116886 | 3685 | 0 | 120572 | 1960.00 | 1540.00 | 0 | 1877 | 0 | 11815.00 | 0.00 |
| 2011/12 | 71667 | 2562 | 0 | 74239 | 2784.60 | 2369.97 | 0 | 3862 | 0 | 23890.95 | 0.00 |
| 2012/13 | 84131 | 2212 | 0 | 86343 | 3840.00 | 2720.00 | - | 63967 | 505 | 512764.00 | 2297.00 |
| 2013/14 | 105001 | 802 | 0 | 105803 | 3686.00 | 2182.00 | - | 43910 | 1,252 | 363733.00 | 5347.00 |
| 2014/15 | 87231 | 50 | 0 | 87281 | 3822.00 | 2331.00 | - | 3081 | 0 | 12280.00 | 0.00 |
| 2015/16 | 60691 | 0 | 0 | 60691 | 4633.00 | 0.00 | - | 4790 | 267 | 45143.06 | 1584.55 |
| 2016/17 | 85700 | 161 | 0 | 85861 | 3450.00 | 3381.00 | - | 50696 | 460 | 500602.28 | 1631.23 |
| 2017/18 | 49717 | 805 | 0 | 50522 | 3695.53 | 2720.02 | - | 47696 | | 494192.25 | - |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | | | |
| 2016/17 - 2017/18 | -41.99 | 400.35 | | -41.16 | 7.12 | -19.55 | | -5.92 | | -1.28 | |
| Ongezeko (%) | | | | | | | | | | | |
| 2000/01-2017/18 | 172.71 | -87.76 | | 103.64 | 580.58 | 389.21 | | 2091.91 | | 8617.45 | |

Chanzo: Bodi ya Tumbaku Tanzania

\+ Mauzo ya Tumbaku Moshi ni pamoja na Tumbaku Hewa

1 Msimu ni kati ya April na Machi

\- Takwimu hazikupatikana

## MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI

**Jedwali Na. 41**

| Msimu[1] | Maua yaliyonunuliwa (tani) | | | | Mauzo Nchini: Kiasi (tani) | | | Mauzo Nchini: Thamani (Sh.'000) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kaskazini | Kusini | Jumla | Bei[2] (Sh./kg) | Utomvu (Crude Extract) | Poda | Dawa (Dry Mack) | Utomvu (Crude Extract) | Poda | Dawa (Dry Mack) |
| 2000/01 | 3 | 1463 | 1466 | 400.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2001/02 | 36 | 1699 | 1735 | 420.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2002/03* | 111 | 979 | 1090 | 380.00 | 2 | 90 | - | 106920.00 | 99891.00 | - |
| 2003/04 | 85 | 751 | 842 | 360.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2004/05 | 90 | 910 | 1000 | 360.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2005/06 | - | 2800 | 2800 | 360.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2006/07 | - | 1600 | 1600 | 700.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2007/08 | - | 1470 | 1470 | 1050.00 | - | - | - | - | - | - |
| 2008/09 | - | 1600 | 1600 | 1500.00 | 36.4 | 105.0 | 624.0 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| 2009/10 | - | 1780 | 1780 | 1500.00 | 57.0 | 69.0 | 1035.0 | 37361.00 | 1473.00 | 248.00 |
| 2010/11 | - | 1787 | 1787 | 1500.00 | 57.2 | 69.3 | 69.3 | 37503.70 | 1478.60 | 246.90 |
| 2011/12 | 0 | 5700 | 5700 | 1700.00 | 82.0 | 0.0 | 750.0 | 0.00 | 204.00 | 360919.00 |
| 2012/13 | 0 | 6100 | 6100 | 2400.00 | 84.0 | 0.0 | 2000.0 | 0.00 | 0.00 | 462000.00 |
| 2013/14 | 34 | 2692 | 2726 | 2000.00 | 90.0 | 60.0 | 830.0 | 6900000.00 | 160500.00 | 233000.00 |
| 2014/15 | 31 | 2255 | 2286 | 2500.00 | 76.00 | 30.00 | 430.00 | 133.63 | 116048.05 | 235612.70 |
| 2015/16 | 25 | 1987 | 2012 | 2100.00 | 59.90 | 6.00 | 480.00 | 9450000.00 | 30240.00 | 282240.00 |
| 2016/17 | 39 | 2112 | 2151 | 2050.00 | 53.20 | 162.00 | 727.00 | 6782016.00 | 651810.00 | 436232.00 |
| 2017/18 | 43 | 2356 | 2400 | 2500.00 | 16.00 | 204.00 | 700.00 | 13932947.00 | 869417.00 | 390864.00 |
| Badiliko (%) | | | | | | | | | | |
| 2016/17-2017/18 | 10.2 | 11.6 | 11.6 | 22.0 | -69.9 | 25.9 | -3.7 | 105.4 | 33.4 | -10.4 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | | | | |
| 2000/01-2017/18 | 1340.00 | 61.03 | 63.71 | 525.00 | | | | | | |

Chanzo: Bodi ya Pareto Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Bei ni kwa maua ya daraja la tano

- Takwimu hazikupatikana

* Takwimu hizi hadi December 30 2002, Msimu bado unaendelea

## KOROSHO ZILIZONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

**Jedwali Na. 42**

| Msimu[1] | Zilizonunuliwa (Tani) | | | Bei (shs/kilo) | | Mauzo Nchini | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Gredi ya Juu | Gredi ya Chini | Jumla | Gredi ya Juu | Gredi ya Chini | Kiasi (Kg) | Thamani (sh.'000) |
| 2000/01 | 122283 | - | 122283 | 250.00 | - | 934 | 233 |
| 2001/02 | 64886 | 14394 | 79280 | 300.00 | 180.00 | 2928 | 878 |
| 2002/03 | 79300 | 15700 | 95000 | 360.00 | 290.00 | 5630 | 2122 |
| 2003/04 | 65000 | 15000 | 80000 | 462.00 | 370.00 | 6061 | 2521 |
| 2004/05 | 59425 | 11575 | 71000 | 750.00 | 600.00 | 7013 | 4734 |
| 2005/06 | 61976 | 15470 | 77446 | 600.00 | 480.00 | 10738 | 6354 |
| 2006/07 | 82154 | 8587 | 90741 | 600.00 | 480.00 | 22299 | 13001 |
| 2007/08 | 89639 | 8633 | 98273 | 610.00 | 488.00 | 98273 | 59336 |
| 2008/09 | 48633 | - | 48633 | 700.00 | 560.00 | 48633 | 34043 |
| 2009/10 | 118825 | 355 | 119180 | 1700.00 | 1200.00 | 119180 | 202429 |
| 2010/11 | 65892 | - | 65892 | 1865.00 | - | 65892 | 122889 |
| 2011/12 | 121946 | - | 121946 | 1572.00 | - | 84056 | 123856 |
| 2012/13 | 124723 | 201 | 124924 | 1563.00 | 850.00 | 124924 | 195051 |
| 2013/14 | 174695 | - | 174695 | 1440.00 | - | 174695 | 317944 |
| 2014/15 | 197638 | 295000 | 197933 | 1600.00 | 1100.00 | 197933 | 316220 |
| 2015/16 | 228237 | 3627 | 231864 | 3100.00 | 2442.50 | 231864 | 781140 |
| 2016/17 | 263457 | 1781 | 265238 | | | 265238 | 871463 |
| 2017/18 | 302981 | 10845 | 313826 | | | 313826 | 1191613 |
| Badiliko (%) | | | | | | | |
| 2016/17-2017/18 | 15.00 | 508.89 | 18.32 | | | 18.32 | 36.74 |
| Ongezeko (%) | | | | | | | |
| 2000/01-2017/18 | 147.77 | | 156.64 | -100.00 | | 33500.26 | 511321.98 |

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Korosho

1 Msimu ni kati ya Oktoba mpaka Septemba

\- Takwimu hazikupatikana

**MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA**

Jedwali Na. 43 (Tani)

| Mazao | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | Badiliko % 2016/17 - 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Katani | 25,090 | 36,600 | 34,874 | 37,805 | 38,872 | 41,795 | 36,533 | 43,280 | 18.5 |
| Kahawa | 56,670 | 33,306 | 71,009 | 48,202 | 45,933 | 39,503 | 47,693 | 43,193 | -9.4 |
| Pamba[1] | 163,518 | 225,938 | 351,156 | 245,815 | 202,312 | 149,765 | 164,709 | 269,393 | 63.6 |
| Tumbaku | 120,572 | 74,239 | 86,343 | 105,803 | 87,281 | 60,691 | 85,861 | 50,522 | -41.2 |
| Pareto | 1,787 | 5,700 | 6,100 | 2,726 | 2,286 | 2,011 | 2,151 | 2,400 | 11.6 |
| Chai[2] | 143,127 | 140,941 | 168,500 | 148,490 | 152,485 | 141,328 | 41,495 | 55,426 | 33.6 |
| Korosho | 65,892 | 121,946 | 124,924 | 174,695 | 197,933 | 231,864 | 265,238 | 313,826 | 18.3 |
| Miwa | 3,018 | 2,716 | 2,953 | 2,800 | 3,163 | 2,839 | 556,522 | 568,083 | 2.1 |

Chanzo: : Bodi zinazohusika

1 Yenye mbegu

2 Majani mabichi

# SURA YA 12

# MALIASILI NA UTALII

## Misitu na Nyuki

223. Mwaka 2018, jumla ya tani 30,340 za asali zilivunwa ikilinganishwa na tani 14,082 mwaka 2017. Kati ya hizo, tani 1,095.9 zenye thamani ya shilingi milioni 9,342.5 ziliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na tani 240.8 zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2017 zenye thamani ya shilingi milioni 1,292.0. Ongezeko la thamani ya mauzo ya asali lilitokana na kuimarika kwa bei ya asali katika soko la nje. Aidha, tani 1,440 za nta zilizalishwa mwaka 2018 ikilinganishwa na tani 728 mwaka 2017. Kati ya kiasi hicho, tani 143.0 za nta zenye thamani ya shilingi milioni 1,287.1 ziliuzwa nje mwaka 2018 ikilinganishwa na tani 203.9 zenye thamani ya shilingi milioni 6,879.2 zilizouzwa mwaka 2017. Kiasi cha nta kilichouzwa nje ya nchi kilipungua kwa mwaka 2018 licha ya uzalishaji kuongezeka kutokana na kubadilika kwa bei ya nta katika soko la dunia.

**Jedwali Na 12.1: Mauzo ya Mazao ya Nyuki (Asali na Nta) Nje ya Nchi**

| Mwaka | Asali | | Nta | |
|---|---|---|---|---|
| | Uzito (Tani) | Thamani (Tshs) | Uzito (Tani) | Thamani (Tshs) |
| 2011 | 343.0 | 2,181,319,119 | 534.0 | 3,898,239,826 |
| 2012 | 103.8 | 262,043,582 | 277.0 | 2,582,805,057 |
| 2013 | 83.0 | 287,368,000 | 384.0 | 4,659,954,408 |
| 2014 | 108.2 | 539,927,831 | 271.0 | 3,849,466,035 |
| 2015 | 152.6 | 983,848,159 | 220.2 | 3,238,346,723 |
| 2016 | 259.9 | 1,222,045,655 | 251.9 | 4,549,643,832 |
| 2017 | 240.8 | 1,292,017,450 | 203.9 | 6,879,170,450 |
| 2018 | 1,095.9 | 9,342,538,000 | 143.0 | 1,287,099,000 |

**Chanzo**: Wizara ya Maliasili na Utalii

224. Mwaka 2018, miche ya miti iliyooteshwa ilikuwa milioni 20.4 ikilinganishwa na miche milioni 18.5 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 10.3. Ongezeko hilo lilitokana na mwamko wa upandaji miti kwa jamii kufuatia juhudi za uhamasishaji zilizofanywa na Serikali. Katika kipindi hicho, miche 17,547,823 ilipandwa katika hekta 8,835 na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Aidha, miche 2,845,800 ilipandwa katika mashamba makubwa ya miti yanayomilikiwa na kampuni za *New Forest Company*, *Green Resources* na *TANWAT* kwa kushirikiana na jamii.

225. Mwaka 2018, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania iliendeleza mashamba 23 ya miti kwa kutayarisha mashamba ya kupanda yenye hekta 7,896, kupanda miti katika mashamba mapya manne yenye hekta 5,663, kurudishia miti katika mashamba yaliyovunwa yenye hekta 3,172, na kurudishia miti maeneo ambayo haikuota katika mashamba yenye hekta 2,720. Vile vile, Serikali ilipalilia mashamba yenye ukubwa wa hekta 32,499, kupunguza miti katika hekta 2,508 na kupogoa miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 5,672.

226. Mwaka 2018, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 109.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 103.2 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Hii ilitokana na kuimarika kwa doria kwenye maeneo ya uvunaji, usafirishaji na masoko na kuongezeka kwa uelewa wa wafanyabiashara wa mazao ya misitu kuhusu taratibu na kanuni za kufanya biashara za misitu na nyuki.

**Wanyamapori**

227. Mwaka 2018, sekta ndogo ya wanyamapori ilikusanya jumla ya shilingi milioni 34,274.6 ikilinganishwa na shilingi milioni 29,769.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko wa asilimia 15.1. Ongezeko hilo lilitokana na utumiaji wa mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato (GePG) katika sekta ndogo ya wanyamapori. Katika kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa, siku za doria 356,029 zilifanyika mwaka 2018 katika hifadhi za Taifa, hifadhi ya eneo la Ngorongoro, mapori ya akiba na mapori tengefu ikilinganishwa na siku za doria 262,770 mwaka 2017. Katika doria hizo, vitu na nyara mbalimbali za wanyamapori zilikamatwa ikiwa ni pamoja na: meno ya tembo mazima 413 na vipande 211; bunduki 469; na risasi za aina mbalimbali 386. Kufanyika kwa doria hizo kulipunguza idadi ya matukio ya uhalifu ukiwemo ujangili wa tembo kwa wastani wa asilimia 50 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Kwa mujibu wa Sensa iliyofanyika mwaka 2018 katika mfumo wa ikolojia wa Selous - Mikumi idadi ya tembo ilikuwa takribani 15,500 kama ilivyokuwa katika Sensa ya mwaka 2015. Hii ilitokana na jitihada za Serikali katika kudhibiti ujangili wa tembo.

228. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kukamilisha uanzishwaji wa mfumo wa Jeshi Usu unaojumuisha idara za wanyamapori, misitu na nyuki na Taasisi za Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Wakala wa Huduma za Misitu na Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori ili kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa maliasili. Aidha, watumishi 2,176 kutoka taasisi hizo walipatiwa mafunzo ya kijeshi. Vile vile, marekebisho ya sheria zilizo chini ya sekta ya wanyamapori na misitu yanaendelea ili kuwezesha utekelezaji wa mfumo wa Jeshi Usu.

**Utalii**

229. Mwaka 2018, idadi ya watalii waliotembelea nchini iliongezeka hadi kufikia watalii 1,505,702 ikilinganishwa na watalii 1,327,143 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi, kuboresha kwa huduma za kitalii hususan hoteli na kuwepo kwa mazingira mazuri ya uwekezaji katika biashara ya utalii. Mapato yaliyotokana na utalii yaliongezeka kwa asilimia 10.6 kutoka dola za Marekani milioni 2,199.8 mwaka 2017 hadi dola za Marekani milioni 2,432.9 mwaka 2018. Aidha, watalii 1,168,546 walitembelea Hifadhi za Taifa mwaka 2018 ikilinganishwa na watalii 1,028,564 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Kati ya hao, watalii 726,003 walitoka nje ya nchi na watalii 442,543 walitoka ndani ya nchi kwa mwaka 2018.

230. Mwaka 2018, idadi ya watalii waliotembelea eneo la Hifadhi ya Ngorongoro iliongezeka na kufikia watalii 679,454 ikilinganishwa na watalii 640,458 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Kati ya hao, watalii 410,574 walitoka nje ya nchi na watalii 268,880 walikuwa wa ndani.

231. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi ambapo maandalizi ya utambulisho mpya wa utalii Tanzania ujulikanao kama *Tanzania Unforgettable* ulikamilika; chaneli maalum iitwayo *Tanzania Safari* ilianzishwa kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii; matumizi ya TEHAMA na mitandao ya kijamii yaliimarishwa; ziara za waandishi wa habari wa nje na *bloggers* ziliandaliwa na ofisi za Balozi zetu nje ya nchi zilitumika kutangaza utalii.

232. Mwaka 2018, Serikali kupitia Bodi ya Utalii ilitekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii ikiwemo kushiriki katika maonesho mbalimbali yaliyofanyika nje ya nchi kama *Internationale Tourismus Börse Berlin, China International Expo and Road Show, World Travel Market – London na International Mediterranean Tourism Market.* Vile vile, Serikali iliendelea kuhamasisha utalii wa ndani kupitia maonesho mbalimbali yakiwemo Sabasaba, Nanenane, Wiki ya Utalii Duniani, *Serengeti Cultural Festival, Hydom Tourism Festival,* Karibu Kusini, Tamasha la Mwezi wa Urithi, Onesho la Utalii Nyasa na Kumbukumbu ya Vita vya Maji Maji. Kufuatia jitihada hizo, Serikali ilirekodi na kurusha vipindi 70 vya televisheni na 111 vya redio.

233. Mwaka 2018, Serikali kupitia chuo cha Taifa cha Utalii iliendelea kutoa mafunzo katika fani ya utalii na ukarimu ili kuboresha huduma zitolewazo kwa wageni katika sekta ya utalii. Katika kipindi hicho, washiriki 145 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya uokoaji, mapishi, uongozaji watalii, uongozi,

masoko na usimamizi wa fedha. Vile vile, chuo kilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 611 katika mnyororo wa biashara ya utalii Zanzibar na mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam. Katika kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za utalii, Serikali iliendelea kuanzisha na kurasimisha miradi ya utalii wa kitamaduni ambapo vikundi vya kitamaduni viliongezeka kutoka 66 mwaka 2017 hadi vikundi 76 mwaka 2018.

**Jedwali Na 12.2: Watalii Waliotembelea Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

| Mwezi | 2016 | | 2017 | | 2018 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wageni kutoka nje | Watanzania | Wageni kutoka nje | Watanzania | Wageni kutoka nje | Watanzania |
| Januari | 25,111 | 25,066 | 27,265 | 22,474 | 30,000 | 18,692 |
| Februari | 25,971 | 32,692 | 32,687 | 24,180 | 38,598 | 19,449 |
| Machi | 22,918 | 18,895 | 20,039 | 14,503 | 23,936 | 15,946 |
| Aprili | 11,379 | 17,332 | 14,318 | 14,973 | 12,497 | 10,384 |
| Mei | 13,453 | 18,287 | 15,391 | 14,092 | 16,748 | 12,065 |
| Juni | 23,829 | 25,471 | 36,044 | 25,250 | 33,608 | 20,954 |
| Julai | 25,111 | 25,066 | 50,527 | 22,048 | 55,513 | 40,559 |
| Agosti | 25,917 | 32,692 | 48,756 | 21,863 | 59,635 | 36,394 |
| Septemba | 22,981 | 18,895 | 31,325 | 16,178 | 41,706 | 25,148 |
| Oktoba | 44,575 | 14,527 | 34,551 | 17,066 | 39,537 | 23,467 |
| Novemba | 18,957 | 18,424 | 22,740 | 15,597 | 23,507 | 18,102 |
| Desemba | 24,592 | 18,498 | 57,387 | 41,204 | 35,289 | 27,720 |
| **Jumla** | **284794** | **265845** | **391,030** | **249,428** | **410,574** | **268,880** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii

**Malikale**

234. Mwaka 2018, wageni 53,596 walitembelea vivutio vya malikale ikilinganishwa na wageni 64,709 waliotembelea vivutio hivyo mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 17.2. Hii ilitokana na kupungua kwa ziara za kimafunzo za wanafunzi. Aidha, mapato yaliyotokana na viingilio vya wageni kwenye vivutio vya malikale yaliongezeka kwa asilimia 25.8 kutoka shilingi milioni 125.0 mwaka 2017 hadi kufikia shilingi milioni 157.2 mwaka 2018. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa siku ambazo watalii walikaa nchni. **Jedwali Na. 12.3** linaonyesha idadi ya wageni waliotembelea vivutio vya malikale na mapato yaliyopatikana.

**Jedwali Na. 12.3: Mapato Yatokanayo na Wageni Waliotembelea Vivutio vya Malikale (Shilingi)**

| Kituo | 2016 | | 2017 | | 2018 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wageni | Mapato | Wageni | Mapato | Wageni | Mapato |
| Magomeni | - | - | 304 | 623,000 | 346 | 7,5000 |
| Kaole | 17,544 | 51,460,000 | 14,215 | 19,658,000 | 13,977 | 33,344,000 |
| Isimila | 2,182 | 12,063,000 | 2,278 | 10,040,000 | 2,772 | 11,975,000 |
| Mji Mkongwe | 15,140 | 32,907,500 | 9,519 | 27,393,000 | 8,474 | 30,360,200 |
| Kalenga | 1,528 | 2,478,500 | 1,605 | 2,322,000 | 2,732 | 5,074,000 |
| Kilwa | 3,115 | 22,118,000 | 1,652 | 11,589,500 | 3,048 | 14,311,000 |
| Mbozi | 1,537 | 2,877,000 | 1,637 | 3,354,000 | 3,147 | 6,016,000 |
| Amboni | 9,484 | 22,118,000 | 23,819 | 22,056,000 | 9,667 | 19,905,000 |
| Tongoni | 496 | 1,656,000 | 257 | 1,284,000 | 455 | 1,164,000 |
| Ujiji | 3,715 | 9,056,000 | 3690 | 7,828,000 | 3,826 | 9,054,000 |
| Kwihara | 518 | 991,500 | 540 | 1,100,000 | 362 | 848,000 |
| Kolo | 5,273 | 9,275,000 | 2,259 | 11,575,000 | 1,951 | 17,722,000 |
| Caravan Serai | 4,567 | 10,539,000 | 2,934 | 6,226,500 | 2,839 | 7,344,000 |
| **Jumla** | **65,099** | **177,539,500** | **64,709** | **125,049,000** | **53,596** | **157,192,200** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii- Idara ya Mambo ya Kale

**Uvuvi**

235. Sekta ya Uvuvi iliendelea kusimamia na kudhibiti rasilimali za uvuvi kupitia doria na operesheni maalum; kudhibiti ubora, usalama na viwango vya mazao ya uvuvi; kuimarisha ushiriki wa jamii za wavuvi katika kusimamia rasilimali za uvuvi kupita vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi; na kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo mialo ya kupokelea samaki. Mwaka 2018, sekta ya uvuvi ilitoa ajira kwa wavuvi na wananchi wanaoendelea kutegemea shughuli mbalimbali zikiwemo biashara ya samaki, uchakataji wa samaki na mazao ya uvuvi na utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi.

**Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi**

236. Mwaka 2018, Serikali ilifanya doria za kawaida na operesheni maalum kwa lengo la kudhibiti vitendo vya uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi. Doria na operesheni hizo ziliwezesha kukamatwa kwa nyavu haramu aina ya makila 648,893, timba 11,072, katuli 33, mtando 325, gonga 220, kimia 77, nyavu za dudu/ kuzamia 3,137, kokoro 13,276 na kamba za kokoro zenye urefu wa mita 1,214,957. Aidha, vifaa vilivyokamatwa vilikuwa ndoana 2,114,995, mitumbwi 2966, injini za mitumbwi 1,291, tenki za mafuta 20, taa za sola 1,024, betri za sola 85, magari 2,741 na pikipiki 300. Vile vile, samaki wachanga kilo

240,541, samaki wazazi kilo 189,789, samaki wasioruhusiwa kisheria kilo 227,685, kaa wachanga kilo 1,485, pweza wasiofikia uzito unaokubalika kilo 5,520, mabondo 6,420, kambakoche kilo 278.4 na dagaa kilo 5,500 walikamatwa. Doria na operesheni zilizofanyika ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 6,609 ambapo kesi 78 ziliwasilishwa mahakamani na shilingi bilioni 11.2 zilikusanywa kama faini mwaka 2018.

237. Mwaka 2018, Serikali iliendesha operesheni katika Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi na kukamata mabomu ya milipuko 720, *V-6 explosive* vipande 600,*detonators* 360, mbolea ya urea kilo 324, mitungi ya gesi 68, vifaa vya kuzamia jozi 252 na c*ompressors* 12. Aidha, meli 21 zilikamatwa kwa makosa mbalimbali ambapo kiasi cha shilingi bilioni moja kilitozwa kama faini. Kati ya meli hizo, meli ya Buah Naga Na. 1 ilikamatwa kwa makosa ya kukutwa na mapezi na mikia ya papa 30 bila miili vikiwa na uzito wa kilo 90 ambapo iliamriwa kulipa faini ya dola za Marekani 350,000, sawa na shilingi milioni 770. Serikali ilifanya kaguzi 3,155 za kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwenye viwanda 18 vya uchakataji samaki, mialo 125 ya kupokelea samaki, masoko 31 ya samaki na maghala 52 ya kuhifadhia mazao ya uvuvi.

**Uzalishaji wa Vifaranga vya Samaki na Viumbe Wakuzwao kwenye Maji**

238. Mwaka 2018, uzalishaji wa samaki (sato na kambale) uliongezeka hadi kufikia tani 14,800 zenye thamani ya shilingi milioni 111,000 ikilinganishwa na tani 11,000 zenye thamani ya shilingi milioni 82,500 mwaka 2017. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa mwani uliongezeka na kufikia tani 1,329 zenye thamani ya shilingi milioni 664.5 ikilinganishwa na tani 1,197 zenye thamani ya shilingi milioni 598.5 mwaka 2017. Aidha, tani 371 za kambamiti zenye thamani ya shilingi milioni 5,275.0 zilivunwa na kuuzwa katika Soko la Jumuiya ya Ulaya. Kwa upande wa uzalishaji na upandikizaji wa vifaranga vya samaki, vifaranga 4,080,000 vilikuwa vya perege, 636,000 vya kambale na 11,080,000 vya kambamiti.

**Jedwali Na. 12.4:Uzalishaji wa Samaki wa Maji Baridi (Sato na Kambale) kwenye Mabwawa, Mwani na Kambamiti**

| Mwaka | Uzalishaji Sato na Kambale (Tani) | Thamani ya Sato na Kambale (Shs) (000,000) | Uzalishaji wa Mwani (Tani) | Thamani ya Mwani (000) | Uzalishaji wa kambamiti (Tani) | Thamani ya Kambamiti (000,000) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2008 | 865 | 4,323 | 330 | 65,920 | 120 | 960 |
| 2009 | 936 | 5,616 | 449 | 112,275 | 148 | 1,480 |
| 2010 | 952 | 5,711 | 552 | 165,840 | 131 | 1,310 |
| 2011 | 959 | 5,752 | 689 | 206,550 | 290 | 2,350 |
| 2012 | 972 | 5,832 | 651 | 260,760 | 350 | 3,250 |
| 2013 | 2990 | 17,937 | 401 | 160,440 | 377 | 3,540 |
| 2014 | 3000 | 21,000 | 179 | 89,650 | 320 | 4,000 |
| 2015 | 3118 | 21,826 | 223 | 133,680 | 391 | 5,175 |
| 2016 | 3840 | 26,880 | 1,177 | 627,641 | 407 | 6,975 |
| 2017 | 11,000 | 82,500 | 1,197 | 598,500 | 248 | 3,207 |
| 2018 | 14,800 | 111,000 | 1,329 | 664,500 | 371 | 5,275 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

**Mwenendo wa Uvuvi na Uvunaji wa Samaki na Mazao ya Uvuvi**

239. Mwaka 2018, tani 376,351 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 1.77 zilivunwa ikilinganishwa na tani 387,543 zenye thamani ya trilioni 1.74 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 2.9. Katika kipindi hicho, idadi ya wavuvi ilipungua hadi 202,053 kutoka wavuvi 203,529 na vyombo vya uvuvi vilipungua hadi 58,930 kutoka vyombo 59,338 mwaka 2017. Kati ya kiasi kilichovunwa, tani 323,120 zilitoka maji baridi na tani 53,231 maji chumvi ikilinganishwa na tani 332,373 zilizovunwa kutoka maji baridi na tani 55,170 maji chumvi mwaka 2017. Aidha, ulaji wa mazao ya uvuvi kwa mtu kwa mwaka ulikuwa kilo 7.2 ikilinganishwa na kilo 20.3 zinazopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa. Vile vile, viwanda 22 vya kuchakata mabondo katika Ziwa Victoria vilizalisha kilo 471,579.47 zenye thamani ya shilingi bilioni 161.03 ambazo ziliuzwa nje na kuliingizia Taifa shilingi bilioni 1.06 kama mrabaha.

**Jedwali Na. 12.5: Mwenendo wa Uvunaji wa Rasilimali za Uvuvi**

| Mwaka | Maji baridi | | | Maji chumvi | | | Jumla (Maji chumvi na Baridi) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wavuvi | Vyombo | Uzito (tani) | Wavuvi | Vyombo | Uzito (tani) | Wavuvi | Vyombo | Uzito (tani) |
| 2009 | 135,769 | 45,234 | 288,059 | 36,321 | 7,664 | 47,616 | 172,090 | 52,898 | 335,674 |
| 2010 | 127,280 | 42,337 | 294,474 | 36,321 | 7,664 | 52,683 | 163,601 | 50,001 | 347,157 |
| 2011 | 141,206 | 47,635 | 290,474 | 36,321 | 7,664 | 50,592 | 177,527 | 55,299 | 341,066 |
| 2012 | 147,020 | 49,721 | 322,313 | 36,321 | 7,664 | 50,079 | 182,741 | 56,985 | 365,023 |
| 2013 | 147,644 | 50,120 | 364,602 | 36,321 | 7,664 | 52,846 | 183,431 | 57,385 | 375,158 |
| 2014 | 147,479 | 49,627 | 314,062 | 36,321 | 7,664 | 51,912 | 183,800 | 57291 | 365,974 |
| 2015 | 147,479 | 49,627 | 309,922 | 36,321 | 7,664 | 52,723 | 183,800 | 57291 | 362,645 |
| 2016 | 146,068 | 49,688 | 308,629 | 54,511 | 9,650 | 53,823 | 200,579 | 59,338 | 362,452 |
| 2017 | 146,068 | 49,688 | 332,373 | 54,511 | 9,650 | 55,170 | 203,529 | 59,338 | 387,543 |
| 2018 | 149,018 | 49,688 | 323,120 | 53,035 | 9,242 | 53,231 | 202,053 | 58,930 | 376,351 |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi

### Mwenendo wa Uingizaji na Uuzaji wa Mazao ya Uvuvi Nje

240. Mwaka 2018, tani 44,939.8 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 63,978 wenye thamani ya shilingi bilioni 546.99 waliuzwa nje ikilinganishwa na tani 36,063.2 za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo 101,110 wenye thamani ya shilingi bilioni 407.20 waliouzwa nje mwaka 2017. Kiasi hicho kililiingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 13.52 kama mrabaha ikilinganishwa shilingi bilioni 10.52 mwaka 2017. Aidha, tani 22,752.4 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 44.90 ziliingizwa nchini na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 12.92 ikilinganishwa na tani 22,961.7 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 56.12 zilizoingizwa nchini mwaka 2017.

**IDADI YA WAGENI WALIOTEMBELEA HIFADHI ZA TAIFA NA MAPATO YALIYOPATIKANA**

Jedwali Na. 45

| Mwaka | Nje | Ndani | Jumla | Mapato (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|
| 2015 | 432,124 | 526,110 | 958,234 | 149,957,485,000 |
| 2016 | 439,119 | 518,457 | 957,576 | 175,089,696,000 |
| 2017 | 386,529 | 595,811 | 982,340 | 207,587,218,000 |
| 2018 | 726,003 | 442,543 | 1,168,546 | 214,486,751,736 |
| **JUMLA KUU** | **1,983,775** | **2,082,921** | **4,066,696** | **747,121,150,736** |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

**MAUZO YA BIDHAA ZA MISITU KATIKA MASOKO YA NJE - 2018**

Jedwali Na. 47

| Zao | Kiasi | | Thamani (USD) |
|---|---|---|---|
| | Uzito (kg) | Ujazo (Mita za Ujazo) | |
| Mbao | - | 37,033 | 24,623,059 |
| maji/utomvu wa miwati | 3,834,710 | - | 8,333,160 |
| Unga wa Msandali | 73,290 | - | 1,833,113 |
| Vinyago | 113,027 | 15,381 | 1,060,144 |
| Mbao za Mpingo (Clarinets) | | 134 | 651,473 |
| Mafuta ya Msandali | 69 | | 226,525 |
| Utomvu wa misindano | 257,881 | - | 226,390 |
| Nguzo za Umeme | | 280 | 13,332 |
| Mafuta ya Ubuyu | 52,116 | - | 243,096 |
| Mkwinini (Cinchona) | 92 | - | 3,040 |
| Maganda Mdalasini | 44,000 | | 35,200 |
| Samani | - | 13,713 | 51,000 |
| Gundi ya Arabika | 60,000 | - | 103,130 |
| Mirunda (Mithies) | 60,274 | | 138,000 |
| Venia (Veneer) | - | 3,004 | 586,950 |
| Mazao Mengineyo | 230,510 | 2 | 17,194 |
| **Jumla Kuu** | **4,725,969** | **69,547** | **38,144,806** |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

## IDADI NA MAPATO YATOKANAYO NA UWINDAJI WA KITALII

**Jedwali Na. 48**

| Mwaka | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| | Wawindaji | Watazamaji | Jumla | |
| 2015 | 608 | 393 | 1001 | 28,802,391,200.00 |
| 2016 | 495 | 297 | 792 | 29,136,885,800.00 |
| 2017 | 473 | 291 | 764 | 19,202,957,607.00 |
| 2018 | 503 | 280 | 783 | 20,109,785,000.00 |
| **Jumla Kuu** | **2079** | **1261** | **3340** | **97,252,019,607.00** |

**Chanzo:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Wanyamapori

**UZALISHAJI KATIKA SEKTA YA UVUVI 2000-2018**

Jedwali Na. 50

| Mwaka | Idadi ya Wavuvi | Idadi ya Vyombo | | | Uzalishaji na Mapato | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maji baridi | Maji Chumvi | Jumla ya Vyombo | Maji baridi | | Maji Chumvi | | Jumla | |
| | | | | | Uzito (tani) | Thamani (Sh..) | Uzito (tani) | Thamani (Sh. ) | Uzito (tani) | Thamani (Sh. ) |
| 2000 | 102,329 | 25,014 | 5,157 | 30,171 | 271,000 | 45,500,000 | 49,900 | 32,180,000 | 320,900 | 77,680,000 |
| 2001 | 120,266 | 25,014 | 4,927 | 29,941 | 283,354 | 47,108,668 | 52,935 | 34,113,717 | 336,289 | 81,222,385 |
| 2002 | 124,570 | 31,849 | 4,927 | 36,776 | 273,856 | 54,771,300 | 49,675 | 33,372,136 | 323,531 | 88,143,436 |
| 2003 | 124,570 | 31,225 | 4,927 | 36,152 | 301,855 | 141,073,500 | 49,270 | 34,489,000 | 351,125 | 175,562,500 |
| 2004 | 122,514 | 32,248 | 4,927 | 37,175 | 312,040 | 147,743,000 | 50,470 | 40,376,000 | 362,510 | 188,119,000 |
| 2005 | 133,197 | 32,248 | 7,190 | 39,438 | 320,566 | 256,452,800 | 54,969 | 82,452,930 | 375,535 | 338,905,730 |
| 2006 | 156,544 | 44,362 | 7,190 | 51,552 | 292,519 | 248,640,904 | 48,591 | 37,077,637 | 341,109 | 285,718,540 |
| 2007 | 163,037 | 44,362 | 7,489 | 51,851 | 284,348 | 252,525,198 | 43,499 | 39,210,207 | 327,847 | 291,735,405 |
| 2008 | 170,038 | 44,838 | 7,489 | 52,327 | 281,691 | 194,725,416 | 43,130 | 40,563,641 | 324,821 | 235,289,057 |
| 2009 | 172,090 | 45,234 | 7,664 | 52,898 | 288,059 | 351,394,073 | 47,616 | 56,633,436 | 335,675 | 408,027,509 |
| 2010 | 163,601 | 42,337 | 7,664 | 50,001 | 294,474 | 684,844,020 | 52,683 | 89,639,934 | 347,157 | 774,483,954 |
| 2011 | 177,527 | 47,635 | 7,664 | 55,299 | 290,474 | 1,031,883,681 | 50,592 | 166,954,953 | 341,066 | 1,198,838,634 |
| 2012 | 182,741 | 49,321 | 7,664 | 56,985 | 314,944 | 1,129,349,925 | 50,079 | 177,781,799 | 365,023 | 1,307,131,724 |
| 2013 | 183,431 | 49,721 | 7,664 | 57,385 | 315,008 | 1,248,903,393 | 52,846 | 195,529,127 | 367,854 | 1,444,432,520 |
| 2014 | 183,800 | 49,627 | 7,664 | 57,291 | 314,062 | 1,287,248,813 | 51,912 | 207,649,600 | 365,974 | 1,494,898,413 |
| 2015 | 183,800 | 49,627 | 7,664 | 57,291 | 309,922 | 1,270,856,680 | 52,723 | 210,892,897 | 362,645 | 1,481,749,577 |
| 2016 | 203,529 | 49,688 | 9,650 | 59,338 | 308,772 | 1,274,485,404 | 53,823 | 211,891,899 | 362,595 | 1,486,377,303 |
| 2017 | 203,529 | 49,688 | 9,650 | 59,338 | 332,373 | 1,495,678,680 | 55,170 | 248,262,840 | 387,543 | 1,743,941,520 |
| 2018 | 202,053 | 49,688 | 9,242 | 58,930 | 323,120 | 1,518,667,619 | 53,231 | 250,190,118 | 376,351 | 1,768,857,737 |

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

**MAUZO YA MAZAO YA UVUVI NCHI ZA NJE KWA MWAKA 2017**

Jedwali Na.51

| ZAO | UZITO (TANI) | THAMANI FOB (USD) | FOB (TSH) | USHURU (TSh.) |
|---|---|---|---|---|
| Belly flaps | 17,000 | 2,839 | 6,360,212 | 2,856,450 |
| Blue crab | 594 | 1,780 | 3,986,334 | 333,531 |
| Cowries | 2,000 | 5,994 | 13,422,000 | 269,890 |
| Dried Dagaa/L.Nyasa. | 361,250 | 434,921 | 930,249,962 | 21,901,400 |
| Dried Dagaa/L.Tang. | 100,860 | 486,631 | 623,763,848 | 74,915,713 |
| Dried Dagaa/L.Vict | 3,758,059 | 3,643,409 | 8,264,895,563 | 692,955,170 |
| Dried Dagaa/Marine | 183,912 | 219,106 | 489,537,637 | 193,650,280 |
| Dried fish Maws | 403,734 | 27,274,133 | 61,076,392,131 | 423,717,613 |
| Dried Fish/L.Rukwa | 8,539 | 25,618 | 57,399,811 | 475,000 |
| Dried fish/L.Tang | 133,899 | 463,438 | 1,036,136,297 | 39,834,733 |
| Dried Fish/L.Vict (Kayabo) | 22,536 | 31,066 | 67,982,906 | 15,945,946 |
| Dried Fish/Marine | 2,946 | 8,838 | 19,823,097 | 165,000 |
| Dried Furu/L.Vict. | 1,005,109 | 1,955,698 | 4,442,836,932 | 73,774,230 |
| Dried Salted Fish/L.Rukwa | 47,264 | 73,499 | 165,023,739 | 3,829,550 |
| Dried Shark | 722 | 1,489 | 3,113,200 | 368,360 |
| Dried Shrimps/uduviL.Vict. | 15,910 | 1,509 | 3,340,000 | 879,000 |
| Farmed prawns | 200,888 | 241,065 | 506,236,752 | 33,779,236 |
| Fish Chips | 8,000 | 800 | 1,797,324 | 897,000 |
| Fish Frames/L.Vict | 2,007,000 | 345,474 | 775,850,418 | 42,507,930 |
| Fish Frames/L.Tang | 194,880 | 123,251 | 179,895,000 | 4,358,000 |
| Fish Meal | 414,000 | 16,960 | 37,926,742 | 11,135,800 |
| NP fish skin | 10,014 | 2,154 | 4,828,922 | 560,800 |
| Fresh fish fillets | 6,628,744 | 43,436,626 | 97,363,671,470 | 1,789,851,903 |
| Fresh fish H&G | 1,241,550 | 5,679,042 | 12,733,520,945 | 354,360,070 |
| Fresh fish maws | 130 | 2,850 | 6,391,546 | 263,000 |
| Fresh Fish/L.Tang. | 3,358 | 10,074 | 22,310,242 | 1,060,000 |
| Frozen Crabs | 4,180 | 12,528 | 28,051,980 | 2,812,359 |
| Frozen Cuttle Fish | 2,475 | 7,418 | 16,609,725 | 1,551,908 |
| Frozen fish Chest | 329,348 | 430,603 | 963,915,784 | 56,552,058 |
| Frozen fish fillets | 11,048,756 | 68,070,169 | 151,719,854,740 | 3,107,100,630 |
| Frozen Fish Head | 1,806,944 | 977,249 | 2,191,994,633 | 111,412,495 |
| Frozen fish maws | 339,718 | 15,131,315 | 33,914,000,064 | 629,985,078 |
| Frozen H & G | 1,368,621 | 6,657,472 | 14,598,979,319 | 401,941,861 |
| Frozen Octopus | 1,102,507 | 1,328,648 | 2,820,909,108 | 526,868,725 |
| Frozen Off Cuts | 1,056,388 | 526,334 | 1,177,017,176 | 124,264,433 |
| Frozen Prawns | 3,381 | 9,409 | 21,097,590 | 1,763,844 |
| Frozen sand lobster whole | 6,442 | 19,308 | 40,547,104 | 6,270,618 |
| Frozen Squids | 232,379 | 281,844 | 660,975,893 | 50,809,793 |
| Frozen Tilapia | 50,000 | 149,861 | 314,708,971 | 27,942,125 |
| Live Crabs | 1,007,230 | 2,669,877 | 5,970,210,701 | 1,106,397,553 |
| Live Lobsters | 331,310 | 676,339 | 1,449,702,817 | 323,946,370 |
| Live tropical Fish | 262,651 | 488,454 | 1,042,420,449 | 99,748,825 |
| Prawns Head-on 61 and above | 60,353 | 4,526 | 9,505,598 | 52,954,176 |
| Smorked fish/L.Nyasa | 162,500 | 363,900 | 440,252,805 | 9,720,100 |
| Smorked fish/Mtera Dam | 115,150 | 138,180 | 309,073,297 | 6,439,800 |
| **Jumla** | **36,063,229** | **182,431,698** | **406,526,520,782** | **10,433,128,356** |
| **Samaki Hai - Idadi** | | | | |
| Aquarium fish/L.Nyasa | 30,333 | 90,915 | 203,564,763 | 28,553,762 |
| Aquarium fish/L.Tang | 70,777 | 212,135 | 474,984,447 | 66,625,445 |
| **Jumla Ndogo** | **101,110** | **303,050** | **678,549,210** | **95,179,207** |
| **JUMLA KUBWA** | | **182,734,748** | **407,205,069,992** | **10,528,307,563** |

**MUHTASARI WA MAUZO YA MAZAO YA UVUVI NCHI ZA NJE - 2001-2018**

Jedwali 51A

| Mwaka | Uzito | Samaki Hai wa Mapambo | Thamani | | Ushuru |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kg | Idadi | Tsh | US $ | Tsh |
| 2001 | 41,640,248 | 80,577 | 82,982,764,242 | 95,435,102 | 5,244,333,672 |
| 2002 | 32,662,878 | 28,301 | 99,294,249,903 | 105,779,931 | 5,957,654,995 |
| 2003 | 42,352,738 | 24,500 | 132,862,401,374 | 129,605,815 | 7,789,955,963 |
| 2004 | 46,011,033 | 15,784 | 121,922,686,607 | 112,761,195 | 7,190,356,743 |
| 2005 | 57,289,084 | 21,025 | 162,619,492,949 | 141,597,362 | 9,142,768,084 |
| 2006 | 44,495,623 | 21,741 | 170,184,661,003 | 138,120,145 | 6,236,615,179 |
| 2007 | 57,795,514 | 25,502 | 213,211,258,838 | 173,272,670 | 7,589,576,914 |
| 2008 | 51,426,207 | 33,066 | 205,054,092,453 | 174,409,214 | 6,629,846,700 |
| 2009 | 41,148,261 | 53,188 | 207,447,119,888 | 161,053,646 | 6,410,191,232 |
| 2010 | 39,771,834 | 40,552 | 263,131,442,028 | 187,427,054 | 5,876,103,557 |
| 2011 | 37,996,433 | 61,215 | 233,714,590,011 | 152,973,357 | 6,153,278,023 |
| 2012 | 41,394,268 | 45,550 | 254,901,017,111 | 163,299,366 | 6,819,926,007 |
| 2013 | 38,573,606 | 44,260 | 234,884,628,956 | 147,659,779 | 6,117,769,194 |
| 2014 | 43,354,399 | 42,100 | 1,406,120,001,304 | 832,085,311 | 7,490,632,355 |
| 2015 | 41,059,452 | 87,630 | 547,228,222,096 | 259,286,762 | 13,097,411,199 |
| 2016 | 39,691,462 | 65,841 | 526,985,019,569 | 257,257,100 | 14,302,761,907 |
| 2017 | 36,063,229 | 101,110 | 406,568,122,271 | 182,450,278 | 10,446,850,539 |
| 2018 | 44,939,793 | 63,978 | 546,993,779,393 | 239,680,015 | 13,520,367,822 |
| **JUMLA** | **952,624,027** | **855,920** | **6,033,546,269,898** | **3,995,950,156** | **159,091,264,835** |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Idara ya Uvuvi

**MWELEKEO WA MAUZO YA SANGARA NJE YA NCHI - 2001-2017**

Jedwali 51B

| Mwaka | Uzito | Thamani | | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| | Kg | T.sh | US $ | T.sh |
| 2001 | 39,038,599.7 | 74,928,607,542.3 | 86,178,585.7 | 4,685,276,229.2 |
| 2002 | 29,479,322.7 | 83,005,557,292.2 | 88,231,655.1 | 4,980,333,437.5 |
| 2003 | 37,286,859.2 | 114,779,736,803.6 | 112,049,948.5 | 6,707,948,378.0 |
| 2004 | 30,312,898.3 | 82,356,866,789.0 | 76,261,406.4 | 5,171,324,343.0 |
| 2005 | 53,675,473.7 | 148,785,948,008.6 | 129,184,492.6 | 8,419,301,970.4 |
| 2006 | 39,472,977.7 | 156,160,190,326.6 | 126,829,665.7 | 5,491,786,878.8 |
| 2007 | 50,078,575.6 | 195,242,463,549.7 | 158,442,058.5 | 6,660,034,977.0 |
| 2008 | 38,721,422.2 | 180,366,779,818.2 | 153,740,723.3 | 5,412,912,979.2 |
| 2009 | 28,721,577.0 | 168,368,910,379.9 | 130,644,300.1 | 4,628,409,654.5 |
| 2010 | 27,229,470.7 | 194,012,069,313.9 | 139,666,995.1 | 4,509,670,993.8 |
| 2011 | 25,426,157.2 | 197,899,741,508.3 | 127,601,694.3 | 4,299,987,312.2 |
| 2012 | 28,951,094.7 | 220,149,518,645.6 | 141,189,161.6 | 4,967,311,025.1 |
| 2013 | 33,732,842.7 | 197,578,220,798.6 | 124,551,584.5 | 5,085,642,905.5 |
| 2014 | 24,473,491.8 | 1,131,575,531,076.1 | 665,856,773.0 | 4,569,314,169.6 |
| 2015 | 23,000,579.3 | 528,534,413,018.9 | 250,279,107.2 | 11,251,591,352.1 |
| 2016 | 26,044,655.6 | 345,417,803,263.4 | 177,338,054.4 | 6,964,514,349.1 |
| 2017 | 26,679,946.5 | 376,572,501,425.1 | 168,554,018.9 | 7,057,407,120.5 |
| **JUMLA** | **696,673,517.5** | **4,565,412,920,436.9** | **3,127,323,080.6** | **111,073,431,277.8** |

**Chanzo:** Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Idara ya Uvuvi

**MWENENDO WA BIASHARA YA UTALII 2010-2018**

Jedwali Na. 52

| Maelezo | Kipimo | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya Watalii | Idadi | 782699 | 867994 | 1077058 | 1095884 | 1140156 | 1137182 | 1284279 | 1327143 | 1505702 |
| Watalii wa hotelini | Idadi | 719097 | 753818 | 974448 | 1021766 | 1005058 | 1033555 | 1155851 | 1163752 | 1235905 |
| Mapato | US $ Milion | 1254.5 | 1324.83 | 1712.75 | 1853.28 | 1982.98 | 1901.94 | 2131.57 | 2199.76 | 2432.89 |
| Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini | Siku | 11 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 9 | 10 |
| Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (US $) | *Package Tour* | 328 | 355 | 384 | 372 | 378 | 305 | 351 | 410 | 430 |
| | *Non Package Tour* | 236 | 247 | 230 | 201 | 210 | 141 | 145 | 136 | 125 |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Utalii

**IDADI YA WATALII WALIOINGIA NCHINI NA KIASI CHA FEDHA ZILIZOPATIKANA**

Jedwali Na. 53

| Mwaka | Idadi ya Watalii | Ongezeko kwa Mwaka (%) | Mapato (US $) Milioni | Ongezeko kwa Mwaka (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2000 | 501668 | -20.1 | 739.1 | 0.8 |
| 2001 | 525122 | 4.7 | 725.0 | -1.9 |
| 2002 | 575000 | 9.5 | 730.0 | 0.7 |
| 2003 | 576000 | 0.2 | 731.0 | 0.1 |
| 2004 | 582000 | 1.0 | 746.1 | 2.1 |
| 2005 | 612754 | 5.3 | 823.1 | 10.3 |
| 2006 | 644124 | 5.1 | 950.0 | 15.4 |
| 2007 | 719031 | 11.6 | 1198.0 | 26.1 |
| 2008 | 770376 | 7.1 | 1288.7 | 7.6 |
| 2009 | 714367 | -7.3 | 1159.8 | -10.0 |
| 2010 | 782699 | 9.6 | 1254.5 | 8.2 |
| 2011 | 867994 | 10.9 | 1324.8 | 5.6 |
| 2012 | 1077058 | 24.1 | 1712.8 | 29.3 |
| 2013 | 1095884 | 1.7 | 1853.3 | 8.2 |
| 2014 | 1140156 | 4.0 | 1983.0 | 7.0 |
| 2015 | 1137182 | -0.3 | 1901.9 | -4.1 |
| 2016 | 1284279 | 12.9 | 2131.6 | 12.1 |
| 2017 | 1327143 | 3.3 | 2199.76 | 3.2 |
| 2018 | 1505702 | 13.5 | 2432.89 | 10.6 |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii

**WATALII WALIOTEMBELEA MAMLAKA YA HIFADHI YA NGORONGORO**

Jedwali Na. 54

| Mwaka | Wageni kutoka nje | Watanzania | Jumla ya Watalii |
|---|---|---|---|
| 2009 | 234767 | 203412 | 438179 |
| 2010 | 281513 | 242133 | 523646 |
| 2011 | 281513 | 307086 | 588599 |
| 2012 | 310537 | 254730 | 565267 |
| 2013 | 350970 | 296763 | 647733 |
| 2014 | 332469 | 278221 | 610690 |
| 2015 | 289061 | 278922 | 567983 |
| 2016 | 284794 | 265845 | 550639 |
| 2017 | 391030 | 249428 | 640458 |
| 2018 | 410574 | 268880 | 679454 |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

**IDADI YA WAGENI WALIOTEMBELEA VITUO VYA UTALII**

Jedwali Na. 55

| | 2014 | | 2015 | | 2016 | | 2017 | | 2018 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jina la Hifadhi** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** | **Wageni kutoka Nje** | **Watanzania** |
| ARUSHA | 31,375 | 36,840 | 24,708 | 31,089 | 26,714 | 33,463 | 30,185 | 33,885 | 32,790 | 35,354 |
| GOMBE | 1,120 | 740 | 723 | 895 | 956 | 958 | 1,002 | 968 | 1,194 | 956 |
| KATAVI | 1,928 | 2,541 | 1,200 | 2,445 | 1,159 | 3,066 | 1,190 | 1,910 | 1,482 | 2,369 |
| KILIMANJARO | 52,447 | 2,784 | 41,038 | 3,328 | 43,893 | 3,508 | 47,772 | 2,731 | 51,533 | 2,390 |
| KITULO | 149 | 493 | 70 | 592 | 95 | 311 | 94 | 432 | 179 | 330 |
| LAKE MANYARA | 116,511 | 64,249 | 92,341 | 62,287 | 103,830 | 57,855 | 118,501 | 56,082 | 135,098 | 58,131 |
| MAHALE | 844 | 111 | 896 | 171 | 690 | 166 | 983 | 151 | 886 | 166 |
| MIKUMI | 20,869 | 32,732 | 17,117 | 35,311 | 22,923 | 38,003 | 19,274 | 34,413 | 25,580 | 33,373 |
| MKOMAZI | 695 | 1,115 | 563 | 1,905 | 573 | 1,482 | 594 | 1,700 | 659 | 1,464 |
| RUAHA | 13,490 | 6,718 | 11,558 | 7,403 | 11,233 | 12,958 | 11,217 | 12,161 | 14,381 | 13,219 |
| RUBONDO | 549 | 560 | 447 | 501 | 433 | 739 | 558 | 427 | 465 | 793 |
| SAADANI | 4,042 | 14,527 | 3,143 | 19,854 | 3,548 | 18,722 | 2,530 | 18,603 | 2,976 | 15,048 |
| SERENGETI | 476 | 10,161 | 413 | 13,132 | 201,728 | 174,047 | 474 | 152,216 | 270,946 | 175,084 |
| TARANGIRE | 187,498 | 215,069 | 167,988 | 204,998 | 130,085 | 78,573 | 231,756 | 77,101 | 183,764 | 85,935 |
| UDZUNGWA | 122,019 | 52,847 | 116,590 | 58,585 | 2,759 | 5,557 | 151,681 | 5,268 | 3,420 | 5,530 |
| SAANANE | 3,903 | 5,616 | 2,604 | 6,310 | 464 | 11,102 | 2,617 | 10,088 | 650 | 12,401 |
| **Jumla** | **557,915** | **447,103** | **481,399** | **448,806** | **551,083** | **440,510** | **620,428** | **408,136** | **726,003** | **442,543** |

Chanzo: Wizara ya Maliasili na Utalii - Hifadhi za Taifa (TANAPA)

# SURA YA 13

# MADINI

## Utangulizi

241. Serikali iliendelea kusimamia sekta ya madini ambayo ni mojawapo ya sekta zenye viwango vikubwa vya ukuaji ili kuhakikisha inawanufaisha wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, Serikali ilianzisha Tume ya Madini mwaka 2018 kwa lengo la kuboresha usimamizi katika sekta ya madini.

## Utafutaji Madini

242. Mwaka 2018, leseni 1,687 za utafutaji na uchimbaji wa madini zilitolewa ikilinganishwa na leseni 2,017 zilizotolewa mwaka 2017. Kati ya hizo, leseni 74 zilikuwa za utafutaji madini; leseni 19 za uchimbaji wa kati na leseni 1,594 za uchimbaji mdogo wa madini. Kupungua kwa idadi ya leseni zilizotolewa kulitokana na maboresho ya uhakiki wa leseni zinazokidhi matakwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi 8,716 ya leseni yalipokelewa na kuidhinishwa na Tume ya Madini ikilinganishwa na maombi 71,663 mwaka 2017. Kati ya hayo, maombi 7,985 yalikuwa ya wachimbaji wadogo; maombi 695 ya utafutaji madini; maombi 33 ya uchimbaji wa kati; na maombi matatu ya uchimbaji mkubwa wa madini. Kupungua kwa maombi ya leseni kulitokana na kusimama kwa upokeaji wa maombi ya leseni hadi Tume ya Madini ilipoanza kufanya kazi Aprili 2018.

## Uuzaji wa Madini

243. Mwaka 2018, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 10.3 na kufikia dola za Marekani milioni 1,624.74 kutoka dola za Marekani milioni 1,810.70 mwaka 2017. Hii ilitokana na kuendelea kupungua kwa kiasi cha madini kinachouzwa nje kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 iliyorekebishwa mwaka 2017 ambayo ilizuia usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi kwa lengo la kuyaongezea thamani na kulinda maslahi ya Taifa kwa manufaa ya wananchi.

## Almasi

244. Uzalishaji wa madini ya almasi ulifikia karati 381,302 mwaka 2018 ikilinganishwa na karati 304,456 zilizozalishwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 25.2. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa uzalishaji wa almasi katika mgodi wa *Williamson Diamonds Limited*. Thamani ya mauzo ya

almasi nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 42.3 na kufikia dola za Marekani milioni 96.07 mwaka 2018 kutoka dola za Marekani milioni 67.51 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa bei ya almasi katika soko la dunia katika nusu ya kwanza ya mwaka 2018 pamoja na kuongezeka kwa mauzo ya almasi za rangi ya pinki ambazo huuzwa kwa bei ya juu zaidi ikilinganishwa na bei za almasi za rangi za kawaida.

**Dhahabu**

245. Mwaka 2018, uzalishaji wa dhahabu ulipungua kwa asilimia 9.6 hadi kufikia kilo 39,304 kutoka kilo 43,489 zilizozalishwa mwaka 2017. Upungufu huo, ulitokana na mgodi wa Bulyanhulu kutozalisha dhahabu katika uwezo wake kwa kuendelea kuzalisha dhahabu kutoka kwenye marudio (Tailings Storage Facility). Katika kipindi hicho, thamani ya mauzo ya dhahabu nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 1,454.88 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,636.57 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 11.1. Hii ilitokana na kuendelea kupungua kwa kiasi cha dhahabu ghafi kilichouzwa nje ya nchi.

**Vito vya Thamani**

246. Mwaka 2018, jumla ya kilo 284,321.19 za vito ghafi vya thamani zilizalishwa ikilinganishwa na kilo 1,186,237 zilizozalishwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 76.0. Upungufu huo ulitokana na kusimama kwa uzalishaji katika mgodi wa TanzaniteOne kwa mwaka mzima pamoja na zuio la usafirishaji wa madini ghafi ya vito nje ya nchi.

**Makaa ya Mawe**

247. Mwaka 2018, uzalishaji wa makaa ya mawe uliongezeka kwa asilimia 12.4 na kufikia tani 627,652 kutoka tani 558,553 zilizozalishwa mwaka 2017. Hii ilitokana na kuendelea kuimarika kwa uzalishaji wa makaa ya mawe katika mgodi ya TANCOAL, Magamba, Edenvile International (T) Ltd na Kabulo. Aidha, thamani ya mauzo ya makaa ya mawe iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 34.26 mwaka 2018 kutoka dola za Marekani milioni 22.25 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 54.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanunuzi wa makaa ya mawe kutoka nje na ndani ya nchi.

**Madini Mengine**

248. Mwaka 2018, uzalishaji wa kaolini uliongezeka hadi kufikia tani 129,382.64 kutoka tani 13,815.62 zilizozalishwa mwaka 2017. Ongezeko hilo

lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kaolini katika viwanda vya marumaru vilivyopo Kibaha na Mkuranga. Thamani ya mauzo ya kaolini iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani 119,296.24 mwaka 2018 kutoka dola za Marekani 62,380.38 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 91.2. Uzalishaji wa madini ya bati ulifikia tani 8.04 ikilinganishwa na tani 91.42 zilizozalishwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 91.2. Upungufu huo ulitokana na zuio la usafirishaji wa madini ghafi nje yakiwemo madini ya bati kufuatia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 iliyorekebishwa mwaka 2017.

249. Mwaka 2018, kiwango cha uzalishaji wa madini ya chumvi kilipungua kwa asilimia 63.6 na kufikia tani 36,392.41 kutoka tani 100,017.07 zilizozalishwa mwaka 2017. Upungufu huo ulitokana na zuio la usafirishaji nje wa madini ghafi ikiwemo chumvi. Aidha, thamani ya mauzo ya chumvi ilikuwa dola za Marekani milioni 1.20 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 3.80 mwaka 2017. Uzalishaji wa chokaa ulipungua kwa asilimia 10.8 na kufikia tani 2,943,555.0 kutoka tani 3,300,898.66 mwaka 2017. Uzalishaji wa madini ya jasi ulikuwa tani 241,259.46 mwaka 2018 ikilinganishwa na tani 123,644.69 zilizozalishwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 95.1. Uzalishaji wa madini ya fedha uliongezeka hadi kufikia kilo 12,041 kutoka kilo 10,911 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya fedha katika migodi ya Shanta (Songwe) na Bulyanhulu (Shinyanga). Vile vile, thamani ya mauzo ya madini ya fedha iliongezeka kwa asilimia 3.4 hadi kufikia dola za Marekani milioni 6.05 mwaka 2018 kutoka dola za Marekani milioni 5.85 mwaka 2017.

**Uongezaji Thamani Madini**

250. Serikali iliendelea kutilia mkazo na kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani wa madini kupitia marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017. Mwaka 2018, jumla ya karati 93,415.72 za madini ya vito yaliyokatwa na kusanifiwa yalithaminishwa kwa thamani ya dola za Marekani milioni 6.03. Aidha, Kituo cha Uongezaji Thamani Madini (Tanzania Gemological Centre) kilichopo Arusha kiliendelea kutoa mafunzo ya usanifu wa madini ya vito ambapo wanafunzi 41 walidahiliwa mwaka 2018 na hivyo kufanya wahitimu katika Kituo hicho kufikia 124 tangu kuanzishwa kwa mafunzo hayo mwaka 2014.

## UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA

Jedwali Na.56

| MADINI | Kipimo | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Almasi | Carat | 80,498 | 28,378 | 127,174 | 179,633 | 252,875 | 216,491 | 237,685 | 304,456 | 381,302 |
| Dhahabu | Kg | 39,448 | 37,085 | 39,012 | 42,534 | 40,481 | 43,293 | 45,155 | 43,489 | 39,304 |
| Gemstones | Kg | 2,646,109 | 1,241,581 | 1,237,625 | 1,692,436 | 3,083,765 | 1,872,915 | 2,554,932 | 1,186,237 | 284,321 |
| Chumvi | Tani | 34,455 | 32,297 | 34,016 | 36,032 | 54,757 | 92,158 | 145,718 | 100,017 | 36,392 |
| Phosphate | Tani | 17,180 | 848,512 | 570,626 | 397,020 | 738,000 | 222,800 | 23,658 | 1,351 | - |
| Limestone | 000 Tani | 1,437 | 202 | 1,224 | 35,529 | 873 | 2,945 | 4,170 | 3,301 | 2,944 |
| Tin Ore | Tani | 3 | - | - | 2 | 79 | 179 | 138 | 91 | 8 |
| Gypsum | Tani | 26,918 | 9,288 | 91,610 | 171,567 | 200,179 | 239,302 | 213,744 | 123,645 | 241,260 |
| Makaa ya mawe | Tani | 179 | 80,710 | 78,672 | 84,772 | 246,128 | 257,321 | 276,030 | 558,553 | 627,652 |
| Pozolana | Tani | 60,320 | 113,489 | 75,193 | 79,452 | 68,925 | 342,628 | 230,045 | 79,085 | 91,645 |
| Kaolin | Tani | 58 | 178 | 1,422 | 907 | 3,809 | 1,953 | 656 | 13,816 | 129,383 |
| Madini ya fedha | Kg | 12,470 | 10,399 | 11,227 | 12,159 | 14,493 | 15,569 | 17,984 | 10,911 | 12,041 |
| Shaba | Pound | 11,741,898 | 7,531,164 | 12,426,025 | 12,749,548 | 14,027,008 | 14,252,341 | 15,762,430 | 2,933,941 | - |
| Bauxite | Tani | 39,326,000 | 29,520,000 | 28,433,930 | 39,977,300 | 25,641,201 | 204,956 | 72,779 | 12,090 | 7,140 |
| Madini ya Ujenzi | 000 Tani | | | | 5,470 | 10,480 | 12,960 | 15,460 | 5,601 | 10,375 |

Chanzo: Wizara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

Carat = 0.205 gm

## MADINI YALIYOUZWA NCHI ZA NJE 2014 - 2018

Jedwali Na. 57

| Aina ya madini | Kipimo | Kiasi kilichouzwa | | | | | Thamani ('000 US $) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| Almasi (Rough) | '000 Carats | 252,875 | 216,491 | 239,305 | 304,456 | 383,391 | 82,053 | 56,003 | 85,090 | 67,510 | 96,066 |
| Almasi (iliyokatwa) | '000 Carats | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Almasi (Contruct goods) | '000 Carats | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Dhahabu | '000 Gramu | 40,481 | 43,358 | 45,155 | 43,490 | 35,864 | 1,640,072 | 1,609,392 | 1,824,815 | 1,636,575 | 1,454,879 |
| Mawe ya thamani | '000 Gramu | 3,083,765 | 1,872,915 | 2,944,107 | 1,185,697 | 284,321 | 49,146 | 46,067 | 60,483 | 53,596 | 28,006 |
| Chumvi | Tani | 54,757 | 92,158 | 145,718 | 100,017 | 36,392 | 5,275 | 5,071 | 4,806 | 3,803 | 1,207 |
| Phosphate | Tani | 738,000 | 222,800 | 23,658 | 1,351 | - | 140 | 126 | 721 | 585 | - |
| Bati | Tani | 79 | 179 | 138 | 91 | 8 | 907 | 959 | 1,499 | 1,037 | - |
| Jasi | Tani | 200,179 | 235,920 | 213,744 | 123,645 | 241,260 | 2,518 | 4,445 | 6,279 | 3,187 | - |
| Grafiti | Tani | 25 | 30 | 1,180 | 128 | 27,810 | 3 | 5 | 2,132 | 18 | 2,418 |
| Fedha | 000Grams | 14,493 | 15,569 | 17,984 | 10,911 | 12,041 | 10,283 | 7,626 | 9,901 | 5,850 | 6,045 |
| Shaba | 0001b | 14,027,008 | 14,252 | 16,247 | 2,934 | - | 43,675 | 35,658 | 35,421 | 7,741 | - |
| Madini ya viwandani | Tani | 98 | 151,297 | 4,769,577 | 708,047 | 783,180 | 9 | 3,254 | 78,491 | 29,896 | 35,783 |
| Bauxite | Tani | 25,641,201 | 204,956 | 74,660 | 12,090 | 7,140 | 20,014 | 325 | 1,242 | 898 | 335 |
| **Jumla ('000 US $)** | | | | | | | **1,854,095** | **1,768,930** | **2,110,877** | **1,810,697** | **1,624,739** |

Chanzo: Wizara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

## SURA YA 14

## VIWANDA NA BIASHARA

**Uzalishaji katika Baadhi ya Viwanda Nchini**

251. Mwaka 2018, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani uliongezeka kutokana na mahitaji makubwa katika soko la ndani na nje. Bidhaa zenye ongezeko zilikuwa: rangi (asilimia 19.4), chuma (asilimia 18.9), nyavu za uvuvi (asilimia 16.3), konyagi (asilimia 14.8), unga wa ngano (asilimia 9.3), sigara (asilimia 6.9), bia (asilimia 3.9), dawa za pareto (asilimia 3.7), biskuti na tambi (asilimia 2.8), saruji (asilimia 1.4), tabaka za mbao (asilimia 1.3) na nguo (asilimia 1.1). Hata hivyo, uzalishaji ulipungua kwa baadhi ya bidhaa kama chibuku (asilimia 7.9), kamba za katani (asilimia 0.9), bati (asilimia 0.5) na betri (asilimia 5.7).

252. Mwaka 2018, gharama za uzalishaji bidhaa viwandani ziliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 7,905,622 kutoka shilingi milioni 7,827,349 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia moja. Hii ilitokana na kuendelea kuongezeka kwa bei za malighafi za viwandani zilizoagizwa kutoka nje ya nchi pamoja na gharama za mishahara ya wafanyakazi.

**Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo**

253. Mwaka 2018, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali uliendelea kutoa mafunzo mbalimbali ambapo wajasiriamali 71,794 walipatiwa mafunzo ikilinganishwa na wajasiriamali 54,894 waliopatiwa mafunzo mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Ongezeko hilo, lilitokana na mwamko wa wajasiriamali katika kutumia fursa za kiuchumi zilizojitokeza. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu kilimo bora, kuzalisha mizinga ya nyuki ya kisasa, kubuni mavazi na ushonaji, usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa mitambo na mashine za aina mbalimbali, matumizi ya mbegu bora, ukamuaji wa mafuta na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali.

254. Mwaka 2018, Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.87 kwa wajasiriamali 3,368 ikilinganishwa shilingi bilioni 6.11 zilizotolewa kwa wajasiriamali 3,738 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 3.9. Upungufu huo ulitokana na changamoto za urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wajasiriliamali waliokopa. Mikopo iliyotolewa iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira 7,477 mwaka 2018 ikilinganishwa na fursa za ajira 9,369 mwaka 2017.

255. Mwaka 2018, Serikali kupitia Mamlaka ya Uendelezaji Biashara Tanzania-*TanTrade* ilitoa mafunzo kwa wazalishaji na wafanyabiashara 487 ikilinganishwa na wazalishaji na wafanyabiashara 410 mwaka 2017. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uelewa wa masuala mbalimbali ya biashara ikiwa ni pamoja na usindikaji bora, ufanyaji wa biashara kwa ushindani, mwongozo wa kuuza bidhaa nje ya nchi, urasimishaji biashara, upatikanaji wa vibali vya biashara na matumizi ya kemikali katika usindikaji wa chakula.

256. Mwaka 2018, huduma za mafunzo kwa wajasiriamali wadogo nchini ziliwezesha kugunduliwa kwa teknolojia 359 ikilinganishwa na teknolojia 312 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 15.1. Teknolojia hizo ziliwezesha kuzalishwa kwa mashine mpya 1,417 ikilinganishwa na mashine mpya 775 mwaka 2017. Kuongezeka kwa teknolojia na mashine mpya zilizozalishwa kulitokana na ushiriki mkubwa wa wananchi kwenye shughuli za uchumi wa viwanda. Vile vile, wajasiriamali 2,075 walipata huduma za ushauri wa matumizi ya mashine mpya ikilinganishwa na wajasiriamali 1,592 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 30.3

**Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa**

257. Mwaka 2018, Serikali kupitia *TanTrade* iliwezesha kampuni 2,956 kushiriki maonesho ya 42 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ikilinganishwa na kampuni 2,520 zilizoshiriki maonesho ya 41 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 17.3. Kati ya kampuni zilizoshiriki maonesho mwaka 2018, kampuni 508 zilitoka nje ya nchi ambapo nchi 33 zilishiriki ikilinganishwa na kampuni 515 kutoka nchi 30 zilizoshiriki mwaka 2017. Katika kipindi hicho, kampuni 483 zilifanya biashara ikilinganishwa na kampuni 405 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 19.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mbinu za kuhamasisha ushiriki kwa kuyafikia makundi mbalimbali ya wafanyabiashara na kampuni kutambua umuhimu wa maonesho katika kutangaza bidhaa zao na kuwafikia wateja wengi kwa wakati mmoja. Aidha, mauzo ya papo kwa papo katika maonesho ya 42 yaliongezeka na kufikia wastani wa shilingi milioni 213.7 ikilinganishwa na wastani wa shilingi milioni 122.1 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 75.

258. Mwaka 2018, Serikali kupitia *TanTrade* ilitafuta masoko ya bidhaa za viungo, asali, korosho, ufuta, mikunde, karanga, muhogo na mafuta ya kula ambapo wazalishaji 176 waliunganishwa na masoko mbalimbali ndani na nje ya nchi. Masoko ya ndani ya viungo yalipatikana katika viwanda vya Bagamoyo na ZANOCP kilichopo Zanzibar. Aidha, masoko ya viungo nje ya nchi yalipatikana Uholanzi na Ujerumani na

masoko ya asali yalipatikana nchi za Ujerumani, Ufaransa, Italia na Uturuki. Masoko ya korosho zilizobanguliwa yalipatikana katika nchi za Azerbaijan, Uholanzi, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uturuki. Masoko ya mikunde yalipatikana nchi za China, India na Uarabuni. Vile vile, Serikali kupitia *TanTrade* na wadau wa biashara wa sekta binafsi ilianzisha kliniki ya biashara ili kuongeza uelewa wa wafanyabiashara katika kutambua fursa za masoko ambapo wafanyabiashara 667 walinufaika.

**Usajili wa Biashara na Viwanda**

259. Mwaka 2018, Serikali kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji Leseni (BRELA) ilitoa leseni 194 za kuanzisha viwanda vipya ikilinganishwa na leseni 142 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 36.6. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya uanzishwaji wa viwanda nchini. Aidha, leseni 6,762 za usajili wa makampuni mapya zilitolewa mwaka 2018 ikilinganishwa na leseni 8,584 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 21.2. Vile vile, utolewaji wa leseni za daraja 'A', usajili wa majina ya biashara na usajili wa alama za biashara na huduma ulishuka kwa asilimia 0.9, 33.1 na 21.9 kwa mtiririko huo.

**Miundombinu ya Masoko ya Bidhaa za Mazao na Mifugo**

260. Uwepo wa miundombinu ya masoko uliwezesha shughuli za masoko kufanyika kwa ufanisi, kuwaunganisha wazalishaji na wanunuaji na kupunguza gharama kwa wazalishaji. Miundombinu hiyo ilisaidia kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kupunguza upotevu wa ubora wa bidhaa. Mwaka 2018, miundombinu ya masoko iliyokuwa inafanya kazi kwa ufanisi katika shughuli za uongezaji thamani wa bidhaa mbalimbali nchini iliongezeka. Aidha, vibaraza vya machinjio viliongezeka kwa asilimia 6.9, bucha (asilimia 11.7), banda la ngozi (asilimia 41.5), maghala (asilimia 6.8) na minada ya awali (asilimia 22.1). Katika kipindi hicho, minada ya mipakani ilikuwa tisa, mashine za kuchakata nyama 86 na mashine za kuchakata maziwa 35 ikilinganishwa na minada ya mipakani mitatu, mashine za kuchakata nyama 12 na mashine za kuchakata maziwa 31 mwaka 2017 mtawalia. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji katika sekta za mazao ya kilimo na mifugo na kuongezeka kwa uelewa wa wakulima na wafanyabisahara juu ya umuhimu wa matumizi ya miundombinu hiyo. Kwa upande mwingine, baadhi ya miundombinu ya masoko ilipungua ambapo minada ya upili ilipungua kwa asilimia 40 na mashine za kuchakata samaki asilimia 26.7. Kupungua huko kulitokana na kuharibika kwa baadhi ya miundombinu,gharama kubwa za uendeshaji na upungufu wa malighafi.

**Jedwali Na. 14.1: Aina ya Miundombinu ya Masoko**

| Miundombinu ya Masoko | 2017 | 2018 | Ongezeko (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| Vibaraza vya Machinjio (Slaughter slab) | 2,148 | 2,297 | 6.9 |
| Bucha | 7,412 | 8,280 | 11.7 |
| Banda la ngozi | 530 | 750 | 41.5 |
| Nyumba za Machinjio (Slaughter house) | - | 394 | - |
| Maghala | 573 | 612 | 6.8 |
| Machinjio (Abattoir) | 72 | 59 | -18.1 |
| Minada ya awali | 362 | 442 | 22.1 |
| Minada ya Upili | 20 | 12 | -40 |
| Minada ya Mipakani | 3 | 9 | 200 |
| Mashine za Kuchakata Nyama | 12 | 86 | 616.6 |
| Mashine za Kuchakata Maziwa | 31 | 35 | 12.9 |
| Mashine za Kuchakata Samaki | 15 | 11 | -26.7 |
| Vituo vya Kukusanyia Maziwa | - | 150 | - |

**Chanzo**: Wizara ya Viwanda na Biashara - Agricultural Routine Data System (ARDS, 2018)

**Mwenendo wa Biashara za Kimataifa**

261. Tanzania imeendelea kuwa na mwenendo mzuri wa biashara na nchi mbalimbali duniani. Mwaka 2018, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda China yaliongezeka kufikia dola za Marekani milioni 144.28 kutoka dola za Marekani milioni 142.3 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Bidhaa zilizoagizwa kutoka China zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,762.78 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,408.10 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 25.2. Aidha, bidhaa za Tanzania zilizouzwa India mwaka 2018 zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 734.27 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 977.6 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 24.9. Bidhaa zilizoagizwa kutoka India zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,218.07 ikilinganishwa na dola milioni 1,077.60 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 13.0. Vile vile, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Japani yalikuwa dola za Marekani milioni 66.72 mwaka 2108 ikilinganishwa na dola milioni 75.7 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 11.9. Bidhaa zilizoagizwa kutoka Japani zilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 398.13 ikilinganishwa na dola milioni 365.2 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 9.0.

262. Mwaka 2018, Tanzania iliendelea kufanya vizuri katika mauzo ya bidhaa kwenda kwenye Jumuiya mbalimbali ikilinganishwa na mwaka 2017. Katika kipindi hicho,

mauzo ya bidhaa za Tanzania katika Jumuiya ya Ulaya yaliongezeka kwa asilimia 12.8, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) asilimia 28.0, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) asilimia 13.8, Umoja wa Afrika asilimia 4.6 na kwenye jumuiya za utatu unaounganisha EAC, SADC na COMESA iliongezeka kwa asilimia 13.7. Ongezeko hilo lilitokana na Tanzania kuuza zaidi bidhaa zenye thamani zitokanazo na madini, mbolea za viwandani, ngano, zao la pamba, chai na minofu ya samaki. Aidha, bidhaa zilizoagizwa kutoka Juimuiya ya Ulaya ziliongezeka kwa asilimia 8.5, Jumuiya ya Afrika Mashariki asilimia 37.4, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika asilimia 0.6, Umoja wa Afrika asilimia 10.4 na jumuiya ya utatu inayounganisha EAC, SADC na COMESA asilimia 13.9.

263. Mwaka 2018, Tanzania iliendelea kuwa na urari chanya katika mauzo ya bidhaa ambapo imeuza zaidi kuliko kununua kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki (asilimia 10.6), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (asilimia 29.8), Umoja wa Afrika (asilimia 5.6) na kwenye Tripartite (EAC, SADC na COMESA asilimia 11.8). Tanzania ilikuwa na urari hasi katika mauzo ya bidhaa zake kwenda Jumuiya ya Ulaya kwa asilimia 4.5.

**Jedwali Na14.2: Biashara kati ya Tanzania na Jumuiya Mbalimbali kwa mwaka 2010 - 2018 (Dola za Kimarekani '000,000)**

| Jumuiya | Maelezo | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko 2018-2017 | Badiliko katika % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ulaya | Bidhaa zilizouzwa | 464 | 554 | 745 | 898 | 792 | 709 | 237 | 441 | 498 | 56 | 12.8% |
| | Bidhaa zilizoagizwa | 1111 | 1074 | 1537 | 2759 | 2895 | 1160 | 558 | 936 | 1016 | 80 | 8.5% |
| | **Jumla** | **1575** | **1628** | **2282** | **3658** | **3687** | **1869** | **794** | **1378** | **1514** | **136** | **9.9%** |
| | **Urari** | **-647** | **-521** | **-792** | **-1861** | **-2103** | **-451** | **-321** | **-495** | **-518** | **-23** | **4.7%** |
| Africa Mashariki (EAC) | Bidhaa zilizouzwa | 450 | 352 | 515 | 419 | 598 | 1062 | 438 | 350 | 448 | 98 | 28.0% |
| | Bidhaa zilizoagizwa | 285 | 264 | 668 | 395 | 706 | 323 | 299 | 220 | 303 | 83 | 37.4% |
| | **Jumla** | **735** | **616** | **1184** | **814** | **1305** | **1385** | **737** | **570** | **750** | **180** | **31.7%** |
| | **Urari** | **165** | **89** | **-153** | **24** | **-108** | **740** | **139** | **129** | **145** | **15** | **11.9%** |
| Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) | Bidhaa zilizouzwa | 625 | 1159 | 1422 | 1244 | 1236 | 1358 | 1018 | 878 | 999 | 122 | 13.8% |
| | Bidhaa zilizoagizwa | 828 | 881 | 1093 | 836 | 773 | 771 | 612 | 601 | 604 | 4 | 0.6% |
| | **Jumla** | **1453** | **2040** | **2515** | **2079** | **2009** | **2129** | **1630** | **1478** | **1604** | **125** | **8.5%** |
| | **Urari** | **-203** | **278** | **329** | **408** | **463** | **587** | **406** | **277** | **395** | **118** | **42.5%** |
| Afrika (CFTA) | Bidhaa zilizouzwa | 1206 | 1518 | 2113 | 2420 | 1620 | 1407 | 1262 | 1420 | 1485 | 65 | 4.6% |
| | Bidhaa zilizoagizwa | 1204 | 1719 | 1836 | 1451 | 1483 | 1012 | 985 | 896 | 989 | 93 | 10.4% |
| | **Jumla** | **2410** | **3237** | **3949** | **3871** | **3103** | **2419** | **2247** | **2316** | **2474** | **158** | **6.8%** |
| | **Urari** | **2** | **-201** | **277** | **969** | **138** | **395** | **278** | **524** | **496** | **-28** | **-5.3%** |
| Tripartite (EAC, SADC, COMESA) | Bidhaa zilizouzwa | 1405 | 1831 | 2350 | 2083 | 2441 | 2986 | 1983 | 1900 | 2160 | 260 | 13.7% |
| | Bidhaa zilizoagizwa | 1246 | 1346 | 1917 | 1396 | 2333 | 1529 | 1376 | 1217 | 1386 | 169 | 13.9% |
| | **Jumla** | **2651** | **3177** | **4267** | **3478** | **4774** | **4515** | **3359** | **3117** | **3546** | **429** | **13.7%** |
| | **Urari** | **160** | **485** | **433** | **687** | **108** | **1457** | **608** | **683** | **775** | **91** | **13.4%** |

**Chanzo:** Wizara ya Viwanda na Biashara

## MATUMIZI YA SARUJI NCHINI

Jedwali Na. 58

| Mwaka | Kutoka Nje | Uuzaji nje | Uzalishaji wa Ndani | Tani | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Matumizi Tani | Badiliko, % |
| 2000 | 7281 | 30497 | 833092 | 809876 | -0.6 |
| 2001 | 56395 | 53517 | 900430 | 903308 | 11.5 |
| 2002 | 149079 | 37203 | 1026082 | 1137958 | 26.0 |
| 2003 | 166446 | 34396 | 1186434 | 1318484 | 15.9 |
| 2004 | 125007 | 37655 | 1280851 | 1368203 | 3.8 |
| 2005 | 120200 | 40430 | 1375222 | 1454992 | 6.3 |
| 2006 | 92711 | 98 | 1421460 | 1514073 | 4.1 |
| 2007 | 101827 | 52170 | 1629890 | 1679547 | 10.9 |
| 2008 | 356468 | 99688 | 1755862 | 2012642 | 19.8 |
| 2009 | 516182 | 57569 | 1940845 | 2399458 | 19.2 |
| 2010 | 566828 | 189321 | 2312055 | 2689562 | 12.1 |
| 2011 | 768343 | 217944 | 2408765 | 2959164 | 10.0 |
| 2012 | 1013986 | 145793 | 2557798 | 3425991 | 15.8 |
| 2013 | 1218453 | 154481 | 2369819 | 3433791 | 0.2 |
| 2014 | 1428995 | 142001 | 2795687 | 4082681 | 18.9 |
| 2015 | 1257578 | 126391 | 3273000 | 4404187 | 7.9 |
| 2016 | 1306732 | 194338 | 4916400 | 6028794 | 36.9 |
| 2017 | 188067 | 226588 | 4397684 | 4359163 | -27.7 |
| 2018 | 315553 | 196449 | 4458856 | 4577960 | 5.0 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Jedwali Na.59

| Aina ya Bidhaa | Kipimo | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Biskuti & tambi | Tani | 7435 | 12053 | 16423 | 17440 | 18225 | 19204 | 15890 | 16451 | 16911 | 2.80 |
| Unga wa ngano | Tani | 444242 | 439926 | 442345 | 516778 | 529797 | 533257 | 498940 | 606432 | 662967 | 9.32 |
| Konyagi | 000 Lita | 11186 | 15432 | 16229 | 20680 | 31963 | 29491 | 28754 | 25555 | 29335 | 14.79 |
| Bia | 000 Lita | 242689 | 323393 | 338041 | 374238 | 379913 | 386310 | 383251 | 396864 | 412555 | 3.95 |
| Chibuku | 000 Lita | 21037 | 23474 | 22359 | 19935 | 20301 | 23028 | 26513 | 22624 | 20819 | -7.98 |
| Sigara | Milioni | 6181 | 6630 | 7723 | 7710 | 8028 | 7837 | 8091 | 7412 | 7921 | 6.87 |
| Nguo | 000 $M^2$ | 103177 | 101820 | 81437 | 97522 | 119458 | 100491 | 76436 | 52052 | 52613 | 1.08 |
| Kamba za katani | Tani | 6872 | 6976 | 7927 | 7542 | 7871 | 8851 | 9216 | 8188 | 8116 | -0.88 |
| Nyavu za uvuvi | Tani | 247 | 164 | 272 | 297 | 279 | 311 | 312 | 196 | 228 | 16.33 |
| Mazulia | 000 $M^2$ | - | - | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - |
| Tabaka za mbao | $M^2$ | - | 30589 | 38871 | 36935 | 38913 | 36317 | 34983 | 37302 | 37769 | 1.25 |
| Dawa za pareto | Tani | 49 | 53 | 70 | 83 | 136 | 118 | 126 | 134 | 139 | 3.73 |
| Mbolea | Tani | - | 11200 | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - |
| Rangi | 000 Lita | 28201 | 31211 | 35025 | 36623 | 38308 | 38372 | 35096 | 40146 | 47928 | 19.38 |
| Bidhaa za petrol | 000 Tani | - | - | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - |
| Saruji | 000 Tani | 2313 | 2409 | 2558 | 2369 | 2795 | 3135 | 4572 | 4398 | 4459 | 1.39 |
| Chuma* | Tani | 33384 | 39955 | 46690 | 48500 | 56752 | 62612 | 65686 | 231591 | 275267 | 18.86 |
| Bati | Tani | 71276 | 76912 | 81427 | 85314 | 86825 | 91385 | 91421 | 84541 | 84132 | -0.48 |
| Aluminium | Tani | 59 | 33 | 23 | 37 | 27 | 32 | 14 | - | - | - |
| Radio | 000 namba | - | - | - | - | - | 0 | 0 | - | - | - |
| Betri | Milioni | 93 | 89 | 68 | 75 | 93 | 87 | 69 | 122 | 115 | -5.74 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

- Hakuna uzalishaji

* Takwimu za uzalishaji wa chuma kuanzia mwaka 2008 - 2018 zimerekebishwa

## VIWANDA - IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

Jedwali Na. 60

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | Walioajiriwa | | | | | | Wengine | | | | | | Jumla | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| 151-4 | Vyakula | 63863 | 67056 | 70409 | 73929 | 77625 | 84611 | 21466 | 22540 | 23667 | 24850 | 26092 | 28441 | 85330 | 89596 | 94076 | 98779 | 103718 | 113052 |
| 155 | Vinywaji | 6919 | 7265 | 7629 | 8010 | 8410 | 9167 | 85 | 89 | 93 | 98 | 103 | 112 | 7004 | 7354 | 7722 | 8108 | 8513 | 9279 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 5103 | 5358 | 5626 | 5908 | 6203 | 6761 | 6 | 6 | 7 | 7 | 7 | 8 | 5109 | 5365 | 5633 | 5915 | 6210 | 6769 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 27102 | 28457 | 29880 | 31374 | 32942 | 35907 | 21151 | 22209 | 23319 | 24485 | 25709 | 28023 | 48253 | 50666 | 53199 | 55859 | 58651 | 63930 |
| 191 | Ngozi, bidhaa za ngozi | 1410 | 1480 | 1554 | 1632 | 1713 | 1868 | 316 | 332 | 348 | 366 | 384 | 419 | 1726 | 1812 | 1902 | 1998 | 2097 | 2286 |
| 201-202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 7209 | 7570 | 7948 | 8346 | 8763 | 9551 | 2209 | 2319 | 2435 | 2557 | 2685 | 2926 | 9418 | 9889 | 10383 | 10903 | 11448 | 12478 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 5391 | 5661 | 5944 | 6241 | 6553 | 7142 | 201 | 211 | 222 | 233 | 244 | 266 | 5592 | 5872 | 6165 | 6473 | 6797 | 7409 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali na Madawa ya serikali | 7209 | 7569 | 7948 | 8345 | 8762 | 9551 | 227 | 238 | 250 | 263 | 276 | 301 | 7436 | 7808 | 8198 | 8608 | 9038 | 9852 |
| 251 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 4286 | 4500 | 4725 | 4961 | 5209 | 5678 | 57 | 59 | 62 | 65 | 69 | 75 | 4342 | 4559 | 4787 | 5027 | 5278 | 5753 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 8093 | 8497 | 8922 | 9368 | 9837 | 10722 | 1292 | 1357 | 1424 | 1496 | 1570 | 1712 | 9385 | 9854 | 10347 | 10864 | 11407 | 12434 |
| 271-369 | Nyinginezo | 30303 | 31818 | 33409 | 35079 | 36833 | 40148 | 17201 | 18061 | 18964 | 19912 | 20908 | 22790 | 47503 | 49879 | 52373 | 54992 | 57741 | 62938 |
| | **Jumla** | **166889** | **175233** | **183994** | **193193** | **202852** | **221108** | **64210** | **67421** | **70792** | **74331** | **78047** | **85072** | **231098** | **242654** | **254786** | **267524** | **280899** | **306180** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda viliyvohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## VIWANDA - GHARAMA ZA KAZI

Jedwali Na. 61 (Sh.milioni)

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | Mishahara | | | | | | Malipo Mengine | | | | | | Jumla | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| 151-4 | Vyakula | 165024 | 166675 | 168341 | 170025 | 431636 | 435952 | 48796 | 49284 | 49777 | 50275 | 79023 | 79813 | 213821 | 215959 | 218119 | 220300 | 510659 | 515765 |
| 155 | Vinywaji | 101137 | 102148 | 103169 | 104201 | 264531 | 267177 | 69423 | 70117 | 70818 | 71526 | 112426 | 113550 | 170559 | 172265 | 173987 | 175727 | 376957 | 380727 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 45051 | 45501 | 45956 | 46416 | 117834 | 119013 | 20349 | 20553 | 20758 | 20966 | 32955 | 33284 | 65400 | 66054 | 66715 | 67382 | 150789 | 152297 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 50198 | 50700 | 51207 | 51719 | 131297 | 132610 | 42794 | 43222 | 43654 | 44090 | 69302 | 69995 | 92992 | 93922 | 94861 | 95810 | 200600 | 202605 |
| 191 | Ngozi, Bidhaa za ngozi | 2852 | 2881 | 2910 | 2939 | 7461 | 7535 | 466 | 470 | 475 | 480 | 754 | 762 | 3318 | 3351 | 3385 | 3419 | 8215 | 8297 |
| 201- 202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 13279 | 13412 | 13546 | 13681 | 34732 | 35079 | 3037 | 3067 | 3098 | 3129 | 4918 | 4967 | 16316 | 16479 | 16644 | 16810 | 39650 | 40047 |
| 210-221-222 | Karatasi, Uchapishaji | 24130 | 24371 | 24615 | 24861 | 63114 | 63745 | 8641 | 8728 | 8815 | 8903 | 13994 | 14134 | 32771 | 33099 | 33430 | 33764 | 77108 | 77879 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali na Mada | 32758 | 33086 | 33417 | 33751 | 85682 | 86538 | 8268 | 8351 | 8434 | 8519 | 13390 | 13524 | 41026 | 41437 | 41851 | 42269 | 99072 | 100062 |
| 251 | Bidhaa za Mpira na Plastiki | 16834 | 17002 | 17172 | 17344 | 44031 | 44471 | 3998 | 4038 | 4079 | 4119 | 6475 | 6540 | 20832 | 21041 | 21251 | 21463 | 50506 | 51011 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 44344 | 44788 | 45236 | 45688 | 115986 | 117146 | 21708 | 21925 | 22144 | 22366 | 35155 | 35506 | 66052 | 66713 | 67380 | 68054 | 151141 | 152652 |
| 271-369 | Nyinginezo | 73154 | 73886 | 74625 | 75371 | 191342 | 193255 | 24588 | 24834 | 25082 | 25333 | 39818 | 40217 | 97742 | 98720 | 99707 | 100704 | 231160 | 233472 |
| | **Jumla** | **568762** | **574449** | **580194** | **585996** | **1487646** | **1502522** | **252068** | **254589** | **257135** | **259706** | **408210** | **412292** | **820830** | **829038** | **837329** | **845702** | **1895856** | **1914814** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO

Jedwali Na. 62

| ISIC (Rev 3) | Shughuli | PATO | | | | | | GHARAMA | | | | | | Thamani Iliyoongezeka (Value Added) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| 151-4 | Vyakula | 4231129 | 4273440 | 4316175 | 4359336 | 6549583 | 6615079 | 2322611 | 2345838 | 2350020 | 2296401 | 3010077 | 3040178 | 1908518 | 1927603 | 1966155 | 2062936 | 3539505 | 3574901 |
| 155 | Vinywaji | 1744910 | 1762360 | 1779983 | 1797783 | 2701037 | 2728047 | 724600 | 731846 | 728859 | 694919 | 808786 | 816874 | 1020310 | 1030514 | 1051124 | 1102864 | 1892251 | 1911174 |
| 160 | Tumbaku na Sigara | 655707 | 662264 | 668886 | 675575 | 1015002 | 1025152 | 245768 | 248226 | 246568 | 232469 | 254737 | 257285 | 409938 | 414038 | 422318 | 443106 | 760265 | 767867 |
| 171-2, 181 | Ufumaji na Ushonaji | 512018 | 517138 | 522309 | 527532 | 792579 | 800505 | 280298 | 283101 | 283592 | 277064 | 362835 | 366463 | 231720 | 234037 | 238718 | 250468 | 429744 | 434041 |
| 191 | Ngozi, bidhaaa za ngozi | 57467 | 58042 | 58623 | 59209 | 88957 | 89846 | 42063 | 42484 | 42753 | 42558 | 60388 | 60992 | 15405 | 15559 | 15870 | 16651 | 28569 | 28855 |
| 201-202 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 155563 | 157119 | 158690 | 160277 | 240805 | 243213 | 68791 | 69479 | 69297 | 66484 | 79878 | 80677 | 86772 | 87640 | 89393 | 93793 | 160927 | 162536 |
| 210-221-22 | Karatasi, Uchapishaji | 281228 | 284040 | 286881 | 289750 | 435327 | 439681 | 191843 | 193761 | 194796 | 193132 | 269555 | 272251 | 89385 | 90279 | 92085 | 96617 | 165772 | 167430 |
| 241-2 | Utengenezaji wa Kemikali na madawa ya Binadamu | 615973 | 622133 | 628354 | 634638 | 953497 | 963032 | 423562 | 427798 | 430133 | 426659 | 596655 | 602621 | 192411 | 194335 | 198222 | 207979 | 356842 | 360411 |
| 251 | Bidhaa za mpira na Plastiki | 632722 | 639049 | 645440 | 651894 | 979423 | 989217 | 446088 | 450549 | 453169 | 450160 | 633295 | 639628 | 186634 | 188500 | 192270 | 201734 | 346128 | 349590 |
| 261-9 | Bidhaa za Madini yasiyo Chuma | 807924 | 816003 | 824163 | 832405 | 1250627 | 1263134 | 475805 | 480563 | 482015 | 473415 | 634686 | 641032 | 332119 | 335440 | 342149 | 358990 | 615942 | 622101 |
| 271-369 | Nyinginezo | 1242153 | 1254575 | 1267121 | 1279792 | 1922793 | 1942021 | 807373 | 815447 | 819210 | 809834 | 1116457 | 1127622 | 434780 | 439128 | 447910 | 469958 | 806336 | 814399 |
| | **Jumla** | **10936795** | **11046163** | **11156625** | **11268191** | **16929630** | **17098926** | **6028804** | **6089092** | **6100412** | **5963094** | **7827349** | **7905622** | **4907992** | **4957072** | **5056213** | **5305097** | **9102281** | **9193304** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA *

Jedwali Na. 63

| Jina la mkoa | Idadi ya Wafanyakazi | | | | | | Idadi ya Waajiriwa | | | | | | Mishahara (TShs. Milioni) | | | | | | Thamani Iliyoongezeka (TShs. Milioni) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| Dodoma | 5032 | 5284 | 3048 | 2895 | 3039 | 3313 | 3239 | 3401 | 2201 | 2090 | 2195 | 2392 | 3848 | 3886 | 7580 | 17729 | 18616 | 18802 | 22501 | 22726 | 64116 | 105955 | 115042 | 116192 |
| Arusha | 15482 | 16257 | 21624 | 22705 | 23840 | 25986 | 13015 | 13665 | 15616 | 16397 | 17216 | 18766 | 36788 | 37156 | 80881 | 60196 | 63206 | 63838 | 222748 | 224976 | 684124 | 359746 | 390599 | 394505 |
| Kilimanjaro | 9034 | 9485 | 16238 | 17049 | 17901 | 19512 | 7073 | 7426 | 11726 | 12312 | 12927 | 14091 | 43613 | 44049 | 51158 | 76247 | 80059 | 80860 | 148593 | 150079 | 432717 | 455668 | 494748 | 499696 |
| Tanga | 12785 | 13425 | 10448 | 12869 | 13513 | 14729 | 10603 | 11133 | 7545 | 9294 | 9758 | 10637 | 22653 | 22880 | 28352 | 95014 | 99765 | 100762 | 165283 | 166936 | 239817 | 567824 | 616523 | 622689 |
| Morogoro | 20992 | 22042 | 38410 | 40331 | 42347 | 46159 | 16739 | 17576 | 27738 | 29125 | 30581 | 33333 | 44971 | 45421 | 34780 | 40309 | 42324 | 42748 | 619838 | 626036 | 294187 | 240895 | 261555 | 264170 |
| Pwani, | 5137 | 5394 | 11216 | 12554 | 13181 | 14368 | 3271 | 3435 | 8100 | 9066 | 9519 | 10376 | 6862 | 6930 | 43754 | 57189 | 60048 | 60649 | 19648 | 19845 | 370094 | 341774 | 371086 | 374796 |
| Dar es Salaam | 53137 | 55794 | 83790 | 86320 | 90635 | 98793 | 43688 | 45872 | 60509 | 62336 | 65453 | 71343 | 163138 | 164770 | 484349 | 813534 | 854210 | 862752 | 1354652 | 1368198 | 4096841 | 4861845 | 5278818 | 5331606 |
| Lindi | 2756 | 2894 | 579 | 1288 | 1352 | 1474 | 1476 | 1550 | 418 | 930 | 977 | 1065 | 925 | 934 | 326 | 362 | 380 | 384 | 4700 | 4747 | 2758 | 2164 | 2349 | 2373 |
| Mtwara | 3231 | 3392 | 3274 | 3733 | 3919 | 4272 | 1680 | 1764 | 2364 | 2696 | 2830 | 3085 | 2464 | 2489 | 4264 | 13490 | 14165 | 14307 | 27969 | 28248 | 36067 | 80622 | 87536 | 88411 |
| Ruvuma | 7015 | 7366 | 2187 | 2408 | 2529 | 2756 | 2520 | 2646 | 1579 | 1739 | 1826 | 1991 | 2159 | 2180 | 3962 | 2721 | 2857 | 2885 | 12690 | 12817 | 33516 | 16260 | 17655 | 17831 |
| Iringa | 9453 | 9926 | 7386 | 6419 | 6740 | 7346 | 6844 | 7186 | 5334 | 4635 | 4867 | 5305 | 11438 | 11553 | 13955 | 32181 | 33790 | 34128 | 64853 | 65502 | 118042 | 192320 | 208815 | 210903 |
| Mbeya | 9576 | 10055 | 7321 | 7687 | 8072 | 8798 | 6246 | 6558 | 5287 | 5551 | 5829 | 6353 | 27089 | 27360 | 13816 | 65472 | 68745 | 69433 | 184137 | 185979 | 116865 | 391272 | 424829 | 429078 |
| Singida | 5281 | 5545 | 3041 | 2975 | 3123 | 3404 | 3480 | 3654 | 2196 | 2148 | 2256 | 2459 | 1686 | 1703 | 1602 | 2354 | 2472 | 2497 | 20053 | 20254 | 13550 | 14070 | 15276 | 15429 |
| Tabora | 2728 | 2865 | 901 | 947 | 994 | 1084 | 1778 | 1867 | 651 | 684 | 718 | 782 | 7078 | 7149 | 11206 | 12986 | 13635 | 13772 | 49174 | 49666 | 94782 | 77606 | 84262 | 85105 |
| Rukwa | 2088 | 2192 | 2097 | 1981 | 2080 | 2267 | 806 | 846 | 1515 | 1431 | 1502 | 1637 | 722 | 729 | 7589 | 7501 | 7876 | 7955 | 34757 | 35105 | 64189 | 44826 | 48671 | 49157 |
| Kigoma | 2652 | 2785 | 2584 | 2411 | 2532 | 2760 | 1321 | 1387 | 1866 | 1741 | 1828 | 1993 | 1470 | 1485 | 1052 | 1264 | 1327 | 1341 | 18215 | 18397 | 8902 | 7556 | 8204 | 8286 |
| Shinyanga | 8966 | 9415 | 3653 | 3547 | 3724 | 4059 | 7201 | 7561 | 2638 | 2561 | 2689 | 2932 | 109752 | 110849 | 18572 | 12898 | 13543 | 13679 | 535417 | 540771 | 157088 | 77083 | 83695 | 84531 |
| Kagera | 12654 | 13287 | 4826 | 4620 | 4851 | 5288 | 9005 | 9455 | 3485 | 3337 | 3504 | 3819 | 8332 | 8415 | 4582 | 6006 | 6306 | 6369 | 52448 | 52973 | 38754 | 35892 | 38970 | 39359 |
| Mwanza | 9133 | 9589 | 12951 | 14148 | 14856 | 16193 | 7317 | 7683 | 9353 | 10217 | 10728 | 11694 | 20983 | 21193 | 51499 | 75414 | 79185 | 79976 | 169923 | 171623 | 435598 | 450689 | 489342 | 494235 |
| Mara | 12611 | 13241 | 4745 | 4533 | 4760 | 5188 | 5969 | 6267 | 3427 | 3273 | 3437 | 3746 | 18615 | 18801 | 3463 | 6589 | 6918 | 6988 | 614399 | 620543 | 29289 | 39377 | 42754 | 43182 |
| Manyara | 10515 | 11040 | 6053 | 6594 | 6924 | 7547 | 7653 | 8036 | 4371 | 4762 | 5000 | 5450 | 9479 | 9574 | 3233 | 3138 | 3294 | 3327 | 45947 | 46407 | 27344 | 18751 | 20359 | 20563 |
| Njombe | 4931 | 5177 | 3360 | 3529 | 3705 | 4039 | 2427 | 2549 | 2427 | 2548 | 2676 | 2917 | 1542 | 1557 | 2536 | 5988 | 6288 | 6350 | 14689 | 14836 | 21450 | 35786 | 38856 | 39244 |
| Katavi | 460 | 483 | 1302 | 1829 | 1920 | 2093 | 294 | 309 | 940 | 1320 | 1387 | 1511 | 32 | 32 | 329 | 1288 | 1352 | 1366 | 1514 | 1530 | 2785 | 7698 | 8358 | 8441 |
| Simiyu | 1988 | 2087 | 2141 | 2248 | 2361 | 2573 | 928 | 974 | 1546 | 1624 | 1705 | 1858 | 237 | 239 | 2404 | 4809 | 5050 | 5100 | 4078 | 4119 | 20333 | 28742 | 31207 | 31519 |
| Geita | 3459 | 3632 | 530 | 772 | 810 | 883 | 2318 | 2434 | 383 | 557 | 585 | 638 | 22887 | 23116 | 288 | 237 | 249 | 251 | 499762 | 504759 | 2439 | 1415 | 1536 | 1551 |
| Songwe | | | 1079 | 1132 | 1189 | 1296 | | | 779 | 818 | 859 | 936 | | | 712 | 1889 | 1984 | 2004 | | | 6019 | 11290 | 12259 | 12381 |
| **Jumla** | **231098** | **242654** | **254786** | **267524** | **280899** | **306180** | **166889** | **175233** | **183994** | **193193** | **202852** | **221108** | **568762** | **574449** | **876245** | **1416806** | **1487646** | **1502522** | **4907992** | **4957072** | **7411668** | **8467124** | **9193302** | **9285235** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013 na Utafiti wa mwaka 2015 na 2016 wa Uzalishaji Viwandani

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

## VIGEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWANDA (Asilimia)

**Jedwali Na. 65**

| Mwaka | Mchango katika Pato la Taifa (Bei za miaka husika) | Ukuaji wa Sekta (Bei za Mwaka 2015) | Mchango katika mauzo nje | Mchango katika mauzo nje yasiyo asilia | Badiliko katika mauzo nje ya bidhaa za viwanda |
|---|---|---|---|---|---|
| 2012 | 9.44 | | 17.6 | 24.90 | |
| 2013 | 9.11 | 3.7 | 20.4 | 28.95 | 3.4 |
| 2014 | 9.12 | 10.0 | 23.3 | 32.63 | 15.6 |
| 2015 | 7.86 | 7.1 | 25.3 | 33.14 | 10.1 |
| 2016 | 7.81 | 10.8 | 19.5 | 23.53 | -20.0 |
| 2017 | 7.67 | 8.2 | 15.0 | 22.44 | -36.5 |
| 2018 | 8.05 | 8.3 | 18.1 | 24.76 | 14.5 |

**Chanzo:** Wizara ya Fedha na Mipango

## SURA YA 15

## UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

### UJENZI

**Mtandao wa Barabara Nchini**

264. Mtandao wa barabara nchini una urefu wa kilometa 86,472. Mtandao huo unajumuisha kilometa 12,176 za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, kilometa 24,082 za barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu nchini na kilometa 50,214 ni barabara za wilaya zinazounganisha wilaya, kata na vijiji.

265. Mwaka 2018, barabara kuu na barabara za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe/udongo zilikuwa na urefu wa kilometa 36,260 ikilinganishwa na kilometa 35,000 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya barabara za wilaya kupandishwa hadhi na kuwa barabara za mikoa. Aidha, barabara nyingine zilizokuwa chini ya halmashauri zilikasimishwa kwa TANROADS. Kati ya kilometa 36,260 za barabara kuu na za mikoa, kilometa 32,852 zilifanyiwa tathmini ambapo kilometa 11,043, sawa na asilimia 34 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 11,681 mwaka 2017. Barabara zenye hali nzuri zilipungua kutokana na kuongezeka kwa barabara za wilaya zenye hali mbaya kwenye mtandao wa barabara zinazohudumiwa na TANROADS. Aidha, kilometa 17,592 sawa na asilimia 54 zilikuwa katika kiwango cha wastani ikilinganishwa na kilometa 16,639 mwaka 2017 na kilometa 4,217 sawa na asilimia 13 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 3,849 mwaka 2017. Barabara zenye hali mbaya ziliongezeka pia kwa kuwa barabara za wilaya zenye hali mbaya zimeongezwa kwenye mtandao wa barabara zinazohudumiwa na TANROADS.

266. Hadi kufikia Desemba 2018, barabara kuu zenye kiwango cha lami na changarawe zilizofanyiwa tathmini zilikuwa na urefu wa kilometa 10,490, sawa na asilimia 31.9 ya mtandao wa barabara kuu ikilinganishwa na kilometa 10,065 mwaka 2017. Kati ya hizo, kilometa 6,325 sawa na asilimia 60.3 za barabara kuu zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 6,324.9 mwaka 2017. Aidha, kilometa 2,951 za barabara kuu sawa na asilimia 28.1 zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 2,734.9 mwaka 2017. Barabara zenye hali ya wastani ziliongezeka kutokana na matengenezo ya mara kwa mara. Vile vile, kilometa 1,214 za barabara kuu sawa na asilimia 11.6 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 977 mwaka 2017. Hali hii ilitokana na kuongezwa kwa barabara za wilaya zenye hali mbaya kwenye mtandao wa barabara zinazohudumiwa na TANROADS.

267. Hadi kufikia Desemba 2018, barabara za mikoa zenye kiwango cha lami na changarawe zilizokuwa na urefu wa kilometa 22,362 zilifanyiwa tathmini ikilinganishwa na kilometa 21,660 mwaka 2017. Kati ya hizo, kilometa 4,718 sawa na asilimia 21 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 5,285 mwaka 2017. Barabara zenye hali nzuri zilipungua kutokana na kuongezwa kwa barabara za wilaya zenye hali mbaya kwenye mtandao wa barabara zinazohudumiwa na TANROADS. Aidha, kilometa 14,641 sawa na asilimia 65.5 zilikuwa katika hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 13,663 mwaka 2017. Barabara zenye hali ya wastani ziliongezeka kutokana na barabara hizo kuendelea kufanyiwa ukarabati kwa wakati. Barabara zenye urefu wa kilometa 3,003 sawa na asilimia 13.4 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 2,712 mwaka 2017. Barabara zenye hali mbaya ziliongezeka kutokana na kuongezwa kwa barabara za wilaya zenye hali mbaya kwenye mtandao wa barabara zinazohudumiwa na TANROADS. **Jedwali Na. 15.1** linaonesha hali ya mtandao wa barabara hadi Desemba 2018.

**Jedwali Na.15.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Hadi Desemba 2018**

| **Aina ya Barabara** | **Hali ya Mtandao wa Barabara** | | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Nzuri** | | **Wastani** | | **Mbaya** | | |
| | **km** | **%** | **km** | **%** | **km** | **%** | **km** |
| Barabara kuu (lami) | 5,771 | 72.2 | 1,248 | 15.6 | 971 | 12.2 | 7,990 |
| Barabara kuu (changarawe/udongo) | 554 | 22.2 | 1,703 | 68.1 | 243 | 9.7 | 2,500 |
| Jumla ndogo | 6,325 | 60.3 | 2,951 | 28.1 | 1,214 | 11.6 | 10,490 |
| Barabara za Mikoa (lami) | 754 | 49.7 | 314 | 20.7 | 449 | 29.6 | 1,517 |
| Barabara za Mikoa (changarawe/udongo) | 3,964 | 19 | 14,327 | 68.7 | 2,554 | 12.3 | 20,845 |
| Jumla ndogo | 4,718 | 21.1 | 14,641 | 65.5 | 3,003 | 13.4 | 22,362 |
| **Jumla kuu** | **11,043** | **33.6** | **17,592** | **53.5** | **4,216** | **12.8** | **32,852** |

**Chanzo:** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

**Matengenezo ya Barabara, Madaraja, Vivuko na Magari**

268. Mwaka 2018, jumla ya kilometa 29,084.60 za barabara kuu na za mikoa zilifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na kilometa 26,712 mwaka 2017

kupitia TANROADS. Urefu wa barabara zilizofanyiwa matengenezo mwaka 2018 uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017 kutokana na hali nzuri ya upatikanaji wa fedha za matengenezo. Aidha, madaraja 2,679 yalitengenezwa ikilinganishwa na madaraja 2,742 mwaka 2017. Idadi ya madaraja yaliyofanyiwa matengenezo ilipungua kutokana na kutumia muda mrefu kufanya matengengezo na ukarabati wa madaraja kufuatia uharibifu uliosababishwa na mvua kubwa zilizonyesha Novemba 2018.

269. Mwaka 2018, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme – TEMESA ilinunua kivuko kipya cha MV Mwanza chenye uwezo wa kubeba tani 250 (sawa na abiria 1000 na magari madogo 36) kwa lengo la kuimarisha huduma ya usafiri katika eneo la Kigongo - Busisi mkoani Mwanza. Katika kipindi hicho, abiria 25, 458,445 na mizigo kilogramu 3,253,166 ilivushwa ikilinganishwa na abiria 25,457,445 na mizigo kilogramu 3,003,166 mwaka 2017. Aidha, Serikali iliendelea kufanya matengenezo ya vivuko vilivyopo, kuboresha miundombinu ya maegesho ya vivuko na kujenga maegesho mapya. Vile vile, Serikali kupitia TEMESA ilitengeneza magari 29,083 ikilinganishwa na magari 14,380 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 102. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa karakana kwa kuweka vitendea kazi vya kisasa na kutoa mafunzo ya kuwaongezea ujuzi mafundi.

**Mtandao wa Barabara Zilizo chini ya TARURA**

270. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ulikabidhiwa mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 108,946.19. Kati ya hizo, barabara za lami zilikuwa na urefu wa kilometa 1,449.55 sawa na asilimia 1.3; barabara za changarawe kilometa 24,405.40, sawa na asilimia 22.4 na barabara za udongo kilometa 83,091.24 sawa na asilimia 76.3. Mtandao wa barabara zilizo chini ya TARURA ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na.15.2**.

**Jedwali Na. 15.2: Hali ya Mtandao wa Barabara kwa Mwaka 2018/19**

| **Aina ya Barabara** | **Hali ya Mtandao wa Barabara (KM)** | | | **Jumla** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Nzuri** | **Inaridhisha** | **Hairidhishi** | | |
| Barabara za Lami | 1,026.27 | 283.37 | 139.91 | 1,449.55 | **1.3** |
| Barabara za Changarawe | 9,732.45 | 9,597.37 | 5,075.58 | 24,405.40 | **22.4** |
| Barabara za Udongo | 13,853.49 | 27,374.52 | 41,863.23 | 83,091.24 | **76.3** |
| **Jumla** | **24,612.21** | **37,255.26** | **47,078.72** | **108,946.19** | **100.0** |

**Chanzo:** TAMISEMI

271. Hadi Machi, 2019, wakala ulifanya matengezo ya barabara yenye urefu wa kilometa 12,855.42, sawa na asilimia 54 ya lengo la mwaka kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.15.3**. Aidha, madaraja mapya 98 na makalavati 1,014 yalijengwa, madaraja 56 yalikarabatiwa na *drift* zenye urefu wa meta za mraba 805.92 zilijengwa.

**Jedwali Na. 15.3: Matengenezo ya Barabara katika Mwaka 2018/19**

| Aina ya Matengenezo | Mpango wa Mwaka 2018/19 | | |
|---|---|---|---|
| | Lengo (km) | Utekelezaji (km) | Asilimia |
| Matengenezo ya mara kwa mara | 13,163.89 | 7,209.38 | 54.8 |
| Matengenezo ya sehemu korofi | 6,201.22 | 2,925.26 | 47.2 |
| Matengenezo Maalum | 3,574.33 | 2,720.78 | 76.1 |
| **Jumla** | **22,939.44** | **12,855.42** | **56.0** |
| Makalavati na Mifereji ya maji | Ukarabati madaraja 120, ujenzi madaraja mapya 117 na makalavati 2,276, kujenga "Drift" zenye urefu wa meta za mraba 3,358 | Madaraja 56 yamekarabatiwa, madaraja mapya 98 yamejengwa na makalavati 1,014, kujenga "Drift" zenye urefu wa meta za mraba 805.92 | 38 |

**Chanzo:** TAMISEMI

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

272. Mwaka 2018, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya shilingi bilioni 746 ikilinganishwa na shilingi bilioni 793 zilizokusanywa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 5.9. Aidha, fedha zilizopelekwa kwa taasisi zinazotekeleza miradi ya barabara inayofadhiliwa na Mfuko zilikuwa shilingi bilioni 771 ikilinganishwa na shilingi bilioni 758 mwaka 2017. Vilevile, Bodi ilifanya ukaguzi wa miradi ya barabara 523 ikilinganishwa na miradi 762 mwaka 2017. Kupungua kwa miradi iliyokaguliwa kulitokana na upanuzi wa wigo wa ukaguzi ambapo kiliongezwa kipengele cha ukaguzi wa kifedha mbali na ukaguzi wa kiufundi pekee uliokuwa ukifanyika hapo awali.

**Wakala wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

273. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kusimamia miradi 420 ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali ikilinganishwa na miradi 292 mwaka 2017. Hadi Desemba 2018, jumla ya miradi 168 ya ukarabati wa nyumba na majengo ilisimamiwa ikilinganishwa na miradi 128 mwaka 2017. Kuongezeka kwa ujenzi na ukarabati wa miradi ya nyumba na majengo ya

Serikali kulitokana na Wakala kuendelea kutumia teknolojia mpya ya ujenzi na ukarabati wa majengo; mitambo mipya ya kisasa ikiwemo mitambo ya kuchanganya zege yenye uwezo wa kukoroga mita za ujazo 60 za zege kwa saa moja; ununuzi wa vifaa vya kupima ubora wa majengo bila ya kuyaharibu; ununuzi wa malighafi za ujenzi kutoka viwandani; na kutoza ada ndogo ya usimamizi wa ujenzi na ukarabati. Aidha, idadi ya nyumba zilizopangishwa kwa watumishi wa Serikali na nyumba za biashara zilizopangishwa kwa watu mbalimbali ziliongezeka hadi kufikia nyumba 5,992 mwaka 2018 kutoka nyumba 5,941 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana uhitaji mkubwa wa makazi yenye ubora na gharama nafuu.

**Bodi ya Usajili wa Wakandarasi**

274. Mwaka 2018, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilisajili jumla ya wakandarasi 832 ikilinganishwa na wakandarasi 875 mwaka 2017 sawa na upungufu wa asilimia 4.9. Usajili huu unafanya jumla ya wakandarasi waliosajiliwa hadi Desemba, 2018 kufikia 9,897 ikilinganishwa na wakandarasi 9,065 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Aidha, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 3,575 ikilinganishwa na miradi 3,600 mwaka 2017. Kusajiliwa kwa miradi michache kulitokana na upungufu wa usajili wa wakandarasi. Vile vile, Bodi ilifanya ukaguzi wa miradi 3,827 ambapo miradi 2,748 sawa na asilimia 72 haikuwa na mapungufu na miradi 1,079 sawa na asilimia 28 ilikuwa na mapungufu. Mapungufu hayo ni pamoja na: kutosajiliwa kwa wakandarasi na mradi; kutoweka mabango ya miradi; na kutozingatia sheria ya afya na usalama wa wafanyakazi. Hatua za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya wakandarasi wa miradi iliyokutwa na mapungufu ni pamoja na kutozwa faini, kusimamishwa kwa muda na wahusika kushtakiwa. Aidha, Bodi ilipeleka mahakamani watuhumiwa 52 waliokuwa wakitekeleza miradi kwa kutumia kampuni au watu wasio wakandarasi ikilinganishwa na watuhumiwa 45 mwaka 2017.

**Bodi ya Usajili ya Wahandisi**

275. Bodi ya Usajili ya Wahandisi ilisajili wahandisi 23,416 mwaka 2018 ikilinganishwa na wahandisi 20,138 mwaka 2017. Kuongezeka kwa usajili wa wahandisi kulitokana na wahitimu wengi kujisajili kutokana na ongezeko la shughuli za kiuchumi zinazohusu taaluma ya uhandisi hasa viwanda vya uzalishaji, ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Kati ya wahandisi waliosajiliwa, 21,386 walikuwa Watanzania na 2,030 wageni. Aidha, Bodi ilisajili kampuni za ushauri 333 ambapo kampuni 232 zilikuwa za Kitanzania na 101 za kigeni ikilinganishwa na kampuni 318 mwaka 2017 ambapo kampuni 224 zilikuwa za kitanzania na 94 za kigeni. Katika kipindi hicho, Bodi ilisajili wahandisi washauri 556 ambapo 426 walikuwa

Watanzania na 130 wageni. Vile vile, Bodi ilisajili maabara 29 za vifaa vya ujenzi na uhandisi.

276. Mwaka 2018, wahandisi 5,814 walipata mafunzo ikilinganishwa na wahandisi 4,695 mwaka 2017. Kati ya hao, wahandisi 3,253 walihitimu mafunzo na kusajiliwa kama wahandisi wataalam. Ongezeko la wahandisi waliopata mafunzo lilitokana na wahandisi kuendelea kutambua umuhimu wa kusajili taaluma zao. Vile vile, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 769 na kukagua miradi 124 ikilinganishwa na miradi 723 iliyosajiliwa na miradi 97 iliyokaguliwa mwaka 2017. Usajili wa miradi uliongezeka kutokana na wadau kutambua umuhimu wa kusajili miradi.

**Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

277. Mwaka 2018, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili wataalam 1,021 ikilinganishwa na wataalam 907 waliosajiliwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Ongezeko hilo lilitokana na wahitimu wengi kujitokeza kufanya mitihani ya Bodi kwa mwaka husika kwa kuhamasishwa na Bodi. Kati ya wataalam waliosajiliwa, 987 walikuwa Watanzania na 34 wageni. Katika kipindi hicho,kampuni 368 za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi zilisajiliwa ikilinganishwa na kampuni 363 mwaka 2017, sawa ongezeko la asilimia 1.4. Ongezeko hilo lilitokana na Bodi kuendelea kuwahamasisha waendelezaji wa majengo kutumia huduma za wataalam waliosajiliwa kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya mwaka 2010. Kati ya kampuni zilizosajiliwa, 359 zilikuwa za Kitanzania na kampuni tisa zilikuwa za kigeni.

278. Mwaka 2018, miradi ya majengo 1,666 ilikaguliwa ikilinganishwa na miradi 1,943 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 14.3. Upungufu huo ulitokana na waendelezaji wengi kuwa na uelewa mdogo wa kutumia huduma za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi katika kuendeleza miradi, hususan waendelezaji wa makazi binafsi. Aidha, miradi ya ujenzi wa majengo 885 ilisajiliwa ikilinganishwa na miradi 800 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 10.6. Ongezeko hilo lilitokana Bodi kuendelea kuelimisha jamii na waendelezaji majenzi kuhusu umuhimu wa kutumia huduma za ushauri za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi katika miradi ya ujenzi. Vile vile, wahitimu 106 walihudhuria mafunzo kwa vitendo katika fani ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi mwaka 2018, ikilinganishwa na wahitimu 47 mwaka 2017.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

279. Mwaka 2018, Baraza la Taifa la Ujenzi lilifanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi 199 ikilinganishwa na miradi 190 mwaka 2017. Aidha, Baraza

lilifanya usuluhishi wa migogoro ya ujenzi 153 ikilinganishwa na migogoro 46 mwaka 2017. Ongezeko la usuluhishi wa migogoro lilitokana na wadau kuelewa haki zao kisheria na kimkataba. Kati ya migogoro 153 iliyosuluhishwa, migogoro mipya 22 ilisajiliwa katika usuluhishi wa awali. Vile vile, Baraza lilitoa mafunzo yaliyohusu sheria na taratibu za usuluhishi wa migogoro katika miradi ya ujenzi kwa wadau 36 wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau 8 mwaka 2017.

## MAENDELEO YA ARDHI

### Utayarishaji wa Hatimiliki, Ukaguzi, na Uhakiki Milki

280. Mwaka 2018, hatimiliki 61,987 za viwanja na mashamba ziliandaliwa katika kanda nane za ardhi ikilinganishwa na hatimiliki 39,418 zilizoandaliwa mwaka 2017. Aidha, ilani 3,500 za ubatilisho zilitumwa kwa wapangaji waliokiuka masharti ya upangaji wa ardhi ikilinganishwa na ilani za ubatilisho 1,242 mwaka 2017. Vile vile, migogoro 6,499 ya ardhi ilitatuliwa kiutawala ikilinganishwa na migogoro 6,811 mwaka 2017. Kwa upande mwingine hatimiliki za kimila 186,186 zilitolewa kwa wananchi mwaka 2018 ikilinganishwa na hatimiliki za kimila 87,703 zilizotolewa mwaka 2017. Ongezeko la utoaji wa hatimiliki za kimila lilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa programu ya kuwezesha kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.

### Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria

281. Mwaka 2018, hatimiliki na nyaraka za kisheria 93,706 zilisajiliwa ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 49,728 zilizosajiliwa mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 88.4. Kati ya hizo, hati za kumiliki ardhi zilikuwa 41,522; hati za umiliki wa sehemu ya jengo/eneo zilikuwa 844; na nyaraka nyingine za kisheria zilikuwa 51,340.

**Jedwali Na.15.4: Usajili wa Hati Miliki na Nyaraka za Kisheria**

| Hati na Nyaraka zilizosajiliwa | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|
| Hati za kumiliki Ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati | 31,254 | 33,257 | 21,743 | 41,522 |
| Hati ya sehemu ya jengo zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati‘Unit Title Act No. 17/2008’. | 1,541 | 1,410 | 827 | 844 |
| Nyaraka za kisheria zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati Sura Na. 334 | 29,546 | 34,682 | 13,821 | 27,716 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura Na. 117 | 13,041 | 20,525 | 13,027 | 21,807 |
| Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika Sura na. 210 | 2,082 | 1,313 | 310 | 1,817 |
| **Jumla** | 77,464 | 91,187 | 49,728 | 93,706 |

**Chanzo:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Uthamini wa Mali kwa Madhumuni Mbalimbali**

282. Mwaka 2018, taarifa za uthamini 26,096 ziliidhinishwa ikilinganishwa na taarifa 14,483 zilizoidhinishwa mwaka 2017. Idadi hii imejumuisha taarifa zilizopokelewa kutoka katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kampuni binafsi za uthamini pamoja na zilizofanywa na Serikali.

**Upimaji wa Mashamba na Viwanja**

283. Mwaka 2018, ramani zenye viwanja 235,752 na mashamba 2,159 ziliidhinishwa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ikilinganishwa na ramani zenye viwanja 170,442 na mashamba 445 zilizoidhinishwa mwaka 2017. Mchanganuo wa viwanja na mashamba yaliyoidhinishwa ni kama ilivyoonekana katika **Jedwali Na.15.5**.

**Jedwali Na.15.5: Upimaji wa Viwanja na Mashamba**

| Mikoa | Milki zilizoidhinishwa mwaka 2016 | | Milki zilizoidhinishwa mwaka 2017 | | Milki zilizoidhinishwa mwaka 2017 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Viwanja | Mashamba | Viwanja | Mashamba | Viwanja | Masham ba |
| Arusha | 1769 | 19 | 1392 | 18 | 3,547 | 17 |
| Pwani | 21539 | 190 | 36974 | 107 | 18,108 | 1,010 |
| DSM | 29985 | 1 | 28079 | 0 | 19,096 | 0 |
| Dodoma | 1653 | 0 | 3622 | 5 | 38,230 | 0 |
| Geita | 1808 | 0 | 5279 | 0 | 4,176 | 0 |
| Iringa | 1893 | 38 | 4531 | 26 | 4,222 | 9 |
| Kagera | 1211 | 9 | 2959 | 2 | 6,160 | 25 |
| Katavi | 767 | 0 | 2858 | 1 | 1,912 | 0 |
| Kigoma | 4773 | 0 | 1893 | 2 | 3,201 | 835 |
| Kilimanjaro | 1284 | 58 | 1532 | 36 | 1,612 | 20 |
| Lindi | 3000 | 4 | 7253 | 0 | 3,113 | 15 |
| Manyara | 1198 | 14 | 1668 | 86 | 3,375 | 4 |
| Mara | 4998 | 0 | 2326 | 16 | 3,003 | 5 |
| Mbeya | 2093 | 15 | 3473 | 17 | 5,015 | 9 |
| Morogoro | 6538 | 4 | 5298 | 73 | 12,050 | 138 |
| Mtwara | 4847 | 2 | 4737 | 1 | 4,413 | 0 |
| Mwanza | 6042 | 0 | 22910 | 0 | 45,494 | 8 |
| Njombe | 1829 | 11 | 2870 | 6 | 5,088 | 60 |
| Ruvuma | 2368 | 0 | 1112 | 0 | 2,513 | 0 |
| Rukwa | 248 | 8 | 2388 | 9 | 792 | 4 |
| Simiyu | 832 | 0 | 2720 | 14 | 3,521 | 0 |
| Singida | 4101 | 1 | 8934 | 8 | 7,233 | 0 |
| Songwe | 1022 | 0 | 98 | 1 | 4,489 | 0 |
| Shinyanga | 4690 | 0 | 5028 | 0 | 22,128 | 0 |
| Tabora | 11524 | 0 | 4265 | 1 | 3,047 | 0 |
| Tanga | 1715 | 17 | 6223 | 26 | 10,214 | 0 |
| **Jumla** | **123,727** | **391** | **170,422** | **455** | **235,752** | **2,159** |

**Chanzo:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

## Mipango ya Matumizi ya Ardhi

284. Mwaka 2018, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 125 iliandaliwa katika wilaya 23 ikilinganishwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 47 iliyoandaliwa katika wilaya 15 mwaka 2017.

**Jedwali Na.15.6: Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Mwaka 2018**

| Mkoa | Wilaya | Jina la kijiji | Idadi ya Vijiji |
|---|---|---|---|
| Arusha | Karatu | Jobay, Qng'dend, Kitete, Endamanagh, Mbuga Nyekundu, Mahhahha, Slahham, Getmock, Kilimamoja, Chemchem, Kambi ya Simba na Huduma | 12 |
| | Ngorongoro | Engaleselo | 1 |
| Njombe | Makete | Ihela, Mago, Malambuli, Ibaga, Isungilo, Ukwama, Ikungula, Ugabwa, Kisasatu and Utengule na Ilindima | 11 |
| | Ludewa | Kipangala, Ntumbati and Mkongobaki | 3 |
| Ruvuma | Mbinga | Paradiso, Ntunduwalo and Ukombozi | 3 |
| | Nyasa | Mtupale, Lundo and Kihuru | 3 |
| Tanga | Muheza | Magambo miembeni, Kazita na Kwemsoso | 3 |
| | Handeni | Bondo, Msomera | 2 |
| | Mkinga | Kuzekibango, Boshakwemtinde | 2 |
| Iringa | Mufindi | Ugeza, Manguli, Usokami, Mkungu, Mapogolo, Lugodalutali, Utosi, Igombavanu, Uhambila and Kibada | 10 |
| Dodoma | Kondoa | Kille cha ng'ombe, Boma ya Ng'ombe, Kwadelo, Itaswi, Haire, Mauno, Chubi, Mnenia, na Kisaki | 9 |
| Simiyu | Bariadi | Nyamikoma, Igabanhilo, Mwantimba, Matongo, Salalia na Senta | 6 |
| Mara | Bunda | Kihumbu, Hunyari, Mariwanda na Sarakwa. | 4 |
| Kigoma | Uvinza | Mlela, Nyanganga, Mgambazi, Rukoma and Lubalisi. | 5 |
| Shinyanga | Shinyanga | Nsalala and Welezo | 2 |
| Lindi | Lindi | Mnara, Chikombe, Mtakuja and Ntauna | 4 |
| | Kilwa | Mchakama, Ngea, Pungutini, Kikole, Kisangi, Kipindimbi, Mitole | 7 |
| Mtwara | Nanyumbu | Nakopi and Chilunda | 2 |
| Morogoro | Kilombero | Mkasu, Bwawani, Mpanga, Idete, Idete B, Ihenga, Chiwakiwa, Mkusi, Nakaguru, Lukorongo, Mngeta, Kidete, Mkangawalo, Ichongoa | 14 |
| | Malinyi | Tanga, Ngoheranga, Kilosa Mpepo, Ihowanja, Mbalinyi, Biro, Kiswago, Sofi Mission, Kalengakero, Usangule A, Usangule B. | 11 |
| | Mvomero | Vinile, Bunduki, Magurue | 3 |
| | Morogoro | Tandai, Amini, Tawa, Kitungwa, Ludewa, Lung'ara | 6 |
| **Jumla** | | | **47** |

**Chanzo:** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, 2018

## Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

285. Mwaka 2018, mashauri mapya 23,002 yalifunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Kati ya hayo, mashauri 19,287 yaliamuliwa na mashauri 27,523 yaliendelea kusikilizwa ikilinganishwa na mashauri 21,561 yaliyoamuliwa mwaka 2017 kati ya mashauri 23,814 yaliyokuwepo.

## MAENDELEO YA MAKAZI

### Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara

286. Mwaka 2018, Shirika la Nyumba la Taifa lilijenga nyumba 2,954 ikilinganishwa na nyumba 2,738 zilizojengwa mwaka 2017. Kati ya hizo, nyumba za bei nafuu zilikuwa 832, za bei ya kati na juu 1188 na za biashara 934 ikilinganishwa na nyumba za bei nafuu 616, za bei ya kati na juu 1188 na za biashara 934 mwaka 2017. Aidha, Watumishi Housing Company ilijenga nyumba 98 mwaka 2018 ikilinganishwa na nyumba 196 mwaka 2017

### Utoaji wa Mikopo ya Nyumba

287. Mwaka 2018, Kampuni ya Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania imewezesha utoaji mikopo ya nyumba 4,996 yenye thamani ya shilingi bilioni 421.07 ikilinganishwa na mikopo ya nyumba 4,174 yenye thamani ya shilingi bilioni 344.84 mwaka 2017.

# SURA YA 16

# MAWASILIANO NA UCHUKUZI

## UCHUKUZI

### Usafiri wa Barabara

288. Mwaka 2018, leseni za vyombo vya usafirishaji zilizotolewa zilifikia 176,282 kutoka leseni 160,915 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 9.5. Kati ya hizo, leseni 46,449 zilitolewa kwa mabasi ya abiria ya masafa marefu na mijini, leseni 113,345 kwa magari ya mizigo yenye uwezo wa kubeba shehena kuanzia tani tatu na kuendelea  na leseni 16,488 zilitolewa kwa pikipiki/bajaji zilizojihusisha na ubebaji wa abiria kibiashara. Ongezeko hilo lilitokana na kutolewa kwa elimu kuhusu umuhimu wa leseni, kuimarika kwa mfumo wa TEHAMA katika utoaji leseni na adhabu kwa watoa huduma wasio na leseni au walio na leseni zilizoisha muda wa matumizi.

**Jedwali Na. 16.1: Mchanganuo wa Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa**

| Leseni | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Mabasi ya Abiria | 47,451 | 46,691 | 46,612 | 46,449 | -0.3 |
| Magari ya Mizigo | 81,567 | 87,383 | 99,484 | 113,345 | 13.9 |
| Bajaj/Pikipiki | 6,054 | 12,900 | 14,819 | 16,488 | 11.3 |
| **Jumla** | **135,072** | **146,974** | **160,915** | **176,282** | **9.5** |

**Chanzo:** SUMATRA

289. Mwaka 2018, ajali za vyombo vya usafirishaji abiria na mizigo kwa upande wa barabara zilipungua kwa asilimia 32.4 kutoka ajali 2,908  mwaka 2017 hadi ajali 1,965. Kati ya ajali  hizo, 620 zilisababishwa na mabasi ya abiria, ajali 469 magari ya mizigo na ajali 876 pikipiki/bajaji. Kupungua kwa ajali kulisababishwa na matumizi ya mfumo wa udhibiti mwendo wa mabasi, upimaji ulevi kwa madereva, matumizi ya madereva wawili kwa safari zilizozidi masaa nane na kaguzi za mara kwa mara zilizoambatana na kufungiwa kwa mabasi yasiyo na ubora wa kutembea barabarani.

**Jedwali Na. 16.2: Mchanganuo wa Ajali za Barabarani**

| Ajali | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko % |
|---|---|---|---|---|
| Mabasi | 1,413 | 842 | 620 | -26.4 |
| Malori | 920 | 607 | 469 | -22.7 |
| Pikipiki Na Bajaji | 2,544 | 1,459 | 876 | -40.0 |
| **Jumla** | **4,877** | **2,908** | **1,965** | **-32.4** |

**Chanzo:** SUMATRA

**Usafiri kwa Kutumia Reli**

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

290. Mwaka 2018, Shirika la Reli Tanzania lilisafirisha shehena ya mizigo tani 379,321 kwa umbali wa kilomita 375,901,609 ikilinganishwa na tani 351,758 kwa umbali wa kilometa 360,955,000 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa bei ya mizigo iliyokwenda Uganda na kuongezeka kwa shehena ya mizigo ya ujenzi wa reli ya kisasa ya kiwango cha *Standard Gauge* kutoka bandari ya Dar es salaam hadi kambi za ujenzi. Katika kipindi hicho, abiria 589,608 walisafirishwa kwa umbali wa kilometa 404,296,156 ikilinganishwa na abiria 566,135 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 386,441,976 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa bei ya usafiri wa treni ya abiria inayokwenda Kigoma.

291. Kwa upande wa huduma ya usafiri wa treni katika jiji la Dar es Salaam, Shirika lilisafirisha abiria 5,382,497 kwa umbali wa kilometa 172,239,904 mwaka 2018 ikilinganishwa na abiria 5,786,360 kwa umbali wa kilometa 185,165,520 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 7.0. Upungufu huo ulitokana na kuhamishwa kwa muda kituo cha kupandia abiria cha stesheni ya Dar es Salaam kwenda kituo cha KAMATA ili kupisha ujenzi wa reli.

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

292. Mwaka 2017/18, TAZARA ilisafirisha tani 220,818 za mizigo ikilinganishwa na tani 171,405 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 28.8. Ongezeko hilo lilitokana na kufanya ukarabati wa mabehewa na matengenezo ya injini na njia za reli.

**Jedwali Na.16.3: Mchanganuo wa Shehena ya Tani za Mizigo Iliyosafirishwa**

| Aina ya mizigo | 2016/2017 | 2017/2018 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|
| Kwenda nje ya Nchi | 84,864 | 99,491 | 17.2 |
| Kutoka nje ya Nchi | 39,541 | 88,067 | 122.7 |
| Ndani ya TAZARA | 47,000 | 33,260 | -29.2 |
| **Jumla** | **171,405** | **2209,818** | **28.8** |

**Chanzo:** TAZARA

293. Mwaka 2017/18, TAZARA ilisafirisha jumla ya abiria 543,196 wa njia kuu ikilinganishwa na abiria 483,856 waliosafirishwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 12.3. Aidha, treni ya Udzungwa ilisafirisha abiria 393,570


wa ikilinganishwa na abiria 294,031 waliosafirishwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 33.9. Kwa upande wa treni ya mjini, abiria 2,418,807 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 2,579,756 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 6.2. Upungufu huo ulitokana na uchache wa mabehewa ya abiria.

**Usafiri wa Anga**

**Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)**

294. Mwaka 2018, kulikuwa na kampuni 43 za usafiri wa ndege zilizotoa huduma ya usafiri wa anga ikilinganishwa na kampuni 45 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 4.4. Upungufu huu ulitokana na baadhi ya kampuni kusitisha safari zake. Abiria waliowasili na kuondoka katika viwanja vya ndege nchini waliongezeka hadi kufikia 5,187,723 kutoka abiria 5,013,430 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa miruko ya ndege kwa wiki kwa watoa huduma, kusainiwa kwa mikataba ya usafiri wa anga kati ya Tanzania na nchi zingine, kuimarika kwa miundombinu ya viwanja vya ndege na kuongezeka kwa shughuli za utalii nchini. Aidha, kwa utaratibu wa *Bilateral Air Service Agreement* - BASA, hadi Desemba 2018, kampuni za ndege za kimataifa (ndani na nje) 28 zilikuwa zinatoa huduma ikilinganishwa na kampuni 30 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 6.7.

**Kielelezo Na. 16.1: Idadi ya Abiria Waliowasili na Kuondoka Nchini**





| | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| NDANI YA NCHI | 1,975,923 | 2,845,985 | 2,733,641 | 2,756,372 | 2,593,862 |
| NJE YA NCHI | 2,903,472 | 2,004,032 | 2,226,011 | 2,257,058 | 2,593,862 |
| JUMLA | 4,879,395 | 4,850,017 | 4,959,652 | 5,013,430 | 5,187,723 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

295. Mwaka 2018, safari za ndege ziliongezeka kufikia 246,072 kutoka 237,382 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa ndege za kampuni ya ATCL. Aidha, mizigo iliyosafirishwa iliongezeka hadi tani 27,910 kutoka tani 27,449 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 1.7. Ongezeko hilo lilitokana na uingizaji wa mitambo ya uwekezaji na ujenzi wa miundombinu kama vile reli ya kisasa kwa kiwango cha *Standard Gauge*.


**Kielelezo Na. 16.2: Idadi ya Safari za Ndege**




| | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| NDANI YA NCHI | 192,088 | 186728 | 190,422 | 194,405 | 202,402 |
| NJE YA NCHI | 38,784 | 38,375 | 42,838 | 42,977 | 43,670 |
| JUMLA | 230,872 | 225,103 | 233,260 | 237,382 | 246,072 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

**Kielelezo Na.16.3: Tani za Mizigo Zilizosafirishwa**




| | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| NDANI YA NCHI | 3,023 | 2,422 | 2,024 | 1,967 | 2,003 |
| NJE YA NCHI | 26,571 | 27,601 | 21,988 | 25,482 | 25,907 |
| JUMLA | 29,594 | 30,023 | 24,012 | 27,449 | 27,910 |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

**Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)**

296. Mwaka 2017/18, Kampuni ya Ndege Tanzania iliendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 11 ndani ya nchi ambavyo ni Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Mtwara, Songea, Tabora na Zanzibar. Aidha kampuni ilitoa huduma ya usafiri wa anga katika kituo cha kikanda cha Hahaya nchini Comoro. Aidha, Kampuni ilisafirisha abiria 242,668 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na abiria 107,207 mwaka 2016/17. Kuongezeka kwa abiria kulitokana na Kampuni kununua ndege moja mpya, kuongezeka kwa ratiba za miruko katika vituo vya Dodoma na Mwanza, na kuboreshwa kwa huduma kwa mteja. Vile vile, Kampuni ilisafirisha mizigo kilo 348,624 ndani ya nchi ikilinganishwa na kilo 127,936 mwaka 2016/17.

Kuongezeka kwa mizigo kulitokana na huduma bora kwa wateja na kuongezeka kwa idadi ya miruko katika vituo vya Dodoma na Mwanza.

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania**

297. Mwaka 2017/18, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia shehena ya mizigo tani milioni 16.2 ikilinganishwa na tani milioni 14.7 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuondolewa kwa utaratibu wa mfumo wa forodha kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa shehena ya mizigo ya nchi jirani; mikakati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kujitangaza kimasoko na kibiashara kwa wateja wa ndani na nje; kuongezeka kwa meli kubwa; na kuongezeka kwa ufanisi wa bandari katika kutoa huduma kwa wateja. Aidha, shehena za mizigo ziliongezeka katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Kigoma. Kwa upande mwingine, shehena katika bandari za Mtwara, Mwanza, Kilwa, Lindi, Mafia na Kyela zilipungua. Kupungua kwa shehena hizo kulitokana na uchache wa meli za kubeba mizigo; kuharibika kwa meli mara kwa mara; na kuendelea kutumika kwa magati binafsi kwa bandari za Ziwa. Shehena iliyohudumia ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 16.4**.

**Jedwali Na. 16.4: Shehena Zilizosafirishwa (Tani, Milioni)**

| Kituo | 2014/2015 | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Bandari Kuu za Mwambao** | | | | | |
| Dar es Salaam | 14.803 | 14.033 | 13.561 | 14.863 | 9.6 |
| Tanga | 0.645 | 0.677 | 0.486 | 0.647 | 33.1 |
| Mtwara | 0.2966 | 0.273 | 0.378 | 0.363 | (3.9) |
| **Jumla Ndogo** | **15.745** | **14.983** | **14.425** | **15.873** | **10.0** |
| **Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu** | | | | | |
| Kilwa, Lindi na Mafia | 0.0 26 | 0.046 | 0.041 | 0.018 | (57.0) |
| Mwanza | 0.129 | 0.123 | 0.124 | 0.085 | (31.8) |
| Kigoma | 0.099 | 0.139 | 0.137 | 0.197 | 43.7 |
| Kyela | 0.002 | 0.0004 | 0.006 | 0.0004 | (94.0) |
| **Jumla Ndogo** | **0.231** | **0.3084** | **0.308** | **0.2995** | **(2.8)** |
| **Jumla Kuu** | **16.001** | **15.2914** | **14.733** | **16.172** | **9.8** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

298. Mwaka 2017/18, kontena zilizohudumiwa na kitengo cha mizigo ya kawaida (General Cargo) kinachosimamiwa na Mamlaka ziliongezeka hadi kontena (TEUs) 117,529 kutoka kontena (TEUs) 108,088 mwaka 2016/17, sawa na asilimia 8.7. Aidha, kitengo cha kontena cha TICTS kilihudumia kontena

(TEUs) 535,515 ikilinganishwa na kontena (TEUs) 445,493 zilizohudumiwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 20.2.

**Jedwali Na. 16.5: Shehena ya Kontena (TEUs) - Bandari ya Dar es Salaam**

| Aina | 2015/2016 | 2016/17 | 2017/18 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| TICTS | 497,769 | 445,493 | 535,515 | 20.2 |
| General Cargo | 130,893 | 108,088 | 117,529 | 8.7 |
| **Jumla Ndogo** | **628,662** | **553,581** | **653,044** | **18.0** |
| Tanga | 8,118 | 8,048 | 7,158 | -11.1 |
| Mtwara | 14,337 | 30,371 | 35,778 | 17.8 |
| **Jumla Ndogo** | **22,455** | **38,419** | **42,936** | **11.8** |
| **Jumla Kuu** | **651,117** | **592,000** | **695,980** | **17.6** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

299. Mwaka 2017/18, abiria 2,185,084 walihudumiwa na Mamlaka ikilinganishwa na abiria 2,037,853 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Katika kipindi hicho, abiria waliohudumiwa na Mamlaka katika bandari za Dar es Salaam na Mwanza waliongezeka wakati abiria waliohudumiwa katika bandari za Kigoma na Kyela walipungua.

**Jedwali Na. 16.6: Idadi ya Abiria Waliohudumiwa**

| Bandari | 2013/14 | 2014/15 | 2015/2016 | 2016/17 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| DSM | 1,412,357 | 1,569,053 | 1,614,831 | 1,848,937 | 1,884,125 |
| Tanga | 12,747 | - | - | 10,508 | 45,820 |
| Mwanza | 735,794 | 340,125 | 206,763 | 165,098 | 246,462 |
| Kigoma | 15,239 | 38,749 | 4,700 | 9,895 | 7,710 |
| Kyela | 12,325 | 15,541 | 1,372 | 3,415 | 967 |
| **Jumla** | **2,188,462** | **1,963,468** | **1,827,666** | **2,037,853** | **2,185,084** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

### Muda wa Meli Kukaa Bandarini

300. Mwaka 2017/18, muda wa meli kukaa bandarini kwa kitengo cha kontena ulipungua hadi siku 1.8 kutoka siku 2.1 mwaka 2016/17. Aidha, muda wa meli kukaa bandarini kwa kitengo cha mizigo ya kawaida uliongezeka na kufikia siku 3.3 kutoka siku 2.7 mwaka 2016/17.Vile vile, katika kitengo cha mafuta muda uliongezeka na kufikia siku 3.3 kutoka siku 3.0 mwaka 2016/17. Kuongezeka kwa muda wa meli kukaa bandarini katika kitengo cha mizigo ya kawaida kulitokana na kuwa na gati moja (Gati Namba 7) lenye kina kirefu na hivyo kusababisha meli kubwa zenye kina kirefu kusubiri nje ya Bandari kabla ya kuingia kuhudumiwa. Kwa upande wa mizigo ya kontena, muda wa kukaa

bandarini baada ya kupakuliwa kutoka melini na kabla ya mteja kuchukua ulikuwa wastani wa siku 10.5 ikilinganishwa na siku 11.5 mwaka 2016/17.

**Shehena za Nchi Jirani**

301. Mwaka 2017/18, tani 5,604,605 za mizigo ya kwenda nchi jirani zilihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na tani 4,785,219 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 17.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa masoko na tija katika kuhudumia shehena za nchi jirani. Shehena za mizigo kwenda nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia ziliongezeka kwa kiwango kikubwa cha asilimia 20.4 na 20.0 kwa mtiririko huo. Hata hivyo, shehena za mizigo kwenda nchi jirani za Rwanda na Uganda zilipungua kwa asilimia 9.0 na 10.0 mtawalia. Hii ilitokana na ushindani mkali kutoka Bandari jirani ya Mombasa kwa kuwa njia ya Kampala hadi Mombasa ni fupi ikilinganishwa na njia ya Kampala hadi Dar es Salaam.

**Jedwali Na.16.7: Shehena za Nchi Jirani**

| Nchi | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| Zambia | 1,818,141 | 1,737,650 | 1,819,069 | 1,705,659 | 2,053,174 |
| J.D. Kongo | 1,352,457 | 1,677,527 | 1,464,847 | 1,141,611 | 1,370,078 |
| Burundi | 346,159 | 332,263 | 351,044 | 363,060 | 425,300 |
| Rwanda | 670,634 | 724,683 | 839,826 | 1,012,889 | 922,134 |
| Malawi | 141,536 | 94,294 | 106,883 | 217,852 | 258,271 |
| Uganda | 122,318 | 127,737 | 156,105 | 239,953 | 215,878 |
| Nyinginezo | 118,206 | 319,298 | 101,693 | 104,195 | 359,770 |
| **Jumla** | **4,569,451** | **5,013,452** | **4,839,467** | **4,785,219** | **5,604,605** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

**Uchukuzi Kwenye Maziwa**

**Kampuni ya Huduma za Meli**

302. Mwaka 2018, abiria 112,222 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 49,885 mwaka 2017. Aidha, tani 25,081 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 12,773 mwaka 2017, sawa na ongezeko asilimia 96.4. Kuongezeka kwa abiria na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na meli za MV.Clarias, MT.Sangara, ML.Wimbi na MV.Umoja kuanza kufanya kazi baada ya kufanyiwa matengenezo.

**Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP)**

303. Mwaka 2018, Kampuni ya SINOTASHIP ilisafirisha shehena tani 598,000 ikilinganisha na tani 580,000 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Ongezeko hilo lilitokana na uhakika wa upatikanaji wa shehena baada ya meli ya MV Changshun II kukodishwa kwa Kampuni ya *COSCO Bulk Carrier* yenye

uzoefu na uwezo mkubwa katika masuala ya usafirishaji wa shehena duniani. Aidha, Kampuni ilihudumia makasha 41,000 katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na makasha 20,880 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 96.4. Kuendelea kuongezeka kwa mizigo kulitokana na Kampuni ya *COSCO Shipping Container Line* kuongeza idadi ya njia za kusafirishia mizigo kutoka njia mbili hadi njia nne.

**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**

304. Mwaka 2018, Mamlaka ya Hali ya Hewa iliendelea kuboresha huduma za hali ya hewa kwa sekta mbalimbali na umma kwa ujumla. Katika kipindi hicho, Mamlaka ilitoa huduma za hali ya hewa katika Bahari ya Hindi kwa meli na boti 3,167 ikilinganishwa na meli na boti 3,100 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Hii ilitokana na Mamlaka kutoa elimu ya matumizi ya huduma za hali ya hewa kwa ajili ya usalama kwenye usafiri wa maji. Vilevile, kiwango cha usahihi wa utabiri wa hali ya hewa wa siku na msimu kiliongezeka hadi asilimia 89.8 ikilinganishwa na asilimia 87.1 mwaka 2017. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu ya hali ya hewa. Aidha, wateja na watumiaji wa huduma za hali ya hewa waliongezeka hadi kufikia 44,287 ikilinganishwa na wateja na watumiaji 42,000 mwaka 2017.

**Jedwali Na. 16.8: Viashiria vya Ufanisi katika Sekta ya Hali ya Hewa**

<table>
<tr><th>Kipimo cha Utendaji (KPI)</th><th>Maelezo</th><th>2016</th><th>2017</th><th>2018</th></tr>
<tr><td>Kiwango cha usahihi wa utabiri wa siku na msimu (Asilimia)</td><td>Usahihi wa Utabiri</td><td>84.0</td><td>87.1</td><td>89.8</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Idadi ya wateja na watumiaji wa huduma za hali ya hewa</td><td>Sekta ya Usafiri wa Anga</td><td>40,082</td><td>42,000</td><td>44,287</td></tr>
<tr><td>Meli na Boti</td><td>2,586</td><td>3,100</td><td>3,167</td></tr>
<tr><td>Huduma mahsusi</td><td>268</td><td>530</td><td>621</td></tr>
<tr><td>Kiwango cha watumiaji na wateja wanaoridhika na huduma za hali ya hewa (Asilimia)</td><td>Kiwango cha kuridhika</td><td>86.0</td><td>88.7</td><td>89.0</td></tr>
<tr><td>Jumla ya fedha zilizowekezwa katika miundombinu ya hali ya hewa (Shs. milioni)</td><td>Uwekezaji Miundombinu ya hali ya hewa</td><td></td><td>485</td><td>4,860</td></tr>
</table>

**Chanzo:** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

## HUDUMA ZA MAWASILIANO

### Huduma za Posta

305. Mwaka 2018, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 12,059,221 ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 6,750,443 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 78.6. Aidha, barua zilizosafirishwa nje ya nchi zilikuwa 3,737,816 ikilinganishwa na barua 1,852,600 mwaka 2017. Kuongezeka kwa usafirishaji wa barua kulitokana na kuimarishwa kwa mikakati ya masoko kupitia "huduma ya posta mlangoni".

306. Mwaka 2018, jumla ya vifurushi 72,433 vilisafirishwa ndani ya nchi ikilinganishwa na vifurushi 68,214 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Aidha, vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi vilikuwa 6,623 ikilinganishwa na vifurushi 3,455 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 91.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa taasisi zilizotumia huduma ya Posta katika usafirishaji wa vifurushi ikiwa ni pamoja na hamasa ya wajasiriamali wadogo kusafirisha sampuli za biashara ndani na nje ya nchi.

307. Mwaka 2018, rejesta 464,377 zilisafirishwa nchini ikilinganishwa na rejesta 347,879 zilizosafirishwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 33.5. Aidha, rejesta zilizotumwa nje ya nchi zilikuwa 40,453 ikilinganishwa na rejesta 22,605 zilizotumwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 79.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa rejesta zinazotumwa kwenda Jijini Dodoma baada ya ofisi za Serikali kuhamia Jijini Dodoma.

308. Mwaka 2018, nyaraka na vipeto vilivyotumwa kwa njia ya haraka (EMS) nchini vilikuwa 753,278 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 719,390 vilivyotumwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Aidha, nyaraka na vipeto vilivyotumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka vilikuwa 16,803 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 13,220 vilivyotumwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 27.1. Ongezeko hilo lilitokana na kutatuliwa kwa changamoto za upatikanaji wa vibali vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi baada ya Serikali kuweka mfumo wezeshi wa upatikanaji wa vibali kupitia wafanyabiashara wakubwa na vikundi. Vile vile, barua na nyaraka 67,193 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji (pCUM) ikilinganishwa na barua na nyaraka 10,944 mwaka 2017. Kuongezeka kwa barua na nyaraka kulitokana na kuboreshwa kwa utoaji huduma ya pCUM na ongezeko la wateja wapya.

309. Mwaka 2018, miamala ya fedha 629 ilihaulishwa kwa njia ya kielektroniki ikilinganishwa na miamala 531 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Katika kipindi hicho, miamala ya fedha 704 ilitumwa kupitia mfumo wa

Kimataifa wa Utumaji Fedha ikilinganishwa na miamala 448 iliyotumwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 57.1. Ongezeko hilo lilitokana na kufunguliwa kwa huduma katika nchi za Zimbabwe na Burundi. Katika kipindi hicho, wateja 170,606 walihudumiwa kupitia huduma ya kufanya malipo kwa uwakala ya Post Giro ndani ya nchi ikilinganishwa na wateja 151,980 waliohudumiwa mwaka 2017. Huduma hii hutumika kulipa pensheni za wastaafu kupitia Mifuko ya Hifadhi za Jamii na gawio la hisa za makampuni yaliyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

**Utoaji wa Leseni**

310. Mwaka 2018, Mamlaka ya Mawasiliano, ilitoa leseni 463 za huduma mbalimbali za mawasiliano ikilinganishwa na leseni 187 mwaka 2017. Ongezeko la utoaji wa leseni lilitokana na kuongezeka kwa huduma mbalimbali za kidigitali pamoja na utoaji wa leseni kwa watoa huduma 231 wa utangazaji mitandaoni kufuatia kuanzishwa kwa sheria mpya ya maudhui mtandaoni. **Jedwali Na. 16.9** linaonesha mchanganuo wa aina za leseni kwa huduma mbalimbali za mawasiliano.

**Jedwali Na. 16.9 : Aina za Leseni 2017 - 2018**

| Aina | 2017 | 2018 |
|---|---|---|
| Leseni za Kusimika Vifaa vya Mawasiliano (Network Facilities Licence) | 1 | 0 |
| Leseni za Kuunganisha huduma za Mawasiliano (Network Services Licence) | 1 | 0 |
| Leseni za Huduma za Mawasiliano (Application Services Licence) – Category A | 1 | 0 |
| Leseni za Huduma za Mawasiliano (Application Services Licence) – Category B | 17 | 3 |
| Leseni za Maudhui (Content Services-Radio Broadcasting Licence) | 6 | 9 |
| Leseni za Maudhui (Content Services- Television Broadcasting Licence) | 1 | 2 |
| Leseni za Ufungaji na Utengenezaji wa Vifaa vya Mawasiliano ya Kieletroniki (Installation and Maintenance of Electronic Communication Equipment Licence) | 22 | 25 |
| Leseni za Kuingiza Nchini Vifaa vya Mawasiliano ya Kieletroniki (Importation of Electronic Communication Equipment Licence) | 17 | 12 |
| Leseni za Kusambaza Nchini Vifaa vya Mawasiliano ya Kieletroniki (Distribution of Electronic Communication Equipment Licence) | 7 | 5 |
| Leseni za Kuuza Vifaa vya Mawasiliano ya Kieletroniki (Selling of Electronic Communication Equipment Licence) | 45 | 266 |
| Leseni za huduma ya msingi ya Posta | 0 | 0 |
| Leseni za Huduma za Kusafirisha Vifurushi na Vipeto (Courier Services Licence) | 25 | 5 |
| Leseni za V-SAT | 6 | 3 |
| Online Content | 0 | 231 |
| Content by subscription (cable) | 2 | 22 |
| **Jumla** | **187** | **463** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

## Huduma za Simu

311. Mwaka 2018, kadi za simu za kiganjani zilifikia 43,621,499 ikilinganishwa na kadi 40,080,954 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa huduma mbalimbali na zawadi za dakika na data kwa makundi mbalimbali ya kijamii, huduma za mitandao ya kijamii na miamala ya kifedha mitandaoni. Katika kipindi hicho, kadi za simu za mezani zilipungua hadi kufikia 124,238 kutoka kadi 127,094 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 2.2. Hadi kufikia Desemba 2018, kulikuwa na jumla ya laini 43,497,261 za mitandao yote kati ya laini hizo, zilizosajiliwa rasmi zilikuwa 43,447,333, sawa na asilimia 99.9 ya laini zote.

312. Mwaka 2018, gharama za kupiga simu ndani ya mtandao ilishuka hadi shilingi 249 kwa dakika kutoka shilingi 264 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 6.0. Gharama za kupiga simu nje ya mtandao zilishuka na kufikia shilingi 320 kwa dakika kutoka shilingi 349 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 8.3. Kwa upande wa simu za nje ya nchi, gharama za kupiga simu ndani ya Afrika Mashariki ilipungua hadi shilingi 731 kwa dakika mwaka 2018 kutoka shilingi 761 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 3.9. Hata hivyo, mwaka 2018 gharama za kupiga simu kwenda mataifa mengine ziliongezeka hadi shilingi 1,443 kwa dakika kutoka shilingi 1,325 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.9.

**Huduma za INTANETI**

313. Mwaka 2018, watumiaji wa huduma za intaneti walikuwa milioni 23.1 ikilinganishwa na milioni 23.0 mwaka 2017. Katika kipindi hicho, watumiaji wa huduma za *fixed wireless* walipungua hadi kufikia watumiaji 135,954 kutoka watumiaji 3,468,188 kufuatia ongezeko la watumiaji wa intaneti kupitia simu za kiganjani.

**Jedwali Na: 16.10: Matumizi ya Intaneti Nchini**

| **Aina ya Huduma** | **2017** | **2018** | **Badiliko (Asilimia)** |
|---|---|---|---|
| *Fixed Wireless* | 3,468,188 | 135,954 | -96.1 |
| *Mobile Wireless* | 19,006,223 | 22,281,727 | 17.2 |
| *Fixed Wired* | 520,698 | 725,279 | 39.3 |
| **Jumla** | **22,995,109** | **23,142,960** | **0.6** |

**Chanzo**: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Huduma za Utangazaji**

314. Hadi kufikia Desemba 2018, huduma za utangazaji wa luninga kwa kutumia ving'amuzi ilifikia watumiaji 2,769,841 ikilinganishwa na watumiaji 2,236,577 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 23.8. Aidha, watumiaji wa huduma za utangazaji kupitia *satellite* waliongezeka kwa asilimia 72.7 hadi watumiaji 985,594 kutoka watumiaji 570,124 mwaka 2017. Mgawanyo wa watumiaji wa huduma za utangazaji ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 16.11**.

**Jedwali Na: 16.11 Watumiaji wa Huduma za Utangazaji**

| Aina | 2017 | 2018 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|
| *Digital Terrestrial Television (DTT)* | 1,508,229 | 1,626,023 | 7.8 |
| *Satellite* | 570,124 | 985,594 | 72.7 |
| *Cable* | 158,224 | 158,224 | 0 |
| **Jumla** | **2,236,577** | **2,769,841** | **23.8** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

315. Hadi Desemba 2018, vijiji 6,501 vilifikishiwa huduma ya mawasiliano ikilinganishwa na vijiji 5,666 mwaka 2017. Halmshauri 10 ziliunganishwa kwenye miundombinu ya Mkongo ambapo mitambo 12 ya *Video Conference* ilifungwa katika makao makuu ya mikoa na taasisi za Serikali. Aidha, kupitia watoa huduma binafsi, miundombinu ya mawasiliano ilifikishwa katika ofisi 147 za halmashauri; vituo 66 vya posta; vituo 121 vya polisi; hospitali za wilaya 150; mahakama 26; na shule za sekondari 455. Vile vile, Serikali iliendelea kuboresha uendeshaji wa kituo cha Taifa cha *Data* Dar es Salaam na kuendelea na kazi ya usanifu wa ujenzi wa vituo viwili vya Taifa vya data katika maeneo ya Dodoma na Zanzibar.

**Sayansi, Teknolojia na Ubunifu**

**Uendelezaji wa Rasilimali Watu**

316. Mwaka 2018, Serikali iliendelea na juhudi za kuongeza rasilimali watu katika teknolojia na tasnia ya ubunifu nchini. Katika kipindi hicho, wanafunzi 4,135 walidahiliwa katika Chuo Kikuu cha Ardhi ikilinganishwa na wanafunzi 4,180 mwaka 2017. Aidha, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili wanafunzi 4,630 (wanaume 3,746 na wanawake 884) ikilinganishwa na wanafunzi 4,218 waliodahiliwa mwaka 2017 (wanaume 3,509 na wanawake) 709. Vile vile, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi wapya 1,499 (wanaume 1,203 na wanawake 296) ikilinganishwa na udahili wa wanafunzi 2,089 (wanaume 1,648 na wanawake 441) mwaka 2017.

**Udhibiti wa Mionzi**

317. Mwaka 2018, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilipokea na kutathimini maombi 376 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na maombi 384 ya mwaka 2017. Kati ya hayo, maombi 371 yalipata vibali baada ya kukidhi matakwa na vigezo vya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya mwaka 2003. Vigezo hivyo vinahusisha chanzo cha mionzi, sifa za kitaaluma za msafirishaji na mtumiaji na mpango wa uhifadhi wa

kudumu wa mabaki ya chanzo cha mionzi. Aidha, Tume ilipima kiasi cha mionzi kwa wafanyakazi 1,100 kutoka katika vituo 320 ikilinganishwa na wafanyakazi 423 kutoka vituo 68 mwaka 2017. Kiwango cha mionzi kwa wafanyakazi ndani ya miezi mitatu kilikuwa chini ya 5 mSv ambacho kinakubalika kimataifa. Mwaka 2018, kulikuwa na vituo vipya 78 vya watumiaji wa vyanzo vya mionzi na hivyo kufikia jumla ya vituo 900 vinavyotumia mionzi nchini. Tume ilikagua vituo 546 vinavyotumia mionzi na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama wa watumiaji na mazingira ikilinganishwa na vituo 23 vilivyokaguliwa mwaka 2017.

318. Mwaka 2018, Tume iliendelea kudhibiti usalama wa mionzi katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Mtwara, Mwanza, Kigoma na Tanga pamoja na mipaka ya Namanga, Horohoro, Sirari, Mutukula, Holili, Tarakea, Kabanga Tunduma, Rusumo, Mtambaswala, Kasumulu na Kilambo. Vile vile, Tume ilidhibiti usalama wa mionzi katika viwanja vya ndege vya kimataifa vya Kilimanjaro na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika kipindi hicho, Tume ilifanya upimaji wa viwango vya mionzi kwenye sampuli 7,067 ambapo sampuli 2,827 ziliingizwa nchini na sampuli 4,240 zilisafirishwa nje. Kati ya hizo, sampuli za mbolea zilikuwa 79, sigara 147, sampuli za wanyama 478 na sampuli za chakula 6,363.

319. Mwaka 2017, Tume ilikagua vituo vya mionzi katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga na Mtwara pamoja na Mipaka ya Namanga, Tarakea, Sirari, Holili, Horohoro, Mtukula, na Tunduma ili kutathmini hali ya vifaa vinavyotumika iwapo vinakidhi matakwa ya sheria. Katika maeneo yaliyokaguliwa, Tume ilifanya upimaji wa viwango vya mionzi kwa sampuli 2,012 ikilinganishwa na sampuli 1,806 za mwaka 2016. Kati ya hizo, sampuli 1,002 zilikuwa za vyakula vilivyoingia nchini, sampuli 602 za vyakula vilivyosafirishwa nje ya nchi, sampuli 238 za vyakula vya wanyama na sampuli 58 za sigara. Aidha, mwaka 2017 Tume ilikarabati vifaa 43 vya elektroniki, vifaa tisa (9) vya ukaguzi na uhakiki wa vifaa vya ujenzi wa barabara (troxler gauges) pamoja na mashine ya uhakiki wa mionzi (calibration irradiation machine).

## HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

### Sekta ya Habari

320. Mwaka 2018, magazeti na majarida 42 yalisajiliwa upya ikilinganishwa na magazeti na majarida 161 yaliyosajiliwa mwaka 2017, ikiwa ni matakwa ya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2017 zinazoelekeza pamoja na mambo mengine leseni za magazeti na majarida kuhuishwa kila mwaka.

321. Hadi Desemba 2018, kulikuwa na magazeti 201, vituo vya redio 162 na luninga 35. Aidha, vituo nane vya redio na vitatu vya luninga vilisajiliwa mwaka 2018 ikilinganishwa na vituo sita vya redio na vitatu vya televisheni vilivyosajiliwa mwaka 2017. Kuongezeka kwa usajili wa vituo vya redio kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za utangazaji hususan katika maeneo yasiyokuwa na huduma hiyo nchini.

**Jedwali 16.12: Vituo vya Magazeti, Redio na Luninga Vilivyosajiliwa**

| Mwaka | Idadi ya Magazeti/Majarida | Idadi ya Vituo vya Redio | Idadi ya Vituo vya Luninga |
|---|---|---|---|
| 2010 | 8 | 14 | 1 |
| 2011 | 41 | 12 | 0 |
| 2012 | 29 | 12 | 0 |
| 2013 | 36 | 4 | 0 |
| 2014 | 23 | 8 | 3 |
| 2015 | 39 | 22 | 1 |
| 2016 | 26 | 23 | 6 |
| 2017 | 161 | 6 | 3 |
| 2018 | 42 | 8 | 3 |

**Chanzo:** Idara ya Habari-MAELEZO, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

**Maendeleo ya Sanaa**

322. Mwaka 2017/18, Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali 183 vya utengenezaji wa filamu, makala za filamu na picha jongevu kwa kampuni za ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na vibali 153 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 19.6. Kati ya hivyo, vibali 46 vilitolewa kwa kampuni za ndani na 137 kwa kampuni za nje. Kuongezeka kwa utoaji wa vibali kulitokana na kuimarika kwa mifumo ya taarifa na uzingatiaji wa sheria kwa watengenezaji wa filamu kutoka ndani na nje ya nchi.

**Jedwali 16.13: Idadi ya Vibali vya Kutengeneza Filamu Vilivyotolewa Nchini**

| Mwaka | Vibali vya Wageni | Vibali vya Watanzania | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2011/12 | 84 | 21 | 105 |
| 2012/13 | 123 | 30 | 153 |
| 2013/14 | 125 | 33 | 158 |
| 2014/15 | 133 | 36 | 169 |
| 2015/16 | 137 | 31 | 168 |
| 2016/17 | 123 | 30 | 153 |
| 2017/18 | 137 | 46 | 183 |

**Chanzo:** Bodi ya Filamu Tanzania.

**Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)**

323. Mwaka 2017/18, Baraza la Kiswahili la Taifa liliandaa vipindi 847 ambavyo vilirushwa kupitia radio na luninga ikilinganishwa na vipindi 87 vilivyorushwa mwaka 2016/17. Kuongezeka kwa vipindi vilivyotayarishwa kulitokana na kuongeza wigo wa kutumia vyombo vya habari. Aidha, redio za Kiss FM na Idhaa ya Kiswahili ya Redio ya Umoja wa Mataifa ziliongezwa katika kurusha vipindi vya Kiswahili. Kwa upande mwingine, Baraza lilipitia miswada 63 ili kutoa ithibati ya lugha kwa vitabu vinavyokusudiwa kutumika shuleni ikilinganishwa na miswada 61 iliyopitiwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Ongezeko hilo lilitokana na mwamko wa waandishi na wachapishaji kutafuta ithibati ya lugha kabla ya kuchapisha vitabu.

324. Mwaka 2017/18, BAKITA ilitafsiri nyaraka 1,607 na kuhariri nyaraka 39 ikilinganishwa na nyaraka 268 na nyaraka 10 zilizotafsiriwa na kuhaririwa mwaka 2016/17 kwa mtiririko huo. Ongezeko hilo lilitokana na mwamko wa asasi mbalimbali pamoja na watu binafsi kuwasilisha nyaraka zao BAKITA ili zitafsiriwe na kuhaririwa. Aidha, BAKITA ilitoa huduma za ukalimani katika mikutano mitatu mwaka 2017/18. Kwa upande wa ubainishaji makosa ya matumizi ya lugha katika vyombo mbalimbali vya habari, makosa 848 yalibainishwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na makosa 805 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 5.3. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya wanahabari kutokuwa makini katika kutumia lugha kwa ufasaha.

**Jedwali Na. 16.14: Idadi ya Huduma Zilizotolewa**

| Mwaka | Vipindi vya redio na Luninga | Huduma ya Ithibati | Huduma ya Tafsiri | Huduma ya Ukalimani | Huduma ya Uhariri | Makosa yaliyobainika kutumiwa katika vyombo vya habari. |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2010 | 156 | 24 | 300 | 3 | 9 | 1,300 |
| 2011 | 156 | 27 | 350 | 4 | 10 | 1,248 |
| 2012 | 156 | 25 | 280 | 5 | 9 | 1,248 |
| 2013 | 156 | 30 | 400 | 5 | 10 | 1,120 |
| 2014 | 156 | 24 | 410 | 3 | 7 | 1,010 |
| 2015 | 118 | 121 | 320 | 3 | 8 | 1,200 |
| 2016 | 110 | 60 | 350 | 2 | 20 | 1,048 |
| 2017 | 87 | 61 | 268 | 3 | 10 | 805 |
| 2018 | 847 | 63 | 1,607 | 3 | 39 | 848 |

**Chanzo:** Baraza la Kiswahili la Taifa

**Maendeleo ya Michezo**

325. Mwaka 2018, vilabu vya michezo 212 vilisajiliwa ikilinganishwa na vilabu 288 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 26.4. Aidha, vyama vya michezo 23 vilisajiliwa ikilinganishwa na vyama 29 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 20.7. Vile vile, vituo 18 vya michezo vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 13 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 38.5. Ongezeko hilo lilitokana na mwitikio mkubwa wa wadau wa michezo kuanzisha vituo vipya vya michezo. Katika kipindi hicho, wakuzaji na mawakala wa michezo 29 walisajiliwa ikilinganishwa na wakuzaji na mawakala 14 waliosajiliwa mwaka 2017. Kuongezeka kwa wakuzaji na mawakala kulitokana na mabadiliko ya sheria ambayo inatambua michezo ya kulipwa hivyo kupelekea mwitikio mkubwa wa usajili wa wakuzaji na mawakala hususan katika mchezo wa ngumi za kulipwa.

**Jedwali Na. 16.15: Usajili wa Vilabu,Vyama,Vituo na Wakuzaji na Mawakala wa Michezo**

| Mwaka | Vilabu vya Michezo | Vyama vya Michezo | Vituo vya Michezo | Wakuzaji /Mawakala wa Michezo |
|---|---|---|---|---|
| 2011 | 168 | 5 | 2 | |
| 2012 | 339 | 26 | 5 | |
| 2013 | 285 | 37 | 12 | |
| 2014 | 464 | 17 | 7 | |
| 2015 | 224 | 15 | 12 | |
| 2016 | 331 | 9 | 15 | |
| 2017 | 288 | 29 | 13 | 14 |
| 2018 | 212 | 23 | 18 | 29 |

**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

Jedwali Na. 67

| Maelezo | Kipimo | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli | KM | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 | 2707 |
| Magari ya Moshi: | Namba | 25 | 22 | 20 | 45 | 45 | 30 | 44 | 44 | 30 |
| Mvuke | Namba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Dizeli: | Namba | 25 | 22 | 20 | 45 | 45 | 30 | 44 | 44 | 30 |
| Mainlain | | 21 | 19 | 16 | 38 | 38 | 21 | 40 | 40 | 28 |
| Shunting | | 4 | 3 | 4 | 7 | 7 | 9 | 4 | 4 | 2 |
| Jumla ya mabehewa: | Namba | 1071 | 1326 | 1162 | 1200 | 1214 | 1155 | 426 | 426 | 327 |
| Abiria | Namba | 50 | 53 | 36 | 91 | 91 | 56 | 56 | 56 | 71 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 648 | 658 | 635 | 681 | 590 | 561 | 22 | 22 | 18 |
| Mafuta | Namba | 179 | 335 | 208 | 178 | 203 | 196 | 123 | 123 | 95 |
| Mifugo | Namba | 88 | 88 | 80 | 39 | 64 | 64 | 27 | 27 | 27 |
| Mengineyo | Namba | 106 | 192 | 203 | 211 | 266 | 278 | 198 | 198 | 116 |
| Uchukuzi | Namba | | | | | | | | | |
| Abiria | 000 | 284 | 227 | 339 | 373 | 170 | 196 | 1707 | 2150 | 6012 |
| Mizigo | Tani'000 | 265 | 138 | 154 | 185 | 127 | 283 | 102 | 170 | 357 |

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

## RELI YA UHURU - TAZARA

Jedwali Na. 68

| Maelezo | Kipimo | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli Kuu | Km | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 | 1860 |
| Magari ya Moshi | Namba | 16 | 15 | 13 | 13 | 15 | 16 | 17 | 21 | 21 | 18 |
| Reli Kuu | Namba | 11 | 10 | 9 | 9 | 11 | 13 | 12 | 14 | 12 | 13 |
| Ya kujongeza | Namba | 5 | 5 | 4 | 5 | 4 | 3 | 6 | 7 | 7 | 5 |
| Mabehewa ya abiria | Namba | 53 | 36 | 36 | 35 | 52 | 50 | 51 | 56 | 49 | 60 |
| Abiria | Namba | 44 | 31 | 30 | 30 | 45 | 44 | 43 | 48 | 40 | 51 |
| Chakula | Namba | 3 | 2 | 3 | 2 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 | 4 |
| Vifurushi | Namba | 6 | 3 | 3 | 3 | 4 | 3 | 5 | 4 | 5 | 5 |
| Mabehewa ya mizigo | Namba | 1412 | 1620 | 930 | 858 | 1391 | 1101 | 1142 | 1221 | 1033 | 1068 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 1174 | 1381 | 795 | 765 | 1229 | 966 | 1007 | 1077 | 972 | 998 |
| Mifugo | Namba | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mafuta | Namba | 196 | 197 | 93 | 59 | 104 | 82 | 82 | 89 | 26 | 70 |
| Barafu | Namba | 7 | 7 | 7 | 0 | 5 | 5 | 5 | 5 | 0 | 0 |
| Mengineyo | Namba | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| Breki | Namba | 16 | 16 | 16 | 16 | 35 | 30 | 30 | 32 | 30 | 34 |
| Ballast | Namba | 17 | 17 | 17 | 17 | 17 | 17 | 17 | 17 | 4 | 15 |
| Uchukuzi mizigo (Tani) | 000 | 333 | 540 | 248 | 259 | 245 | 33 | 81 | 96 | 171 | 268 |
| Abiria | 000 | 923 | 758 | 414 | 678 | 654 | 287 | 327 | 440 | 443 | 154 |

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

\+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini Tanzania

**USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM**

Jedwali Na. 69

| Maelezo | Kipimo | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 1600 | 742 | 1426 | 1617 | 1684 | 1688 | 1744 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 Tani | 24496 | 13359 | 23278 | 31614 | 31278 | 31287 | 32513 |
| Jumla ya abiria | 000 Namba | 375 | 347 | 1000 | 1612 | 1735 | 1874 | 1901 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000 Dwt | 10122 | 5547 | 9082 | 14601 | 13580 | 13761 | 14401 |
| **Bidhaa zilizopakuliwa** | **000 Dwt** | **9018** | **3899** | **7998** | **11901** | **11260** | **11460** | **11683** |
| Za kawaida | 000 Dwt | 5021 | 2682 | 4495 | 6657 | 6087 | 6376 | 6199 |
| Saruji | 000 Dwt | - | - | - | - | - | - | - |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 Dwt | 3997 | 1217 | 3489 | 4882 | 4772 | 4740 | 5483 |
| Mengineyo1 | 000 Dwt | 0 | 0 | 14 | 362 | 401 | 344 | - |
| **Bidhaa zilizopakiwa** | **000 Dwt** | **1105** | **414** | **808** | **2499** | **2031** | **2045** | **2452** |
| Za kawaida | 000 Dwt | 1033 | 391 | 763 | 2137 | 1915 | 1986 | 2353 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 Dwt | 72 | 23 | 45 | 362 | 116 | 59 | 99 |
| Mengineyo1 | 000 Dwt | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mabadilishano (*Transhipment*) | 000 Dwt | 15 | 0 | 275 | 201 | 289 | 256 | 267 |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, mollasses, tallow fats n.k

\- Takwimu hazikupatikana

## USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

| Maelezo | Kipimo | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 232 | 92 | 64 | 63 | 87 | 72 | 144 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 1378 | 700 | 990 | 1018 | 1258 | 1041 | 780 |
| Jumla ya abiria | 000 Namba | 2865 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 45820 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000Dwt | 608 | 271 | 536 | 645 | 677 | 486 | 647 |
| **Bidhaa zilizopakuliwa** | **000Dwt** | **1051** | **5357** | **437** | **561** | **614** | **436** | **503** |
| Za kawaida | 000Dwt | 436 | 3171 | 437 | 483 | 398 | 141 | 183 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000Dwt | 615 | 2186 | 0 | 78 | 216 | 295 | 319 |
| **Bidhaa zilizopakiwa** | **000Dwt** | **166** | **912** | **100** | **83** | **63** | **50** | **144** |
| Za kawaida | 000Dwt | 166 | 912 | 100 | 83 | 63 | 50 | 144 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000Dwt | - | - | - | - | - | - | - |
| Mabadilishano (*Transhipment* ) | 000Dwt | - | - | - | - | - | - | - |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

\- Takwimu hazikupatikana

## USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

| Maelezo | Kipimo | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 498 | 339 | 428 | 46 | 113 | 105 | 69 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 1557 | 1245 | 1343 | 593 | 460 | 457 | 589 |
| Jumla ya abiria | 000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000 DWt | 178 | 144 | 248 | 248 | 375 | 378 | 363 |
| **Bidhaa zilizopakuliwa** | **000 DWt** | **309** | **894** | **149** | **109** | **158** | **91** | **69** |
| Za kawaida | 000 DWt | 55 | 274 | 140 | 108 | 147 | 91 | 69 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 DWt | 254 | 620 | 9 | 1 | 10 | 0 | 0 |
| **Bidhaa zilizopakiwa** | **000 DWt** | **123** | **70** | **100** | **139** | **218** | **286** | **294** |
| Za kawaida | 000 DWt | 113 | 70 | 100 | 139 | 218 | 286 | 294 |
| Mafuta (*Petroleum)* | 000 DWt | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mabadilishano (*Transhipment*) | 000 DWt | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

## HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 70

| Maelezo | Kipimo | 2009 | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi Ndogo Posta | Namba | 202 | 171 | 105 | 65 | 74 | 74 | 65 | 65 | 66 | 57 |
| Franchised Post Offices | Namba | 81 | 81 | 151 | 112 | 89 | 89 | 90 | 90 | 87 | 87 |
| Ofisi Kubwa | Namba | 170 | 170 | 163 | 147 | 160 | 160 | 158 | 158 | 154 | 157 |
| **Jumla** | Namba | **453** | **422** | **419** | **324** | **323** | **323** | **313** | **313** | **307** | **301** |
| Masanduku Binafsi | 000 | 117 | | 146 | 162 | 173 | 142 | 160 | 160 | 161 | 161 |
| Masanduku Yaliokodishwa | 000 | 87 | 120 | 130 | 140 | 148 | 128 | 138 | 138 | 143 | 157 |
| Maombi Yasiotimizwa | 000 | 4 | 0 | 21 | 28 | 25 | 18 | 4 | 1 | 1 | 3 |
| Mifuko Pekee Iliyokodishwa | Namba | 62 | 183 | 361 | 278 | 212 | 260 | 180 | 180 | 342 | 675 |
| Barua Zilizotumwa bila Vifurushi | Mill. | 14 | 29 | 27 | 15 | 26 | 15 | 10 | 4 | 5 | 9 |
| Regista na Barua za Amana | 000 | 377 | 480 | 347 | 397 | 568 | 455 | 402 | 297 | 269 | 280 |
| Vifurushi Nchini | 000 | 9 | 15 | 10 | 15 | 29 | 12 | 17 | 36 | 51 | 63 |
| Vifurushi Nje | 000 | 2 | 7 | 11 | 12 | 9 | 5 | 9 | 2 | 3 | 4 |
| Leseni za kuuza stamp | Namba | 6256 | 25145 | 28257 | 33311 | 2637 | 3715 | 0 | 0 | 4635 | 6027 |
| **Huduma za Haraka, barua na vifurushi** | " | | | | | | | | | | |
| Ndani ya Nchi | " | 493709 | 283711 | 501635 | 404453 | 620478 | 406732 | 416007 | 452827 | 560710 | 655927 |
| Nje ya Nchi | " | 4012 | 18766 | 16965 | 24347 | 17130 | 20564 | 308288 | 6364 | 9534 | 14346 |
| EMS Money Fax | " | 23165 | 82002 | 36357 | 2940 | 550 | 745 | 748 | 272 | 18 | 0 |
| EMS Fax (Fax message received) | " | 103558 | 31594 | 1595 | 876187 | 544 | 1194 | 3844 | 2518 | 129 | 0 |
| **Overnight Mail Services** | " | | | | 9963 | 115126 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | " | 68912 | 76983 | 115403 | 50082 | 87051 | 46652 | 53639 | 57605 | 24966 | 14553 |
| Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa | " | 13934 | 2752 | 12040 | 10652 | 18784 | 8700 | 9130 | 113448 | 2120 | 5346 |
| **Huduma za gari ndogo** | | | | | | | | | | | |
| Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa | " | 268 | 0 | 193 | 24095 | 849 | 714 | 9576 | - | - | 2919 |
| Amna za Haraka Zilizotolewa | " | 20057 | 8169 | 4717 | 3087 | 2034 | 845 | 58423 | 272 | 127 | 104 |
| Amana za Haraka Zilizolipwa | | 23069 | 11881 | 17397 | 516 | 555 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Amana za Haraka za Nje ya Nchi** | | | | | | | | | | | |
| Zilizotumwa | " | 1030 | 1027 | 998 | 369 | 478 | 325 | 221 | 220 | 8 | 11 |
| Zilizopokelewa | " | 150 | 150 | 217 | 77 | 83 | 227 | 283 | 116 | 43 | 37 |
| Amana za Posta zilizouzwa | " | 8831 | 1924 | 633 | 414 | 684 | 261 | 251 | 107 | 45 | 2 |
| Amana za Posta Zilizolipwa | " | 5490 | 3262 | 1662 | 252 | 166 | 67 | 25 | 18 | 8 | 0 |
| **Benki ya Akiba (Transaction)** | | | | | | | | | | | |
| Uwekaji Amana (Deposit) | " | 9535 | 18863 | 13438 | 6260 | 21491 | 12732 | 21541 | 261423 | 59249 | 108972 |
| Uchukuaji Amana (Withdrawal) | " | 11663 | 23025 | 72358 | 17527 | 37556 | 12807 | 18098 | 45449 | 76926 | 133531 |

Chanzo: Shirika la Posta

**IDADI YA WANAOTUMIA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI**

Jedwali Na. 71

| Kampuni | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **A. Simu za Kiganjani** | | | | | | | | | | |
| Mobitel/Tigo | 4477510 | 5450766 | 6370796 | 6297288 | 8624638 | 11115991 | 11677344 | 11044520 | 12583640 | 13.9 |
| Vodacom | 8670536 | 11625773 | 9357672 | 10288972 | 11810064 | 12714297 | 12419425 | 12714297 | 14143657 | 11.2 |
| Airtel | 6021091 | 6993418 | 8356095 | 8995824 | 9551977 | 11047505 | 10456117 | 10571110 | 10954621 | 3.6 |
| Zantel | 1715985 | 1524601 | 3083889 | 1814444 | 1730105 | 1839391 | 1085642 | 934991 | 1153623 | 23.4 |
| Benson/Smart | 2396 | 1558 | 725 | 528 | 528 | 1560343 | 803251 | 131501 | 132292 | 0.6 |
| TTCL Mobile | 246019 | 225578 | 221663 | 210766 | 296618 | 304214 | 293495 | 175717 | 587191 | 234.2 |
| Sasatel | 24827 | 5824 | 4810 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| Hallotel | | | | | | 1226678 | 3438509 | 3799691 | 3942237 | 3.8 |
| **Jumla Ndogo** | **21158364** | **25827518** | **27395650** | **27607822** | **32013930** | **38581741** | **36735274** | **35572136** | **39555024** | 11.2 |
| **B. Simu za Mezani** | | | | | | | | | | |
| TTCL | 159054 | 159364 | 166148 | 158935 | 140391 | 138754 | 127112 | 127009 | 124220 | -2.2 |
| Zantel | 15457 | 1699 | 10219 | 6064 | 10883 | 4065 | 2485 | 85 | 18 | -78.8 |
| **Jumla Ndogo** | **174511** | **161063** | **176367** | **164999** | **151274** | **142819** | **129597** | **127094** | **124238** | -2.2 |
| **Jumla Kuu** | **21332875** | **25988581** | **27572017** | **27772821** | **32165204** | **38724560** | **36864871** | **35699230** | **39679262** | **11.1** |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

## SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+

Jedwali Na.73

| Maelezo | Kipimo | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tani-Kilometa: | | | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 000 | 9482 | 1662 | 1932 | 6154 | 3052 | 60042 | 3937 | 863107 | 32095 |
| Zilizotumika | 000 | 2888 | 268 | 815 | 2503 | 117 | 30889 | 1756 | 89092 | 17526 |
| Matumizi | % | 30.5 | 16.0 | 42.0 | 40.7 | 3.8 | 54.4 | 46.9 | 10.3 | 54.6 |
| Viti-kilometa: | | | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 000 | 59724 | 7140 | 15131 | 54665 | 3680 | 21693 | 37877 | 225259 | 231943 |
| Vilivyotumika | 000 | 30527 | 2946 | 10209 | 27279 | 946 | 11472 | 20692 | 122532 | 158203 |
| Matumizi | % | 51.1 | 41.0 | 67.0 | 50.0 | 25.7 | 52.8 | 56.0 | 54.4 | 68.2 |
| Abiria ++ | 000 | 41 | 9 | 11 | 35 | 56 | 31 | 28 | 129 | 279 |
| Mizigo ya ziada | Tani | 8 | 2 | 0 | 45 | 0 | 53 | 1 | 41 | 55 |
| Mizigo mingine | Tani | 145 | 4 | 5 | 35 | 45 | 42 | 7 | 50 | 220 |
| Shehena za Posta | Tani | 30 | 0 | 0 | 25 | 405 | 4 | - | 32 | 119 |

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria waliolipa nauli kamili

- Takwimu hazikupatikana

# SURA YA 17

## NISHATI

### Ufuaji wa Umeme

326. Mwaka 2018, uwezo wa uzalishaji wa umeme ulifikia MW 1,600.86 kutoka MW 1,424.60 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 12.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji umeme kwa kutumia mitambo ya Kinyerezi II kutoka MW 55.94 mwaka 2017 hadi MW 248.22 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulifikia saa za gigawati 7,354.79 ikilinganishwa na saa za gigawati 7,115.32 zilizozalishwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Kati ya hizo, saa za gigawati 7,058.09 zilizalishwa kwenye gridi ya Taifa; saa za gigawati 179.17 zilizalishwa kwenye vituo nje ya gridi ya Taifa; na saa za gigawati 117.53 ziliingizwa kwenye gridi ya Taifa kutoka nje ya nchi.

327. Mwaka 2018, mchanganuo wa umeme uliozalishwa katika gridi ya Taifa unaonesha kuwa: umeme wa mitambo ya nguvu za maji ulikuwa saa za gigawati 2,234.43; gesi saa za gigawati 4,788.08 na mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 35.58. Umeme uliozalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO ulikuwa saa za gigawati 5,754.06 mwaka 2018 ikilinganishwa na saa za gigawati 5,469.57 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Ongezeko hili lilitokana na kuingizwa kwa MW 248.22 kutoka kituo cha kufua umeme cha Kinyerezi II. Aidha, kampuni binafsi kwa pamoja zilizalisha saa za gigawati 1,483.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,539.97 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 3.7. Kwa upande mwingine, umeme ulionunuliwa kutoka nchi jirani za Kenya, Uganda na Zambia ulikuwa saa za gigawati 117.53 mwaka 2018 ikilinganishwa na saa za gigawati 105.79 mwaka 2017, sawa na asilimia 1.6 ya umeme wote uliozalishwa mwaka 2018.

328. Mwaka 2018, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 6,290.7 ikilinganishwa na saa za gigawati 5,956.18 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Umeme uliopotea kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme ulikuwa saa za gigawati 1,064.1 sawa na asilimia 14.5 ya umeme uliozalishwa mwaka 2018 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,159.10 sawa na asilimia 16.3 ya umeme uliozalishwa mwaka 2017. Kupungua kwa upotevu wa umeme katika mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme kulitokana na kukamilika kwa mradi wa kusafirisha umeme wa Makambako-Songea pamoja na ujenzi wa kituo cha kusambaza umeme cha Makambako, Njombe na Songea.

**UWEZO WA MITAMBO YA UMEME NA KIASI CHA UMEME ULIOZALISHWA KWA VITUO MWAKA 2018**

Jedwali Na. 74

| Kituo | 2018 | |
|---|---|---|
| | Uwezo (MW) | Umeme Uliozalishwa (GWh) |
| Kidatu | 204.0 | 759.8 |
| Kihansi | 180.0 | 772.6 |
| Mtera | 80.0 | 232.3 |
| New Pangani Falls | 68.0 | 53.6 |
| Hale | 21.0 | 46.9 |
| Nyumba ya Mungu | 8.0 | 339.5 |
| Uwemba | 0.8 | 0.0 |
| Mwenga | 4.0 | 16.8 |
| Yovi | 1.0 | 6.5 |
| Matembwe | 0.6 | 2.0 |
| Darakuta | 0.3 | 0.2 |
| Andoya | 1.0 | 3.8 |
| Tulila | 5.0 | 0.3 |
| **Jumla Ndogo - Hydro** | **573.7** | **2,234.4** |
| Ubungo Gas Plant I | 102.0 | 492.5 |
| Tegeta Gas Plant | 45.0 | 150.3 |
| Ubungo Gas Plant II | 129.0 | 912.2 |
| Zuzu | 7.4 | 0.7 |
| Nyakato | 63.0 | 30.1 |
| Kinyerezi I | 150.0 | 857.2 |
| Kinyerezi II | 248.2 | 897.7 |
| **Jumla Thermal** | **744.6** | **3,340.7** |
| IPTL | | |
| Songas | 189.0 | 1,468.2 |
| Imports from SPPs | 9.5 | 14.8 |
| **Jumla Wazalishaji Binafsi** | **198.5** | **1,483.0** |
| **Jumla Grid** | **1,516.8** | **7,058.1** |
| **MATAWI MENGINE (ISOLATED STATIONS)** | | |
| Kigoma | 8.3 | 28.0 |
| Songea | 8.3 | 6.3 |
| Mpanda | 4.2 | 11.8 |
| Mbinga | 2.0 | 2.2 |
| Ngara | 2.5 | 3.0 |
| Biharamuro | 4.1 | 1.8 |
| Mafia | 2.2 | 5.0 |
| Tunduru | 3.0 | 6.9 |
| Ludewa | 1.3 | 1.2 |
| Liwale | 0.8 | 3.0 |
| Somanga | 7.5 | 5.1 |
| Sumbawanga | 5.0 | 1.0 |
| Kasulu | 2.5 | 9.1 |
| Kibondo | 2.5 | 5.3 |
| Loliondo | 5.0 | 1.4 |
| Namtumbo | 0.3 | 0.9 |
| Mtwara | 22.0 | 86.4 |
| Inyonga | | |
| Madaba | 0.5 | 0.2 |
| Bukoba | 2.6 | 0.4 |
| Ngombeni | | |
| Tulila | | |
| Andoya | | |
| Umeme kutoka nchi jirani | | 117.5 |
| **Jumla Nje ya Gridi** | **84.1** | **296.7** |
| **Jumla Kuu ya Umeme – Nchi Nzima** | **1,600.9** | **7,354.8** |

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

**MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI**

Jedwali Na. 75 **GWH**

| Mwaka | Tanzania Bara | | | Zanzibar | Jumla | Umeme uliopotea | Jumla ya umeme uliotengenezwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wateja wadogo (D1) | Wateja wa Kati (T1) | Wateja Wakubwa (T2,T3 & T8) | T5 | | | |
| 2011 | 328.8 | 1270.8 | 2118.0 | 277.2 | 3994.7 | 1158.8 | 5153.5 |
| 2012 | 320.8 | 1480.1 | 2301.8 | 298.6 | 4401.4 | 1048.3 | 5449.6 |
| 2013 | 280.6 | 1747.0 | 2560.4 | 218.7 | 4806.7 | 1139.6 | 5946.2 |
| 2014 | 217.0 | 1891.0 | 2595.0 | 348.5 | 5051.5 | 1135.3 | 6186.8 |
| 2015 | 148.8 | 2082.7 | 2721.1 | 344.6 | 5297.1 | 1119.8 | 6416.9 |
| 2016 | 345.3 | 2263.4 | 2887.2 | 375.6 | 5871.5 | 1220.7 | 7092.2 |
| 2017 | 301.5 | 2371.0 | 2893.3 | 390.4 | 5956.2 | 1159.1 | 7115.3 |
| 2018 | 319.8 | 2481.9 | 3075.0 | 414.0 | 6290.7 | 1064.1 | 7354.8 |

Chanzo: Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

## MAUZO YA UMEME KWA MIKOA

Jedwali Na. 76

| Mkoa | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dodoma | 83 | 86 | 94 | 105 | 111 | 116 | 137 | 150 | 161 |
| Arusha | 269 | 240 | 286 | 316 | 326 | 311 | 357 | 366 | 383 |
| Manyara | 19 | 20 | 23 | 24 | 25 | 26 | 29 | 32 | 32 |
| Kilimanjaro | 124 | 118 | 138 | 144 | 154 | 151 | 182 | 179 | 182 |
| Tanga | 209 | 219 | 245 | 264 | 266 | 300 | 322 | 330 | 354 |
| Morogoro | 179 | 163 | 207 | 221 | 232 | 212 | 240 | 243 | 275 |
| Coast | 106 | 116 | 142 | 171 | 199 | 220 | 260 | 302 | 393 |
| Dar-es-Salaam | 1615 | 1387 | 1548 | 1932 | 2118 | 2229 | 2398 | 2413 | 2482 |
| Lindi | 13 | 14 | 15 | 18 | 23 | 22 | 24 | 23 | 26 |
| Mtwara | 27 | 30 | 34 | 35 | 9 | 51 | 49 | 48 | 53 |
| Ruvuma | 21 | 21 | 24 | 27 | 28 | 31 | 34 | 35 | 42 |
| Iringa | 101 | 92 | 102 | 105 | 107 | 112 | 107 | 98 | 104 |
| Mbeya | 139 | 132 | 150 | 153 | 170 | 164 | 177 | 178 | 187 |
| Singida | 26 | 23 | 29 | 32 | 35 | 47 | 43 | 44 | 46 |
| Tabora | 97 | 95 | 103 | 109 | 60 | 52 | 57 | 56 | 61 |
| Rukwa | 17 | 19 | 19 | 20 | 22 | 23 | 28 | 27 | 26 |
| Kigoma | 16 | 18 | 21 | 23 | 25 | 28 | 29 | 35 | 40 |
| Shinyanga | 313 | 310 | 279 | 280 | 359 | 417 | 428 | 372 | 339 |
| Kagera | 44 | 29 | 55 | 53 | 54 | 60 | 72 | 77 | 91 |
| Mwanza | 215 | 200 | 224 | 231 | 241 | 236 | 262 | 283 | 288 |
| Mara | 110 | 109 | 108 | 125 | 134 | 135 | 142 | 157 | 166 |
| Njombe | | | | | | - | 69 | 36 | 35 |
| Katavi | | | | | | - | 4 | 11 | 11 |
| Geita | | | | | | - | 34 | 43 | 49 |
| Simyu | | | | | | - | 8 | 18 | 22 |
| Songwe | | | | | 6.4 | 11.4 | 5 | 10 | 29 |
| **Jumla Tanzania Bara** | **3743.0** | **3440.5** | **3845.5** | **4388.0** | **4702.8** | **4952.6** | **5495.9** | **5565.8** | **5876.7** |
| Zanzibar | 174.0 | 277.2 | 298.6 | 218.7 | 348.5 | 344.6 | 375.6 | 390.4 | 414.0 |
| **JUMLA** | **3917.0** | **3717.8** | **4144.1** | **4606.7** | **5051.3** | **5297.1** | **5871.5** | **5956.2** | **6290.7** |

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

**Utafutaji Mafuta na Gesi**

**Gesi Asilia**

329. Uzalishaji wa gesi asilia katika visima vya Songosongo na Mnazi Bay ulifikia futi za ujazo milioni 59,142.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na futi za ujazo milioni 47,456.9 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 24.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia kwenye mtambo wa uzalishaji umeme wa Kinyerezi II na katika kiwanda cha saruji cha Dangote. Aidha, mauzo ya gesi asilia iliyozalishwa katika visima vya Songo Songo na Mnazi Bay yalikuwa dola za Marekani milioni 63.1 mwaka 2018 ikilinganishwa na dola milioni 42.3 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 49.2.

**Jedwali na 17.1: Uzalishaji wa Gesi Asilia Songo Songo na Mnazi Bay**

| Mwaka | Futi za Ujazo (SCF) | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | SongoSongo | Mnazi Bay | Kiliwani North | |
| 2018 | 28,736,840,000 | 30,405,160,000 | - | 59,142,000,000 |
| 2017 | 29,496,560,000 | 17,960,300,000 | - | 47,456,860,000 |
| 2016 | 29,747,400,000 | 5,792,141,976 | 2,783,497,464 | 48,323,024,922 |
| 2015 | 31,384,100,000 | 783,595,488 | - | 37,176,241,976 |
| 2014 | 33,061,500,000 | 715,942,883 | - | 33,845,095,488 |
| 2013 | 35,217,410,590 | 673,870,408 | - | 35,933,353,479 |
| 2012 | 36,233,010,000 | 664,980,487 | - | 36,906,880,408 |
| 2011 | 30,970,500,000 | 454,123,320 | - | 31,635,480,487 |
| 2010 | 27,633,000,000 | 323,686,310 | - | 28,087,123,320 |
| 2009 | 23,593,000,000 | 321,239,550 | - | 23,916,686,310 |
| 2008 | 20,084,000,000 | 258,186,803 | - | 20,405,239,550 |
| 2007 | 19,705,000,000 | - | - | 19,963,186,803 |
| 2006 | 17,907,000,000 | - | - | 17,907,000,000 |
| 2005 | 14,704,000,000 | - | - | 14,704,000,000 |
| **Jumla** | **378,473,320,590** | **58,353,227,225** | **2,783,497,464** | **455,402,172,743** |

**Chanzo**: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Jedwali Na. 17.2: Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Gesi Asilia ya Songo Songo na Mnazi Bay (Dola za Marekani)**

| Mwaka | Songo Songo | Mnazi Bay | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2018 | 22,406,171 | 40,683,088 | 63,089,259 |
| 2017 | 22,795,142 | 19,466,121 | 42,261,263 |
| 2016 | 38,172,718 | 13,818,715 | 51,991,433 |
| 2015 | 43,854,236 | 1,921,965 | 45,776,201 |
| 2014 | 58,761,119 | 1,762,977 | 60,524,096 |
| 2013 | 50,582,385 | 1,592,879 | 52,175,264 |
| 2012 | 35,026,145 | 1,525,251 | 36,551,396 |
| 2011 | 38,337,903 | 1,444,856 | 39,782,759 |
| 2010 | 25,607,621 | 1,080,131 | 26,687,753 |
| 2009 | 21,403,804 | 396,109 | 21,799,913 |
| 2008 | 19,521,646 | 388,449 | 19,910,095 |
| 2007 | 16,861,492 | 305,236 | 17,166,727 |
| 2006 | 14,966,409 | - | 14,966,409 |
| 2005 | 9,019,384 | - | 9,019,384 |
| **Jumla** | **417,316,175** | **84,385,777** | **501,701,952** |

**Chanzo:** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

**Uagizaji Mafuta**

330. Mwaka 2018, mafuta yaliyoingizwa nchini yalikuwa lita za ujazo milioni 5,742.8 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 5,361.5 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mafuta yaliyoagizwa kwa matumizi ya ndani pamoja na kusafirisha nje ya nchi. Mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani yaliongezeka hadi kufikia lita za ujazo milioni 3,267.0 mwaka 2018 kutoka lita za ujazo milioni 3,193.2 mwaka 2017. Aidha, lita za ujazo milioni 2,475.8, sawa na asilimia 43.1 ya mafuta yote yaliyoagizwa mwaka 2018 zilisafirishwa kwenda nchi jirani ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 2,168.2 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 14.2. Ongezeko hilo lilitokana na ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam uliovutia wafanyabiashara wengi kutoka nchi jirani.

**Jedwali Na. 17.3: Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Mwaka 2018**

| Mwezi | Dizeli (Lita) | Petroli (Lita) | Mafuta ya Taa/Ndege (Lita) | Mafuta Mazito (Lita) | Jumla (Lita) |
|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 178,806,958 | 113,119,767 | 25,534,256 | - | 317,460,981 |
| Februari | 143,998,717 | 81,547,784 | - | 6,267,454 | 231,813,955 |
| Machi | 122,574,372 | 74,140,463 | 37,596,783 | - | 234,311,618 |
| Aprili | 127,935,793 | 87,977,280 | 21,214,797 | - | 237,127,870 |
| Mei | 126,233,574 | 113,637,925 | 14,076,112 | - | 253,947,611 |
| Juni | 114,957,559 | 94,948,135 | - | 7,707,045 | 217,612,739 |
| Julai | 151,662,966 | 68,807,490 | 18,137,976 | - | 238,608,432 |
| Agosti | 194,445,718 | 71,963,112 | 37,060,565 | - | 303,469,395 |
| Septemba | 106,810,171 | 63,591,461 | - | - | 170,401,632 |
| Oktoba | 105,100,634 | 82,278,578 | 46,557,721 | - | 233,936,933 |
| Novemba | 102,456,265 | 63,558,269 | 19,831,911 | 9,611,630 | 195,458,075 |
| Desemba | 145,875,577 | 87,656,965 | 21,958,196 | - | 255,490,738 |
| Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi *(Localized Transit)* | 171,793,687 | 192,458,161 | 13,115,663 | - | 377,367,511 |
| **Jumla Kuu** | **1,792,651,991** | **1,195,685,390** | **255,083,980** | **23,586,129** | **3,267,007,490** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Jedwali Na. 17.4: Mafuta Yaliyopitishwa Nchini kwenda Nchi Jirani Mwaka 2018**

| Mwezi | Dizeli (Lita) | Petroli (Lita) | Mafuta ya Taa/ Ndege (Lita) | Mafuta Mazito (Lita) | Jumla (Lita) |
|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 168,577,723 | 95,306,369 | 18,546,925 | 8,473,509 | 290,904,526 |
| Februari | 129,290,775 | 73,105,753 | - | - | 202,396,528 |
| Machi | 103,545,314 | 80,402,160 | 30,276,946 | - | 214,224,420 |
| Aprili | 128,569,889 | 89,406,459 | 17,937,196 | - | 235,913,544 |
| Mei | 176,501,733 | 115,071,445 | 16,265,737 | - | 307,838,915 |
| Juni | 125,237,294 | 90,940,279 | - | 6,436,196 | 222,613,769 |
| Julai | 142,958,655 | 79,122,077 | 23,352,109 | - | 245,432,841 |
| Agosti | 180,691,191 | 115,657,770 | 29,832,595 | 4,145,848 | 330,327,404 |
| Septemba | 112,665,135 | 94,759,588 | - | - | 207,424,723 |
| Oktoba | 170,610,546 | 30,349,587 | 35,408,085 | | 236,368,218 |
| Novemba | 127,953,470 | 67,489,833 | 13,658,633 | - | 209,101,936 |
| Desemba | 107,494,026 | 29,630,147 | 13,465,075 | - | 150,589,248 |
| Ondoa Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized transit) | 171,793,687 | 192,458,161 | 13,115,663 | - | 377,367,511 |
| **Jumla Kuu** | **1,502,302,064** | **768,783,306** | **185,627,638** | **19,055,553** | **2,475,768,561** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

**Mwenendo wa Bei za Mafuta**

331. Mwaka 2018, bei za mafuta katika soko la dunia zilibadilika kulingana na nguvu ya soko ambapo kiwango cha juu cha wastani wa bei ya mafuta ya petroli kilikuwa mwezi Julai na kwa mafuta ya dizeli na mafuta ya taa kilikuwa mwezi Desemba. Katika kipindi hicho, wastani wa bei za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kwa tani katika soko la dunia ulikuwa dola za Marekani 661, 622 na 645 ikilinganishwa na dola 540, 484 na 503 mwaka 2017 kwa mtiririko huo. Bei hizo, ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 22.4 kwa mafuta ya petroli, asilimia 28.5 kwa mafuta ya dizeli na asilimia 28.2 kwa mafuta ya taa. Kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia kulitokana na kupungua kwa uzalishaji wa mafuta katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Nchi Zinazozalisha Mafuta Duniani (OPEC), vikwazo vya kiuchumi kwa nchi ya Iran,

mivutano ya kisiasa na mapigano ya mara kwa mara katika nchi ya Libya pamoja na matatizo ya kiutawala katika nchi ya Venezuela. Vile vile, kupanda kwa bei ya mafuta kulitokana na ongezeko la uhitaji wa bidhaa ya mafuta kwa nchi ya China kufuatia kufungwa kwa vinu vya kuzalisha mafuta kwa ajili ya ukarabati.

**Jedwali Na. 17.5: Bei za Mafuta katika Soko la Dunia (f.o.b) – Dola za Marekani kwa Tani za Ujazo**

| **Aina ya Mafuta** | **Petroli** | | | **Dizeli** | | | **Mafuta ya Taa** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwezi/Mwaka** | **2016** | **2017** | **2018** | **2016** | **2017** | **2018** | **2016** | **2017** | **2018** |
| Januari | 398 | 497 | 574 | 258 | 421 | 530 | 284 | 442 | 570 |
| Februari | 357 | 502 | 600 | 280 | 468 | 549 | 312 | 499 | 587 |
| Machi | 431 | 542 | 599 | 333 | 485 | 581 | 361 | 504 | 587 |
| Aprili | 467 | 557 | 646 | 352 | 505 | 607 | 381 | 510 | 624 |
| Mei | 497 | 531 | 615 | 401 | 470 | 573 | 425 | 476 | 624 |
| Juni | 498 | 555 | 632 | 429 | 480 | 580 | 451 | 497 | 633 |
| Julai | 440 | 521 | 718 | 397 | 455 | 674 | 419 | 474 | 633 |
| Agosti | 464 | 503 | 710 | 389 | 454 | 655 | 411 | 464 | 691 |
| Septemba | 478 | 510 | 710 | 399 | 462 | 639 | 425 | 485 | 673 |
| Oktoba | 512 | 560 | 711 | 449 | 516 | 653 | 473 | 529 | 673 |
| Novemba | 471 | 600 | 712 | 417 | 546 | 699 | 440 | 570 | 693 |
| Desemba | 532 | 599 | 707 | 461 | 549 | 721 | 498 | 587 | 756 |
| **Wastani wa Bei** | **462** | **540** | **661** | **380** | **484** | **622** | **407** | **503** | **645** |
| **Wastani wa Ongezeko (Asilimia)** | | **16.9** | **22.4** | | **27.4** | **28.5** | | **23.6** | **28.2** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

332. Kufuatia kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia mwaka 2018, wastani wa bei katika soko la ndani ulipanda ikilinganishwa na wastani wa bei mwaka 2017. Wastani wa bei za ukomo za mafuta katika soko la ndani mwaka 2018 uliongezeka hadi shilingi 2,318 kwa lita moja ya mafuta ya petroli; shilingi 2,229 kwa mafuta ya dizeli; na shilingi 2,188 kwa mafuta ya taa kutoka shilingi 2,004; shilingi 1,873; na shilingi 1,832 mwaka 2017 kwa mtiririko huo. Hii ni sawa na ongezeko la bei kwa wastani wa asilimia 15.7 kwa

mafuta ya petroli, asilimia 19.0 kwa mafuta ya dizeli na asilimia 19.4 kwa mafuta ya taa.

**Jedwali Na. 17.6: Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Ndani**

| Mwezi/ Mwaka | Petroli Sh/Lita | Dizeli Sh/Lita | Mafuta ya Taa Sh/Lita | Mwezi/ Mwaka | Petroli Sh/Lita | Dizeli Sh/Lita | Mafuta ya Taa Sh/Lita |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 1,890 | 1,732 | 1,700 | Januari | 2,167 | 2,018 | 2,031 |
| Februari | 1,959 | 1,861 | 1,852 | Februari | 2,226 | 2,065 | 2,055 |
| Machi | 2,060 | 1,913 | 1,852 | Machi | 2,227 | 2,134 | 2,059 |
| Aprili | 2,057 | 1,925 | 1,858 | Aprili | 2,315 | 2,205 | 2,154 |
| Mei | 2,027 | 1,844 | 1,842 | Mei | 2,227 | 2,145 | 2,154 |
| Juni | 2,052 | 1,888 | 1,825 | Juni | 2,282 | 2,164 | 2,192 |
| Julai | 1,978 | 1,830 | 1,830 | Julai | 2,409 | 2,329 | 2,192 |
| Agosti | 1,867 | 1,719 | 1,719 | Agosti | 2,384 | 2,292 | 2,271 |
| Septemba | 1,989 | 1,887 | 1,811 | Septemba | 2,373 | 2,273 | 2,247 |
| Oktoba | 1,993 | 1,897 | 1,810 | Oktoba | 2,368 | 2,304 | 2,247 |
| Novemba | 2,014 | 1,999 | 1,938 | Novemba | 2,396 | 2,385 | 2,280 |
| Desemba | 2,160 | 1,984 | 1,942 | Desemba | 2,436 | 2,436 | 2,368 |
| **Wastani Mwaka 2017** | **2,004** | **1,873** | **1,832** | **Wastani Mwaka 2018** | **2,318** | **2,229** | **2,188** |
| **Wastani Mwaka 2016** | **1,845** | **1,673** | **1,644** | **Wastani Mwaka 2017** | **2,004** | **1,873** | **1,832** |
| **Badiliko (Asilimia)** | **8.6** | **12.0** | **11.4** | **Badiliko (Asilimia)** | **15.7** | **19.0** | **19.4** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

### Nishati Jadidifu

#### Nishati ya Mionzi ya Jua

333. Mwaka 2018, uzalishaji wa umeme wa jua kwa mfumo wa gridi ndogo (solar mini grid) katika maeneo ambayo hayajafikiwa na gridi ya Taifa ulifikia megawati 7 ikilinganishwa na megawati 5 mwaka 2017. Matumizi ya nishati ya jua iliyozalishwa kupitia mfumo wa umeme wa jua majumbani (solar home systems) yalifikia megawati 18 ikilinganishwa na megawati 15 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 20.0. Aidha, Serikali ilibainisha na kuhakiki maeneo yanayofaa kwa ajili ya uzalishaji wa nishati ya umeme wa jua ili kujua uwezo wa maeneo hayo katika kuzalisha umeme. Maeneo yaliyobainishwa na kuhakikiwa ni Same (Kilimanjaro), Zuzu (Dodoma) na Manyoni (Singida).

**Maporomoko ya Maji**

334. Mwaka 2018, kiwango cha uzalishaji umeme kupitia maporomoko madogo ya maji kilifikia megawati 58.2 ikilinganishwa na megawati 55.0 zilizozalishwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Ongezeko hilo lilitokana na kukamilika kwa miradi ya maporomoko ya maji ya Andoya (Mbinga) megawati 0.5; Madope (Njombe) megawati 1.7 na Luponde (Njombe) megawati 1.

**Nishati mbadala kwa ajili ya kupikia majumbani (LPG)**

335. Mwaka 2018, uhamasishaji wa matumizi ya gesi ya kupikia majumbani (LPG) uliendelea kufanyika ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni. Aidha, mifumo ya usambazaji wa gesi ya mitungi (LPG) iliimarika na kufanya matumizi ya gesi ya mitungi kufikia takribani asilimia 7 kutoka asilimia 5 mwaka 2017.

# SURA YA 18

# MAJI

## Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

336. Serikali iliendelea na mikakati ya kuhifadhi vyanzo vya maji ambapo hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya vyanzo vya maji 298 vilitambuliwa kuwa katika hatari ya kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu ikilinganishwa na vyanzo vya maji 261 mwaka 2017. Kati ya hivyo, vyanzo 91 viliwekewa mipaka na vipo katika hatua mbalimbali za kutangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji ikilinganishwa na vyanzo 85 mwaka 2017.

337. Mwaka 2018, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya usambazaji maji. Aidha, vituo vya kupima wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi vilikuwa 1,067 ikilinganishwa na vituo 694 mwaka 2017. Hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya sampuli 5,668 za maji safi zilikusanywa na kuchunguzwa ambapo sampuli 5,169 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya majumbani, sampuli 312 kwa ajili ya mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo vya maji na sampuli 187 kwa ajili ya ufuaji wa umeme.

338. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa sampuli 4,459, sawa na asilimia 86.3 kwa ajili ya matumizi ya majumbani zilikidhi vigezo vya ubora vinavyokubalika na sampuli 710 sawa na asilimia 13.7 hazikukidhi vigezo. Kutokidhi vigezo vya ubora kulitokana na uwepo wa viwango vikubwa vya madini ya *Fluoride*, *Manganese*, Chuma, *Sulphate*, *Nitrate* na chumvichumvi pamoja na vijidudu kwenye sampuli zilizochukuliwa katika maeneo mbalimbali nchini.

339. Mwaka 2018, sampuli za maji 499 zilikusanywa na kuchunguzwa kwa ajili ya kuhakiki ubora wa maji yanayotumika katika shughuli nyingine ambapo viwandani zilikuwa sampuli 289, ujenzi (43), umwagiliaji (98) na utafiti (69). Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa sampuli zote 499, sawa na asilimia 100 zilikidhi viwango vya ubora wa maji kwa matumizi husika. Aidha, hadi Desemba 2018, sampuli 405 za majitaka yanayoruhusiwa kwenye mazingira zilihakikiwa na kubainika kuwa sampuli 339 sawa na asilimia 83.7 hazikukidhi viwango vya ubora wa majitaka unaokubalika. Hii ni kutokana na uwepo wa

viwango vikubwa vya *Chemical Oxygen Demand* na *Biochemical Oxygen Demand* pamoja na viwango vidogo vya *Dissolved Oxygen.*

**Huduma ya Maji Vijijini**

340. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maji ili kuimarisha huduma za maji vijijini. Hadi kufikia Desemba 2018, miradi 1,659 ya maji vijijini ilikamilika katika halmashauri zote nchini na miradi 482 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikilinganishwa na miradi 1,493 iliyokamilika katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Aidha, miundombinu ya maji iliyojengwa ilikuwa na vituo vya kuchotea maji 131,370 vyenye uwezo wa kuhudumia wananchi 32,842,500 sawa na asilimia 83.9 ya wananchi waishio vijijini. Kati ya vituo hivyo, 86,780 vinafanya kazi na kutoa huduma kwa watu 25,659,290 sawa na asilimia 64.8 ikilinganishwa na vituo 85,286 mwaka 2017 vilivyokuwa vinafanya kazi na kutoa huduma kwa watu 21, 321,500 sawa na asilimia 58.7. Kuwepo kwa vituo visivyofanya kazi kulitokana na uwezo mdogo wa wananchi katika kusimamia na kugharamia uendeshaji miradi ya maji. Katika kutatua changamoto hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanza kubadilisha mitambo inayotumia nishati ya dizeli kusukuma maji na kufunga mitambo inayotumia nishati ya jua ili kuwapunguzia wananchi gharama za uendeshaji na matengenezo.

**Huduma za Maji Mijini**

341. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kujenga, kukarabati na kupanua miradi ya maji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira mijini. Miradi hiyo ilichangia kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma za maji kwenye miji mikuu ya mikoa kutoka asilimia 78 mwaka 2017 hadi asilimia 80 mwaka 2018. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa maji katika miji mikuu ya mikoa uliongezeka hadi kufikia mita za ujazo milioni 149.35 kutoka mita za ujazo milioni 148.82 mwaka 2017. Aidha, wateja waliopata huduma ya maji waliongezeka hadi kufikia 513,050 kutoka wateja 462,790 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 11.

342. Upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 64 mwaka 2018 kutoka wastani wa asilimia 60 mwaka 2017. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa maji uliongezeka kufikia mita za ujazo milioni 62.15 kutoka mita za ujazo milioni 62.01 mwaka 2017 .Vile vile, wateja wanaopata huduma ya maji waliongezeka kutoka wateja 161,925 mwaka 2017 hadi kufikia wateja 173,360 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 7.1.

343. Katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya miji ya Kibaha na Bagamoyo, wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama uliongezeka kutoka asilimia 75 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 85 mwaka 2018. Uzalishaji wa maji katika maeneo hayo ulikuwa mita za ujazo 504,000 kwa siku ukilinganisha na mahitaji ya mita za ujazo 544,000. Mamlaka ya DAWASA iliongeza wateja wanaopata huduma ya maji kutoka 207,477 mwaka 2017 hadi wateja 230,715 mwaka 2018.

**UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYO NA MAJI MIJINI**

Jedwali Na. 77

| Mamlaka | Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo) | Mapato (TShs) | Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo) | Mapato (TShs) |
|---|---|---|---|---|
| | 2017 | | 2018 | |
| Arusha | 16,063,140 | 13,266,008,384 | 15,855,281 | 14,217,491,604 |
| Babati | 2,197,237 | 1,996,989,394 | 2,171,167 | 2,081,921,523 |
| Bukoba | 2,579,696 | 2,402,314,859 | 3,108,330 | 2,155,596,478 |
| Dodoma | 14,342,862 | 15,784,277,531 | 14,133,296 | 14,432,195,493 |
| Iringa | 5,064,617 | 8,253,626,402 | 4,816,026 | 7,438,654,131 |
| Kigoma | 2,340,622 | 1,727,740,848 | 2,899,655 | 1,401,397,427 |
| Lindi | 391,293 | 229,473,270 | 782,362 | 428,571,295 |
| Mbeya | 14,874,398 | 10,109,520,093 | 13,799,430 | 10,283,182,014 |
| Morogoro | 10,678,558 | 8,192,719,085 | 11,503,479 | 9,648,877,386 |
| Moshi | 11,851,809 | 8,346,772,210 | 11,504,048 | 8,710,378,486 |
| Mtwara | 2,990,362 | 3,350,692,910 | 3,414,928 | 3,195,032,315 |
| Musoma | 5,368,089 | 3,028,380,267 | 6,500,625 | 2,595,585,907 |
| Mwanza | 28,943,933 | 24,442,226,082 | 28,143,030 | 23,110,801,495 |
| Shinyanga | 3,964,787 | 5,319,707,891 | 3,844,976 | 5,358,301,189 |
| Singida | 2,415,323 | 2,500,977,359 | 2,506,742 | 2,655,530,728 |
| Songea | 2,926,061 | 2,550,495,722 | 2,821,306 | 2,745,616,563 |
| Sumbawanga | 3,574,900 | 2,452,594,849 | 2,623,216 | 1,227,268,381 |
| Tabora | 4,462,058 | 6,587,593,839 | 4,935,898 | 4,065,238,488 |
| Tanga | 10,135,778 | 11,552,081,699 | 10,259,291 | 12,347,980,872 |
| Mpanda | 1,020,865 | 515,082,997 | 943,574 | 568,916,237 |
| Bariadi | 185,375 | 143,533,808 | 186,667 | 165,347,800 |
| Njombe | 1,174,500 | 822,846,568 | 1,184,152 | 954,726,211 |
| Geita | 1,272,343 | 461,359,520 | 1,412,883 | 649,172,951 |
| **Jumla** | **148,818,606** | **134,037,015,587** | **149,350,362** | **130,437,784,974** |

Chanzo: Wizara ya Maji na Umwagiliaji

**MAHITAJI NA KIWANGO CHA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI**

Jedwali Na. 78

| Mamlaka | Mahitaji ya Maji kwa Mwaka | Wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa mwaka 2018 (Asilimia) |
|---|---|---|
| Arusha | 33,480,000 | 47% |
| Babati | 2,884,000 | 75% |
| Bukoba | 4,643,486 | 67% |
| Dodoma | 16,560,000 | 85% |
| Iringa | 5,840,000 | 82% |
| Njombe | 3,114,533 | 38% |
| Mpanda | 3,472,250 | 27% |
| Kigoma | 8,067,656 | 36% |
| Lindi | 2,059,902 | 38% |
| Mbeya | 16,875,000 | 82% |
| Morogoro | 20,235,912 | 57% |
| Moshi | 14,682,960 | 78% |
| Mtwara | 4,299,184 | 79% |
| Musoma | 8,640,000 | 75% |
| Mwanza | 40,586,250 | 69% |
| Geita | 5,457,600 | 26% |
| Bariadi | 2,068,748 | 9% |
| Shinyanga | 6,942,200 | 55% |
| Singida | 4,114,260 | 61% |
| Songea | 5,064,120 | 56% |
| Sumbawanga | 4,745,000 | 55% |
| Tabora | 9,846,630 | 50% |
| Tanga | 11,612,286 | 88% |
| Vwawa- Mlowo | 3,083,459 | 24% |
| **Jumla** | **238,375,436** | |

Chanzo: Wizara ya Maji

## SURA YA 19

## ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

**Elimu ya Awali**

344. Mwaka 2018, wanafunzi 1,422,868 waliandikishwa katika elimu ya awali ikilinganishwa na wanafunzi 1,517,670 walioandikishwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 6.2. Kati ya hao, wasichana walikuwa 702,786, sawa na asilimia 49.4 ya wanafunzi wote na wavulana walikuwa 720,082. Upungufu wa uandikishaji katika elimu ya awali ulitokana na utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila malipo ambapo idadi kubwa ya wanafunzi walijiunga darasa la kwanza bila kupitia elimu ya awali. Wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa 1,334,726 mwaka 2018 ikilinganishwa na wanafunzi 1,436,322 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 7.1. Kati ya hao, wasichana walikuwa 659,618 na wavulana 675,108. Katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 88,142 ikilinganishwa na wanafunzi 81,348 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Kwa upande wa uandikishaji katika ngazi za mikoa, mkoa wa Mwanza uliandikisha idadi kubwa ya wanafunzi ambao walikuwa asilimia 7.6 ya wanafunzi wote ikifuatiwa na Kagera asilimia 6.6. Mkoa wa Katavi ulikuwa na uandikishaji mdogo kuliko mikoa mingine wa asilimia 1.5.

345. Uwiano wa mwalimu mwenye sifa kwa wanafunzi katika elimu ya awali kwa shule za Serikali ulikuwa 1:146 mwaka 2018 ikilinganishwa na 1:183 mwaka 2017 wakati kiwango halisi cha uwiano unaokubalika ni 1:25. Kufuatia hali hiyo, Serikali inaendelea kuongeza jitihada za kutoa ajira kwa walimu wa elimu ya awali pamoja na kuimarisha mafunzo ya ualimu wa elimu ya awali katika vyuo vya ualimu vya Serikali ili kupata wahitimu wengi na kufikia uwiano unaokubalika.

**Elimu ya Msingi**

346. Mwaka 2018, idadi ya shule za msingi ilikuwa 17,562 ikilinganishwa na shule 17,357 mwaka 2017. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 16,149 ikilinganishwa na shule 16,140 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 0.1. Aidha, idadi ya shule zisizo za Serikali iliongezeka kutoka 1,217 mwaka 2017 hadi shule 1,413 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 16.1.

347. Mwaka 2018, idadi ya wanafunzi katika elimu ya msingi ilikuwa 10,111,671 ikilinganishwa na wanafunzi 9,317,791 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Kati ya hao, wavulana walikuwa 5,046,571 na wasichana walikuwa 5,065,100 (asilimia 50.1). Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali iliongezeka kutoka wanafunzi 8,969,110 mwaka 2017 hadi wanafunzi 9,717,309 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 8.3. Kati yao, wasichana walikuwa 376,524 na wavulana 417,356. Vilevile, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa rika lengwa (miaka 7-13) kiliongezeka hadi asilimia 91.1 kutoka asilimia 84.0 mwaka 2017. Serikali inaendelea na juhudi za kushirikisha wananchi hususan katika ujenzi wa miundombinu ikiwemo madarasa kwa kutumia mfumo wa *Force Account* kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza na hivyo kuongeza ubora wa elimu. Vile vile, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa jamii inaelimishwa juu ya umuhimu wa elimu katika kuleta maendeleo ya nchi kwa kuhakikisha wanafunzi wanaotakiwa kuwa shuleni wanakua shuleni wakati wa masomo. Kutokana na juhudi hizo, idadi ya wanafunzi wanaoacha shule ilipungua kutoka wanafunzi 117,927 mwaka 2016 hadi wanafunzi 66,142 mwaka 2017.

348. Mwaka 2018, idadi ya walimu wenye sifa katika shule za Serikali ilikuwa 179,341 ikilinganishwa na walimu 179,291 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 0.03. Uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ulikuwa 1:52 mwaka 2018 ikilinganishwa na uwiano wa 1:42 mwaka 2017. Upungufu huu ulitokana na kuondolewa kwa walimu wasiokuwa na sifa kwenye utumishi wa umma. Uwiano stahiki wa mwalimu kwa mwanafunzi kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa ni 1:40.

**Elimu ya Sekondari**

349. Mwaka 2018, idadi ya shule za sekondari ilikuwa 4,883 ikilinganishwa na shule 4,796 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 1.8. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 3,635 na shule zisizo za Serikali 1,248 mwaka 2018. Aidha, wanafunzi 2,148,466 walikuwa kidato cha kwanza hadi cha sita ikilinganishwa na wanafunzi 1,908,857 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Vile vile, wanafunzi waliojiunga na kidato cha kwanza hadi cha nne mwaka 2018 walikuwa 1,991,021 ikilinganishwa na wanafunzi 1,767,890 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Kufuatia ongezeko hilo, Serikali ilishirikiana na wadau mbalimbali katika ujenzi wa miundombinu ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya wanafunzi. Kwa upande mwingine, idadi ya walimu katika shule za sekondari

ilikuwa 102,982 ikilinganishwa na walimu 110,163 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 6.5. Upungufu huo ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo baadhi ya walimu kuachishwa kazi kutokana na ukosefu wa sifa za kiutumishi.

350. Mwaka 2018, watahiniwa 358,427 walifanya mtihani wa kidato cha nne ambapo watahiniwa 284,126 walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 79.3 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 76.7 mwaka 2017. Aidha, mwaka 2017, jumla ya watahiniwa 62,233 walifanya mtihani wa kidato cha sita ambapo wanafunzi 58,556, sawa na asilimia 94.1 walifaulu ikilinganishwa na watahiniwa 64,861 waliofanya mtihani mwaka 2016 ambapo wanafunzi 63,499 walifaulu, sawa na ufaulu wa asilimia 97.9.

**Elimu katika Vyuo vya Ualimu**

351. Mwaka 2017/18 idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu ilikuwa ni 20,962 ikilinganishwa na wanachuo 20,324 mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Kati ya hao, wanaume walikuwa 14,618 na wanawake 6,344. Aidha, vyuo vya ualimu vya Serikali vilikuwa na wanachuo 17,390 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na wanachuo 16,861 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Kati ya hao, wanawake walikuwa 4,662 na wanaume walikuwa 13,268. Vile vile, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu visivyo vya Serikali ilikuwa 3,032 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na wanachuo 3,463 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 12.4. Upungufu huo ulitokana na kukosekana kwa wanafunzi wenye sifa stahiki sambamba na gharama ya kujiunga katika vyuo husika.

**Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu**

352. Mwaka 2017/18, Serikali ilikagua taasisi 11,864 za elimu ikilinganishwa na taasisi 12,389 zilizokaguliwa mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 4.2. Hii ilitokana na upungufu wa vitendea kazi ikiwemo magari hususan kwa shule zilizo katika maeneo ambayo hayafikiki kirahisi. Lengo la ukaguzi ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa katika ngazi zote za elimu inakuwa na ubora na viwango vinavyostahili. Serikali inaendelea kuongeza juhudi kwa kuhakikisha Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule inapatiwa vitendea kazi ili kuweza kuleta ufanisi na kuweza kufikia malengo.

**Jedwali 19.1: Ukaguzi wa Taasisi za Elimu Hadi kufikia Machi, 2018**

| Taasisi/Shule/ Vituo/Vyuo | Idadi iliyolengwa kukaguliwa (2017/18) | Idadi halisi iliyokaguliwa (2017/18) | Kiwango cha utekelezaji (% ya idadi iliyokaguliwa) |
|---|---|---|---|
| Shule za Awali | 8380 | 3333 | 39.8 |
| Shule za Msingi | 8380 | 6434 | 76.8 |
| Shule za kiujuzi baada ya Msingi"*Post Primary Vocational Centres*" | 288 | 26 | 9.0 |
| Shule/Vituo vya Elimu Maalum | 278 | 40 | 14.4 |
| Vituo vya Elimu ya Watu Wazima | 2253 | 268 | 11.9 |
| Shule za Sekondari | 2376 | 1701 | 71.6 |
| Vyuo vya Ualimu | 132 | 62 | 47.0 |
| **Jumla** | **22,087** | **11,864** | **53.7** |

**Chanzo:** Taarifa za Uthibiti Ubora wa Shule za Kanda, 2017/18, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia

**Elimu ya Ufundi na Mafunzo**

353. Mwaka 2017/18, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo iliongezeka hadi wanafunzi 128,940 kutoka wanafunzi 128,121 mwaka 2016/17. Kati ya hao, wanaume walikuwa 68,973 na wanawake walikuwa 59,967 (asilimia 46.5). Aidha, katika kuhakikisha programu zinazotolewa zinakaguliwa na zinakidhi viwango, Serikali iliboresha ofisi nane za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi za kanda ili kuweza kuzalisha wataalamu kulingana na uhitaji wa soko.

**Elimu ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi**

354. Mwaka 2017/18, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi ilikuwa 119,184 ikilinganishwa na wanafunzi 130,079 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 8.4. Kati ya hao, wanaume walikuwa 80,050 na wanawake walikuwa 39,134 (asilimia 32.8). Upungufu huu ulitokana na wanafunzi wengi kuendelea kujiunga na elimu ya sekondari kufuatia utekelezaji wa sera ya elimumsingi bila malipo. Aidha, Serikali iliendelea na ukarabati wa vyuo 20 kati ya vyuo 55 vya maendeleo ya wananchi ili kuhakikisha wanafunzi wengi wanajiunga katika vyuo hivyo kwa lengo la kukuza uchumi na maendeleo katika maeneo wanayoishi.

**Elimu ya Juu**

355. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu nchini ilikuwa 230,339 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na wanafunzi 242,240 mwaka 2016/17, sawa na upungufu wa asilimia 4.9. Kati ya hao, wanawake walikuwa 90,159 (asilimia 39.) na wanaume walikuwa 140,180. Upungufu huu ulitokana na baadhi ya vyuo kufungiwa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini kutoa programu ambazo zilikuwa hazina wanataaluma wenye uwezo wa kufundisha programu hizo.

356. Mwaka 2018/19, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliratibu utoaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 412.4 kwa wanafunzi wa elimu ya juu 119,214. Kati ya hao, wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliopata mikopo walikuwa 40,114 (wanafunzi yatima 8,344, wenye ulemavu 722 na kutoka kaya maskini wanafunzi 31,048). Aidha, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ilipanga kukusanya shilingi bilioni 150 hadi Juni, 2019 kutoka kwa wanufaika ambapo hadi Januari 2019, jumla ya shilingi bilioni 108.9 zilikua zimekusanywa.

**SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO**

Jedwali Na. 80 (Namba)

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2000 | 43643 | 36734 | 31132 | 25456 | 6654 | 6143 | 149762 |
| 2001 | 47204 | 45078 | 30531 | 29188 | 7198 | 6601 | 165800 |
| 2002 | 56101 | 50371 | 36989 | 29045 | 7711 | 7126 | 187343 |
| 2003 | 52863 | 60643 | 36906 | 35653 | 7780 | 6885 | 200730 |
| 2004 | 98738 | 67294 | 46546 | 36385 | 8353 | 7572 | 264888 |
| 2005 | 134963 | 109398 | 46188 | 46489 | 9710 | 8444 | 355192 |
| 2006 | 196391 | 151448 | 72167 | 42584 | 18211 | 9691 | 490492 |
| 2007 | 401011 | 218060 | 105770 | 70796 | 21789 | 11668 | 829094 |
| 2008 | 395930 | 332393 | 175353 | 95214 | 25240 | 11743 | 1035873 |
| 2009 | 480529 | 308131 | 159789 | 167355 | 31201 | 12695 | 1159700 |
| 2010 | 382207 | 398870 | 293519 | 279995 | 26065 | 20674 | 1401330 |
| 2011 | 403873 | 396724 | 380528 | 279117 | 30265 | 25164 | 1515671 |
| 2012 | 457321 | 386250 | 355740 | 343376 | 31206 | 28859 | 1602752 |
| 2013 | 444532 | 506036 | 193901 | 302963 | 30581 | 26698 | 1504711 |
| 2014 | 479089 | 506170 | 356787 | 178246 | 33619 | 26899 | 1580810 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 467982 | 366396 | 263981 | 278690 | 45533 | 47007 | 1469589 |
| 2017 | 491535 | 443614 | 296034 | 236775 | 53749 | 43494 | 1565201 |
| 2018 | 587186 | 480327 | 358960 | 278239 | 57287 | 52687 | 1814686 |
| Badiliko (% ) | | | | | | | |
| 2017 - 2018 | 19.5 | 8.3 | 21.3 | 17.5 | 6.6 | 21.1 | 15.9 |

Chanzo: Wizara ya Elimu,Sayansi naTeknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

## IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA

Jedwali Na.80A

| | 2017 | | | 2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Elimu ya msingi** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** | **Waume** | **Wake** | **Jumla** |
| Jumla ya wanafunzi wate walioandikishwa Darasa Ia I-VII | 4629215 | 4688576 | 9317791 | 5046571 | 5065100 | 10111671 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa Ia I-VII | 4453570 | 4515540 | 8969110 | 4848367 | 4868942 | 9717309 |
| Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa Ia I-VII | 175645 | 173036 | 348681 | 198204 | 196158 | 394362 |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi | 96387 | 101176 | 197563 | - | - | - |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za Serikali | 85908 | 93383 | 179291 | - | - | - |
| Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi | 10479 | 7793 | 18272 | - | - | - |
| **Elimu ya Sekondari** | | | | | | |
| Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI | 947407 | 961450 | 1908857 | 1056498 | 1091968 | 2148466 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI | 781077 | 784124 | 1565201 | 894647 | 920039 | 1814686 |
| Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI | 166330 | 177326 | 343656 | 161851 | 171929 | 333780 |
| Idadi ya walimu katika shule za Serikali | 71707 | 38456 | 110163 | - | - | - |
| Idadi ya walimu katika shule za binafsi | 55333 | 34142 | 89475 | - | - | - |
| Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari | 16374 | 4314 | 20688 | - | - | - |

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

- Takwimu Hazikupatikana

## IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali Na. 80 B

| | 2017 | | | 2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Aina ya Taasisi** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** | **Serikali** | **Binafsi** | **Jumla** |
| Shule za Msingi | 16140 | 1217 | 17357 | 16109 | 1065 | 17174 |
| Shule za Sekondari | 3604 | 1192 | 4796 | 3614 | 1145 | 4759 |
| Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari) | - | - | - | - | - | - |
| Elimu ya Ufundi na Mafunzo | - | - | - | - | - | - |
| **Jumla** | **19744** | **2409** | **22153** | **19723** | **2210** | **21933** |

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

- Takwimu hazikupatikana

## MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU

**Jedwali Na. 80C**

| Aina | Mwaka wa Kwanza | | | Mwaka wa Pili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla |
| **Masomo ya Art** | | | | | | | | | |
| Cheti (pre services) | 2086 | 1257 | 3343 | 772 | 462 | 1234 | 2858 | 1719 | 4577 |
| Astashahada(in services) | 216 | 148 | 364 | 736 | 415 | 1151 | 952 | 563 | 1515 |
| Astashahada(pre services) | 1271 | 695 | 1966 | 2372 | 1293 | 3665 | 3643 | 1988 | 5631 |
| **Masomo ya Sayansi** | | | | | | | | | |
| Cheti (pre services) | 104 | 95 | 199 | 0 | 0 | 0 | 104 | 95 | 199 |
| Astashahada(in services) | 125 | 86 | 211 | 373 | 223 | 596 | 498 | 309 | 807 |
| Astashahada(pre services) | 4333 | 744 | 5077 | 1901 | 706 | 2607 | 6234 | 1450 | 7684 |
| **Elimu Maalum** | | | | | | | | | |
| Astashahada(pre services) | 45 | 41 | 86 | 284 | 179 | 463 | 329 | 220 | 549 |
| **Jumla** | **8180** | **3066** | **11246** | **6438** | **3278** | **9716** | **14618** | **6344** | **20962** |

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia

**IDADI YA WANAFUNZI WANAOSOMA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU KWA JINSI KWA MWAKA 2016/2017**

Jedwali Na.80 D

| Jina la Chuo | Idadi ya Wananfunzi | | | Idadi ya Walimu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla |
| UNIVERSITY OF DAR-ES-SALAAM {UDSM) | 17600 | 9209 | 26809 | 1929 | 584 | 2513 |
| SOKOINE UNIVERSITY {SUA) | 5280 | 2218 | 7498 | - | - | 517 |
| DAR-ES-SALAAM INSTITUTE OF TECHNOLOGY {DIT) | 3603 | 623 | 4226 | 165 | 27 | 192 |
| MBEYA INSTITUTE OF SCIENCE AND TECHNOLOGY | 3454 | 655 | 4109 | 204 | 29 | 233 |
| INTERNATIONAL MEDICAL AND TECHNOLOGICAL UNIVERSITY {IMTU) | 468 | 277 | 745 | 65 | 10 | 75 |
| WELL BUGANDO UNIVERSITY COLLEGE OF HEALTH SCIENCES {WBUCHS) | 1564 | 1054 | 2618 | 110 | 35 | 145 |
| SAINT AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA {SAUT) | 4492 | 2989 | 7481 | 181 | 96 | 277 |
| MWENGE UNIVERSITY COLLEGE OF EDUCATION {MWUCE) | 2990 | 1348 | 4338 | 64 | 43 | 107 |
| MOSHI UNIVERSITY COLLEGE OF COOPERATION AND BUSSINESS STUDIES | 1880 | 1626 | 3506 | 111 | 36 | 147 |
| STEFANO MOSHI MEMORIAL UNIVERSITY COLLEGE | 295 | 275 | 570 | 30 | 17 | 47 |
| RUAHA UNIVERSITY COLLEGE | 3016 | 1932 | 4948 | 109 | 39 | 148 |
| IRINGA UNIVERSITY | 2022 | 1676 | 3698 | 81 | 28 | 109 |
| MKWAWA UNIVERSITY OF COLLEGE EDUCATION | 2897 | 1041 | 3938 | 113 | 64 | 177 |
| THE AGAKHAN UNIVERSITY | 99 | 101 | 200 | 32 | 13 | 45 |
| JORDANI UNIVERSITY COLLEGE | 1472 | 1026 | 2498 | 73 | 39 | 112 |
| MZUMBE UNIIVERSITY | 5687 | 2609 | 8296 | 212 | 81 | 293 |
| COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION-DAR | 2940 | 2807 | 5747 | 127 | 31 | 158 |
| UNIVERSITY OF DODOMA INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING | 2302 | 2315 | 4617 | 73 | 22 | 95 |
| MADINI INSTITUTE- DODOMA | 445 | 84 | 529 | 43 | 7 | 50 |
| DODOMA UNIVERSITY {UDOM) | 15898 | 7099 | 22997 | 528 | 226 | 754 |
| ARUSHA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY | 1975 | 1722 | 3697 | 76 | 18 | 94 |
| HUBERT KAIRUKI MEMORIAL UNIVERSITY {HKMU) | 675 | 720 | 1395 | 34 | 22 | 56 |
| ECKERNFORDE TANGA UNIVERSITY | 957 | 568 | 1525 | 28 | 3 | 31 |
| ARDHI UNIVERSITY {UCLAS) | 2471 | 1669 | 4140 | 170 | 71 | 241 |
| INSTITUTE OF SOCIAL WORK | 761 | 1593 | 2354 | 43 | 17 | 60 |
| ST. JOHN COLLEGE OF ENGINEERING & TECHNOLOGY | 741 | 898 | 1639 | 11 | 30 | 41 |
| ARUSHA UNIVERSITY | 839 | 734 | 1573 | 10 | 47 | 57 |
| ST. JOSEPH UNIVERSITY COLLEGE OF ENGINEERING AND TECHNOLOGY | 3051 | 828 | 3879 | 73 | 26 | 99 |
| ARUSHA TECHNICAL COLLEGE | 1242 | 375 | 1617 | 69 | 12 | 81 |
| MUHIMBILI HEALTH ALLIED SCIENCES UNIVERSITY {MUHAS) | 2053 | 1008 | 3061 | 163 | 141 | 304 |
| INSTITUTE OF ADULT EDUCATION | 1205 | 1496 | 2701 | 70 | 30 | 100 |
| DARES SALAAM UNIVERSITY COLLEGE OF EDUCATION | 3818 | 1850 | 5668 | 74 | 132 | 206 |
| MWL. NYERERE MEMORIAL UNIVERSITY | 2048 | 2204 | 4252 | 75 | 108 | 183 |
| MARIAN UNIVERSITY | 562 | 248 | 810 | 23 | 5 | 28 |
| MUSLIM UNIVERSITY | 1467 | 926 | 2393 | 49 | 13 | 62 |
| EASTERN AFRICA STATISTICS TRAINING CENTRE | 241 | 104 | 345 | 18 | 9 | 27 |
| ST. JOHN UNIVERSITY OF TANZANIA | 1791 | 1317 | 3108 | 72 | 32 | 104 |
| COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION-DODOMA | 901 | 871 | 1772 | 34 | 8 | 42 |
| LOCAL GOVERNMENT TRAINING INSTITUTE (LGTI) | 1927 | 1153 | 3080 | 59 | 17 | 76 |
| KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL UNIVERSITY COLLEGE (KCMC) | 1234 | 858 | 2092 | 106 | 53 | 159 |
| CENTRE FOR EDUCATION DEVELOPMENT IN HEALTH ARUSHA (CEDHA) | 14 | 17 | 31 | 7 | 4 | 11 |
| LIVESTOCK TRAINING (LITA TENGERU) | 263 | 203 | 466 | 18 | 4 | 22 |
| HORTICULTURE RESEARCH AND TRAINING INSTITUTE (TENGERU) | 29 | 35 | 64 | 11 | 6 | 17 |
| ST. AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA-ARUSHA BRANCH | 652 | 440 | 1092 | 24 | 14 | 38 |
| TENGERU INSTITUTE OF COMMUNITY DEVELOPMENT (TICD) | 378 | 699 | 1077 | 22 | 10 | 32 |
| TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA | 1659 | 1167 | 2826 | 37 | 14 | 51 |
| MOUNT MERU UNIVERSITY | 621 | 429 | 1050 | 48 | 12 | 60 |
| NELSON MANDELA AFRICAN INSTITUTION OF SCIENCE AND TECHNOLOGY | 157 | 81 | 238 | 38 | 19 | 57 |
| JOMO KENYATTA UNIVERSITY OF AGRICULTURE AND TECHNOLOGY | 200 | 159 | 359 | 4 | 1 | 5 |
| DAR ES SALAAM MARIRIME INSTITUTE (DMI) UNIVERSITY | 461 | 51 | 512 | 33 | 5 | 38 |
| SEBASTIAN KOLOWA UNIVERSITY | 768 | 415 | 1183 | 56 | 18 | 74 |
| TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY UNIVERSITY (TIA) | 2876 | 3712 | 6588 | 39 | 4 | 43 |
| THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA | 29107 | 17834 | 46941 | 199 | 120 | 319 |
| SAINT AUGUST UNIVERSITY OF TANZANIA (SAUT)-Mbeya branch | 1233 | 748 | 1981 | 38 | 15 | 53 |
| TEOFILO KISANJI UNIVERSITY-Mbeya | 870 | 468 | 1338 | 35 | 12 | 47 |
| INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT UNIVERSITY | 4842 | 3386 | 8228 | 122 | 33 | 155 |
| MZUMBE UNIIVERSITY-DAR CAMPUS | 758 | 792 | 1550 | 18 | 9 | 27 |
| TUMAINI UNIVERSITY -DAR | 862 | 1110 | 1972 | 36 | 17 | 53 |
| TEOFILO KISANJI UNIVERSITY-DAR | 210 | 207 | 417 | 17 | 6 | 23 |
| **JUMLA** | **154323** | **94059** | **248382** | **6309** | **2544** | **9370** |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

- Takwimu hazikupatikana

**SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO**

Jedwali Na. 81 (Namba)

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2000 | 30789 | 26601 | 23469 | 20430 | 5894 | 5011 | 112194 |
| 2001 | 36305 | 30820 | 25004 | 20762 | 5892 | 5116 | 123899 |
| 2002 | 41593 | 34209 | 27540 | 20681 | 6418 | 5534 | 135975 |
| 2003 | 46891 | 38506 | 26385 | 21650 | 6430 | 4859 | 144721 |
| 2004 | 48752 | 46167 | 33240 | 24476 | 8847 | 6229 | 167711 |
| 2005 | 45276 | 46321 | 32063 | 29248 | 9183 | 7046 | 169137 |
| 2006 | 46968 | 48013 | 42878 | 29796 | 9569 | 7956 | 185180 |
| 2007 | 47437 | 46927 | 41340 | 35746 | 11299 | 8667 | 191416 |
| 2008 | 42971 | 43232 | 43177 | 35980 | 12576 | 8594 | 186530 |
| 2009 | 44255 | 36384 | 37064 | 34061 | 11851 | 9096 | 172711 |
| 2010 | 56620 | 57876 | 50778 | 46820 | 12269 | 13006 | 237369 |
| 2011 | 63282 | 67205 | 65859 | 54521 | 11083 | 11926 | 273876 |
| 2012 | 65058 | 69403 | 64453 | 61209 | 9684 | 11713 | 281520 |
| 2013 | 70060 | 77407 | 67998 | 65637 | 8592 | 9651 | 299345 |
| 2014 | 109784 | 96732 | 76574 | 66898 | 8865 | 7686 | 366539 |
| 2015 | - | - | - | - | - | - | - |
| 2016 | 70844 | 81499 | 72970 | 73231 | 21091 | 17731 | 337366 |
| 2017 | 71160 | 79548 | 77168 | 72056 | 24146 | 19578 | 343656 |
| 2018 | 64844 | 71685 | 74932 | 74848 | 24030 | 23441 | 333780 |
| Badiliko (% ) | | | | | | | |
| 2017 - 2018 | -8.9 | -9.9 | -2.9 | 3.9 | -0.5 | 19.7 | -2.9 |

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

# SURA YA 20

## AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

### AFYA

**Vituo vya Kutolea Huduma za Afya**

357. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ambapo vituo vya kutolea huduma za afya viliongezeka kwa asilimia 5.7 na kufikia vituo 8,119 kutoka vituo 7,678 mwaka 2017. Kati ya vituo hivyo, Serikali ilikuwa inamiliki asilimia 71 ya vituo vyote, Mashirika ya dini asilimia 12, Taasisi za Serikali asilimia 3 na vituo binafsi asilimia 15. Aidha, hospitali zilikuwa asilimia 3.6, vituo vya afya asilimia 10.7 na zahanati asilimia 85.7. Katika kipindi hicho, wagonjwa wa nje walikuwa 41,052,012 ikilinganishwa na wagonjwa 35,082,840 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 17.0. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali kusogeza huduma za afya karibu na wananchi pamoja na kuhamasisha matumizi ya bima za afya. Aidha, wagonjwa wa kulazwa walipungua kutoka 1,650,224 mwaka 2017 hadi wagonjwa 1,359,264 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, idadi ya vitanda vya wagonjwa iliongezeka kutoka vitanda 60,952 mwaka 2017 hadi vitanda 61,203 mwaka 2018.

**Huduma za Afya kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja**

358. Mwaka 2018, watoto 1,568,832 walizaliwa ikilinganishwa na watoto 1,498,488 mwaka 2017. Watoto hao walipata huduma za chanjo ili kuzuia magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya kupooza, kuharisha, pepopunda, pneumonia, homa ya ini na surua. Chanjo zilizotolewa zilikuwa OPV ambayo ilichanjwa kwa asilimia 91, PETNT3 asilimia 97, PV3 asilimia 96 na Rota2 asilimia102. Kutolewa kwa chanjo hizo kwa ufanisi kumeifanya Tanzania kuendelea kuwa katika kiwango cha juu zaidi cha asilimia 90 kilichowekwa na Shirika la Afya Duniani. Katika kipindi hicho, dozi za chanjo mbalimbali zilinunuliwa na kusambazwa nchini zikiwemo dozi 443,600 za HPV, BCG dozi milioni mbili, bOPV milioni mbili, Rota 1,801,500, IPV 1,048,600, Surua Rubella 107900, na Pentavalet 1,517,000.

**Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

359. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo bajeti ya dawa iliongezwa kutoka shilingi bilioni 251.5 mwaka 2016/17 hadi shilingi bilioni 269 mwaka 2017/18. Ongezeko hilo la bajeti limewezesha upatikanaji wa dawa muhimu zinazofuatiliwa *(tracer medicine)* katika vituo vya kutolea huduma za afya kufikia asilimia 94.4. Aidha, aina 312 za dawa zilipatikana katika Bohari Kuu ya Dawa ikilinganishwa na aina 135 za dawa zilizokuwa zinapatikana mwaka 2017. Katika kipindi hicho, kiwango cha upatikanaji wa aina 312 za dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya kilikuwa asilimia 76 ikilinganishwa na kiwango cha asilimiia 89.6 cha aina 135 za dawa mwaka 2017. Serikali ilinunua mashine za X-ray 11 za kidigitali na kupelekwa katika hospitali za Ruvuma, Chato, Morogoro, Simiyu, Magu, Singida, Nzega, Njombe, Bukoba, Amana na Katavi. Vile vile, Serikali ilikamilisha kufunga na kupewa kibali na Tume ya Nguvu za Atomiki – Tanzania kwa ajili ya Mashine hizo katika hospitali 5 za Ruvuma, Chato, Morogoro, Simiyu na Magu kwa ajili ya kuanza kutoa huduma.

**Afya ya Uzazi na Mtoto**

360. Mwaka 2018, wajawazito 2,260,120 walihudhuria kliniki ikilinganishwa na wajawazito 2,092,940 mwaka 2017. Mwongozo wa utoaji huduma za afya ya uzazi na mtoto unaelekeza wajawazito kuanza huduma kabla ya majuma 12 ya ujauzito na kuhudhuria kliniki angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito ili waweze kupata huduma muhimu. Katika kipindi hicho, asilimia 28 ya wajawazito waliweza kufanya hudhurio la kwanza kabla ya majuma 12 ikilinganishwa na asilimia 17 mwaka 2017. Aidha, wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara nne waliongezeka kutoka asilimia 46.2 mwaka 2017 hadi asilimia 63.7 mwaka 2018 . Mikoa yenye kiwango kidogo cha hudhurio la nne kliniki ilikuwa ni Njombe asilimia 44.2, Simiyu asilimia 45.9, Mara asilimia 48.1, Tanga asilimia 50.4, Manyara asilimia 51.7, Dodoma asilimia 52.3 na Iringa asilimia 52.4. Kwa upande mwingine, huduma ya kumkinga mama mjamzito dhidi ya Malaria iliimarika ambapo asilimia 81.1 ya wajawazito walipatiwa kinga mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 66.1 mwaka 2017. Aidha, asilimia 97.2 ya wajawazito waliohudhuria kliniki walipimwa VVU ambapo asilimia 3.9 waligundulika kuwa na VVU ikilinganishwa na asilimia 4.2 waliogundulika mwaka 2017. Kati ya waliogundulika na VVU, asilimia 99 walianzishiwa dawa za ARV ili kuimarisha afya zao pamoja na kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

361. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika vituo vya afya ili viweze kutoa huduma za dharura za upasuaji ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kutoa mtoto tumboni (CEmONC) pindi inapohitajika. Katika kipindi hicho, vituo vya afya 304 viliboreshwa sawa na asilimia 58 ya vituo 527 vinavyomilikiwa na Serikali. Maboresho hayo yalihusisha ujenzi na ukarabati wa vyumba vya upasuaji, wodi za akina mama wajawazito, vyumba vya maabara na nyumba za watumishi.

**Lishe**

362. Mwaka 2018, Serikali ilifanya Utafiti wa Kitaifa wa Hali ya Lishe katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na mikoa 5 ya Zanzibar ili kubaini viwango vya hali ya lishe nchini. Utafiti huo ulifanyika kwa kaya zaidi ya 18,000 na kuhusisha watoto 14,000 wenye umri chini ya miaka mitano na wanawake zaidi ya 10,000 walio kwenye umri wa kuzaa. Vile vile, katika utafiti huo sampuli 10,000 za chumvi inayotumika katika kaya zilipimwa kiwango cha madini joto kwa lengo la kuangalia kiwango cha matumizi ya chumvi yenye madini joto katika kaya. Kwa upande wa hali ya udumavu wa watoto walio chini ya miaka mitano, matokeo yalionesha kuwa kiwango cha udumavu kwa watoto walio chini ya miaka mitano kimeshuka hadi kufikia asilimia 31.8 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 34 mwaka 2015/16. Mwenendo huu unaonesha kufikiwa kwa kiwango kilichowekwa na nchi cha kushusha udumavu kwa angalau asilimia 1 kila mwaka kuanzia mwaka 2015/16 kwa lengo la kushusha udumavu hadi kufikia asilimia 28 ifikapo mwaka 2020/21.

**Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa**

363. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya kibingwa nchini na hivyo kupunguza gharama zilizotokana na kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Aidha, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilifanya upandikizaji wa figo kwa wagonjwa 38 toka kuanzishwa kwa huduma hii mwaka 2017. Kutokana na kupatikana kwa huduma hii nchini, Serikali inatumia wastani wa shilingi milioni 20 ikilinganishwa na wastani wa shilingi milioni 100 kama mgonjwa angepelekwa nje ya nchi.

364. Mwaka 2018, huduma za kibingwa ziliendelea kutolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete na Hospitali ya Benjamin Mkapa. Huduma zilizotolewa ni pamoja na upandikizaji wa figo, upasuaji wa moyo, upasuaji wa mifupa ya fahamu na ubadilishaji wa nyonga na upandakizaji wa vifaa vya kusaidia usikivu. Aidha,

Serikali iliendelea kuimarisha mapambano dhidi ya saratani ikiwemo saratani ya mlango wa kizazi katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road. Vile vile, Serikali ilisogeza huduma za tiba ya saratani karibu na wananchi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya.

365. Katika kuboresha utoaji wa huduma za kibingwa, Serikali ilinunua mashine kubwa tatu za kisasa za kupimia sampuli za damu ambazo ni ERBA XL 600, DYMIND DH 76 na COBAS e 411 zilizowezesha utoaji wa huduma bora katika vipimo vya *Full Blood Picture, Clinical Chemistry na Immunoasays*. Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ilinunua mashine ya vipimo vya kemia uhai (*Cobas Integra 400 plus*) ambayo ina uwezo wa kufanya vipimo zaidi ya 400 kwa saa na kuchukua sampuli 75 za damu kwa wakati mmoja.Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ilikamilisha kufunga mashine ya kusoma X-ray kidigitali (CR mashine) pamoja na mashine tatu za kisasa za LINAC na CT Simulator**.** Ongezeko la mashine hizo ziliiwezesha Taasisi kuwa na mashine tano za tiba ya mionzi zenye uwezo wa kutibu wagonjwa 100 kwa siku na hivyo kupunguza muda wa kusubiria tiba kutoka wiki sita hadi chini ya wiki nne.

**Udhibiti wa Malaria**

366. Mwaka 2018, Serikali iliendelea na kampeni ya "*Si Kila Homa ni Malaria*" kwa kuhakikisha katika vituo vya kutolea huduma za afya kuna vipimo vya malaria. Kampeni hiyo iliwezesha kuokoa kiasi kikubwa cha dawa za malaria kilichokuwa kinatumika kutibu homa ambazo si malaria. Katika kipindi hicho, vipimo 23,545,575 vya vitendanishi vya malaria pamoja na dozi 8,662,590 za dawa ya mseto zilinunuliwa kwa ajili ya matibabu ya malaria. Vile vile, vichupa 891,862 vya dawa ya malaria ya sindano na dozi 9,328,333 za dawa ya SP kwa ajili ya kumkinga mama mjamzito na malaria zilinunuliwa. Aidha, jumla ya vyandarua 3,286,774 vilinunuliwa na kusambazwa mwaka 2018. Kiwango cha ugonjwa wa malaria kwa watoto chini ya miaka mitano kilifikia asilimia 7.3 kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015/16 na kwa wajawazito kilifikia asilimia 6.6 kutoka asilimia 7.1 mwaka 2017.

### Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu

367. Mwaka 2018, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya afya iliendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu. Katika kipindi hicho, jumla ya wagonjwa 47,967 waligundulika kuwa na vijidudu vya kifua kikuu ikilinganishwa na wagonjwa 44,714 waliogundulika mwaka 2017. Kwa upande mwingine, asilimia 99 ya wagonjwa waliokuwa na maambukizi ya kifua kikuu walipimwa VVU ambapo asilimia 31 walikutwa na VVU ikilinganishwa na asilimia 97 ya wagonjwa wa kifua kikuu waliopimwa VVU mwaka 2017 na asilimia 34 kugundulika kuwa na VVU. Kufuatia hali hii, Serikali ilihakikisha kuwa wagonjwa wote wa kifua kikuu wanaogundulika kuwa na VVU/UKIMWI wanaanzishiwa dawa za ART kwa ajili ya kupunguza makali na kufubaza virusi vya UKIMWI.

### Mafunzo kwa Watumishi wa Kada ya Afya

368. Mwaka 2018, wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya walifikia 18,996 ikilinganishwa na wanafunzi 16,214 mwaka 2017. Kati ya hao, wanafunzi 5,226 walijiunga kwenye vyuo vya Serikali na wanafunzi 13,770 kwenye vyuo binafisi katika programu za uuguzi na ukunga, sayansi shirikishi za afya na wahudumu wa afya ya jamii. Aidha, wanafunzi 27,683 walifanya mitihani ya kuhitimu mafunzo katika ngazi mbalimbali ambapo wanafunzi 18,289 walikuwa wa sayansi shirikishi, 7,013 wa uuguzi na ukunga na 2,381wahudumu afya ya jamii.

## MAENDELEO YA JAMII

### Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

369. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya maendeleo ya jamii katika ngazi za astashahada, stashahada, shahada, stashahada ya uzamili na shahada ya uzamili. Mafunzo hayo yalitolewa kupitia vyuo nane vya maendeleo ya jamii vya Buhare, Mlale, Misungwi, Rungemba, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli pamoja na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Katika kipindi hicho, wanafunzi waliodahiliwa waliongezeka kwa asilimia 34.4 hadi kufikia wanafunzi 4,597 (wanawake 3,104 na wanaume 1,493) kutoka wanafunzi 3,420 (wanawake 2,146 na wanaume 1,274) mwaka 2017. Ongezeko hilo lilitokana na ukarabati wa majengo na miundombinu katika vyuo nane vya maendeleo ya jamii pamoja na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Aidha, idadi ya wahitimu waliongezeka kutoka 2,665 (wanawake 1,564 na wanaume 1,101) mwaka 2017 hadi kufikia wahitimu 3,196 (wanawake 1,847 na wanaume 1,349) mwaka 2018.

370. Mwaka 2018, jumla ya wanafunzi 1,064 (wanawake 614 na wanaume 450) walidahiliwa katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii ikilinganishwa na wanafunzi 1,185 (wanawake 385 na wanaume 800) mwaka 2017. Aidha, idadi ya wanafunzi waliohitimu iliongezeka kutoka wanafunzi 1,122 (wanawake 722 na wanaume 400) mwaka 2017 hadi kufikia wanafunzi 1,598 (wanawake 1,100 na wanaume 498) mwaka 2018. Vile vile, Chuo cha Ustawi wa Jamii - Kisangara kiliendelea kutoa mafunzo kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi ya astashahada na stashahada. Chuo hicho kilidahili wanafunzi 158 (wanawake 115 na wanaume 43) mwaka 2018 ikilinganishwa na wanafunzi 85 (wanawake 58 na wanaume 27) waliodahiliwa mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 85.9.

**Maendeleo ya Wanawake**

371. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuweka mazingira wezeshi katika kuleta usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake nchini ili kuwa na maendeleo jumuishi katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, Serikali iliwawezesha wanawake kupata masoko ya huduma na bidhaa wanazozalisha kupitia maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Katika kipindi hicho, jumla ya wanawake wajasiriamali 103 kutoka katika Halmashauri tisa ambazo ni Wilaya ya Songwe, Chamwino, Bahi, Mbeya Jiji, Arusha Jiji, Manispaa ya Moshi, Dodoma Jiji, Iringa Manispaa, na Tanga Jiji waliwezeshwa kushiriki katika maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi yaliyoandaliwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Maonesho hayo yaliwawezesha wanawake wajasiriamali kujifunza mbinu mbalimbali za kuboresha bidhaa na kupata uzoefu kuhusu upatikanaji wa masoko kutoka kwa washiriki wa mikoa na nchi nyingine. Kutokana na juhudi hizo, ushiriki wa wanawake wajasiriamali katika maonesho uliongezeka kutoka 1,183 mwaka 2017/18 hadi wanawake 1,286 mwaka 2018/19.

**Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto**

372. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kutoa huduma za malezi ya kambo ili kumuwezesha mtoto kulelewa katika familia ambayo inakidhi matakwa kulingana na Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009. Katika kipindi hicho, jumla ya watoto 54 (wasichana 30 na wavulana 24) walio katika mazingira hatarishi walipata huduma za kuasili na malezi ya kambo ikilinganishwa na watoto 61 (wasichana 33 na wavulana 28) waliopata huduma hizo mwaka 2017.

373. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kutoa huduma za msingi pamoja na huduma za msaada wa kisheria kwa watoto walio katika mkinzano na sheria na wanaolelewa katika mahabusu tano za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Jumla ya watoto 354 (wasichana 34 na wavulana 320) walio katika mkinzano na sheria waliwezeshwa kupata huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu na elimu ikilinganishwa na watoto 291 (wasichana 13 na wavulana 278) mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 21.6. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uelewa wa vyombo vya sheria (polisi na mahakama) ambapo watoto walioshtakiwa na kukosa dhamana walipelekwa kwenye mahabusu za watoto badala ya mahabusu za watu wazima. Aidha, uelewa uliongezeka kutokana na kutolewa kwa mafunzo ya uendeshaji wa mashauri ya watoto mahakamani kwa mahakimu, waendesha mashtaka, mawakili na maafisa ustawi wa jamii katika mikoa ya Tanga, Tabora, Singida, Dodoma, Kigoma, Mara, Mwanza, Njombe, Iringa, Mbeya na Songwe.

374. Mwaka 2018, jumla ya watoto 64 (wasichana 7 na wavulana 57) walio katika mkinzano na sheria walichepushwa kutoka katika mfumo rasmi wa haki jinai kwa kuwarekebisha tabia na kuwaunganisha na familia zao ikilinganishwa na watoto 126 (wasichana 24 na wavulana 102) waliochepushwa mwaka 2017. Vile vile, watoto wa kiume 30 walihukumiwa na kupelekwa katika Shule ya Maadilisho Irambo-Mbeya ikilinganishwa na watoto 35 wa kiume waliohukumiwa mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 14.3. Shule ya Maadilisho Irambo inatumika kutoa marekebisho ya tabia kwa watoto waliohukumiwa kwa makosa mbalimbali ya jinai pamoja na fursa ya watoto hao kuendelea na elimu ya msingi.

375. Mwaka 2018, Serikali iliendelea na jitahada za kuhakikisha kuwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanapata malezi bora. Katika kipindi hicho, jumla ya leseni 48 za maombi ya makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi zilitolewa ikilinganishwa na leseni 18 mwaka 2017. Utoaji wa leseni umewezesha wadau kuchangia katika upatikanaji wa huduma za msingi kwa watoto hao na hivyo kuwezesha jumla ya makao ya watoto yenye usajili kufikia 141. Aidha, jumla ya watoto 13,420 (wasichana 6,651 na wavuana 6,769) walipata huduma za msingi mwaka 2018 ikilinganishwa na watoto 6,132 (wasichana 2,972 na wavulana 3,160) waliopata huduma hizo mwaka 2017. Vile vile, Serikali iliendelea kuwawezesha watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani kwa kuwapatia huduma za msingi ikiwemo malazi, afya, elimu, mafunzo na kuwaunganisha na familia zao. Jumla ya watoto 2,826 walipata huduma hizo

mwaka 2018 ikilinganishwa na watoto 6,393 waliotambuliwa na kupewa huduma mwaka 2017.

**Huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto**

376. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Jumla ya watoto 7,123 (wasichana 4,701 na wavulana 2,422) waliandikishwa katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ikilinganishwa na watoto 6,075 mwaka 2017. Aidha, idadi ya walezi katika vituo hivyo ilikuwa 2,482 ikilinganishwa na walezi 1,882 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 31.9. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Serikali kuhimiza wamiliki wa vituo vya kulelea watoto mchana kuajiri walezi wa kutosha kulingana na idadi ya watoto kwenye vituo. Vile vile, jumla ya vituo 67 vya kulelea watoto wadogo mchana vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 196 vilivyosajiliwa mwaka 2017 na kufanya jumla ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kufikia 1,170 mwaka 2018.

**Huduma za Ustawi kwa Wazee**

377. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kuwezesha utoaji wa huduma za msingi za chakula, malazi, mavazi na matibabu kwa wazee wasiojiweza katika makazi 17 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali. Aidha, wazee 510 wasiojiweza (wanawake 234 na wanaume 276) walipatiwa huduma za msingi katika makazi hayo mwaka 2018 ikilinganishwa na wazee 514 wasiojiweza (wanawake 247 na wanaume 267) waliopata huduma mwaka 2017.

378. Katika kuhakikisha wazee wanapata matibabu bure, Serikali iliendelea na jitihada za kuwatambua wazee katika Halmashauri 185 za Tanzania Bara ambapo hadi kufikia Desemba 2018 jumla ya wazee 1,897,031 walitambuliwa. Mwaka 2018, jumla ya wazee 247,771 (wanawake 160,043 na wanaume 87,728) walipata vitambulisho vya matibabu bure ikilinganishwa na wazee 506,943 (wanawake 220,312 na wanaume 286,631) waliopata vitambulisho mwaka 2017.

**Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

379. Mwaka 2018, Serikali iliendelea kusimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kuchangia maendeleo ya Taifa ambapo mashirika 516 yalisajiliwa, ikilinganishwa na mashirika 385 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 34. Ongezeko hilo lilitokana na zoezi la uhakiki la mwaka 2017 lililohimiza usajili chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na.24 ya

mwaka 2002. Kati ya mashirika 516 yaliyosajiliwa, mashirika 37 yalisajiliwa katika ngazi ya kimataifa, 462 ngazi ya kitaifa, 13 ngazi ya wilaya na manne ngazi ya mkoa. Hadi kufikia Desemba 2018, mashirika 8,948 yalisajiliwa katika hatua za cheti na cheti cha ukubalifu katika ngazi za wilaya, mkoa, Taifa na kimataifa.

**IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA**

Jedwali Na. 84

| Aina ya Vituo | 2015 | | | 2016 | | | 2017 | | | 2018 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Binafsi** | **Serikali** | **Jumla** | **Binafsi** | **Serikali** | **Jumla** | **Binafsi** | **Serikali** | **Jumla** | **Binafsi** | **Serikali** | **Dini** | **Jumla** |
| Zahanati | 1419 | 4724 | 6143 | 1421 | 4789 | 6210 | 1435 | 4925 | 6360 | 986 | 5055 | 659 | 6700 |
| Vituo vya Afya | 211 | 507 | 718 | 259 | 508 | 767 | 277 | 527 | 804 | 127 | 551 | 156 | 834 |
| Hospitali | 128 | 124 | 252 | 146 | 119 | 265 | 150 | 123 | 273 | 50 | 127 | 108 | 285 |
| Nyinginezo* | 133 | 3 | 136 | 39 | 15 | 54 | 182 | 8 | 190 | 225 | 21 | | 246 |
| Maternity/Nursing Homes | | | | | | 50 | 50 | 1 | 51 | 52 | 2 | | 54 |
| **Jumla** | **1891** | **5358** | **7249** | **1865** | **5431** | **7346** | **2094** | **5584** | **7678** | **1440** | **5756** | **923** | **8119** |

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

* Ni pamoja na kliniki

**HUDUMA ZA AFYA : WANAFUNZI WALIOFAULU MAFUNZO YA AFYA**

Jedwali Na.85

| Aina ya Mafunzo | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 |
|---|---|---|---|---|---|
| Doctor of Medicine (MO) | - | 204 | 869 | 1072 | - |
| Advanced Diploma in AMO Anaesthesia | - | 3 | 3 | 8 | 0 |
| Advanced Diploma in Clinical Dentistry | - | 7 | 7 | 1 | 11 |
| Advanced Diploma in Clinical Medicine | 59 | 130 | 36 | 56 | 116 |
| Advanced Diploma in Ophthalmology | - | 10 | 4 | 2 | 7 |
| Advanced Diploma in Vector Control | 7 | 12 | 3 | - | 2 |
| Diploma in Clinical Medicine | - | 700 | 440 | 394 | 1256 |
| Diploma in Dental Laboratory Technology | 4 | 4 | 4 | 3 | 6 |
| Diploma in Dental Therapy | - | 47 | 26 | 53 | 52 |
| Diploma in Diagnostic Radiography | - | 55 | 55 | 91 | 105 |
| Diploma in Environmental Health Science | 116 | 136 | 75 | 35 | 26 |
| Diploma in Health Laboratory Sciences | 44 | 120 | 194 | 223 | 180 |
| Diploma in Health Personnel Education | 23 | 29 | 21 | 29 | 10 |
| Diploma in Medical Laboratory Sciences | 44 | 194 | 40 | 64 | 180 |
| Diploma in Nursing and Midwifery | 508 | 1804 | 1060 | 623 | 1734 |
| Diploma in Occupational Therapy | - | 12 | - | - | 16 |
| Diploma in Optometry | - | 11 | 10 | 15 | 2 |
| Diploma in Pharmaceutical Sciences | 40 | 184 | 137 | 88 | 160 |
| Diploma in Physiotherapy | 26 | 20 | 7 | 13 | 6 |
| Certificate in Clinical Medicine | - | 830 | 110 | 138 | 1330 |
| Certificate in Medical Laboratory Sciences | - | 506 | 271 | 217 | 486 |
| Certificate in Health Record Technology | - | 48 | 16 | 50 | 11 |
| Certificate in Pharmaceutical Sciences | - | 150 | 150 | 132 | 215 |
| Certificate in Nursing | - | 2740 | 3288 | 1645 | 4232 |
| | 871 | 7956 | 6826 | 4952 | 10143 |

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

**IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA**

Jedwali Na. 86

| Mwaka | Wagonjwa wa Nje | | | Jumla ya Wagonjwa waliolazwa |
|---|---|---|---|---|
| | Hospitali | Zahanati | Vituo vya Afya | |
| 1995 | 355483 | 6785925 | 545921 | 240707 |
| 1996 | 604023 | 9530361 | 927606 | 541781 |
| 1997 | 711222 | 10003245 | 1052326 | 559949 |
| 1998 | 750465 | 10112305 | 1134242 | - |
| 1999 | 812891 | 10321654 | 1242354 | 626700 |
| 2000 | 989101 | 13697988 | 1874346 | 626700 |
| 2001 | 1167139 | 17218371 | 2511624 | 680263 |
| 2002 | 1328395 | 19695356 | 3258520 | 701568 |
| 2003 | 1491909 | 22935688 | 3659615 | 1390273 |
| 2004 | 1532028 | 23552460 | 3758027 | 2125388 |
| 2005 | 1619700 | 24900276 | 3973085 | 2237146 |
| 2006 | 1754925 | 26979136 | 4304787 | 2837252 |
| 2007 | 1842671 | 28328093 | 4520026 | 2979115 |
| 2008 | 1934805 | 29744498 | 4746027 | 3128071 |
| 2009 | 2128286 | 32718948 | 5220630 | 3440870 |
| 2010 | 2341114 | 35990843 | 5742693 | 3784957 |
| 2011 | 2622048 | 39917117 | 6431816 | 4239152 |
| 2012 | 2815529 | 41333522 | 6657817 | 4388108 |
| 2013 | 2903275 | 42682479 | 6873056 | 4529971 |
| 2014 | 5910725 | 14008692 | 475295 | 1665935 |
| 2015 | 4480781 | 25072487 | 6006466 | 1858956 |
| 2016 | 4984645 | 20859281 | 6515219 | 1775835 |
| 2017 | 5266252 | 21115639 | 7050725 | 1650224 |
| 2018 | 4675045 | 27473506 | 8903461 | 1359264 |

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,Jinsia, Wazee na Watoto

**IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI**

Jedwali Na. 87

| Aina ya Huduma | 2017 | | | | Jumla | 2018 | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Shirika la Umma | Shirika la Kujitolea/Dini | Binafsi | | Serikali | Shirika la Kujitolea/Dini | Binafsi | |
| Hospital za Mkoa | 6931 | 260 | 0 | 0 | 7191 | 7523 | 0 | 0 | 7523 |
| Hospitali za Wilaya | 6683 | 0 | 6618 | 0 | 13301 | 6802 | 6750 | 0 | 13552 |
| Hospitali nyingine | 224 | 97 | 2705 | 529 | 3555 | 336 | 2889 | 710 | 3935 |
| Vituo vya Afya | 9429 | 258 | 3820 | 2185 | 15692 | 9794 | 3868 | 2205 | 15867 |
| Zahanati | 13299 | 250 | 4110 | 3554 | 21213 | 13602 | 4160 | 3564 | 21326 |
| **Jumla** | **36566** | **865** | **17253** | **6268** | **60952** | **38057** | **17667** | **6479** | **62203** |

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,Jinsia, Wazee na Watoto